# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## KIMEANDIKWA NA

## SAYYID MUJTABAA MUUSAWIY LARI

### KUHUSU MWANDISHI

Sayyid Mujtaba Mussawi Lari ni mtoto wa marehemu Ayatullah Sayyid Ali Asghar Lari mmojawapo wa wanachuoni na watu mashuhuri katika jamii ya Iran. Babu yake alikuwa marehemu Ayatullah Hajj Sayyid Abd ul-Husayn Lari ambaye alipigania uhuru wakati wa mapinduzi ya kikatiba. Wakati wa kipindi kirefu cha mapambano yake dhidi ya serikali dhalimu ya wakati huo, alijaribu kuanzisha serikali ya Kiislamu na alifaulu kufany hivyo kwa kipindi kifupi huko Larestan.

Sayyid Mujtaba Musawi Lari alizaliwa mwaka 13/4/1935 kwenye jiji la Lar ambako alihitimu elimu yake ya Msingi na masomo ya mwanzo ya Kiislamu. Mnamo mwaka wa 1332/1953, aliondoka Lar na akaenda Qum kuendelea na masomo yake ya elimu ya Kiislamu, akiwa anafundishwa na maprofesa na waalimu wa taasisi ya Kidini, pamoja na wanazuoni wakuu katika maarifa ya sheria (maraji).

Mnamo mwaka wa 1341/ 1962, akawa mshiriki katika Maktabil-Islam, gazeti la kidini na kisayansi lililokuwa lianaandika mfululizo wa makala kuhusu maadili ya Kiislamu. Makala hizi baadaye zilikusanywa na kuchapishwa kitabu kilichoitwa Ethical and psychological Problems. Matoleo tisa katika kitabu hiki kwa lugha ya kiajemi (Fursi) yamechapishwa, na pia kimetafsiriwa katika lugha ya Kiarabu na hivi karibuni kwa Kifaransa.

Mnamo mwaka 1342/1963. Alisafiri kwenda Ujerumani kutibiwa, na alirudi Iran baada ya miezi kadhaa, aliandika kitabu kiitwacho 'The face of Western Civilization'. Kitabu hiki kinajumuisha mazungumzo ya kulinganisha ustaarabu wa Kimagharibi na Kiisilamu, ndani ya kitabu hiki, mwandishi anataka kuthibitisha, kwa njia ya utambuzi, kifikira na ulinganisho kamili, ubora wa utambuzi na mambo mengi ya ustaarabu wa Uislamu kwa ule wa Magharibi. Kitabu hiki hivi karibuni tu kimechapishwa tena kwa mara ya saba. Mnamo 1349/1970, kitabu hiki kilitafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza na mtaalam wa mambo ya nchi za Mashariki, F.G. Goulding, na kilichochea hisia za watu huko Ulaya. Makala kuhusu kitabu hiki zilionekana kwenye magazeti kadhaa ya kimagharibi na BBC ilifanya mpango wa mahojiano na mtarjumi huyo ambapo sababu za kutafsiri na jinsi kilivyopelekwa hapo Uingereza zilizungumziwa. Tafsiri ya Kiingereza ya kitabu hiki hadi sasa imechapishwa mara tatu huko Uingereza, mara tano Iran na mara mbili Marekani.

Mnamo takriban miaka mitatu baada ya kuchapishwa tafsiri ya Kiingereza, Rudolf Singler, profesa wa chuo Kikuu wa Kijerumani alikitafsiri katika lugha ya Kijerumani, na tafsiri hiyo ilithibitisha kuwa yenye kuvutia huko Ujerumani. Mmojawapo wa viongozi wa chama cha Social Democratic Party alimtaarifu Mtarjumi katika barua kwamba kitabu hicho kimeacha mvuto wa kina juu yake yeye, na kusababisha yeye kubadilisha maoni yake kuhusu Uislamu, na kwamba angelipendekeza

Kitabu hicho kisomwe na marafiki zake. Tarjuma ya lugha ya Kijerumani imerudiwa kuchapishwa mara tatu hadi sasa.

Tafsiri za Kiingereza na Kijerumani za kitabu hiki zilichapishwa na Wizara ya Mwongozo wa Kiislamu kwa ajili kuisambaza zaidi nje ya Iran kupitia Wizara ya mambo ya Nje na taasisi ya mafunzo ya Kiislamic nchi za nje. Wakati huo huo ilipochapishwa tafsiri ya kwanza ya lugha ya Kijerumani, mwanachuo Muislamu wa asili ya kihindi aitwaye Maulana Raushan Ali alikitarjumi kitabu hiki katika lugha ya Urdu kwa lengo la kukisambaza India na Pakistani. Tarjumi hii ya Urdu imechapishwa mara tano hadi sasa. Sayyid Mujtaba Musawi Lari pia ameandika kijarida kuhusu Tawhid (upweke wa Mwenyezi Mungu), ambacho kilitafsiriwa Uingereza na kuchapishwa mara kadhaa Marekani.

Mnamo mwaka 1343/1964, aliasisi taasisi ya kutoa msaada huko Lar kwa madhumuni ya kueneza Uislamu, kutoa mafunzo ya Kiislamu kwa vijana walioko vijijini, na kuwasaidia wasiojiweza. Taasisi hii iliendelea kufanya kazi hadi 1346/1967. Taasisi hii ilitekeleza mambo makuu kama kuwapeleka wanafunzi wa sayansi za Kidini vijijini kufundisha Uislamu kwa watoto na vijana, kuwagawia maelfu ya watoto wa shule nguo, vitabu, vifaa vya kuandikia, kujenga idadi ya misikiti, mashule, zahanati mijini na vijijini, na huduma nyingine nyingi.

Sayyid Mujtaba Musawi Lari aliyaandama matakwa yake katika maadili ya Kiislamu, akiandika makala mpya kuhusu somo hilo. Mnamo mwaka wa 1353/1974, mkusanyiko wa makala hizi, zilizopitiwa upya na kuongezewa maneno, zilitoka katika muundo wa kitabu kilichoitwa 'The Function of Ethics in Human Development.' Kitabu hiki kimechapishwa mara sita hadi sasa.

Mnamo mwaka 1357/1978, alisafiri hadi Marekani kwa mwaliko wa Taasisi ya Kiislamu nchini humo. Halafu akaenda Uingereza, Ufaransa na baada ya kurudi Iran alianza kuandika mfululizo wa makala kuhusu itikadi za Uislamu kwa ajili ya gazeti la Sorouch. Makala hizi baadaye zilikusanywa na kutengenezwa kitabu chenye juzuu nne kuhusu imani za misingi za Uislamu (tauhid, uadilifu wa Mwenyezi Mungu, utume, uimamui, na ufufuo) kwa jina la 'The Foundations of Islamic Doctrine.' Kitabu hiki chenye juzuu nne kimetafsiriwa katika lugha ya Kiarabu, sehemu zake zingine zikiwa tayari zimekwisha chapishwa mara tatu. Tafsiri ya Kiingereza ya juzuu ya kwanza ya kazi hii ndio imetengeneza kitabu hiki cha sasa; juzuu zilizosalia pia zitatafsiriwa na kuchapishwa. Tafsiri za Urdu, Hindi na Kifaransa pia zimo katika mpango wa kutayarishwa; juzuu mbili za lugha ya Kifaransa zimekwishatokea.

Mnamo mwaka wa 1359/1980, Sayyid Mujtaba Musawi Lari aliasisi Taasisi huko Qum iitwayo 'Office for The Diffusion of Islamic Culture Abroad.' Husambaza bure nakala za vitabu vyake vilivyotafsiriwa kwa watu wapendao kuzisoma duniani pote. Taasisi hii pia imechukua shughuli ya kuchapisha Qur'ani kwa lengo la kuisambaza kwa Waislamu binafsi, Taasisi na shule za Kidini hapa Afrika.

## NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la: "God and His Attributes." Sisi tumekiita: "Mwenyezi Mungu na Sifa Zake." Kitabu hiki, "Mwenyezi Mungu na Sifa Zake" ni kazi ya kielimu iliyofanywa na Mwanachuoni mahiri, Sayyid Mujtaba Musawi Lari. Mwandishi wa kitabu hiki ameichambua itikadi ya Kiislamu na Umoja wa Mungu (tawhid) kwa kutumia uhojaji wa kifilosofia na maneno mepesi. Ili kukamilisha kazi yake hii ametegemea sana juu ya Sunna na nukuu nyingi kutoka kwenye Qur'an Tukufu.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya 'Al-Itrah Foundation' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Salman Shou kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.

## UTANGULIZI

Ombwe la kielimu na kiitikadi linazidi kumsogeza mwanadamu mbali na utambuzi wa ukweli kuelekea kwenye dimbwi la upotovu. Leo tunashuhudia nguvu nyingi za ubunifu wa mwanadamu zikipotea bure pale anapofumbia macho ile bahari yenye utajiri na mawimbi ya utamaduni na fikra ambayo dini inaitengeneza na vile anavyoyaruhusu maisha yake ya kisomi kunyongwa na itikadi za dunia ya kisasa.

Leo, mawazo mbali mbali yanawasilishwa kwenye kizazi cha wakati wetu chenye kiu na ambacho kimechanganyikiwa, mawazo ambayo yanatokana na dhana potovu za juu juu za wanafalsafa na wanazuoni wenye peo finyu. Mawazo haya yanajifanya kujaribu kujibu mahitaji ya kizazi cha sasa, lakini hayapendekezi maana yoyote au lengo la maisha. Muundo wa mwelekeo mmoja wa fikira ambao ndio msingi wa mawazo haya sio malezi yanayofaa kwa ajili ya akili nyeti za zama zetu hizi, na wala haustahili hata kufikiriwa katika mazingira yoyote yale ambamo akili na busara bado vinakuwa na mshiko juu ya uhai.

Hapawezi kuwa na wasiwasi kwamba tofauti mbalimbali kubwa, ukatili, mateso na ghasia ambayo yanaweza kuonekana katika historia yote, yanatokana na ikhtilafu ambazo zinaitawala dunia yenyewe na maisha ya mwanadamu.

Tunaamini kwamba Uislamu na itikadi yake, iliyoegemea kwenye tawhiid, ikiwa na, kama ilivyo, mlolongo mpana wa chambuzi za kifalsafa na kisayansi za kina za dunia yenye madhumuni na uhalisia wa nje, na kumfahamisha mwanadamu juu ya mielekeo yote ya uhai wake, una uwezo wa kutatua kimsingi ikhtilafu zote na kutowiana kote na kummuongoza mwanadamu katika mwelekeo wa kitendo cha ubunifu kilichokubalika cha kumhakikishia mustakabali wake.

Kila mfumo wa imani, ingawa kanuni zake zinaweza kuwa zimeenea na misingi yake ikawa ya kudumu, inahitaji kuwasilishwa upya kwa kila kizazi kwa mujibu wa mazingira ya zama hizo. Wenye fikra na walezi wa kiroho, ambao wamezoena na ari ya wakati na wenye kuelewa haja ya utafiti zaidi katika shughuli za msingi ili kukabiliana na mageuzi yanayoletwa na falsafa na sayansi za kisasa, ni lazima kwa hiyo, watoe mazingatio ya uangalifu, makini na yenye upeo mpana juu ya maswali haya, wakichukua vyanzo vya Kiislamu. Ni lazima wawasilishe ukweli, kama mwelekeo mpana na endelevu wa Uislamu unavyotaka kwamba uwasilishwe, na kuizoesha dunia na kanuni za kimantiki za Uislamu.

Kitabu hiki cha sasa ni juhudi za kuwasilisha, kwa njia fupi na hai, uchunguzi wa misingi ya kiimani ya Uislamu, kwa kuchanganya mantiki ya kifalsafa kwa urahisi wa maneno. Kwa vile lengo letu limekuwa ni kuwasilisha kazi fupi kiasi, tumejizuia kutokana na kunukuu maoni ya wanafalsafa na wanasayansi mbalimbali kwa kirefu. Sehemu ya kwanza ya kazi yetu inashughulika na mada za tawhid na uadilifu. Tunategemea kwamba itakuwa ni mchango wa kufanya yajulikane maoni ya Uislamu juu ya maswali haya ya msingi. Sayyid Mujtaba Musavi Lari, Qum, Julai 15, 1981.

1

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

# SOMO LAKWANZA

## USTAWI WA IMANI KATIKA VIPINDI MBALIMBALI

Miongoni mwa mada za msingi za kielimu zinazohusu maisha ya binadamu, masuala ya kidini yanachukua umuhimu wa pekee. Kwa kweli, kila mara zimekuwa zinazingatiwa kama tatizo la msingi kwa ustawi na hatima ya mwanadamu na zimetengeneza utambuzi wa kina sana na ujuzi mkubwa. Wanachuo na watafiti wamefanya uchunguzi mpana sana kuhusu sababu za asili zilizomfanya binadamu ajihusishe na mambo ya Kidini, kufuatilia utafiti wao kwa mtazamo wa pekee na utaratibu ambao hutawala maamuzi na maoni yao.

Ukweli wa jambo hili ni kwamba tangu nyakati za kabla ya historia, itikadi na imani kila mara vimekuwa ndio sehemu ya mtindo wa jamii ya wanadamu; sio zamani au wakati huu ambapo inawezekana kukuta jamii ambayo ndani yake masuala ya kidini hayakulelewa. Qur'ani Tukufu imetaja kwenye Aya kadhaa kuhusu ukweli wa kihistoria kwamba Mitume waliotumwa toka mbinguni siku zote walijitokeza kwenye umma zilizopita ambako, pamoja na athari zao za kiroho zenye manufaa, vile vile walichukua nafasi muhimu katika kubuni ustaarabu wa kibinadamu.

Uchunguzi wa jinsi ambavyo maisha ya mwanadamu yameendelea taratibu na ujuzi kupanuka, pamoja na ujuzi uliotokana na upeo wa mbali sana wa historia, unaonyesha kwamba binadamu aliambatana na imani ya kidini kabla hajawa na utambuzi kamili wa mbinu za maamuzi ya busara. Kipindi cha kwanza cha ujuzi na utendaji wa mwanadamu, kwa hiyo, hakuchukui ubora juu ya vipindi vya mwanzoni kabisa vya dini na imani. Inawezekana hata kudaiwa kwamba jitihada za mwanadamu katika nyanja

za dini na imani zimeonyesha bidii kubwa sana na za kudumu zaidi kuliko juhudi zake katika eneo la ujuzi na sanaa, kwani elimu ya ukweli unaokuvuka mipaka ambao ndio kiini cha cha dunia ya uhai ni mgumu zaidi na inayopatikana kwa taabu kuliko kiini cha vitu vile ambavyo ujuzi na sanaa daima huhangaikia kuvipata. Hali halisi ya msingi ya jua lenye utukufu, ambalo ndio kitu dhahiri kuliko vitu vyote, ilibakia bila kujulikana kwa binadamu kwa karne nyingi na mwenendo na athari zake vilipewa tafsiri za kila aina; ingawa hapana mtu aliyeweza kukanusha kuhusu kung'ara kwa miale yake, akili za watu wengi zilibakia gizani kuhusu kujulikana kwake.

Kwa hiyo, utambuzi wa ukweli mkubwa hauwezekani bila uchunguzi wa kimantiki, maamuzi na kusoma kunakoeleweka. Endapo ushirikina na visa-asili (hekaya) vya kidini vinaweza kupatikana miongoni mwa watu wa kale, na muda wote vikiingizwa kwenye tabia mpya kwa sababu ya upungufu na udhaifu wa kifikira na mipaka finyu ya ujuzi, hii haimaanishi kwamba dini pamoja na kiwango chake cha nadharia, ni udanganyifu. Kwa usahihi zaidi, dini huonyesha ubora na uhuru wa matamanio ya Kidini katika vina vya nafsi na moyo wa mwanadamu. Zaidi ya hayo, kutoka kwenye sayansi ambayo inatafuta kuchunguza nyakati za kabla ya historia, hatuwezi

kutegemea kwamba itagundua zaidi kuhusu dini za kale kuliko masalia ya hekaya na ushirikina unaoweza kufumbulika kwenye mabaki ya mtu wa kale na chini ya ardhi.

Kwa kuwa mwenendo wa binadamu na shughuli zake daima huambatana na sifa mbili zilizo wazi; ubora na uhuru, kwa upande moja, na ufahamikaji na ueneaji pote duniani miongoni mwa jamii ya spishi, kwa upande mwingine - kimantiki, moja kwa moja inaonyesha kwamba tunatakiwa tutoe namna ya chimbuko kwa ajili ya mwenendo na shughuli hiyo kutoka katika kina cha moyo wa mwanadamu. Kuwepo kwa jambo endelevu la aina hiyo kwenye hali ya umilele na kilimwengu, muda wote wa historia na kabla ya historia haliwezi kuchukuliwa kama athari za desturi na mazoea; ni udhihirashaji wa kiu ya dahari na silika ya lazima kwa ajili ya ukweli. Imani zote za kidini na vipengele na aina zao zinazotofautiana zinatoka kwenye chanzo kimoja kinachobubujika na chenye hazina kubwa - ni asili ya dahari ya mwanadamu, ambao haukulazimishwa kutoka nje wala haikuwa ajali.

Kwanza kunakuja kuwepo katika moyo wa binadamu, uwezo wa kukubali imani, na halafu imani yenyewe kuchukua muundo wake. Mwelekeo huo huo wa ndani unaomlazimisha mtu kufanya uchunguzi na utafiti wa kisomi ili aweze kufahamu ukweli ndio dalili ya binadamu kuhitaji elimu ya kidini. Hii, kwa kweli, haina maana kwamba hali ya ndani na maelekezo ni lazima yaambatane na imani sahihi na iliyoundwa kikamilifu. Kama vile ambavyo mwili unavyohitaji viini rutubishi bila ya tamaa hii, haionyeshi uzuri na ukamilifu wa chakula, roho nayo pia hutafuta chakula chake - yaani imani na itikadi - kwa msisitizo ikitafuta utambuzi wa Mola wake na kutamani kuomba kwenye lango lake. Lakini silika ambayo inailazimisha roho kutafuta haiwezi kutambua na kutathmini imani na kanuni za imani, kubainisha ukweli na uwongo.

Wanachuo wanakubaliana kwamba imani za kidini kila mara zimefungamanishwa na maisha ya binadamu. Hata hivyo, maoni yao yanatofautiana kuhusu viini vya misingi vya dini na mambo ambayo yameshika nafasi muhimu katika kuanzishwa na kuendelea kwake. Uamuzi wao katika jambo hili, kwa ujumla umetegemezwa kwenye uchunguzi wa dini za kishirikina na imani za kale, na matokeo yake ni kwamba, maamuzi yao, kwa uchambuzi wa mwisho, yanakuwa na mapungufu na bila mantiki. Ni kweli kwamba dini fulani, zisizofungamana na kanuni za ufunuo wa ki-Mwenyezi Mungu, zimeathiriwa katika muonekano na kukua kwao na mazingira ya kijamii na mambo mengine yanayofanana na hayo. Hata hivyo, haina mantiki kuhusisha misingi yote ya imani na mielekeo ya kidini na mazingira ya kinyenzo au hali ya kiuchumi na mahitaji, kwa hofu ya nguvu zinazoogofya za kiasili, kwa ujinga au kwa fikira zilikataliwa na sayansi.

Bila shaka, moja wapo ya mambo katika kujitokeza kwa mawazo ya kinyume na dini na kundi la watu wanaomkana Mwenyezi Mungu, ni mafundisho ya udanganyifu, upungufu na upotovu wa kiakili wa wafuasi wa baadhi ya dini. Upekee na tofauti za tabia za kila dini, kwa hiyo lazima zichambuliwe moja baada ya nyingine wakati wa kuchunguza sababu ambazo zimemfanya binadamu kuwa mfuasi wa dini hiyo.

Katika matukio mengi ya kihistoria, dini inaweza kuonekana kutawala mahusiano yote. Endapo dini ingekuwa si jambo la msingi, ingekuwa imefungika moja kwa moja kwenye dhamira za kimaada. Hata hivyo, ni jambo gani ambalo lingewapa watu wa dini uimara na ushupavu wa aina hiyo kwa ajili ya kukidhi malengo yao ya kidini? Je, ilikuwa ni kwa sababu ya mategemeo ya manufaa ya utajiri wa kidunia na manufaa mengine ya kibinafsi ambayo yalifanya matatizo machungu yaliyotokana na balaa na shida kuwa na ladha tamu katika nafsi zao? Kinyume chake, tunaona kwamba walitoa utajiri wao wote, maendeleo yao na utashi wa kibinafsi, kwenye hisia na maadili ya kidini, hadi kufika kiasi cha kujitolea nafsi zao kwa mapenzi makubwa.

Kwenye hadithi inayomhusu Firauni na wachawi wake, tunasoma kwamba aliwaita waganga wake wote wa mazingaombwe ili wamshinde Musa (a.s) yule mtu aliyesemeshwa na Mwenyezi Mungu, wakiwa na matumaini kwamba kwa werevu na uwezo wao wa kichawi, wangeweza kumlazimisha kusalimu amri. Lakini shukurani kwa uwezo wa kimiujiza aliopewa Musa, walishindwa na wakarejea kwenye imani ya kweli. Firauni mwenye hasira, ambaye kiburi chake kilivunjwa, akaanza kuwakashifu na kuwatishia, akiwaambia kwamba angewaadhibu kwa mateso mabaya kuzidi yote - yaani kuwakata miguu yao. Lakini, mageuzi ya kina sana yalikwisha kufanyika katika nyoyo zao; walibakia kuwa imara na madhubuti mbele ya vitisho na kurairai kwa Firauni na mateso yake makali. Wachawi hao wakajibu, kwa ushupavu sana;

فَاقْضِ مَا أَنتَ قَاضٍ ۖ إِنَّمَا تَقْضِي هَـٰذِهِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٧٢﴾

"....basi fanya unavyotaka kufanya, unaweza kutoa hukumu inayohusiana na maisha haya ya dunia tu." (Surat-Twaha; 20:72).

Hili lilikuwa ni onyesho la wazi la nguvu ya utashi wa asili wa kutaka kupata ukweli na uhalisi ndani ya binadamu anapokabiliwa na dhuluma uonevu na nguvu za kikatili. Watu ambao waliishi kati kati ya chombo cha Firauni na walikuwa wanafaidika nacho, walinyanyua vichwa vyao na kuasi na walikuwa tayari kujitoa mhanga. Mwelekeo maalum wa mtu kwenye masuala ya kidini, kwa hiyo hauwezi kuelezwa kwa kigezo cha tafsiri ya manufaa ya kidunia; kinyume chake matukio kama lile la wachawi huonyesha ubora wa maana za kidini kwa binadamu.

Imani zisizo na mantiki hazifungamani na masuala ya kidini tu. Kabla hazijasafishwa sawasawa, elimu nyingi zilikuwa zimechanganywa na ushirikina. Watu waliona njia yao kutoka kwenye upandisha mashetani na uchawi kwenda kwenye tiba za kweli na zenye manufaa na kutoka kwenye alkemi za uongo kuja kwenye kemia halisi. Hapana mtu anayeweza kudai kwamba endapo mtu alifanya kosa mara moja wakati wa kutafuta kitu, kwa hiyo, analazimika kubakia kwenye makosa wakati wote na kamwe hatapata njia ya kuufikia ukweli. Wale watu wanaoamini katika falsafa za kisayansi na ubora na mbinu ya majaribio, wanakubali kwamba majaribio yao yanaweza kuleta matokeo yasiyo sahihi ingawa kwa namna moja au nyingine watayapatia hadhi ya ukweli.

Watu wanaomkana Mwenyezi Mungu husisitiza uamuzi wa kwamba Mwenyezi Mungu ni matokeo ya fikira ya mwanadamu. Kwa mfano, mwanafalsafa Mwingereza, Betrand Russell, anauona woga wa nguvu za

asili kutokea kuwa chanzo cha dini. "Kwa maoni yangu, dini zaidi ya yote imetokana na woga wa kisichojulikana, woga wa kifo, woga wa kushindwa, hofu ya mambo ya siri na yaliyofichikana. Kwa nyongeza, kama ambavyo imekwisha kuandikwa, hisia hujitokeza na kumwezesha kila mtu kudhani kwamba anaye msaidizi katika matatizo yake yote na jitihada zake."[1]

Haya ni madai tu, ambayo hayaungwi mkono na ushahidi wowote. Samuel King anasema, "Chanzo cha dini kimegubikwa na usirisiri. Miongoni mwa nadharia zisizo na idadi za wasomi kuhusu somo hili, baadhi huonekana zenye mantiki kuzidi zingine, lakini hata ile bora kuliko zote inakabiliwa na upinzani kutoka katika mta zamo wa uthibitisho wa kisayansi. Haziwezi kuvuka mipaka ya mazingira ya makisio ya kimantiki. Kwa hiyo, kupo kutokukubaiana kukubwa sana miongoni mwa wataalamu wa elimu ya jamii kuhusu chanzo cha dini."[2] Hata hivyo, tunaweza kujibu kwamba hata kama tunakubali chanzo na msingi wa hamasa ya imani ya binadamu juu ya kuwepo muumba imeonekana kuwa ni hofu, hii haithibitishi kwa vyovyote vile kwamba kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ni mzaha mzaha usio na ukweli.

Endapo hofu ilimsukuma binadamu kutafuta kimbilio na kama katika kutafuta huko aligundua ukweli yakini, yaani Mwenyezi Mungu, je, kuna haja ya kufanya upinzani wowote dhidi ya hilo? Kama hofu ni sababu ya ugunduzi wa kitu fulani, hivi tunaweza kusema kwamba kitu hicho ni cha kubuni na si cha kweli kwa sababu woga ndio uliomsukuma binadamu kukitafuta kitu hicho? Kwa hakika haingekuwa na mantiki kushikilia, kwa mfano, kwamba elimu ya tiba haina ukweli kwa sababu binadamu ameitafuta na kuivumbua kwa sababu ya woga yaani hofu ya maradhi na kifo? Ukweli wa jambo hili ni Katika mambo yote na matukio ya maisha, kuamini Mungu Mmoja aliye na hekima ni hifadhi halisi na msaada madhubuti.

Hili ni jambo tofauti kabisa mbali na kama ndivyo au sivyo kwamba msukumo wa binadamu kutafuta kitu hiki ni woga wa mabadiliko ya maisha na kutafuta kimbilio au hapana. Mambo haya mawili yapo mbali mbali kabisa na lazima yachunguzwe kila moja kwa upande wake. Bila shaka katika hatua za zamani za maisha yake, binadamu kwa kweli alikuwa mateka wa hofu ya kufedhehesha na kuumiza alipokabiliwa na matukio ya kimaumbile ya kutisha kama vile mafuriko, matetemeko ya ardhi na maradhi. Jinamizi la hofu lilitupa kivuli chake chenye kisirani katika vipengele vyake vyote vya maisha yake na fikira zake, na katika mapambano yasiyoisha aliyoyaendesha dhidi ya udhaifu na hofu, alitafuta msaada ambapo angeweza kupata hifadhi kutoka kwenye mazingira yake ya kuogofya na kupata amani ya kina. Hatimaye, kwa bidii kali, alilishinda jinamizi la unyonge na hofuna akapata ushindi wa dhahiri.

Uchunguzi wa hatua tofauti tofauti kuhusu maisha ya binadamu wa kale, na ugunduzi wa ushahidi kwamba woga ulikuwepo katika fikira za binadamu, hauthibitishi kwamba woga na ujinga ndio tu mambo ya msingi

1. Russell, Why I am not a Christian, uk. 37.
2. King, Sociology; uk. 99 kwamba elimu ya tiba ni kweli halisi, bila kujali kama msukumo wa asili wa mwanadamu kugundua sayansi ya tiba ilikuwa hofu ya maradhi na kifo au mambo mengine.

yaliyomfanya binadamu aielekee dini. Dai la aina hii litakuwa ni matokeo ya kuona eneo moja tu la jambo hili. Uamuzi wa jumla unaweza tu kufanywa kutokana na utafiti na uchunguzi wa kihistoria ambapo utimilifu wa historia, pamoja na vipindi tofauti vyote katika maisha ya binadamu, umechunguzwa na kufanyiwa utafiti, si pembe moja ya kihistoria yake pana na yenye sura mbalimbali.

Hofu kutawala mambo ya binadamu na unyonge wao katika vipindi maalum na vyenye mipaka si lazima vifanywe kuwa msingi wa uamuzi wa jumla kuhusu vipindi vyote. Haitakuwa ni uamuzi wa haraka mno kusema kwamba fikira zote za kidini na hisia ya mwanadamu, mwelekeo wa kumwabudu Mwenyezi Mungu katika nyakati zote tangu zama za kale pamoja na huu wa sasa, zimesababishwa hivi hivi tu na hou, kwa kuogopa ghadhabu ya maumbile, ya vita na magonjwa? Kwa kweli hasa, wale ambao wameridhika kwa uthabiti hasa miongoni mwa watu kwa hali yoyote ile sio wale wanyonge mno. Wale ambao, jinsi wakati unavyopita, wamenyanyua juu bendera ya dini ni wale wenye nguvu sana na imara katika watu. Imani ya mtu kamwe haiongezeki kwa kuwiana na unyonge wake, na kiongozi wa watu katika mambo ya imani ya kidini si mtu wa mbele sana miongoni mwao katika udhaifu, unyonge na kuishiwa nguvu.

Je, Imani katika dini ya maelfu ya wanachuo na wanafikra ni matokeo ya woga wao juu ya dhoruba, matetemeko ya ardhi na magonjwa? Inawezekana mwelekeo wao kwenye dini, uchunguzi wa kisomi, wa mantiki na uthibitisho madhubuti, kudhaniwa kuwa ni kwa sababu ya ujinga wao na kutokutambua kwao sababu asilia za matikio? Ni lipi litakuwa jibu la mtu mwenye akili?

Zaidi ya hayo mtu kuingia kwenye dini si kwa sababu ya kupata amani ya aina fulani. Badala yake, mtu huanza kufurahia matunda mazuri ya dini - amani na utulivu, baada ya kupata imani na kusadikisha. Kwa maoni ya wanazuoni waliongozwa Ki-Mungu, dunia ni ufupisho kamili wa sababu na hoja zilizopangwa uzuri, mfumo sahihi wa ulimwengu unaoshuhudia kuwepo kwa chanzo kitambulikanacho kwa elimu na uwezo. Michirizi ya upakaji rangi usioeleweka na unaotatiza haiwezi kuchukuliwa kuwa dalili ya msanii stadi, lakini michirizi iliyo sahihi na ubunifu wenye maana huo ndio ushahidi wa hakika wa kuwepo kwa fundi rangi mwenye ujuzi.

Pia wapo watu wanaoiangalia imani katika ukweli ulioko nje ya mipaka ya asili kuwa kama matokeo ya mambo ya uchumi. Hufanya juhudi kubwa kuanzisha uhusiano fulani baina ya dini na uchumi. Wanadai kwamba wakati wote dini imekuwa katika huduma ya ubeberu na unyonyaji na kwamba ilikuwa uvumbuzi wa tabaka utawala na unyonyaji kama njia ya kuvunja upinzani wa umma unaonyonywa. Wanadai kwamba, dini imekuwa ikitumiwa kuwapumbaza wavuja jasho wasiojiweza na kuwahimiza waendelee kuridhia kutojiweza kwao. Hapana shaka kwamba, kama kwa kitu kingine chochote kile hapa duniani, dini inaweza kutumiwa vibaya. Inapobadilishwa kutoka kwenye malengo yake ya kweli, inakuwa ni silaha mikononi mwa wenye kufaidika ambao wanataka kuyaweka mataifa utumwani. Hata hivyo, huku kutumika vibaya kwa dini kusiwape wabinafsi kisingizio cha kushambulia kidhalimu kila kitu chenye jina la dini. Lazima pawepo na utenganisho uliowazi baina ya dini potovu zilizobuniwa na

ubeberu kwa lengo la kuwapumbaza watu, na zile halisi za kweli na zenye kujenga.

Inawezekana kwamba katika jamii nyingi za binadamu, hali mbaya ya kiuchumi, kuvia na kukosa maendeleo vinaweza kuwepo sambamba na imani ya kidini. Lakini, kuwepo pamoja huku hakuwezi kulazimisha kuwepo uhusiano wa kawaida; mmoja hauwezi kuwasilishwa kama sababu ya mwingine. Wakati fulani tunaona jamii inafaidi maendeleo na ustawi kiuchumi ambao umeambatana kwa kina sana na dini, ambapo jamii nyingine ambayo inafaidi vivyo hivyo hali nzuri ya kiuchumi iko kinyume kabisa na dini. Vivyo hivyo, kwenye mazingira ya umasikini na kukosa maendeleo, nuru ya dini inaweza kutoweka ambapo kwenye mazingira mengine kama hayo, mvuto wa dini unaweza kuwa kwenye kilele chake. Kutokuwepo kwa ulingano wa wazi baina ya hali ya uchumi na kuwepo au kuanguka kwa mvuto wa kidini na uthibitisho uliowazi wa ukweli kwamba kutokea kwa wakati mmoja (kwa mambo mawili) hakutoshi kuanzisha uhusiano wa kawaida. Jambo fulani maalum lazima liwepo kusababisha kutokeza au kutoweka kwa mojawapo kuunganishwa na kuwepo au kutokuwepo kwa jingine.

Tunaweza kuona wazi kabisa huku kutokuwepo kwa ulingano katika jamii mbili ambazo zote zipo kwenye utawala dhalimu wa tabaka la wanyonyaji. Katika mojawapo ya hizo jamii mbili, dini imeondoka kabisa kwenye mazingira yake, ambapo kwenye jamii nyingine mvuto wake umepanuka. Uhalisi wa lengo unatuonyesha kwa hiyo kwamba, mtu anavutwa kwenye dini na mazingira mbalimbali ya nje. Popote pale ambapo dini inaonyesha mvuto wake, mtu lazima atafute dhamira ya msingi ya ndani kabisa katika hali asili hususia ya dini, sio katika mazingira ya uchumi. Kwa nyongeza, tunapoyachunguza yale malengo ya dini za ki-Mungu, tunafikia uamuzi kwamba mahitaji ya kuwepo kwa ustawi na kuanzishwa kwa mfumo wa uchumi wa haki ambao unaegemezwa kwenye dini yamekuwa mojawapo ya sababu za kutumwa Mitume. Hii, pia ni sababu mojawapo ambayo imewafanya watu wamevutiwa kwenye dini na ni moja wapo ya manufaa ambayo jamii ya binaadamu imepata kutoka humo.

2

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA PILI

### UNDANI WA NAFSI YA MWANADAMU HUMLAZIMISHA KUMTAFUTA MWENYEZI MUNGU

Nje ya mfumo wa hisia za mwili wake, mwanadamu anayo maeneo makubwa mno na muhimu ambayo kwa hali yoyote ile hayakufungiwa katika utaratibu wa mwili wake. Ili kuweza kugundua vipengele hivyo na hatua zilizo nje ya muundo wa mwili na ukubwa wa kiwiliwili chake, mtu lazima atafute muundo wa ndani na wa kiroho wa binadamu na kufahamu ule upeo mpana wa asili yake yenye mambo mengi, pamoja na udhihiri nyeti na wa kiungwana wa hisia na silika zake.

Mlolongo wa namna maalumu za ufahamu zinakuwemo katika nafsi ya binadamu ambazo zimejiotea mizizi ndani yake zenyewe, zinachomoza kutoka kwenye namna hasa ya hulka ya mwanadamu, na na kuchomoza kwao hakupasiki na jambo lolote la nje ya mwili wake. Miongoni mwa tambuzi hizi ni hisia za kuwajibika kwenye amana, haki, kuwa mkweli na mwaminifu. Kabla hajaingia kwenye uwanja wa sayansi na ujuzi na vyote vinavyohusika navyo, mtu ana uwezo wa kutambua ukweli fulani kwa njia ya utambuzi huu wa asili. Lakini baada ya kuingia kwenye eneo la sayansi na falsafa na kuujaza ubongo wake na shuhuda mbali mbali na tasfiri ya mambo, anaweza akasahau tambuzi zake za kawaida na za asili au akaanza kuzitilia mashaka. Ni kwa sababu hii kwamba binadamu anapokwenda kinyume na tabia yake ya asili kufafanua imani kwa maneno, tofauti huanza kujitokeza.

Kuelekea kwenye dini na kumuamini Mwenyezi Mungu, katika hatua zake za mwanzo huvutia kwenye sababu za kisilika na tambuzi za asili, lakini halafu huendelea kukua na kugeuka kwa msaada wa mantiki na tafakari. Mizizi ya hisia asili katika silika za mwanadamu imekwenda ndani mno na wakati huo huo, huonekana wazi na dhahiri sana hivyo kwamba endapo mtu anatakasa akili yake na roho yake kuhusu fikira za kidini na zisizo za kidini na halafu akajiangalia mwenyewe na dunia ya viumbe, kwa wazi kabisa ataona kwamba anasonga kuelekea upande fulani akiwa na msafara mzima wa viumbe. Bila ya utashi wowote au hiari upande wake, huanza maisha yake mahali fulani, na halafu tena bila hiari yake husonga mbele kwenda mahali pengine ambapo hapajui. Na ukweli huu huu unaweza kuonekana juu ya viumbe vyote vya asili, vikijiendesha kwa namna ya usahihi na kwa mpango.

Endapo mtu anayeona vizuri, akiwa bado yu katika hali ya kimaumbile, atayaangalia mazingira yanayomzunguka, kwa wazi kabisa atahisi kuwepo kwa nguvu kuu ambayo inamzunguka yeye na dunia yote. Katika umbile lake mwenyewe, ambalo ni sehemu ndogo sana ya dunia kubwa, ataona ujuzi, nguvu na utashi wa kuishi, na atajiuliza ni vipi ujuzi, nguvu na utashi havingeweza kuwepo katika dunia kwa jumla. Ni huu mpango uliofanyiwa mahesabu kwa ustadi mkubwa na mwendo wa dunia ambao humlazimisha mwanadamu kukubali kuwepo kwa uwezo wa akili ya fani zote ambayo,

ikiwa ipo nje ya dunia ya kimaumbile, lakini hata hivyo inaisanifu na kuiamuru, isipokuwa kwa kukubalika hili, mpangilio huu wa dunia hauwezi kuelezeka. Mtu yeyote anaye tathmini nafasi yake hapa duniani anaweza kutambua kwamba kuna nguvu inayomuumba yeye, ikamleta yeye hapa, inayomtia usongefu ndani mwake, na halafu tena humwondoa, bila ya ruhusa au msaada wake kutakiwa kwa ajili ya lolote katika haya.

Kiongozi mkuu wa mashahidi, Hussein bin Ali (a.s) alisema katika dua yake ya siri kwa Muumba wake; "Inawezekanaje kufasiri kuweko Kwako kutoka kwenye kitu ambacho kinakutegemea Wewe kwa kuwepo kwake? Kwa nini huna hali ya kudhihirika kama wengine wasio wewe waliyonayo, ili kwamba iweze kukufanya Wewe uwepo dhahiri? Ni lini ulifichika kamwe kutoka kwenye jicho la ndani ili labda uweze kuhitaji uthibitisho uwe kama mwongozo wa kuelekea kwako Wewe? Ni lini ambapo ulikuwa kamwe mbali na sisi hivyo kwamba ishara na dalili Zako labda zingeweza kutusogeza karibu na Wewe? Limepofuka jicho ambalo halikuoni Wewe unapolitazama kulilinda na kuliongoza!

"Ee Mwenyezi Mungu, Wewe ambaye umejidhihirisha Mwenyewe kwa ufahari wako, unawezaje kuwa umefichika ambapo unaonekana na kudhihirika? Unawezaje kuwa haupo ambapo kwa kuonekana kwako kusiko na ukomo unawaangalia waja Wako?"[1] Hapana mahali popote na wakati wowote ambapo kitu kimetengenezwa bila mtengenezaji wake kuonekana, wala tendo bila mtendaji. Utafutaji wa kiungo baina ya chanzo na athari hujitokeza kutokea kwenye silika ya ndani ya mwanadamu; utambuzi wa uhusiano hauwezi kuondolewa kutoka kwa mtu yeyote.

Vivyo hivyo, hisia za kidini, kumtafuta Muumba, pia haiwezekani kuondolewa kutoka kwa mtu yeyote. Hata mtoto ambaye hana uzoefu wa dunia, wakati wowote asikiapo sauti au aonapo msongo, ki-silika atageuzia nadhari yake kwenye chanzo cha sauti au msongo. Misingi yote ya maisha halisi na ujuzi inasimama kwenye kukubali sababu kwa kila athari. Kanuni ya uhusiano, kwa kweli ni dhahiri kabisa ambayo haitoi mwanya wowote. Jiolojia, fizikia, Kemia, elimujamii, uchumi - katika hizi na elimu zingine, utafiti una lengo la kubainisha sababu na mambo yanayoamua uhusiano. Kwa ufupi, ni dhahiri kwamba elimu na ujuzi si lolote zaidi ya utafutaji wa vyanzo; maendeleo na kusonga mbele katika mambo ya binadamu hutokana na uchunguzi unaofanywa na wasomi kuhusu vyanzo vya mambo.

Kama ingekuwa inawezekana sisi kugundua kutoka kwenye kiumbe kimoja au pembe moja ya ulimwengu alama ya kujianzisha au kujiumba chenyewe kikamilifu, tungeridhika katika kueneza mfano huo moja kwa mpangilio wote wa viumbe. Kama mambo yalivyo, si muhimu kwamba kanuni ya usababisho kila mara ijioneshe kwetu katika miundo inayojulikana. Aina mbalimbali na wingi wa vyanzo viko kiasi kwamba mtafiti anayejihusisha na jambo moja tu labda atashindwa kupambanua visababisho vyote. Hata hivyo, katika mambo yote ya mwanadamu, maalum na ya kawaida, yaliyopita na yajayo, katika mazingira ya mtu mmoja au ya jamii, hakuna nukta hata moja inyoweza kuonekana kuwa ya bahati mbaya.

---

1. Du'aul-Arafa ndani ya Mafatih al-Janan, uk. 265.

Si tu kwamba upo mpangilio mahususi ambao ni wa asili katika kuumbwa kwa kila kitu peke yake; pia kunakuwepo na ya kuonekana katika uhusiano wa kila jambo na jambo jingine, vile vile na uhusiano wa kila kitu na mazingira ambamo kinakuwemo, utaratibu stadi uliokokotolewa vizuri sana. Mathalani, katika kuukuza mti, kanuni za anga na ardhi zinafanya kazi katika uelewano kamili na muundo wa mizizi na matawi yake. Pia upo uhusiano wa wanyama na mti ule kwa vile wanapata chakula kutoka humo. Inawezekanaje kwamba pawepo na bahati mbaya katika asili ya utaratibu wa uhusiano wa aina hiyo?

Endapo jambo lingepata umbo katika ngazi fulani katika muundo wa kiumbe, bila kufahamu na katika misingi ya kubahatisha, hali hii ingetoa maandalizi mazuri sana kwa ajili ya kutoweka na kuangamia kwa dunia. Kwa sababu hitilafu ndogo sana katika usawa wa vitu asili na dosari ndogo sana katika kanuni angavu za ulimwengu ingetosha kusababisha vitu kukosa amari zao na viumbe vya angani kugongana, na kutokea kwa mlipuko mkubwa na kuangamia kwa dunia. Kama asili ya dunia ingeegemea kwenye kuweko bahati mbaya, kwa nini nadharia hata za wapenda anasa za dunia zimetegemewa kwenye kufikiria kupanga, mpangilio uliopangwa, kukosekana hali ya bahati mbaya? Kama dunia yote ni matokeo ya kubahatisha na bahati mbaya, ni kitu gani kile ambacho hakikutokea kwa msingi wa kubahatisha? Endapo kitu kilichopo sasa kilikuja kuwepo kama kiumbe si kwa sababu ya kubahatisha, ni sehemu gani muhimu na sifa zake zake ambazo zinazokibainisha na je zinaweza kutumika katika vitu vingi na vya namna nyingi mbali mbali vya ulimwengu?

Sasa kwa kuwa kubahatisha kunapingana na mpangilio na upatanifu, inaonekana kwamba kitu chochote kinachokuwa na mabaki ya upangaji, ubunifu na ukokotozi kitakuwa hakitangamani vizuri na hakiendelei, kwa sababu dhana za upangaji, usanii na mpangilio mzuri zimepingana na kubahatisha na hali ya uwezekano. Kudhani kwamba mfumo wa kubahatisha ndio muundombinu kwa ajili ya ulimwengu na kanuni yake inayotawala haitegemei uthibitisho wowote wa kimantiki au ushahidi wa kisayansi haiwezi kukubaliwa kuwa ni ufumbuzi wa uhakika kwenye jiometri ya muundo wa maumbile.

Wakati ambapo sayansi za majaribio zinaonyesha kwamba elementi na vipengele vya asili haviwezi kutoa mvuto wowote wa kujitegemea na havina uumbaji; ambapo uzoefu wetu wote, hisia zetu za fahamu na mafuhum zetu za kimantiki yanaelekeza kwenye maamuzi kwamba katika maumbile hakuna kinachotokea bila ya sababu na chanzo na kwamba vitu vyote vimetengenezwa kwenye mfumo madhubuti na kanuni maalum - ikiwa yote haya ndio hali halisi yenyewe, inashangaza kuona watu wengine wanageuzia migongo yao kwenye kanuni za kisayansi, mafuhum muhimu na mapendekezo yaliyo egemezwa kwenye tafakuri, na kukataa kuwepo kwa Muumba.

Elimu na vipengele vya kimazingira ni miongoni mwa sababu ambazo ama huzuia fahamu za asili za binadamu zisijioneshe, au kinyume chake, kuziimarisha. Kila chenye kujionyesha chenyewe kutoka kwenye chanzo cha silika hufanana katika mpangilio wake na mlolongo wa asili. Wale ambao wameachwa huru na kufuata mwelekeo wa asili wa maumbile yao

bila ya kufungwa na mazoea na ambao tabia yao ya kina zaidi haikupambwa na maneno na muonekano, wanaweza kusikiliza vizuri zaidi wito wa nafsi zao za ndani zaidi na kuweza kupambanua baina ya matendo mema na mabaya, imani za kweli na za uongo. Kutokuwa na maadili ya dini, hali ambayo kwa kweli ni kuipa kisogo asili ya maumbile, kwa hiyo, ni nadra sana kuonekana miongoni mwa watu kama hao.

Endapo mtu anawaambia kwamba dunia haina mpangilio wenye kukaa ndani na kwamba inatokana na hali ya kutukia (isiyo ya uhakika), akiyapamba maneno yake kwa istilahi za kifalsafa, hatakuwa na athiri juu ya watu kama hao, kwa sababu watazikataa nadharia zake kwa ajili ya asili yao ya kimaumbile. Watu ambao wamenasa katika mitandao ya sayansi wanaweza kuwa mateka wa shaka na utatanishi kama matokeo ya istilahi zenye ushawishi. Elimu finyu ambayo hutia msukumo wa kiburi kwa binadamu ni kama mfano wa kipande cha kioo kilichopakwa rangi ka kuwekwa mbele ya kiupenyo cha akili na maumbile ya asili; yeyote mwenye akili hii huona dunia imetiwa rangi kidogo na ujuzi wake na elimu yake. Hudhania kwamba ukamilifu wa ukweli ni ule anaouona kupitia kwenye kipenyo chembamba cha fahamu zake na akili ambavyo ni nyara rahisi ya rangi. Kama hali ilivyo, hatuna maana kwamba binadamu aache kuendeleza akili yake ili ajiepushe na upotovu. Hata hivyo, asije akawekewa mipaka na ujuzi wake na elimu yake au asijigambe kwa hiyo elimu na ujuzi wake wenye kikomo.

Watu walio wengi, badala ya kufanya maarifa na ujuzi wao kuwa ngazi ya kunyanyua uwezo wa akili zao ili waweze kufikia kiwango cha juu zaidi, wanabaki wametulia na kufungiwa kwenye uzio wa kuta nne za dhana na masharti. Hali ya asili ya mwanadamu, pindi anapohisi hatari, haraka hukimbilia kwenye msaada wake. Mtu anapobanwa na shida na matatizo makubwa sana, wakati mambo ya kilimwengu yanapompa kisogo, anapokuwa hana njia yoyote ya kuzifikia rasilimali za kimaisha na anazama kama bua kwenye machafuko ya mabadiliko na kifo kipo karibu sana naye - ndipo dhamira ya kutoka moyoni humwongoza kisilika na kumwelekeza kwenye chanzo cha msaada kisichokuwa cha kilimwengu. Hutafuta msaada kutoka kwa yule ambaye uwezo wake upo juu ya uwezo wowote ule, na huelewa kwamba ni yule Muumba mwenye huruma na mwenye nguvu zote ambaye anaweza kumsaidia kwa kutumia uwezo wake usio wa kawaida na kumwokoa.

Kwa sababu ya utambuzi wake, kwa nguvu zake zote binadamu hutafuta msaada wa yule aliye mtakatifu sana ili amwondoshe kwenye hatari na kwenye faragha ya moyo wake, anahisi uwezo na nguvu ya muweza huyo zikifanya kazi kwqa ajili ya mwokovu wake. Mtu mmoja wakati fulani alimuomba Imamu Sadiq (a.s) amwongoze kuelekea kwa Mola wake Mlezi, akasema kwamba maneno ya wapinzani yalimtatanisha. Imamu akamuuliza, "Umewahi kusafiri kwa meli? Akajibu, "Ndio."

Imamu: "Je, imewahi kutokea kwamba meli ikaingiza maji na hapakuwepo na mtu wa kuwaokoeni ili msizame kwenye mawimbi ya tufani ya bahari?"

Jibu: "Ndio." Imamu: "Wakati huo wa hatari na katika hali hiyo ya kukatisha tamaa, je, ulikuwa na hisia kwamba nguvu isiyopimika na yenye uwezo mkubwa ingeweza kuwakuokoeni kwenye balaa lenu la kutisha?"

Jibu: "Ndio, hivyo ndivyo ilivyokuwa."

Imamu: **"Ni Mwenyezi Mungu Mwenye uwezo ambaye ndio chanzo cha mategemeo na kwake Yeye watu ndiko wanakotazamia kwa matumaini pale ambapo milango yote inapokuwa imefungwa."**[1] Hata watu waasi na wapenda dunia wenye uwezo ambao hawautambui uwezo usio na kikomo wa Mwenyezi Mungu, wanapofurahia utawala wao, hubadilika wanaponasa kwenye mtego wa kushindwa na kuangamia. Husahau kumkana kwao Mwenyezi Mungu ambako madhehebu yao ya mazingira na ya kianasa za dunia ulivyojipandikiza ndani yao na kwa moyo mkunjufu kabisa hugeukia kwenye asili ya viumbe vyote na chanzo cha nguvu zote.

Historia imeorodhesha mifano mingi sana ya watu kama hao ambao walipata kuwa waathirika wa matatizo na hali za mitihani hivyo kwamba vumbi la upotofu liliondolewa ghafla kutoka kwenye tabia zao za asili na kutoka kwenye vina vya nafsi zao na wakarejea kwa Muumba asiye na kifani. Kwa kuongezea kwenye rasilimali za ndani ambazo ni za asili katika nafsi ya binadamu na humsaidia yeye kugundua ukweli hivyo kwamba, akiwa huru kutokana na dhana na vikwazo vya kiakili husonga mbele akifuata njia ya tabia yake ya asili, na kiwango cha nje cha mwongozo na maonyo pia ni muhimu kwa ajili ya kumwelekeza njia na kuimarisha hali yake ya asili. Ni mwongozo ndio unaorekebisha sifa za ki-uasi na kuilinda akili na tabia ya asili kutoka kwenye upotovu na utiifu kwa miungu wa uwongo. Mitume walipelekwa kwa madhumuni ya kuwafanya watu wajihadhari na utambuzi wenye utatanishi, wa tabia zao za asili, ili kuufanya mwelekeo wao wa ki-Mungu ufuate mkondo unaostahili, na kuyanyanyua matarajio yao makubwa.

Amirul-Mu'minina [(a.s)] amesema: **"Mwenyezi Mungu aliwatuma Wajumbe Wake miongoni mwa watu ili waweze kuwahoji kuhusu ahadi yao na Mwenyezi Mungu, kuwakumbusha watu kuhusu neema za Mwenyezi Mungu zlizosahaulika, kuzungumza nao kwa namna ya kuwaonya, kuzindua hekima iliyojificha ndani mwao, na kuwaonesha ishara za uwezo wa Mwenyezi Mungu."**[2]

Mwongozo na nasaha za aina hiyo kwa jinsi yoyote ile haimaanishi kuzimwa kwa nuru ya dhamira endelevu ya mwanadamu kumnyima uhuru na uwezo wake wa kufikiri na kuchagua. Hii, kinyume chake, ni aina ya msaada kwenye mielekeo na silika bayana, kuziwezesha kukua na kuendelea. Ni kupitia mwongozo na nasaha ambapo wanadamu wanaondolewa kwenye vifungo na kuwezeshwa kunufaika kutokana na mpanuko wote wa maumbile yao ya asili na kusitawi pamoja na viumbile wenzao wote. Qur'anii inasema:

---

1. Biharul-Anwaar, Juz. III, uk. 41.
2. Nahajul-Balaghah, kilichohaririwa na Subhi Salih, uk. 43.

وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ ۚ فَالَّذِينَ آمَنُوا بِهِ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَاتَّبَعُوا النُّورَ الَّذِي أُنزِلَ مَعَهُ ۙ أُولَـٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٥٧﴾

". . . Anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao. Basi wale waliomuamini yeye, na wakamtukuza, wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye, hao ndio wenye kufaulu."[1]

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّـهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ ﴿٢٤﴾

"Enyi mlioamini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapokuiteni kwa yale yatakayokupeni uzima."[2]

يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَتْكُم مَّوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِّمَا فِي الصُّدُورِ ... ﴿٥٧﴾

"Enyi watu! Yamekufikieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi, pozo la yale yaliyomo vifuani, . . .[3]

Watu wa kwanza waliokubali wito wa Mitume walikuwa watu wenye mioyo safi na dhamira zilizoongoka. Safu za washindani wao zilikuwa na wale waliotegemea juu ya mamlaka bandia na utajiri au walijawa na kiburi kwa sababu ya ujuzi wao mdogo na wenye mapungufu, akili zilizochafuliwa na udanganyifu, kwa namna ambayo kwamba jeuri yao isiyo na msingi, ilizuia uwezo wa kina na matamanio yao kustawi.

Mwanazuoni fulani amesema hivi: "Katika mambo ya kiroho, pia kanuni ya usambazaji na kuhitaji huwepo. Kama haja ya dini isingekuepo katika tabia ya asili ya binadamu, mahitaji yaliyotolewa na Mitume yangepotea bure. Tunaona kwamba ugawaji wa Mitume ulipata wateja; mawazo yao yenye mipango mingi, yasiyo na shaka na sahihi kabisa yalipata wafuasi na waunga mkono wengi. Huu ni uthibitisho kwamba haja ya dini inakuwepo ndani ya mwanadamu na dhamiri yake ya kina kabisa."[4]

Kwa kweli, mafundisho ya msingi ya Mitume wote yalikuwa wito wa kumwamini Mwenyezi Mungu mmoja, sio ya kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Walibatilisha thamani ya masanamu, jua, mwezi na nyota kuabudiwa, ili kwamba kiu ya ya mwanadamu ya kina na ya kimaumbile kwa ajili ya ibada isitoshelezwe na kuvikimbilia vitu vya maumbo ya nje kama hivi na wanaweza, badala yake, kutafuta malengo na maadili yao kwenye safina imara na kupanda kwenye madhumuni halisi ya ibada. Mioyo yao inapaswa ifungamane na ulinzi usio na kikomo, na kwa imani ambayo daima inapanda, wao wanapaswa wakati wote kusonga mbele kuelekea kwenye chanzo cha maadili yote na wema, hatimaye kufikia kwenye malengo yao.

Aina zote za kuabudu miungu wengi za ukana dini - mfumo wa kale ambao ni kuabudu masanamu namuundo ulioendelea, wa kisasa, ambao

---

1. Al-A'araf;7:157.
2. Anfal; 8:24.
3. Yunus; 10: 57.
4. Kuna maelekezo ya wazi kwenye jambo hili katika maneno yafuatayo ya Imam as-Sajjad (a.s.): "Umetakasika na kutukuka, Ewe Mola Wangu, Ambaye unaujua uzito wa mbingu zote! Umetakasika na kutukuka ewe Mola Wangu, unayejua uzito wa ardhi yote! Umetakasika na kutukuka ewe Mola Wangu, unayeujua uzito wa giza na mwanga! Umetakasika na kutukuka ewe Mola Wangu, unayeujua uzito wa kivuli na hewa!" (Sahifa-yi Saniya, Du'a ya 55.).

tamaa ya anasa - ni matokeo ya kukengeuka asili ya maumbile. Maendeleo ya elimu kuhusu uzoefu wa kidini ambayo yanatokea pote duniani yamesababisha ugunduzi mwingi ambao unaruhusu maamuzi muhimu ya uhakika yaweze kufikiwa.

Ikiegemezwa kwenye takwimu nyingi kiasi zilizokusanywa na wataalamu wa sosholojia, wanaakiologia (wachambuzi wa elimu ya kale), wana anthropogia (elimu ya asili ya binadamu), historia ya dini sasa ina changanua silika ya kidini, pamoja na uanzishwaji, imani, desturi na vipengele ambavyo vinaijenga jamii, kwa namna mpya ambayo inatofautiana sana na maelezo yaliyotolewa kabla ya hapo. Sasa hivi kuna wimbi la fikra ambalo kwa muda wote linaendelea kuwavutia wafuasi wapya kutoka kwenye madhehebu mbali mbali wanaosema kwamba hisia za kidini ni kijenzi cha msingi, cha asili na madhubuti cha roho ya binadamu na kwamba ni njia ya asili ya kutambua yaliyo ghaibu. Mnamo kama mwaka wa 1920, mwanafalsafa wa Kijerumani aitwaye Rudolf Otto aliweza kudhibitisha kwamba sambamba na dalili za kiakili na maadili ndani ya mwanadamu, pia zipo dalili za kimantiki ya hali ya juu sana ambazo hujenga hisia za kidini. Sifa zinazomhusu Mwenyezi Mungu kama vile uwezo, ukuu na zenye kuvuka mipaka zina madhumuni ya kusisitiza kwamba utakatifu hauwezi kurahisisishwa kuwa dhana nyingine. Hii ni namna inayojitegemea ambayo haiwezi kupatikana kutokana na namna nyingine na haiwezi kuhusishwa na dhana nyingine yoyote, kimantiki au vinginevyo.

Mojawapo ya upekee wa zama hizi kwa kweli, ni utafutaji wa kipimo cha nne katika dunia ya asili kiitwacho "Wakati". Kama vilivyo vipimo vingine, ni lazima kiingiliane na miili, na kwa hiyo hakuna mwili uliopo katika duniani ambacho kimeepukana na wakati ambao unatokana na msongo na mabadiliko. Vivyo hivyo ni sifa ya zama hizi kwamba tafiti za wanachuo zimeongozea kwenye ugunduzi wa 'kipimo cha nne' cha nafsi ya mwanadamu - hisia za kidini[1].

Vipimo vingine vitatu au hisia vinakuwa na hisia ya dadisi, hisia ya maadili na hisia ya ubora. Hisia ya kidini au dhana ya utakatifu, ni kipimo cha nne na cha msingi zaidi cha hisia. Kihulka kila mtu anao mvuto na mwelekeo kwa kile kilichoko nje ya maumbile, tofauti na huru kutokana na zile hisia zingine tatu. Kwa kugunduliwa kwa hisia ya kidini, jela ya nafsi yake, yenye nyuso tatu, iliporomoka na ikathibitika kwamba mielekeo ya kidini ya mwanadamu imeota mizizi kwa kujitawala kabisa ndani ya utu wake. Ilijitokeza yenyewe hata nyakati zile ambazo watu walikuwa wanaishi ndani ya misitu na mapangoni.

Licha ya ubora wake, kujitawala na kufaa kwa hisia za udadisi, maadili, ubora na nafasi zilizoichukua katika kutokeza kwa elimu, maadili na ujuzi, ilikuwa ni hisia ya kidini iliyoandaa mazingira kwa ajili ya utendaji wa hisia hizi tatu, ikizisaidia kusonga mbele katika njia yao na kugundua siri za ulimwengu ulioumbwa. Kwa mtazamo wa muumini, dunia imesanifiwa katika msingi wa kanuni na mpango sahihi uliokusudiwa vizuri. Imani hii kwa Mwenyezi Mungu mwenye kuamuru na mwenye hekima huzindua

1. Hiss-i-Dini, kilichotafsiriwa na Mhandisi Bayani.

hisia ya udadisi kwa lengo la kutafuta na kugundua kanuni na siri za maumbile ambazo zimeegemea kwenye mlolongo wa sababu namotokeo yake. Mchango wa hisia ya kidini katika kukuza na kuendeleza tabia tukufu kabisa za binadamu, katika kurekebisha hisia zake na kurutubisha silika zake za maadili na wema, haupingiki. Wale wanaofuata maamrisho ya dini wanauona kama mmoja wa wajibu wao muhimu sana wa kidini, kudhibiti silika zao na kupata sifa nzuri za hali ya juu. Fikra ya kidini pia imekuwa kipengele chenye kulea hisia za kisanaa. Watu wa kale walitengeneza kazi zao za kisanaa endelevu sana ili kuwatukuza miungu wao. Mahekalu ya ajabu ya China, mapiramidi makubwa ya Misri, masanamu ya aina ya kipekee ya Mexico, usanifu majengo ulioboreshwa na wakustaajabisha ya Mashariki ya Kiislamu -yote haya yalitegemea sana kwenye hisia ya kidini.

Wanasaikolojia wanaamini kwamba upo uhusiano baina ya hali ya balehe na kujitokeza kwa ghafla kwa hisia za kidini. Katika kipindi hiki cha maisha, hata kwa watu ambao siku za nyuma hawakujali mambo ya dini, hisia ya kidini inachukua mkazo maalum. Hapana shaka kwamba, wito wa ndani hujionyesha kwa jinsi ambayo kwamba hakuna kizuizi kinachoweza kuzuia njia yao. Hata hivyo vipengele fulani kama vile propaganda za upinzani vinaweza kupunguza hisia za ndani kwa ndani na fikra sahihi, ingawa vishawishi kama hivyo haviwezi kuishia kwenye ung'oaji kabisa wa uwelekeo huo. Endapo vikwazo kama hivyo vitaondolewa, hisia zilizo imara huanza tena utendaji wao na kujionesha kwa namna ya jitihada zao endelevu za ndani kwa ndani.

Tunafahamu kwamba zaidi ya nusu karne imepita tangu mapinduzi ya kikomunisti ya Jumuiya ya Kisovieti, lakini mizizi ya dini ipo hai kwenye vina virefu vya nafsi za watu wa Sovieti. Licha ya juhudi zote ambazo zimefanywa katika kipindi hiki kirefu na watawala za kuifuta dini, wameshindwa kuondoa hisia ya kidini kutoka kwa watu.

Kuwapo kwa fikra za maslahi ya kidunia, kwa hiyo, hakupingani na ukweli kwamba kumwamini Mwenyezi Mungu ni jambo la kawaida kwa mwanadamu. Endapo madhehebu fulani itaondoka kwenye mkondo wa maumbile ya asili na hapo ikajifanya ya kipekee kusuiana na madhehebu zingine, kwa dunia ya sasa na katika nyakati zilizopita, hali hii haiwezi kufikiriwa kama ni kukanusha ile hoja kwamba kumwamini Mwenyezi Mungu ni kawaida kwa binadamu; tofauti inakuwepo katika nyanja zote. Kile ambacho historia inakionesha na kwamba madhehebu ya tamaa za kidunia ilianzishwa mnamo karne ya sita na saba kabla ya Yesu Isa (a.s).

3

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA TATU

### MWENYEZI MUNGU NA MANTIKI YA JARIBIO (JARABA)

Bila shaka, hali ya kijamii, mambo ya kihistoria na kielimu, na aina mbali mbali za kazi za binadamu ni mambo ambayo haviwezi kuwa bila mvuto juu ya uonyeshaji kwa vitendo wa mwelekeo wa ndani wa mtu na tabia zake za kiroho na kihisia. Ingawa hali hizi mbali mbali hazisababishi ulazima wowote au umuhimu katika uchaguzi wa mwelekeo wa mtu, zinaweza kusababisha kuwepo kwa mazingira yanayofaa zaidi kwa ajili ya uchaguzi wa aina fulani, kwa hiyo kutoa mchango muhimu kuhusu jinsi binadamu anavyoviona vitu. Hali hizi wakati mwingine zinaweza hata kujionesha katika umbo la kikwazo kwenye uhuru wa mtu na uwezo wa kuchagua. Kama matokeo ya uzoefu zaidi wa maamuzi ya kisayansi na ya kimajaribio, akili ya binadamu kwa kawaida huelekea kuonea haya kwa kiasi fulani maamuzi halisi ya kiakili kabisa, hususan kama jambo linalofanyiwa uchunguzi sio yakinifu na halina maana.

Kwa ujumla, uwezo wa kiakili za mtu hupata nguvu na ustadi kwenye eneo ambamo zinatumiwa sana. Mambo yaliyoko nje ya eneo hilo, kwake (binadamu) huonekana kuwa si ya kweli au si halisi au vizuri zaidi ni jambo la hatua ya pili au linalohusika kidogo sana na jambo analolishughulikia maalum hasa. Kwa hiyo, mwanadamu huelekea kuhukumu kila kitu kwa namna ya kipekee. Mojawapo ya vipengele viharibifu na vinavyo potosha sana katika fikra zihusuzo Mwenyezi Mungu ni kuziwekea mipaka fikra ndani ya mantiki ya elimu za kimajaribio na kushindwa kutambua viwango na mipaka ya mantiki hiyo. Kwa kuwa wataalamu wa sayansi za majaribio kutumia nguvu zao zote za kiakili kwenye elimu za kihisia, wanakuwa wageni kwa mambo yaliyoko nje ya utambuzi wa hisia.

Ugeni huu, umbali huu kutoka kwenye mambo yasiyohusiana na hisia, imani hii isiyo ya kawaida juu ya data zinazotokana na sayansi za majaribio, hufikia kiwango kiasi kwamba kupima na kufanya majaribio huunda muundo wote wa akili na mtazamo wa dunia wa wataalamu kama hao. Wanaona majaribio kama ndio nyenzo pekee inayokubalika na njia ya utambuzi, kama kigezo pekee Wanakitegemea hicho kutatua matatizo yote. Kazi ya sayansi hizo ni kufafanua uhusiano baina ya mambo; lengo lao ni kuthibitisha uwiano baina ya matukio, si baina ya Mwenyezi Mungu na matukio. Katika sayansi za majaribio, mwanadamu hahusiki kabisa na Mwenyezi Mungu. Mtu asiwe na matumaini ya kuweza kutambua ukweli wa hisia za juu kwa kutumia kigezo cha hisia, au kamuona Mwenyezi Mungu ndani ya maabara.

Sayansi hizo haziwezi kufanya majaribio ya maabara juu kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na halafu wafikie uamuzi kwamba endapo kitu hakionekani kimwili na hakiwezi kuthibitishwa kwa njia ya majaribio ya maabara na ukokotozi wa kimahesabu, kwa hiyo, kitu hicho hakina ukweli. Kwa kweli hakuna jaribio lolote linaloweza kufanywa na kupambanua kama kitu kisicho cha ki-maada kipo au hakipo, kwa sababu ni kitu hicho tu

ambacho kinaweza kukanushwa kwa njia ya majaribio kinachoweza kuthibitishwa kwa njia ya majaribio. Sayansi na metafizikia ni aina mbili za elimu ambazo zina kiwango sawa cha uhalali na usahihi. Kanuni ya metafizikia haitokani na majaribio wala haiwezi kukanushwa na majaribio.

Maelfu ya majaribio ya kisayansi yanabuniwa ili yathibitishe kwamba vitu vyote ni vya ki-maada, yote yatashindwa kufikia malengo yao. Mwanasayansi wa majaribio anayo haki ya kusema, "Nimevumbua hiki na hiki," au "Sijagundua hiki na hiki." Hana haki ya kusema, "Kitu hiki na kile havipo." Mbinu za maabara, pamoja na utata wao na hali ya juu ya maendeleo, haziwezi kupata njia kupitia yasiyojulikana, giza na dunia iliyopanuka ya vitu vya asili, ambavyo ndio kiini cha majaribio, haziwezi kufahamu ukweli wote uliojificha katika kiini cha chembe zisizo na kikomo na haziwezi kuvumbua hata asili halisi ya kitu.

Mbinu inayotegemea majaribio imekuwa na manufaa sana katika kuendeleza utambuzi wa mwanadamu wa mpangilio sahihi wa maumbile, na inaweza kutoa msingi ulio dhahiri na mpya kwa ajili ya kumwamini Mola Mlezi kupita kwenye uchunguzi wake wa utaratibu wa uumbaji, kwani inaashiria kuwepo kwa Muumba mtambuzi na mwenye uwezo. Hata hivyo, nia na madhumuni ya wana sayansi katika utafiti na uchunguzi katika masuala ya maumbile na siri za dunia kwa ujumla si kwa sababu ya kumtambua Muumbaji wa uhai. Ikiwa katika mkondo wa kuendelea kukua kwake katika mikono ya watafiti, sayansi wakati wote imekuwa inagundua siri za kuwepo kwa maumbile bila ya wanasayansi kujitokeza, kwa njia ya sayansi yao, kutoka kwenye ujuzi mfinyu na wenye mipaka ambao wameupata kutoka kwenye hatua yao ya utafiti wa sasa.

Endapo wangelikuwa wafanye hivyo, wangelifahamu uunganishwaji wa mambo na kujiweka chini kwa vitu vyote kwenye utaratibu uliowekwa, na kwa hiyo, kupata hatua nyingine mbili za ziada za ujuzi na utambuzi. Kwanza wangeweza kuwianisha data zao zote za kihisia na majaribio, na halafu wangeweza kutoa uamuzi wa busara na kufanya tafsiri. Bila kukubali kuwepo kwa Muumba mwenye busara, haiwezekani kutoa tafsiri kwa kusadikisha ukamilifu wa data zenye tofauti zinazotokana na elimu mbalimbali na uhusiano uliopo baina yao.

Kwa matendo, hata hivyo, kazi na mbinu za fikra ya kisayansi ni kuunda kanuni na kufanya utafiti bila marejeo kwa Mwenyezi Mungu, hivyo kwamba mfumo wa fikra ambamo Mwenyezi Mungu hahusishwi unakuwa mhimili ambao juu yake kazi ya kisayansi huugeukia, na kusababisha mwanadamu kuwa mgeni na chochote kilichopo nje ya upeo wa fikra hiyo. Wakati huo huo, maisha ya kivitendo ya mwanadamu yanasihusiana na elimu bila kuepukika. Matokeo yanayotokana na ujuzi unaotegemea majaribio yanajumuisha mielekeo yote ya ki-maada ya maisha, kuwafunga wanadamu kwenye kuta zao nne zisizopenyeka, na ni vigumu sana kupata nyenzo yoyote ya kawaida miongoni mwa njia za maisha ya mwanadamu.

Hali hii kwa ulazima huongeza kuamini kwa binadamu katika sayansi na huathiri tabia yake, kumdukizia nafsini mwake hali ya mashaka na wasiwasi. Juu ya hayo, manufaa ya hali ya asili ya kitu kilichofanyiwa uchunguzi kwa kutumia sayansi ya majaribio kinagusika na kiko dhahiri kwa kila mtu, kwa tofauti kubwa sana ikilinganishwa na masuala ya

metafizikia. Vivyo hivyo, vitu vya kimaada ambavyo vimechunguzwa kwa kutumia sayansi ya majaribio vinaeleweka sana, ambapo kinyume chake ni kweli katika masuala ya metafizikia.

Kuwasilisha masuala ya kidini kwa kutumia mbinu isiyo sahihi iliyofuatwa na kanisa la zama za kati (1100-1500A.D), ikichanganywa na uadui kwenye udhihirikaji wote wa sayansi, ilikuwa ndio jambo muhimu sana katika kuifanya sayansi ya majaribio kuonekana yenye kupendelewa zaidi kuliko yale ya mambo kifalsafa na ya kimaada. Kwa ufupi, sayansi ilionekana kupingana cha dini, si kwenda sambamba nayo. Mara mantiki ya majaribio ilipofuzu katika kumwaga fikra zote ndani ya umbo lake, ilibadili sura ya mtazamo wa wanadamu juu ya dunia kwa kiwango ambacho kwamba walisadiki kwamba huo tu ndio ulikuwa msingi kwa ajili ya kukubali ukweli wa kitu. Waliiteua kuwa ndio mamlaka ya mwisho na wakaona kwamba haiwezekani kuthibitisha kuwepo kwa kitu chochote ambacho hakitambuliki kwenye akili.

Hivyo, mwana sayansi anayetegemea majaribio, ambaye hafahamu utaratibu wa watu wanaomjua Mwenyezi Mungu, anakubali na kuona kuwa ni sawa katika maisha yake, kila kinacholingana na mantiki na fikra ya kisayansi. Hujichukulia mwenyewe haki ya kukanusha chochote kisichochukuana na desturi yake ya kisayansi. Utaratibu wake ni imani kamili katika majaribio na kuiona kuwa ni ndio uthibitisho pekee wa usahihi wa maamuzi yoyote. Katika hali kama hii, ambapo msingi wote wa fikra za kidini unapuuzwa, mwanasayansi anajikuta hana kanuni zozote za kumwezesha kutafsiri yale masuala madogo madogo ya kidini ambayo hujitokeza katika namna ya amri na makatazo. Akiwa amezoea kabisa lugha ya kisayansi na kutegemea kanuni, anakuwa amejifunga kabisa kwenye desturi yake na kudhani amri za dini zinazoshurutisha, zilizo rahisi na zinazoeleweka, kuwa hazina maudhui au thamani.

Njia hii ya fikira ina dosari na si sahihi. Ingawa sayansi zina fomula (kanuni) changamani za ajabu na sahihi, ambazo kuzielewa kwake huhitaji uchunguzi wa kina na mgumu, fomula hizo hizo huondoka kwenye nyanja ya sayansi mara ziingiapo katika maisha yetu ya kawaida, hujitenga na lugha ya kifundi ya wana sayansi. Kama isingekuwa hivi, zingedhibitiwa kutumika kwenye vituo vya kisayansi na viwanda, maktaba na vituo vya utafiti.

Kila mtu anaweza kutumia vifaa kama simu na radio. Hali ni hiyo hiyo kwa nyenzo na zana za kisayansi. Juu ya usahihi na uchangamano wao, maelekezo kidogo yenye utaalamu yatamwezesha mtu yeyote kuzitumia. Mtu aliyebobea na mtaalam huwa hawatoi maarifa ya umakenika na ya ufundi kwa wanunuzi wa kifaa, badala yake, hufupisha maelezo yao katika sentensi fupi fupi yale matokeo ya kazi ngumu zilizovumiliwa na wavumbuzi. Kwa hiyo, si haki na ni kinyume cha mantiki ya kisayansi kujaribu kulazimisha amri za dini (ambazo haziwezi kufupishwa kuwa fomula za kisayansi, ambapo zikiwa rahisi na za kila mahali) kwenye tabia ya dhana na maoni ya mtu, na halafu zitangazwe kwamba hazina thamani na si za maana, huku wakipuuza wajibu wao wa kimaamuzi na athari zao za maana sana katika maisha yetu. Maelezo ya kivitendo huzaa matunda yao

wakati yanapotamkwa katika lugha inayoeleweka kwa ujumla na kuwa na mguso kwa kila mtu na maisha ya kijamii.

Zaidi ya hayo, endapo ingedhaniwa kwamba amri na maelekezo ya dini yangeamuliwa na ufahamu, uelewa na muonjo wetu hapangekuwepo na haja ya wahyi na Mitume; tungeweza kuanzisha dini zetu wenyewe! Mara nyingi mwanadamu huwa hazioni dosari zake, akishughulishwa kama alivyo na nguvu zake. Mwenye kuabudu sayansi wa dunia ya leo anajivunia sana pia ujuzi wake kama matokeo na maendeleo ambayo yameyapatikana kutoka kwenye sayansi za majaribio kiasi kwamba anajidhania yeye mwenyewe kwamba ameshinda na kwa ushindi huo amechukua umiliki wa dunia ya ukweli. Lakini, hapana mtu ambaye wakati wowote ameweza kudai kwamba amepata ujuzi wa siri zote za ulimwengu na kuondosha mapazia yote kutoka kwenye dunia ya maumbile ya asili.

Mtu lazima achukuwe mtazamo mpana zaidi juu ya hali halisi na atambue ni jinsi gani tone la elimu yake lilivyo dogo likilinganishwa na bahari ya siri zilizofichika ambazo zinatukabili sisi. Baada ya kila ugunduzi wa kisayansi, msururu zaidi wa mambo yasiyojulikana hujitokeza. Katika karne zote ambapo mwanadamu amekuwa akifanya kazi bila kupumzika pamoja na rasilimali zake zote ili aweze kuijua dunia kwa kadiri iwezekanavyo, matokeo pekee ya jitihadi zake yamekuwa ugunduzi wa mambo machache miongoni kwa siri nyingi za ulimwengu. Ni hatua chache tu zimechukuliwa katika njia hii, na kuna lundo kubwa la yasiyojulikana yaliyoizunguka elimu ya mwanadamu kama wingu.

Kwa hiyo, mtu lazima atathimini kwa uhakika zaidi upeo wa utambuzi wa sayansi za hisia na sehemu zao zinazofaa kwa shughuli na athari. Mawazo yote yaliyokuwepo hapo kabla ambayo ni kama vizuizi kwenye njia ya kwenye ukweli lazima yaachwe kwa ajili ya uchambuzi sahihi.

Bila shaka, sayansi za majaribio zinaweza kutujulisha vipengele vya nje tu vya jambo; ni vitu vya ki-maada na mambo yakinifu ambavyo vinakuja kwenye upeo wa uchunguzi wao na vinaweza kuathirika kwenye majaribio ya maabara. Utaratibu wa sayansi katika kufanikisha malengo yao, wakiwa wanatafuta kupata faida kutoka kwenye kila ongezeko dogo katika ujuzi, ni uchunguzi na majaribio. Kwa kuwa shughuli ya msingi wa sayansi ya majaribio ni uchunguzi wa dunia ya nje, ili kuweza kuwa na uhakika kwamba nadharia fulani ya kisayansi ni sahihi, lazima tuilinganishe na ulimwengu wa nje ili kuijaribu. Endapo dunia ya nje inathibitisha kwa kufaa zaidi, sisi tunaikubali; laa kama sivyo, basi hatuikubali.

Kwa hiyo, kuzingatia lengo na utaratibu wa sayansi ya majaribio, lazima tuhoji endapo kama ukweli wa metafizikia unategemea kwenye kipimo cha hisia na kufanyiwa majaribio? Hivi hoja yoyote ya majaribioya kisayansi lazima ina haki ya kuingilia kati masuala ya imani na itikadi? Je, kuna sehemu yoyote ya sayansi ya majaribio inayohusika na Mwenyezi Mungu? Ili kuweza kugundua usahihi na kutokuwa sahihi kwa jambo katika sayansi za majaribio, ni muhimu kufanya matumizi ya mabadiliko na ya kuondoa vipengele tulivyopewa, pamoja na mazingira yake. Utaratibu huu hautumiki kwenye uhai wa ki-mungu, wa milele, usiobadilika na wa vitu vingi.

Ujuzi yakinifu ni taa ambayo inaweza kumulika baadhi vitu visivyojulikana kwa miale yake lakini si taa ambayo inaweza kuondosha

giza lote. Kwani elimu ya mfumo hutegemea kuufahamu ujumla wake wote kabisa na namna ya ufahamu ambayo inaweza kuunganisha wenyewe sehemu zote za utambuzi, na kusababisha mtazamo wa mbali mtimilifu kabisa. Sasa kuifungia elimu ya mwanadamu kwenye kikomo cha sayansi za hisia hauwezi kumfikisha mtu kwenye mtazamo wa mbali kamili, bali kwenye ufahamu wa eneo la ndani zaidi la nafsi.

Kama tunamwamini Mwenyezi Mungu au laa, kwa kweli haina uhusiano na sayansi za majaribio, kwa sababu kwa kuwa kiini cha uchunguzi wao ni maada, sayansi zinazojihusisha na mambo yanayoonekana hayana haki ya kujieleza yenyewe kwa kukubali au kukataa kuhusu jambo lolote lisilokuwa la ki-maada. Kwa mujibu wa imani ya kidini ya madhehebu mbali mbali, Mwenyezi Mungu sio mtu - hana mwili. Hawezi kufahamika kwa kutumia milango ya fahamu. Yeye ameupindukia muda na nafasi (havihitajii). Yeye ni Ambaye kuwepo kwake hakutawaliwi na mipaka ya kidunia na nafasi haiwezi kumbana. Kwa hiyo, Yeye ameepukana na kuhitaji na ametukuka katika dhati yake juu ya upungufu wa aina yoyote.

Anavijua vipengele vya ndani sana na vya nje vya ulimwengu. Dunia ipo wazi mbele Yake. Mwisho kabisa, Anacho kiwango cha juu kabisa cha ukamilifu na ametukuka zaidi kuliko chochote kinachomhusu Yeye kinachoweza kuingia kwenye akili ya mwanadamu. Hatuwezi kabisa kuujua msingi wa dhati Yake, tukiwa tuna upungufu wetu wenyewe na wa uwezo wetu, akili na nyenzo za upambanuzi. Kwa sababu hii; endapo ukivichunguza vitabu vyote vya sayansi ya majaribio, hutakuta utajo hata kidogo wa majaribio kuhusu Mwenyezi Mungu au uamuzi wowote umetolewa kuhusu Mwenyezi Mungu.

Hata kama tutachukulia utambuzi wa hisia kuwa ndio njia pekee ya kugundua ukweli, hatuwezi kuthibitisha kwa kutegemea utambuzi wa hisia, kwamba hakuna kitu chochote kinachokuwepo nje ya ulimwengu wa hisia. Madai kama hayo, yenyewe yatakuwa si ya kutegemea majaribio, yakiegama kwenye ushahidi usiokuwa wa hisia au majaribio. Hata kama wafuasi wa madhehebu ya kidini walikuwa hawana uthibitisho wa kutetea madai yao, kuhitimisha kwa uthabiti na kwa nguvu kwamba visivyokuwana uhai, vimeenea nje ya upeo wa hisia, ungekuwa ni uchaguzi usio wa kisayansi, ulio tegemea kwenye dhana na minong'ong'oni.

Watu wengine hujaribu kutangaza njozi hizi kwa kuisingizia sayansi na kuonyesha uchaguzi wao kuwa umetokana na fikra ya kisayansi. Hata hivyo, katika mchanganuo wa mwisho, ukanushaji unaohusishwa kwenye madai kama hayo hayana thamani ya sayansi na falsafa, na vilevile yanapingana na mantiki ya majaribio. Kwenye kitabu kiitwacho 'The Elementary Principles of Philosophy'. George Pulitzer anasema, "kukidhania kitu ambacho hakikalii muda na nafasi na hakiathiriwi na mabadiliko wala maendeleo, ni jambo lisilowezekana."

Ni wazi ya kwamba maneno haya yanaakisi njia fulani ya fikra ambayo haijui inatafuta nini. Kama ingejua inachokitafuta, pia ingeelewa namna ya kukitafuta. Kwa kuwa shughuli ya aina hii ya fikra inazunguka kwenye maumbile na himaya ya hisia, ni kawaida kwamba itachukulia kama ni kitu ambacho hakiwezekani, kila kile kilichopo nje ya eneo la shughuli yake na kuwepo kwake ambako hakuwezi kuthibitishwa kwa njia ya majaribio ya

hisia. Itaiona imani katika ukamilifu wake hasa kama ni kinyume na muundo wa fikara ya kisayansi. Hata hivyo, wasomi wanaojishughulisha na elimu asilia wanakabiliwa na lundo kubwa la vitu visivyojulikana kuhusu dunia hii hasa, na vya dhahiri, visivyo na uhai ingawaje wakati wote vina mawasiliano nayo (mbali na ulimwengu wa maada, wenye miujiza na siri nyingi zisizo na idadi, haihusishi hili tufe la dunia tunayoishi tu). Wasomi kama hao, kwa hiyo, wanayo haki yakusema tu, "Kwa vile nyanja za kimiujiza zipo nje ya upeo wa zana zangu za kitaalamu, ninanyamaza kimya na sitakanusha. Wangewezaje kujiruhusu kutoa madai ambayo yangesababisha elimu pana kiasi cha kama mpango wa ulimwengu wote, ambapo ujuzi wao wa mpango wote wa uhai unakaribia sufuri?

Kuna uthibitisho gani wa kuhakikisha madai kwamba uhai ni sawa na kitu cha ki-maada na kwamba dunia yote ya uhai imejaa vitu vya kimaada? Ni mwanasayansi gani anayeikataa metafizikia ambaye ameweza kusimamisha kanusho lake juu ya mantiki au ushahidi, au kutoa ushahidi kwamba nje ya kutokuwepo uhai, hakuna kitu kilichopo nje ya uwanja wa hisia? Ingawa sayansi haikatai kwa uwazi na uhakika kabisa kila kitu kisichojulikana kwa sababu tu kwamba haina uwezo wa kukifikia kwa kutumia nyenzo na vifaa vyake, badala yake inangojea kwa uvumilivu siku ambapo kitu hicho kitavumbuliwa, wapenda anasa za dunia wala hawaliendei suala la kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kwa shaka na wasi wasi, kwa misingi ya maoni yao ya kimakosa na haraka, wanatangaza uamuzi wao kwamba hakuna Muumbaji!

Watu kama hawa huanzisha vigezo na viwango fulani kwa ajili ya matumizi yao; na hawapo tayari kutumia kigezo kingine kilichoanzishwa kwa makusudi fulani katika eneo lililokusudiwa. Mathalan, kamwe hawatatumia kigezo ambacho kinatumika kwenye uso wa kitu kupimia mwili, lakini inapokuja kwenye kupima dunia ya hisia nyingi wanajaribu kumpima Mwenyezi Mungu, roho na msukumo, kwa kutumia nyenzo hizo hizo wanazotumia kupima dunia yakinifu. Wanapojikuta hawawezi kupata ujuzi wowote wa viumbe kamili husika, wanaendelea kukana kuwepo kwa vitu hivyo.

Sasa kama mtu aliyefungwa kwenye mantiki ya majaribio atapenda kukubali ukweli wa ulimwengu kwa kadiri tu alivyoruhusiwa na uzoefu wa hisia na kukanusha chochote kilichopo nje ya hilo, lazima atambue kwamba hii ni njia ambayo amejichagulia mwenyewe, si matokeo ya uchambuzi wa majaribio ya kisayansi. Aina hii ya itikadi bandia ya usomi na uwezo wa kiakili hutokana na uasi wa kisomi na mtu kuacha asili yake halisi.

Huyo Mwenyezi Mungu ambaye mwanasayansi wa kawaida, anataka "kuthibitisha" kwa kutumia nyenzo zake na vifaa vyake, kwa hali yoyote ile, sio mungu asilani kwa mtazamo wa wale wanaomcha Mwenyezi Mungu.

4

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA NNE

### KUAMINI UKWELI WA KISICHOONEKANA KUNAHUSISHA MENGI ZAIDI YA MWENYEZI MUNGU

Sifa moja wapo ya Mwenyezi Mungu wa pekee kwa elimu na ibada ya Ambaye Mitume na viongozi wa kidini wanatuitia ni kwamba Yeye hafikiwi kabisa na hisia za utambuzi. Kwa nyongeza, Anazo sifa za kutokuwa na mwanzo au mwisho. Wa kuwepo kila mahali, Ha. Katika dunia yote ya maumbile na uhai wa kihisia ishara Zake zina madhubuni ya kuwepo kwake na matakwa Yake yanaonekana kila mahali katika dunia hii iliyo uhai, mambo yote ya maumbile vikitangaza uwezo wa ile Dhati yenye hekima.

Kwa kweli, dhati kama hiyo ambayo binadamu hawezi kuitambua kwa milango yake ya fahamu, ambayo kwa vyovyote vile haikupambwa kwa rangi za kimaada, na ambayo hailingani na uzoefu na mawazo yetu ya kawaida, ni vigumu sana sisi kuidhania. Pindi inapokuwa vigumu kudhania kuwepo kwa kitu, inakuwa rahisi kukataa (kuwepo kwake). Watu wanaotaka kutatua suala la kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kwa kutumia muundo wa mipaka yao wenyewe ya ki-akili na ufinyu wa mawazo huwa wanahoji inawezekana vipi kuamini kitu kisichoonekana.

Wanashindwa kuzingatia ukweli kwamba utambuzi wa fahamu, ambayo imewekewa mipaka, inaweza kumsaidia mwanadamu kujua na kutambua muundo mmoja tu wa asili; haiwezi kugundua miundo mingine ya asili na kupenya ukubwa wote wa maumbile. Viungo vya fahamu havituruhusu kuendelea hatua moja mbele kuvuka ng'ambo ya vipengele vya nje ya tukio, kwa namna ile ile tu ambayo sayansi za majaribio haziwezi kubeba fikra ya mwanadamu kuvuka mipaka ya hisia za kiwango cha juu zaidi.

Endapo mwanadamu, kwa kupitia nyenzo na vigezo vya kisayansi, hawezi kutambua kuwepo kwa kitu, hawezi kukanusha kuwepo kwa kitu hicho kwa sababu tu hakiendani na vigezo vya kilimwengu, isipokuwa labda atupe baadhi ya ushahidi kwamba hicho kitu husika hakiwezekani. Tunagundua kuwepo kwa kanuni ya busara kutoka ndani ya utimilifu wa tukio kwamba ina uwezo wa kutafsiri. Endapo, basi, kusimama kwa hoja ya ukweli wa kisayansi kunawezekana tu kwa njia ya hisia za moja kwa moja, itakuwa hapana budi kuacha ukweli mwingi wa kisayansi, kwani mambo mengi ya kisayansi hayawezi kutambulika kwa njia ya uzoefu wa kihisia au kufanya vipimo.

Kwa kadiri ambavyo uhakika wa dunia ya kimaada uhusikanavyo, hakuna mtu mwenye busara ambaye atachukulia kikawaida kutokukiona au kutokigusa kwake kitu maalum katika maisha yake ya kila siku kuwa sababu ya kutosha kukikataa. Hataweza kuhukumu kwamba hakipo, kitu chochote kinachoshindwa kuingia kwenye upeo wa utambuzi wake wa hisia. Vivyo hivyo hili litasisitiza ukweli wenye nguvu zaidi wa vitu visivyo vya ki-maada.

Tunapokuwa kuhakikisha sababu ya jambo katika majaribio ya kisayansi, hali hii haituelekezi kukanusha kanuni ya usababishaji. Sisi tutasema tu kwamba sababu hatuijui kwa sababu kanuni hiyo inajitegemea juu ya jaribio maalum tu; hakuna jaribio linaloweza kukanusha kuwepo kwa asili. Je, sio kweli kwamba vitu vyote tunavyokubali na kuamini kwamba vipo, vina uwepo wake wenye uhusiano wa jinsi ile ile kama ya kwetu au kama ya vitu vile tunavyoviona kwa macho? Je, tunaweza kuona au kuhisi kila kitu katika dunia hii maumbile? Hivi ni Mwenyezi Mungu tu ndiye ambaye hatuwezi kumwona kwa fahamu zetu? Wayakinifu (wa ki-maada) wote wanatambua kwamba vitu vingi tunavyovijua vinakuwa na maada na uhalisia ambao hatuwezi kuhisi na kidesturi hatuvijui. Vipo viumbe visivyoonekana vingi tu hapa ulimwenguni.

Maendeleo ya sayansi na ujuzi katika zama hizi vimegundua ukweli mwingi sana wa aina hii, na mojawapo ya milango yenye mafanikio sana katika utafiti wa kisayansi ni ubadilishaji vitu vya kimaada kuwa nguvu ya nishati. Wakati viumbe na maumbile yayoonekana katika ulimwengu huu vinapotaka kuzalisha nishati, hulazimika kubadili sura zao za asili na kugeuka kuwa nishati. Sasa, je, nishati hii - mhimili ambamo huzunguka misogeo mingi na mabadiliko ya ulimwengu - inaonekana na kugusika? Tunajua kwamba nishati ni chanzo cha nguvu lakini asili ya nishati bado inabakia ni kitendawili.

Tuchukue umeme ambamo nyingi ya sayansi yetu, ustaarabu wetu na maisha vimetegemea. Hakuna mtaalamu wa fizikia kwenye maabara yake - au mtu awaye yeyote, juu ya jambo hilo, ambaye anashughulika na vifaa na zana za umeme - anayeweza kuuona umeme wenyewe au kuhisi na kugusa uzito au ulaini wake. Hakuna mtu anayeweza kutambua moja kwa moja njia ya umeme kwenye waya; anaweza tu kutambua kuwepo kwa mkondo wa umeme kwa kutumia vifaa muhimu.

Fizikia ya kisasa inatuambia kwamba vitu ambavyo tuna hisia ya utambuzi ni thabiti, vigumu na imara, na hakuna nguvu inayoonekana kwa macho katika kusogea kwao. Lakini licha ya muonekano na wa nje, kwa kweli kile tunachokiona na kutambua ni mlundikano wa chembe ndogo ndogo (atomu) ambazo wala sio thabiti, ngumu, wala imara; vyote hivi si chochote isipokuwa migeuko, mabadiliko na misogeo. Kile ambacho viungo vyetu vya hisia vinadhania kuwa ni imara na hakisogei kinakosa uimara na utendaji na kutosogea; kinavikusanya vyote; misogeo, mabadiliko na maendeleo kwa pamoja, bila ya hili kutambulika kwetu sisi kwa njia ya uchunguzi wa hisia wa moja kwa moja.

Hewa inayotuzunguka ina uzito mkubwa na hutoa shinikizo wakati wote kwenye mwili, kila mtu hubeba shinikizo la kilo 16,000 la hewa. Lakini hatuhisi usumbufu kwa sababu shinikizo la hewa limewekwa sawa na shinikizo la ndani ya mwili lenyewe. Ukweli huu wa kisayansi uliothibitishwa ulikuwa haujulikani hadi wakati wa Galileo na Pascal, na hata sasa hivvi hisia zetu haziwezi kutambua[1]. Sifa zilizotolewa kwenye vipengele vya kimaumbile na wanasayansi katika misingi ya majaribio ya hisia na maamuzi ya kimantiki haziwezi kutambuliwa moja kwa moja.

1. Hiss-i-Dini, kilichotafsiriwa na Mhandisi Bayani.

Mathalani mawimbi ya radio yapo kila mahali na bado hayaonekani popote. Hakuna mahali maalum ambapo hakuna nguvu ya mvutano ya kitu fulani chenye umbo, lakini kwa hali yoyote hii haikiondoi kwenye kuwepo kwake au kupunguza umbo lake.

Fikra kama vile uadilifu, uzuri, mapenzi, chuki, uadui, hekima ambazo hutengeneza ulimwengu wetu wa kiakili, hazina uwepo unaoonekana na wa wazi kabisa au mwelekeo mdogo kabisa wa kimwili; hata hivyo, tunazifikiria kuwa ni ukweli. Mwanadamu hajui kiini cha umeme, mawimbi ya radio au nishati, ya elektroni na nutroni, hutambua kuwepo kwao kwa njia ya matokeo na athari zao tu.

Uhai ni dhahiri kwamba upo; hatuwezi kukanusha kwa vyovyote. Lakini tutaweza kuupima vipi na kwa kutumia njia gani tunaweza kupima kasi ya fikra na dhana? Kutokana na yote haya ni wazi kabisa kwamba kukanusha chochote kilichopo nje ya upeo wa uoni wetu wa kiakili na kusikia ni kinyume na mantiki na kanuni za kawaida za akili. Kwa nini wakana Mwenyezi Mungu wanashindwa kutumia kanuni za kawaida za sayansi kuhusu suala mahsusi la kuwepo kwa uwezo unaotawala maumbile yote? Myakinifu fulani wa Misri alikwenda Makka ili aanzishe mjadala na huko 8

alikutana na Imamu Sadiq (a.s). Imamu akamwambia, "Anza kuuliza maswali yako." Myakinifu kutoka Misri hakusema kitu. Imamu: "Unakubali kwamba dunia ina juu na chini?" Mmisri: "Ndio." Imamu: "Kwa hiyo unajuaje kile kilichomo chini ya ardhi?" Mmisri: "Sijui, lakini nadhani hakuna chochote chini ya ardhi." Imamu: "Kudhania ni dalili ya kutokuwa na uwezo unapokabiliwa na jambo ambalo huna uhakika nalo. Sasa niambie, umewahi kamwe kwenda juu angani?" Mmisri: "Hapana."

Imamu: "Hii ni ajabu ya kiasi gani kwamba hujawahi kwenda Magharibi au Mashariki, kwamba hujateremka chini ya ardhi au kuruka juu angani hadi mbinguni, au kupita juu yake ili ujue yaliyoko huko, lakini hata hivyo unavikanusha vile vilivyopo huko. Mtu yeyote mwenye busara angeweza kukataa ukweli wa kile asichokijua? Na unakanusha kuwepo kwa Muumba kwa sababu huwezi kumwona kwa macho yako!" Mmisri: "Hakuna mtu aliyewahi kuzungumza nami kwa namna hii kabla yako." Imamu: "Kwa hiyo, kwa kweli unayo mashaka kuhusu kuwepo kwa Mwenyezi Mungu; unadhani Anaweza kuwepo na Anaweza asiwepo?"

Mmisri:"Labda ndivyo" Imamu: "Ewe mtu, mikono ya mtu asiyejua haina uthibitisho wowote; asiyejua kamwe hawezi kuwa na ushahidi wa aina yoyote. Ufahamu vema kwamba kamwe hatuna wasi wasi wa aina yoytote au kusitasita kuhusu kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Je, hulioni jua na mwezi, mchana na usiku, vinapishana wakati wote na vikifuata njia maalum iliyowekwa? Kama vina uwezo wao vyenyewe, hebu viondoke kwenye njia zao na visirudi tena. Kwa nini wakati wote vinarudi? Endapo viko huru katika kubadilishana na kubiringika kwao, kwa nini usiku haugeuki kuwa mchana na mchana kuwa usiku? Ninaapa kwa Jina la Allah kwamba vitu hivi havinav uhuru wa kuchagua katika misogeo yao; ni Yeye Ndiye husababisha vitu hivi kufuata njia iliyowekwa; ni Yeye Ndiye anayeviamuru vitu hivi: na ukuu na ufahari ni vya kwake pekee." Mmisri: "Unasema kweli!"

Imamu: "Kama unadhani kwamba maumbile na muda vinawapeleka watu kimbele mbele, sasa kwa nini wao haviwarudishi kinyume nyume? Na kama vinaweza kuwarudisha nyuma, kwa nini haviwapeleki kimbele mbele? Tambua kwamba mbingu na ardhi vinatii matakwa Yake. Kwa nini mbingu haziporomoki na kuanguka ardhini? Kwa nini matabaka ya ardhi hayapinduki chini juu na kwa nini hayapandi na kufika juu mbinguni? Kwa nini hao waishio juu ya ardhi hawagandamani?" Mmisri: "Mwenyezi Mungu Ambaye ni Mola na Mlezi wa mbingu na ardhi ndiye anayevilinda vitu hivi visiporomoke na kuangamia." Yale maneno ya Imamu sasa yalianzisha mwanga wa imani kuangaza kwenye moyo wa Mmisri; aliukubali ukweli na akaingia kwenye Uislamu[1].

Tusije tukasahau kwamba sisi tumefungwa ndani ya mfumo wa maada na mapana yake; hatuwezi kubunia kitu kisichokuwa na mipaka kwa kutumia tabia zetu za kawaida za kifikra. Endapo tutamuambia mwanakijiji kwamba kuna jiji kubwa na lenye watu wengi liitwalo London, akilini mwake atafikiria juu ya kijiji kikubwa, labda mara kumi zaidi ya ukubwa wa kijiji chake, na itakuwa hivyo hivyo kuhusu majengo yake, jinsi watu wanavyovaa, namna wanavyo endesha maisha yao na wanavyoingiliana katika shughuli zao. ataona kwamba tabia za watu kila mahali ni hizo hizo kama zilivyo kijijini kwake.

Jambo pekee tunaloweza tu kumwambia ili kusahihisha namna yake isiyo sahihi ya kufikiria ni kwamba London kwa kweli ni sehemu ya makazi ya watu, lakini sio ya namna unayodhania wewe, na hali zake sio za namna moja na zile unazoona pale kijijini kwako mwenyewe. Tunachoweza kusema kuhusiana na Mwenyezi Mungu ni kwamba Mwenyezi Mungu yupo, na kwamba Yu ana uhai, uwezo na ujuzi, lakini kuwepo Kwake na ujuzi na uwezo wake sio vya namna ile tuliyo na mazoea nayo. Kwa njia hii tunaweza, kwa kiwango fulani, kuepuka mipaka iliyowekwa katika uelewa wetu. Kwa myakinifu vile vile, ni vigumu yeye kutambua kiini cha msingi wa vitu asili (maada).

Ingawa inaonyesha kuwa vitu vyenye kuhisia ni vitu tunavyojua kwa uwazi na ufasaha zaidi, hatuwezi kutegemea moja kwa moja juu ya vitu hivyo pekee katika mambo ya kisayansi na kifalsafa. Tukiweka pembeni misimamo yote yenye shabiki, lazima tutathmini asili halisi ya vitu vya hisia na kiwango ambacho vinaweza kumsaidia mwanadamu katika kugundua ukweli. Vinginevyo, vitatupotosha, kwa sababu utambuzi wa hisia unahusiana tu na sifa fulani za mielekeo ya nje ya vitu vyenye kuhisia. Hauwezi kutambua ukamilifu wa sifa hizo au asili na kiini tu cha vitu vyenye kuhisi, tukiviacha vitu visivyokuwa na hisia.

Jicho ambalo ndio njia ya uhakika zaidi ya utambuzi wa ukweli, mara nyingi, hushindwa kutuonyesha sisi ukweli. Jicho linaweza kutazama mwanga pale tu ambapo urefu wa mawimbi yake haupungui 4% ya mikroni (kipimo cha urefu wa mamilioni ya mita) na sio zaidi ya 8% ya microni na, kwa hiyo, haliwezi kuona mwanga wa juu zaidi ya rangi ya urujuani au chini zaidi ya rangi nyekundu. Zaidi ya hayo, makosa yanayofanywa na

1. Biharul Anwar, Juz. III, uk. 51-53.

utambuzi wa hisia hutengeneza sehemu muhimu kwenye vitabu vya saikolijia: jicho linajulikana kwa kufanya makosa mengi sana.

Rangi tunazozitambua katika ulimwengu wa nje, kwa kweli, si rangi. Hiyo ni mitetemo iliyoko kwenye marefu tofauti ya mawimbi. Uzoefu wa hisia zetu za macho, una marefu mbalimbali ya mawimbi ya mwanga, kwa mujibu wa utaratibu wake mahsusi kama rangi. Kwa maneno mengine, kile tunachokitambua kwa njia ya hisia zetu kimewekewa mipaka na muundo na uwezo wa hisia hizo. Mathalan, muundo wa hisia za macho katika wanyama fulani kama vile ng'ombe na paka husababisha waone uhalisi wa nje wa kitu usiobadilika, kama kimepakwa rangi. Kutokana na maoni ya uchunguzi wa kisayansi, utaratibu ndani ya hisia za macho ya mwanadamu ambao humruhusu kuona rangi haupo wazi kabisa na nadharia ambazo zimetangulizwa hadi sasa zote ni za kubuni. Suala la uwezo wa mtu kuona rangi halieleweki vizuri na lenye utata.

Ili kuweza kuona jinsi hisia ya mguso inavyoweza kudanganywa, unaweza kujaza maji kwenye mabakuli matatu: la kwanza yajazwe maji ya moto sana, la pili maji ya baridi sana, na la tatu maji ya vuguvugu. Halafu weka mkono mmoja kwenye maji ya moto na mwingine kwenye maji ya baridi, na uiache humo kwa muda kiasi. Kisha iweke mikono yote kwenye maji ya vuguvugu, na utaona kwa mshangao wako mkubwa kwamba utapata hisia zinazohitilafiana. Mkono moja utakuambia kwamba yale maji ya vuguvugu ni ya baridi sana, na mwingine utadai kwamba ni ya moto sana. Kwa kweli, maji ni yale yale, na joto lake linafahamika.

Sasa, akili na mantiki zinasema kwamba haiwezekani maji kuwa moto na baridi kwa wakati mmoja, kuwa na sifa mbili zinazo tofautiana. Ni hisia ya mguso ndio yenye dosari, baada ya kupoteza hali yake ya kujidhibiti kama matokeo ya yale mabakuli mawili ya maji ambamo mikono ilitumbukizwa. Inachokihisi kinatofautiana na ukweli, na mantiki na akili hulionesha kosa hilo. Ikiwa hali ni hii, tutawezaje kutegemea utambuzi wa hisia bila ya mwongozo wa kigezo cha akili na fikira? Je, kuna njia yoyote ya kujilinda dhidi ya dosari za utambuzi wa hisia zaidi ya uamuzi wa busara? Wakati fulani mtu alimuuliza Amirul-Mu'minin (a.s), "Je, umewahi kumuona Mola Wako?"

Yeye akajibu: **"Sitamwabudu kamwe Mola ambaye siwezi kumwona!"** Huyo mtu halafu akauliza: "Wewe ulimwona vipi? Hebu tuelezee." Yeye (a.s.) akajibu: **"Ole wako wewe! Hakuna mtu ambaye amewahi kumuona Yeye kwa jicho halisi, lakini nyoyo zilizojaa ukweli wa imani zimemzingatia Yeye."**[1] Kwa hiyo ni uamuzi wa akili ndio unaopewa dhamana ya kusahihisha makosa ya utambuzi wa hisia, na chanzo cha uamuzi huo kiko nje ya upeo wa himaya ya hisia. Kwa hiyo, utambuzi wa hisia hauwezi kuzalisha uoni wa kiakili wenye uhalisi, manufaa yake ni ya mazoezi ya vitendo tu. Wale wanaotegemea utambuzi wa hisia pekee katika uchunguzi wao hawataweza kuyatatua kamwe matatizo ya uhai na kitendawili cha maumbile.

Kutokana na tathmini ya ufanisi wa utambuzi wa hisia, tunafikia hitimisho kwamba hata kwenye nyanja ya hisia za kimajaribio, yenyewe

1. Tafsir al-Mizan, Juz. VIII, uk.255.

peke yake haiwezi kutoa ujuzi wa uhakika kwa mtu na kumwongoza kwenye ukweli. Kwa ukweli wenye nguvu zaidi, hali itakuwa ni vivyo hivyo katika mambo ambayo yapo nje ya upeo wa utambuzi wa hisia. Wafuasi wa metafizikia (falsafa ya uchunguzi wa chanzo cha uhai na maarifa) wanasadiki kwamba kama ilivyo katika njia ile ile ambamo majaribio na upimaji ndio mbinu za uchunguzi na utambuzi zinatakiwa kufuatwa kwenye sayansi ya hisia, ni uwezo wa kufikiria ndio njia ya kugundua ukweli kwenye mambo yahusuyo falsafa ya kuchunguza chanzo cha uhai na maarifa - metafizikia.

### UMUHIMU WA KANUNI ZA UHAI

Sayansi inasema kwamba ni uhai ndio unaoumba uhai. Maisha ya viumbe hai yanawezekana tu kwa njia ya kizazi, kuzaana na kutengenezeka upya kwa aina husika. Hakuna chembe ya uhai hata moja ambayo imegundulika kuzaliwa na kiini asili kisicho na uhai. Hata aina ndogo za viumbe vyenye uhai, kama vile kuvu na vimelea, haviwezi kuwepo na kukua isipokuwa pawepo na kisababisho ambacho chenyewe ni kishiriki katika uhai kiwe ni chenye kuonekana kwenye mazingira yake.

Kwa mujibu wa ushahidi wa sayansi, dunia ilipita kwenye vipindi virefu ambapo hapakuwepo na uwezekano wa uhai kwa sababu ya joto kali sana lililokuwepo. Hapakuwa na uoto wowote ulioweza kuonekana kwenye uso wa sayari hii na hapakuwepo na mito au chemchem. Angahewa ilijaa metali zilizoyeyuka na milipuko ya volkano. Baadaye, wakati ambapo gamba la dunia lilipoanza kupoa, ni vitu visivyo na uhai tu ndivyo vilivyoweza kuonekana kwa mamilioni ya miaka. Kwa ufupi wakati wote wa kukurukakara zote za mabadiliko zilizofanyika kwenye uso wa ardhi, hapakuwepo na dalili za uhai juu yake. Ni vipi basi uhai ulivyojitokeza ghafla?

Hapana shaka uhai ulitokeza muda fulani baada ya kutokeza kwa ardhi; ni kwa muda mrefu kiasi gani utengenezaji huo ulifanyika na jinsi ulivyotokea, hilo halijukani. Kwa karne nyingi watafiti wamekuwa wakijitahidi kwenye maabara zao kugundua muujiza wa uhai, hili jambo la ajabu kwelikweli, lakini hadi sasa hawajakaribia hata kidogo kukifumbua kitendawili hiki. Mtafiti mmoja ameandika kwenye kitabu kiitwacho 'Distant World' "ni neno kichawi lililoje hili, la uhai! Je, hivi kuishi kulikuja kuwepo kutokana na kutokuwepo kitu chochote? Hivi dutu ya viumbehai inaweza kutokana na dutu viumbe visivyo hai? Au upo mkono fulani wenye uwezo na ubunifu unaofanya kazi hii? Wakati mwingine inapendekezwa kwamba inawezekana uhai umekuja kwenye sayari yetu kutoka kwenye maumbile mengine ya kimbingu, kwa sababu wakati ambapo aina ya chini sana ya uhai - viini vya mbegu za mboga - vinavyoogelea kwenye angahewa ya umbile la kimbinguni hupanda kufikia kilele cha juu sana, miale ya jua inaweza kuvibeba kwa njia ya shinikizo hadi kwenye anga, hivyo kwamba hatimaye vinafika kwenye uso wa umbile jingine la kimbinguni ambamo hustawi na kujiendeleza.

"Nadharia tete hii haiashirii maendeleo japo kidogo tu katika kupata ufumbuzi wa kitendawili hiki kikubwa, kwa sababu endapo nadharia hii ingekuwa ya kweli, bado hatujajua ni jinsi gani uhai ulivyojitokeza, ama ulitoka kwenye mojawapo ya sayari zilizopo kwenye mfumo wa jua na

sayari zake au mojawapo ya 'Nyota ya Shiraa.' Kama vile ambavyo saa haikutengenezwa kwa kulundika pamoja springi, vikorokoro, bolti na nyenzo, vivyo hivyo, pia uumbaji wa uhai hauwezekani bila kuwepo moyo - yaani kile kinachouweka uhai kwenye msongo - na wito ambao hutamka 'kuwa hai!'" Tunatambua kwamba maada ndani mwake na yenyewe inakosa uhai na kwamba hakuna elementi ya kimaada yenye kumiliki uhai bila ya kusaidi wa.

Hivyo basi, uhai hauwezi kufikiriwa kutokea kutokana na uchanganyaji wenye mpangilio mzuri wa chembehai zinazounda kitu. Swali linajitokeza kwamba kwa nini kitu chenye uhai hakiwezi kujinakili kama kilivyo isipokuwa kwa kuzaliana na kuota upya kwa spishi husika. Utendaji wa kikemikali na athari zake wakati wote zinaendelea katika viumbe visivyo na uhai bila ya dalili yoyote ya uhai kuonekana ndani yao. Kusema kwamba kitu cha kimaada kina mwelekeo wa mkusanyiko na kwamba uhai ghafla hujitokeza wakati wa maendeleo na mabadiliko yake ni kufafanua jambo la uhai na lenye umuhimu ambalo tunalitambua kihisia; sio kuelezea chimbuko la uhai na sababu yake.

Zaidi ya hayo, chembechembe za maada kiasili hazikuwa hazikuwa zenye kutofautiana zenyewe kwa zenyewe; kwa hiyo ni lazima kuna sababu iliyofanya kazi kuleta mkusanyiko wa baadhi yao na kuzuia mkusanyiko wa zingine. Na ni sababu gani ya baadhi ya chembe chembe kupewa uhai na zingine kunyimwa uhai? Jambo pekee la kutokea kutokana na mchanganyiko wa elementi mbili au zaidi ni kwamba kila elementi inaipatia elementi nyingine baadhi ya sifa ilizokuwa nazo; inawezekanaje itoe zawadi ya kitu ambacho hainacho? Elementi zinapata sifa ya pamoja kama matokeo ya kuchanganyika, sifa ambayo haiwezi kutoka nje ya sifa ambazo kila elementi inazo, lakini uhai pamoja na tabia yake ya kipekee haina kufanana kokote na sifa za maada.

Uhai unajionyesha wenyewe katika njia ambazo kwamba maada haiziwezi, na katika namna nyingi, kwa kweli, uhai hutawala maada. Ingawaje uhai huonekana kutegemea maada, yenyewe maada ikiwa ndio umbile linaloupokea uhai, msogeo, dhamira na hatimaye utambuzi na ujuzi huonekana kwenye maada pale tu uhai unapotupa miale yake juu yake. Kwa hiyo, sio haki kujaribu kutafsiri uhai kilingana na athari za kikemikali.

Ni kipengele kipi kinachotengeneza chembechembe kwa aina nyingi tofauti na kwa mipango tofauti na halafu kikaziweka kwenye muundo uliofikiriMwenyezi wa? Kinachotayarisha chembechembe zinazozaliana ambazo huhamisha tabia na upekee wa akina baba kwa watoto wao, bila ya kosa hata kidogo kutokea katika utekelezaji wa shughuli hiyo. Tunaona kwamba chembehai zinazo tabia fulani mahsusi katika sehemu zao mbalimbali, miongoni mwao ikiwa ni ukarabati, ujenzi upya, uhifadhi wa spishi, na uwezo wa mabadiliko.

Kila chembehai ndani ya mwanadamu hufanya kazi katika wakati unaotakiwa na kwa namna inayotakiwa. Mgawanyo wa kazi na utendaji wake miongoni mwa chembehai ni wa kipekee. Zimegawanywa katika idadi inayihitajika kuhakikisha ukuaji wa mwili, na kila chembehai huenda pale mahali ilipopangiwa kwenye ubongo, mapafu, ini, moyo na figo. Mara chembehai zinapokuwa zimechukua nafasi zao zilizopangiwa, hazishindwi

hata kwa nukta moja katika kutekeleza kazi zao muhimu; zinatawanya na kuondoa vitu visivyohitajika na visivyo na maana na kutunza hasa tu ule ujazo wao unaolingana.

Kuhusisha upambanuzi huu wa kipekee ambao unalengo la kuunda, kwa uwiano unaostahili, viungo na sehemu, vinavyohitajiwa na viumbe hai, kwenye mambo yatendayo bila kufikiri na yasiyo na fahamu ni tafsiri isiyotosheleza kabisa. Ni mtu gani mwenye mawazo huru ambaye angekubali ukosefu wa mantiki kama huu? Uhai, kwa hiyo, ni nuru inayoangaza kutoka kwenye upeo wa juu sana juu ya vitu vya kimaada ambavyo vina uwezo wa kuipokea; inaviweka vitu hivyo kwenye msogeo na kuweka kila kimoja kitaalamu kabisa mahali pake maalumu.

Ni utashi wenye mwongozo wa Muumba, uwezo Wake wa kuamua kwa njia ambayo inahakikisha mwendo na ukuaji kuelekea kwenye ukamilifu, na hekima Yake yenye maarifa mengi na yenye athari nyingi, ambayo ndio inayouweka muujiza mkuu wa uhai, na sifa zake zote, kwenye vitu visivyo na uhai.

Mtu ambaye anautambu a ukweli huona uelekeo wa kudumu wa uhai ukipita kwenye kiini cha kitu kinachobadilika na kutembea. Humtafakari Mwenyezi Mungu katika hali Yake ya kuendelea uumbaji na uanzilishaji, msukumo Wake usio na kikomo wa vitu vyote kuelekea kwenye ukamilifu.

5

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA TANO

### KUONEKANA MWENYEZI MUNGU KATIKA MAUMBILE

Dunia ya maada na maumbile, inayochukuliwa kama kitu kizima kilichoumbwa, ndio ushahidi mzuri sana, wa dhahiri na ulioenea sana, bila upinzani, juu ya ujuzi wa Mwenyezi Mungu. Utashi wenye busara ya Kanuni ya Milele unaweza kugundulika kutoka kwenye kutendeka huku hasa kwa mabadiliko ya vitu. Ni dhahiri kwamba miale Yake ya milele inatoa uhai na mahitaji kwa viumbe vyote, na kwamba viumbe wote wanapata uhai na maendeleo yao kutoka Kwake.

Kuchunguza viumbe tofauti ulimwenguni, siri za kitabu cha uumbaji, kurasa ambazo zote zina shahidilia kwenye shughuli za akili ya juu sana katika uumbaji wake, hutoa, halafu ushahidi ambao wakuegemeza elimu na imani juu ya Muumba mwenye hekima, Ambaye uwezo wake huonekana kidogo tu kwenye mpangilio wa viumbe kwa utukufu wao wote na ukubwa wao. Zaidi ya haya, ni uthibitisho ulio rahisi na kueleweka kwa urahisi ambao unakosa utata na uzito mkubwa wa ushahidi wa kifalsafa. Ni njia ya uchunguzi na tafakuri ambayo ipo wazi kwa wote; kila mtu anaweza kunufaika nayo, wanafikra na wanazuoni na umati wa watu wa kawaida.

Kila mtu, kwa kadiri anavyoruhusiwa na uwezo wake na upeo wa kuona kwake, anaweza kuona katika jambo zima la uumbaji dalili za uunganikaji, utulivu, umasukusudi wa dhati kabisa, na kukuta katika kila moja ya chembechembe zisizo idadi za maumbile, uthibitisho thabiti wa kuwepo kwa chanzo cha viumbe. Marekebisho kamili ya kila aina ya mnyama kufuatana na hali za maisha yake ni ishara kubwa ya Mwenyezi Mungu; kila aina imeumbwa pamoja na vifaa vyote muhimu vinavyohitajika katika hali ya maisha yake. Musa, (amani iwe juu ya Mtume wetu pamoja na yeye), ambaye alizungumza na Mwenyezi Mungu, alitumia ushahidi huu ili aoneshe kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kwa Firauni. Yeye Firauni akawaambia Musa na nduguze:

قَالَ فَمَن رَّبُّكُمَا يَا مُوسَىٰ ﴿٤٩﴾ قَالَ رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَىٰ ﴿٥٠﴾

"Ni nani Mola Wenu ewe Musa? Akasema "Mola Wetu ni yule aliyekipa kila kitu umbo lake. . ." (20:49-50).

Vivyo hivyo Imam Sadiq (a.s.) alimwambia Mufadhal, "Tazama kwa uangalifu lile umbo la maumbile ya ndege; uone jinsi alivyoumbwa mwepesi na mdogo katika ujazo ili kumwezesha kuruka. Ndege alipewa miguu miwili tu badala ya minne ambayo wanyama wengine wamepewa na vidole vinne tu kati ya vitano ambavyo wanavyo katika kila mguu. Ndege wana vifua nyembamba vilivyochongoka, ili waweze kuelea hewani na kuruka kwa urahisi kuelekea kila upande. Miguu mirefu ya ndege imekaa vizuri chini ya mkia wake na mabawa yake, na mwili wake wote umefunikwa na manyoya ili hewa iweze kupenya humo na kumwezesha kuruka. Kwa kuwa chakula cha ndege ni pamoja na mbegu na minovu ya wanyama ambavyo wanavila bila kutafuna, basi hawana haja ya meno.

Badala yake, Mwenyezi Mungu amewambia ndege mdomo mgumu na wenye ncha kali ambao hauwezi kuvunjiki wakati unaponyofoa nyama au kuumia wakati wa kukusanya nafaka. Ili kumuwezesha kiumbe huyu kukisaga chakula ambacho hakukitafuna, amepewa mfumo wa kusagia chakula wenye nguvu na mwili wenye joto. Zaidi ya hayo, ndege huzaana kwa kutaga mayai ili waweze kubakia wepesi kiasi cha kutosha kuwawezesha kuruka; endapo watoto wao wangekuwa wakulie matumboni mwao, wangekuwa wazito sana kuweza kuruka."

Halafu Imam akarejea kwenye kanuni ya jumla, akisema, **"Kwa hiyo upekee wote wa umbile la ndege huendana na mazingira yake na namna ya maisha yake."**[1] Suala la lugha ya wanyama - ile njia ambayo kwamba wanyama wanawasiliana wao kwa wao - ni dalili nyingine ya ki-ungu. wanyama wanayo aina maalumu ya lugha ambayo huwawezesha kuwasiliana wao kwa wao.

Qur'ani Tukufu inaelezea kisa cha mdudu chungu akiongea na Nabii Suleiman (a.s):

قَالَتْ نَمْلَةٌ يَا أَيُّهَا النَّمْلُ ادْخُلُوا مَسَاكِنَكُمْ لَا يَحْطِمَنَّكُمْ سُلَيْمَانُ وَجُنُودُهُ وَهُمْ لَا يَشْعُ رُونَ ﴿١٨﴾

"Akasema mdudu chungu: Enyi wadudu chungu! Ingieni majumbani mwenu, asikupondeni Suleiman na majeshi yake, hali hawatambui." (Naml: 27: 18).

Wanasayansi wa sasa wamegundua mtandao changamano wa mawasiliano miongoni mwa wanyama ambao ni mgumu zaidi na uliosahihi kuliko mfumo wetu wenyewe wa mawasiliano. Crissy Morrison anaandika: "Kama tukimweka nondo jike karibu na dirisha la chumba chetu, hutoa ishara nyororo ambazo nondo dume huzipokea kutoka kwenye umbali wa kuangaza na kutuma ishara zake mwenyewe katika kujibu. Kwa kiasi chochote utakachoweza kutaka wewe kuvuruga mawasiliano haya, hutaweza Mwenyezi Mungu na sifa zake 51 kufanya hivyo. Je, kiumbe huyu mnyonge anabebea aina fulani ya transimita, au huyu nondo dume anacho kinasio kilichojificha kwenye kipapasi chake?

"Senene husugua miguu yake kwa pamoja, na sauti inaweza kusikika kwa umbali wa kilomita moja wakati wa usiku wa kimya na mtulivu. Ili aweze kumwita mwenzi wake, nondo dume huweka tani sitini za hewa katika mwendo na senene jike hupeleka jibu la kusisimua kwa kuposa kwake kwa kwa njia ya kimwili, pamoja na kwamba inavyoonekana hakuna sauti inayosikika kutoka kwake. "Kabla ya kuvumbuliwa kwa radio, wanasayansi walidhani kwamba wanyama waliwasiliana wao kwa wao kwa njia ya harufu. Endapo dhana hii ingekuwa kweli, bado ingekuwa ni jambo la muujiza, kwa sababu harufu ingekwenda kupitia hewani ili iweze kufika kwenye pua za mdudu jike. Hali hii ni mbali kabisa na suala la ama upepo unavuma au hapana na jinsi gani mdudu jike angeipata harufu na kutambua inatoka wapi, na kumwezesha kujua mwenzi wake aliko.

"Leo hii, shukrani kwa njia changaman za hali ya juu za kitaalamu, tumepata uwezo wa kuwasiliana na kila mmoja wetu kwa masafa marefu

1. Biharul-Anwaar, Juz. III, uk. 103-104.

sana. Radio ni uvumbuzi wa kipekee kabisa, unaotuwezesha kuwasiliana mara moja. Lakini matumizi ya uvumbuzi huu hutegemea waya na sisi kuwepo mahali fulani. Nondo bado yupo mbali sana na sisi kwa mbele yetu."[1] Kuchagua sayansi za kimajaribio kama njia ya kuchunguza miujiza ya dunia isiyo na kikomo kuna manufaa mengine ndani yake zaidi ya kuwa karibu na kila mtu. Ni ule utambuzi wa maajabu ya maumbile na utaratibu uliomo ndani yake ambao kwa kawaida humuunganisha mwanadamu na Mwenyezi Mungu Ambaye ameuumba; utambuzi wa aina hii humuonesha binadamu sifa za ukamilifu, ujuzi na uwezo usio na kikomo ambao humuainisha Muumba na Chanzo cha viumbe wote.

Mpangilio huu ulio sahihi unaashira lengo fulani, mpango, hekima pana na kubwa. Ubunifu gani, uwezo gani, ujuzi gani ambao Yeye Ameuwekeza katika dunia yote ya uhai, katika udogo kabisa na ukubwa kabisa wa uumbaji wake wenye kulandana - katika ardhi, katika angahewa, katika maumbile ya ki-mbinguni, katika moyo wa mawe, na kwenye viini vya chembehai! Tunapozungumzia juu ya 'Mpango' lazima ieleweke kwamba fikira hii ya mpangilio inatumika kwa kitu ambapo sehemu zake mbali mbali kwa namna fulani zinahusiana kwa namna ambavyo kwa ulinganifu zinafuatia lengo maalum; ushirikiano wa sehemu hizo lazima pia uwe umezingatiwa. Ingawa wale wanaokanusha kuwepo kwa mpangilio katika ulimwengu kwa ujumla hawakatai kuwepo kwa chanzo hai (kwa vile wanakubali kanuni za usababisho), kinachomaanishwa na kanuni ya ujuzi wa pande mbili katika maumbile ni ile sababu ya msingi, na hii - ikimaanisha kama ifanyavyo kuingilia kati kwa lengo na makusudi kwenye jambo asilia - wao hukataa.

Kwenye Ayah zake nyingi sana, Qur'anii Tukufu inamualika binadamu kutafakari kuhusu mpangilio wa uumbaji ili kwamba watu walio wengi waweze, kwa njia rahisi iwezekavyo, kutambua kuwepo kwa Muumba wa Pekee. Hizi ni baaadhi ya Ayah husika:

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنفَعُ النَّاسَ وَمَا أَنزَلَ اللَّـهُ مِنَ السَّمَاءِ مِن مَّاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِن كُلِّ دَابَّةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيَاحِ وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٦٤﴾

"Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na kuhitilafiana usiku na mchana, na marikebu ambazo hupita baharini pamoja na viwafaavyo watu, na maji aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mawinguni, na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na akaeneza humo kila aina ya wanyama; na mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayoamrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi, bila shaka zimo ishara kwa watu wenye kuzingatia." (Baqarah: 2:164).

اللَّـهُ الَّذِي رَفَعَ السَّمَاوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلٌّ يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَمًّى يُدَبِّرُ الْأَمْرَ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُم بِلِقَاءِ رَبِّكُمْ تُوقِنُونَ ﴿٢﴾

"Mwenyezi Mungu aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona; kisha akatawala kwenye Arshi, na akalitiisha jua na mwezi, kila kimoja

1. Morrison, Raz'i Afarinish, uk. 102-104.

kinaendelea mpaka muda uliowekwa. Yeye ndiye anayeliendesha kila jambo, na anazipambanua Ayah ili mpate kuwa na yakini kukutana na Mola wenu." (Rad: 13:2).

وَهُوَ الَّذِي مَدَّ الْأَرْضَ وَجَعَلَ فِيهَا رَوَاسِيَ وَأَنْهَارًا ۖ وَمِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ جَعَلَ فِيهَا زَوْجَيْنِ اثْنَيْنِ ۖ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٣﴾

"Na ndiye aliyeitandaza ardhi na akaweka humo milima na mito. Na katika kila matunda akafanya dume na jike. Huufunika usiku juu ya mchana. Hakika katika haya zimo Ishara kwa wenye kufikiri." (Rad; 13:3).

Endapo tunakubali na kukimbilia kila nadharia ambayo imewekwa na wataalam na watafiti, hata ile nadharia ya mabadiliko kuhusu kutokeza kwa spishi za aina mbali mbali zinazoonekana duniani, hakuna hata nadharia moja itakayoeleweka bila kuwepo kwa nguvu kamili, uingiliaji kati wa utashi, utambuzi, na lengo na makusudio ya mwisho. Uumbaji wa pole pole katika mpangilio wa maumbile pia unaonesha kwa uwazi uingiliaji kati kwa utashi na utambuzi katika utaratibu wake; hatua zote katika mwendo na maendeleo ya maumbile zimetegemezwa kwenye chaguo na azimio sahihi kabisa, na maumbile kamwe hayajatofautiana kwenye njia yake yaliyowekewa hata kidogo katika mamilioni ya miaka.

Ni kweli kwamba katika hatua za mwanzo za kupata uthibitisho wa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kutoka kwenye mpangilio wa ulimwengu zimetumika kumbukumbu za majaribio, na kwamba sehemu za hoja zimejengwa kwa msaada wa hisia, uchunguzi wa maumbile na uchunguzi wa majaribio. Hata hivyo, kwa kweli hoja hiyo si ya majaribio lakini hasa zaidi ni ya kimantiki, ambayo inatuongozea nje ya maumbile na kutuelekeza kwenye ukweli ulio nje ya uwezo wa binadamu ambao uko mbali na maumbile. Uthibitisho wa majaribio unahusu uhusiano baina ya sehemu mbili za maumbile, ambazo kila moja lazima iwe ya utambuzi wa kihisia ili kuruhusu uhusiano baina ya sehemu hizo mbili kuanzishwa.

Tunapokisia kiwango cha ujuzi na utambuzi wa mtu kwa kupima kazi zake na mafanikio yake, hatupo katika uvumbuzi wa majaribio, kwani kiwango cha ujuzi na akili za mtu sio kitu chenye wingi wa kugusika kwa ajili ya sisi kutegemea majaribio moja kwa moja upande wetu sisi.Bila shaka, mtu moja kwa moja anapata utashi, akili, na fikira ndani ya nafsi yake mwenyewe, lakini huwa hana utambuzi kama huo wa kuwepo kwa vitu hivyo kwa wengine; hawezi kuvifikia.

Tunatambua kuwepo kwa akili na fikira ndani ya watu kwa kuangalia kazi zao na mafanikio yao, ingawaje hakuna uthibitisho wa kimajaribio juu ya kuwepo kwa vitu hivyo ndan ya watu hao. Sasa ugunduzi wa akili ndani ya watu wengine kwa njia ya kazi zao na mafanikio yao, upo kwenye ushahidi wa kimantiki, sio matokeo ya majaribio kwa maana ya akili na kazi zake kuwa vyenye kuvutika moja kwa moja kwenye uchunguzi wa moja kwa moja ili kwamba uhusiano wao uweze kugundulika. Ugunduzi huu pia haupo kwenye ulinganishaji wa kimantiki kwa maana ya kuonesha utambulisho baina ya mtu mmoja na wengine wote.

Ikiwa basi, kwamba utambuzi wa fikira na akili ndani ya watu haufanyiki kwa njia ya uthibitisho wa kimajaribio, ni dhahiri kwamba hoja ya

mpangilio katika ulimwengu na uhusiano wake na chimbuko la ki-Mungu pia haipo katika jamii ya uthibitisho wa kimajaribio.

Kutoka kwenye mtazamo mwingine, kwa kuwa mwanadamu siye muumbaji wa maumbile bali yeye ni sehemu yake, matendo yake katika dunia ya maumbile yanawakilisha kuanzishwa kwa uhusiano baina ya sehemu tofauti za dunia hiyo. Lengo na madhumuni yanayotafutwa na mwanadamu katika ukusanyaji wa mlolongo wote wa elementi za kimaada (kwa mfano, katika kujenga jengo, kutengeneza motokaa, au kiwanda) kuna husiana na nafsi yake mwenyewe, ni kusema kwamba, lengo na makusudio ya mwisho ni mtengenezaji mwenyewe, sio kile kitu kilichotengenezwa. Uhusiano baina ya sehemu ya vile vitu vilivyotengenezwa, kwa hiyo ni uhusiano ambao si wa kimaumbile; kwa kuthibitisha uhusiano huo, mtengenezaji anataka kutimiza malengo yake mwenyewe na kukumbukia mapungufu yake mwenyewe, kwani juhudi zote za mwanadamu ni msongo wa kutoka kwenye uwezekano na kwenda kwenye hali halisi na kutoka kwenye mapungufu kwenda kwenye ukamilifu.

Hata hivyo, sifa hizi mbili hazitumiki katika uhusiano baina ya vitu vilivyoumbwa, na yule muumbaji - Mwenyezi Mungu. Uhusiano baina ya seheMwenyezi mu tofauti na kazi za Mwenyezi Mungu ni wa kimaumbile, na lengo la kiumbe kilichoumbwa halina uhusiano na Muumbaji. Yakiwekwa mbalimbali, makusudio ya matendo ya Mwenyezi Mungu yote yanahusiana na matendo yenyewe, si kwa Wakala, kwa kuwa hekima ya Mwenyezi Mungu inalazimu kwamba Yeye apaswe kusababisha viumbe wote kufikia ukamilifu wao.

Wakati wa kutengenezwa hoja ya mpangilio wa ulimwengu tunajaribu kuthibitisha kuwepo kwa mtengenezaji afananaye na mtengenezaji binadamu, mtengenezaji wa ki-Mungu, kwa kweli, pia atakuwa kiumbe kilichoumbwa kwa kiwango cha mwanadamu; kuthibitisha kuwepo kwa mtengenezaji kama huyo ni jambo tofauti kabisa na kuthibitisha kuwepo kwa Mtengenezaji na Muumbaji wa viumbe wote. Kwa mtazamo wa kisayansi, kujianzisha mwenyewe kwa jambo hakuwezekani; ile nadharia ya ki-Marx kwamba dunia ya kimaada wakati wote anabadilika na kuelekea kwenye hali za juu zaidi ni dhahiri inapingana na kumbukumbu za kisayansi na ukweli wa kimaumbile. Mielekeo yote na misongo katika nyanja ya madini ninatokana ama kwa sababu ya kuingilia kati kwa utashi nje ya vitu au mvutano, kubadilishana, na ukusanyikanaji na maumbo mengine.

Katika ulimwengu wa mimea, maendeleo, kukua na kuongezeka hutokea kama matokeo ya kunyesha mvua, mwanga wa jua na kupata yale madini muhimu kutoka kwenye udongo. Hali ni ile ile kwa ulimwengu wa wanyama. Hali ni ile ile kwa ulimwengu wa wanyama, isipokuwa kwamba hapo kipengele cha mwendo wa hiari kuelekea kile chenye manufaa na muhimu lazima kiongezwe. Katika mifano yote iliyotajwa hivi punde, kuna ushirikiano wa wazi baina ya vitu na viumbe, kwa upande mmoja, na mambo yaliyopo nje yao kwa upande mwingine. Kwa mujibu wa sifa pekee za asili ndani ya kila kiumbe na sheria na kanuni ambazo zinakitawala, haziwezi kukiuka amri ambazo zimepigwa mhuri katika umbile lake.

Ukweli wa kwamba mwanadamu hutambua kwa hisia zake una sifa fulani za pekee. Tunatambua wazi kwamba viumbe katika dunia hii

vinapatwa na mabadiliko ya mara kwa mara na hali ya kutokudumu. Kakita kipindi chote cha kuwepo kwake, kiumbe chochote cha kimaada ama kinakwenda kwa kupitia mkondo wa kukua na kuendelea au kuelekea kwenye kuoza na kudhoofika. Kwa ufupi, hakuna kiumbe cha kimaada katika hatua ya uhai wake kinabakia kama kilivyo na hakibadiliki.

Kuwa na kikomo ni sifa nyingine ya uhai wa kihisia. Kutoka kwenye chembechembe ndogo sana hadi kwenye kundi kubwa la nyota, vitu vyote vinahitaji nafasi na muda; ni kawaida kwamba vitu fulani huchukua nafasi kubwa zaidi au muda mrefu zaidi; na vingine, huchukua muda mfupi zaidi na nafasi ndogo zaidi. Zaidi ya hayo, viumbe vyote vya kimaada vina uhusiano kwa mtazamo wa kuwepo kwao na pia sifa vilivyonazo; sifa yoyote ile kama vile uwezo, utukufu, uzuri na hekima ambazo tunazozitoa kwa vitu, tunafanya hivyo kwa kulinganisha na vitu vingine.

Kutegemea na hali ya kimasharti pia ni miongoni mwa sifa za viumbe hivi. Kuwepo kwa kiumbe chochote tunakowezakutambua kunategemea na ni kwa masharti ya vipengele vingine, na kwa hiyo, kinakuwa kwenye kuvihitajia vipengele hivyo. Hakuna kiumbe kinachoweza kuonekana duniani ambacho kinajitegemea chenyewe tu, ambacho hakina haja na kitu kingine chochote isipokuwa chenyewe tu. Kuhitaji na kutegemea, kwa hiyo, huvizingia viumbe vyote.

Akili na fikara ya mwanadamu vinaweza kuvuka mapazia ya muonekano wa nje, tofauti na hisia zake, na kupenya vina na kadiri za ndani zaidi za kiumbe; vitu hivyo haviwezi kukubali kwamba uhai lazima uwekewe mipaka kwenye viumbe vyenye uhusiano, kikomo, mabadiliko na utegemezi. Kinyume chake, uwezo wa kufikiri kwa dhahiri hutambua umuhimu wa kuwepo, nje ya uwezekano wa kuchunguzika, ukweli thabiti, usiopingika na wenye kujitosheleza ambao juu yake viumbe vingine vinatumainia na kutegemea. Ukweli huu upo wakati wote na mahali popote, endapo haungekuwepo, ukamilifu wa dunia ungekoma kuwepo na ungepoteza ulingano wote wa uhai.

Mara tunapoona utegemezi wa dunia iliyoumbwa na kutambua kwamba hakuna kitu kinachoweza kuwepo bila ya kusaidiwa, tunahitimisha kwamba kuna "Kilichopo kwa Lazima," kwani tunalazimika kuhoji, "ni juu ya kitu gani ambacho kila kiumbe hatimae hutegemea?" Endepo tutajibu, "Hutegemea kiumbe kingine," halafu lazima tuulize, "kiumbe hicho na chenyewe hutegemea nini?" endapo basi jibu litatolewa "Hutegemea kitu ambacho sisi hatujui asili yake," swali linajitokeza, "Je kitu hicho ni cha peke au changamani?"

Kama jibu litakuwa "changamani" halafu tunajibu kwamba changamani pia ni tegemezi juu ya sehemu zake, kwani kwanza kabisa hizo sehemu lazima ziwepo ilihiyo changamani itokee kuwepo. Kwa kuwa maumbile ni changamani, hayawezi kuwa ndiyo 'Kilichopo kwa Lazima.' Kwa hiyo, tunalazimika kusema kwamba kisababisho cha kwanza lazima kiwe peke. Pia lazima kiwe ndani ya mpaka au maana moja na kile 'Kilichopo kwa Lazima,' kwani mlolongo wa kisababisho hauwezi kuendelea bila mpaka.

Ujumla wa dunia, kwa hiyo, unahitaji ukweli ambao unajitegemea na ambao humo ndimo vitu vyote vyenye masharti, ukomo na uhusiano vinamotegemea. Vitu vyote vinauhitaji ukweli huo ili kuvijaza uhai, na

viumbe vyote vyenye uhai vinakuwa na dalili ya uhai wake wa milele, ujuzi, uwezo na hekima. Kwa hiyo, vinaturuhusu sisi kupata ujuzi wenye manufaa kuhusu ukweli huo na kumwezesha kila mtu aliye na akili, mdadisi kufasiri kuwepo kwa Muumbaji.

Kutegemeana kwa pande mbili kwa maada na kanuni za uhai kwa namna yoyote ile hakuelekezi kwenye kujitegemea kwa vitu vya kimaada. Kinyume chake, mambo tofauti yanayotokea kwenye maada, pamoja na uhusiano wao wa karibu, yanaonesha kwamba maada, katika namna yake ya maisha, hulazimika kukubali na kufuata kanuni fulani na desturi ambazo huyasukuma kwenye utaratibu na uelewano. Uhai unategemea juu ya vipengele viwili muhimu. Maada na utaratibu, ambavyo vinahusiana kwa karibu sana na huzaa dunia inayoeleweka na yenye utulivu. Baadhi ya watu huchukulia maada kama yenye kujitegemea na hudhania kwamba yenyewe imepata uhuru huu na kufafanua zile kanuni ambazo zinaitawala. Lakini ni vipi wanaweza kuamini kwamba haidrojeni na oksijeni, elektroni na protoni, zipaswe kwanza kujizalisha zenyewe, halafu ziwe chanzo cha viumbe vingine vyote, na hatimaye kuamuru kanuni zinazojirekebisha zenyewe na ulimwengu wote wa maada?

Uyakinifu unadhania kwamba vitu duni ndio chanzo cha kutokeza vitu vya hali ya juu bila ya kusumbuka kuhakikisha kama kile kitu cha hali ya juu kwa kweli, kinakuwepo katika kiwango cha kile duni. Kama mata ya kiwango duni haiwezi - hata katika kiwango cha juu sana cha maendeleo yake yaani fikra na tafakuri - ama kujiumba yenyewe au kukiuka mojawapo ya kanuni ambazo hutawalia juu yake, kwa hiyo ina maana isiopingika kwamba haiwezi kuumba viumbe vingine na kanuni zinazovirekebisha. Ni vipi, basi inaweza kuaminika kwamba mata duni ingejishughulisha katika uumbaji na uanzishaji wa viumbe vya hali ya kiwango cha juu au kuwa na uwezo wa kutoa uhai kwa vitu vya juu sana? Katika sayansi mpya ya mifumo, kanuni imethibitisha kwamba mifumo yenye elementi zenye uhai ambazo zina lengo au mifumo iliyopangika kwa nje kwa msingi wa programu iliyowekwa, zinaweza kuendelea kwenye mwelekeo wa kupanuka, utaratibu mkubwa zaidi na uboreshaji. Hata hivyo, mifumo yote, ama ya peke au changamani, inahitaji kusaidiwa na, na kuhusishwa na vipengele vya nje yao yenyewe, haziwezi kujijenga zenyewe. Hakuna mfumo au kitu humu duniani kitakachoweza kuumba au kutia utashi kwenye kiungo kinachotembea na kukua isipokuwa kiwe kina kiwango fulani cha dhamira na ufahamu.

Yakiwa yametegemezwa kwenye kanuni ya uwezekano, matokeo ya hamasa huru ya fani zote yanaweza kuwa tu ya mtawanyiko na vurugu, yakielekea kwenye kifo cha namna moja. Kanuni ya uwezekeano pia inakanusha wazi wazi kutokea kwa dunia kwa njia ya kubahatisha, na kuiona kuwa haina mantiki na haiwezekani. Hata makadirio yaliyofanywa kwa msingi wa kanuni ya kimahesabu ya uwezekano yanathibitisha umuhimu wa mwongozo ulio sahihi na upangaji kwa ajili ya dunia, kwa kukubaliana na programu iliyo sahihi na dhamira ya fahamu.

Kwa kweli kanuni ya uwezekano inatoa pigo la uhakika kwa wale wanaoamini nadharia ya kutokea kwa dunia kwa bahati. Endapo tutajaribu kutumia nadharia ua ajali kwenye mfumo wa kawaida au tarakimu ndogo,

utumikaji wake ni wenye kuwezekana, ingawaje hauelekei kabisa. Lakini haieleweki kwamba mtu aweze kubahatisha kamwe kwa njia ya ajali ya kijometri kuelezea mpangilio imara na wenye utulivu uliopo kwenye mfumo changamani wa dunia. Mabadiliko ya kiasi na ya kawaida kwenye mpangilio wa maisha pia hayawezi kuuelezea mgeuko wa dunia; muungano wa elementu zilizo tofauti, na mchanganyiko wa chembechembe za asili kuunda mchanganyiko unaowiana.

Ikiwa kama wakati fulani maumbile yalijishughulisha kwa kujitawala katika kazi za sanaa na utengenezaji, kwa nini sasa hayaonyeshi hatua yoyote katika mwelekeo wa kujibadilisha yenyewe zaidi ya hapo; kwa nini hayaonyeshi tena mabadiliko makubwa yanayojiendesha yenyewe? Hata matukio madogo na ya kawaida hapa duniani husababishia uumbikaji wa sura za kipekee ambazo zinawiana na kuafikiana na lengo la maumMwenyezi bile.

Hii peke yake, yenyewe ni dalili ya ule ukweli kwamba nyuma ya mabadiliko yote makubwa, kuna nguvu makini na yenye uwezo mkubwa inayojishughulisha katika kuumba na kuzalisha mpangilio wa maajabu ya ulimwengu: inatoa umbo kwenye udhahiri wa kipekee wa dunia ya maumbile na kuashiria mpango na utaratibu wa uhai.

Uwiano na upatanishikaji wa mamilioni ya vitu vya maumbile na uhusiano wao kwenye uhai unaweza kuelezwa juu ya msingi wa nadharia moja tu - yaani kwamba tunamtambua kuwepo kwa Muumbaji juu ya mfumo huu mpana Ambaye ameasisi chembe zinazotofautiana za uhai juu ya duniani hii kwa njia ya uwezo usio na mipaka na ukomo na kutayarisha programu kwa ajili ya kila mojawapo ya chembechembe hizo za uhai. Nadhari hii ni kwa kulingana na uhusiano mtulivu ambao tunaouona umewekwa ndani ya viumbe.

Kama hatutakubaliana na nadharia hii, upo uwezekano gani kwamba utulivu wa aina hii ungetokea - ki-ajali na bila madhumuni - miongoni mwa taratibu nyingi za uhai? Ingeaminikaje kwamba mata yenyewe iwe chanzo cha mamilioni ya sifa na tabia na kwa hiyo kuwa inayolingana na Muumbaji mwenye madhumuni, hekima na mjuzi wa yote? Endapo dunia ya uhai isingekuwepo, pamoja na maajabu yake ambayo yanastaajabisha akili na uzuri ambao ujuzi wa mwanadamu hauwezi kufahamu kikamilifu, na endapo ulimwengu ungekuwa na kiumbe cha seli moja tu hai, bado uwezekano kwamba kitu kidogo na kisichokuwana thamani, pamoja na mpangilio uliopo juu yake na hali ya lazima na vifaa kingekuja kuwepo kama bahati tu, uwezekano, ajali, uwezekano kama huo unaashira, tarakimu ndogo sana ambayo haiwezi kueleweka kimahesabu, kwa mujibu wa bingwa wa baiolojia Mswisi aitwaye Charles Unguy.

Chembe zote za viumbe hai, katika maumbo yao ya ndani na uhusiano wao, zinategemea mpangilio ulioimarika. Kujengeka kwao na uhusuano uliopo baina yao ni wa namna ambayo husaidiana zenyewe ili ziendelee kwenye njia zao husika hadi kwenye malengo yaliyoko mbele yao. Zikinufaika kutokana na uhusiano zilionao kwa viumbe vingine hai na kutokana na kuambukizana athari kwao kama livyodhamiriwa na uundwaji wao wenyewe, zina uwezo wa kuelekea kwenye malengo na mwisho wa safari yao.

Mafanikio makubwa ya sayansi ya maada ni kutambua sura na sifa za nje za dunia; kutambua asili na mumbile hailsi ya viumbe vilivyoumbwa na matukio kupo nje ya upeo wa uelewa wa sayansi hizo. Mathalani, mafanikio makubwa sana ambayo mnajimu anaweza kupata, ni kujua kama mabilioni ya matufe kule angani hayabadiliki wa kusogea kwa sababu ya kani-pewa au kama yanaendelea kubiringika ambapo nguvu ya uvutano huyazuia yasigongane na kudumisha utulivu wao. Inaweza pia kupima umbali wao kutoka hapa ardhini na kasi ya mwendo wao na ukubwa kwa njia ya zana za kisayansi. Hata hivyo, hatima ya matokeo ya ujuzi huu wote na majaribio hayavuki upeo wa tafsiri ya nje na ya juujuu ya vipengele vya maumbile, kwani mnajimu (bingwa wa elimu ya anga) hawezi kutambua asili halisi ya nguvu ya mvutano, chimbuko la kani-pewa au namna ya jinsi zilivyo na ule mfumo ambao zinauatumikia vilivyojitokeza kuwepo.

Wanasayansi wanaweza kutafsiri mashine bila kutambua tafsiri ya hiyo nguvu mwendo. Sayansi asilia vivyo hivyo hazina uwezo wa kutafsiri na kuchanganua mamilioni ya mambo ya ukweli ambayo yamewekwa katika maumbile na ndani ya mwanadamu. Mwanadamu amechimba kwenye kiini cha chembe lakini ameshindwa kupata ufumbuzi wa miujiza migumu na iliofichika ya chembe hai moja. Kwa ufupi, ni ngome hizi za miujiza ambazo mabingwa wa sayansi asilia wamekuwa hawana uwezo wa kuzishinda.

Mojawapo ya maajabu ya maumbile ni ule uwiano wa maafikiano uliopo baina ya vitu viwili ambavyo sio vya wakati mmoja. Ulinganifu huu ni wa hali ambayo kwamba mahitaji ya kitu ambacho bado hakijatokeza na kuwepo, tayari yameandaliwa kwenye umbile la kitu kingine. Mfano mzuri wa aina hii ya uwiano unaweza kuonekana kwenye uhusiano baina ya mama na mwana. Miongoni mwa binadamu na mamalia wengine, mara mwanamke anapobeba mimba na jinsi kilenge kinavyokua ndani ya nyumba ya uzazi, tezi ambazo hutengeneza maziwa - aina nzuri na changamani ya lishe - huanza kufanya kazi kwa mvuto wa homoni maalumu. Jinsi kilenge kinavyoendelea kukua, ndivyo lishe hii yenye virutubisho inavyoongezeka wingi wake ili kwamba pindi kilenge kinapokuwa kwenye mlango wa kizazi na kipo tayari kuingia katika dunia hii pana isiyo na mipaka, kirutubisho hiki kinachohitajiwa na mtoto na kinachofaa kwa mahitaji yake yote ya kimwili kinakuwa kipo tayari.

Kirutubisho hiki kilichokwishatengenezwa tayari, kimepatanishwa kabisa na mfumo ambao bado mchanga, wa kusaga chakula wa mtoto. Kimehifadhiwa kwenye ghala iliyofichika - titi la mama, ghala ambayo alipewa mama miaka mingi kabla kichanga hakijapata umbo. Ili kuwezesha ulishaji wa mtoto alliyezaliwa mara, vijitundu vidogo na laini vimewekwa kwenye chuchu za titi lenyewe - kwa kipimo kinacholingana na mdomo wa mtoto - ili maziwa yasitiririke moja kwa moja kwenye mdomo wa mtoto ambaye kwa wakati huo hana uwezo wa kuyameza mwenyewe. Badala yake mtoto anayapata riziki ya kila siku anayoihitaji kutoka kwenye hazina hiyo kwa njia ya kunyonya.

Jinsi mtoto aliyezaliwa anavyozidi kukua, ndivyo mabadiliko yanavyofanyika kwenye maziwa ambayo yanaunganishwa na umri wake. Ni kwa sababu hii kwamba madaktari wa tiba wanaamini kwamba

kunyonyeshwa mtoto mchanga aliyezaliwa punde na mama mwingine ambaye siye aliyemzaa, wakati mwingine si jambo la busara kushauriwa. Hapa swali linajitokeza; si kweli kwamba mahitaji ya kiumbe kutengenezwa kwenye umbile la kiumbe kimoja, kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kiumbe kingine ambacho bado hakipo, ni jambo ambalo kimepangwa na kutabiriwa kwa msingi wa hekima na usahihi? Je, sio kwamba matayarisho haya kwa ajili ya siku zijazo, uhusiano huu wa kistadi na wa kushangaza baina ya viumbe viwili, ni kazi ya nguvu yenye uwezo na hekima isiyo na mfano? Si kwamba hii ni dalili ya wazi ya kuingilia kati kwa nguvu isiyo na kikomo, mbunifu na mpangaji mkuu, ambaye makusudio yake ni kuendeleza uhai na kukua kwa vitu vyote kuelekea kwenye ukamilifu? Tunatambua vizuri kwamba mahesabu sahihi tunayoyaona kwenye misingi ya mashine zote na zana za viwandani ni matokeo ya vipaji na fikra zilizoingizwa kwenye usanifu na utengenezwaji wao. Vivyo hivyo, kwa kutegemea uchunguzi wetu wa busara tunaweza kufikia uamuzi wa jumla wa kifalsafa kwamba popote pale ambapo mpangilio na ukusanyaji unaotegemea uwiano na makadirio unapotakiwa kufuatwa, dhamira, akili na mawazo lazima pia vitafutwe.

Usahihi huo huo ambao unaweza kuonekana kwenye mashine za viwandani ndio utakaoonekana katika kiwango cha juu zaidi na kipekee katika viumbe asili na uumbwaji wao. Hakika kiwango cha maandalizi na mpangilio unaoonekana kwenye maumbile upo katika daraja ya juu sana hivyo kwamba usahihi alioumaliza mwanadamu katika ubunifu wake hauwezi kwa hali yoyote ile kulinganishwa nacho. Wakati bila kusita, tunapotambua kwamba utaratibu wetu wa viwanda ni matokeo ya fikira na mawazo, hatupaswi sisi kuutambua utendaji wa akili isiyo na kikomo, dhamira na ujuzi uliopo kwenye mpango sahihi wa maumbile?

Katika zama hizi, elimu ya madawa imefika katika kiwango cha maendeleo ambacho kinakiruhusu kuondoa figo kutoka kwenye mwili wa binadamu na kuipandikiza kwenye mwili wa mtu ambaye figo zake zimekwama kufanya kazi na ambaye anakaribia kufa. Maendeleo haya kwa uhakika si matokeo ya juhudi ya daktari moja pekee; hii inatokana na urithi wa milenia kadhaa. Shughuli ya upandikizaji sasa ndio hatua ya mwisho katika mlolongo mrefu ambao hatua zake za mwanzo zilikamilishwa na wanasayansi wa siku za mwanzo; mawazo na utambuzi wa wanasayansi yalikuwa yakusanywe kwa miaka elfu kadhaa kabla ya kupandikiza figo kuweza kutokea.

Je, inawezekana kwamba matokeo haya yaweze kupatikana bila ujuzi? Bila shaka hapana: akili za binadamu uwezo mkubwa zililazimika kufanya kazi kwa miaka elfu kadhaa ili upandikizaji wa figo upate kuwezekana. Sasa na tuulize swali jingine. Ni lipi linahitaji ujuzi mwingi na akili zaidi: ni kubadilisha tairi kwenye gurudumu la gari - kazi ambayo inahitaji kiasi fulani cha ufundi stadi - au utengenezaji wa tairi lenyewe? Kazi ipi iliyo ya umuhumu: kutengeneza tairi au kubadilisha tairi? Ingawaje kupandikiza figo ni kazi muhimu katika tiba, inafanana na kubadilisha tairi kwenye gurudumu la motokaa; kazi hii inakosa umuhimu ikilinganishwa na ile ya kutengeneza umbo la figo yenyewe na ile miujiza, ustadi na mahesabu iliyonayo.

Mwanasayansi gani halisi, aliyetawaliwa na uaminifu katika kutafuta ukweli anayeweza kudai leo hii kwamba, wakati ambapo upandikizaji wa figo ni matokeo ya mfululizo wa utafiti wa majaribio ya kisayansi ya karne nyingi, umbo la figo yenyewe halioneshi dalili ya akili bunifu na dhamira, kuwa ni matokeo ya maumbile tu - maumbile yasiyo na ujuzi zaidi au utambuzi kuzidi mwanafunzi wa shule ya chekechea?

Haitakuwa na mantiki zaidi kuweka nadharia ya kuwepo kwa akili, dhamira na maandalizi katika uumbaji na utaratibu wa ulimwengu kuliko kuhusisha uumbaji kwenye mata kitu ambacho hakina akili, mawazo, umakini na uwezo wa kuanzisha mambo mapya? Imani juu ya kuwepo kwa muumbaji mwenye hekima bila shaka ina mantiki zaidi kuliko kuamini katika ubunifu wa mata, kitu kisichokuwa na ama utambuzi, umakini wala uwezo wa kupanga, hatuwezi kuzihusisha kwamba zitokane kwenye maada, tabia na sifa zote za akili tuzionazo hapa duniani na utashi wa mpangilio inaouonyesha.

Mufadhal alimwambia Imam Sadiq (a.s): "Bwana! baadhi ya watu hudhani kwamba huu utaratibu na usahihi tuuonao hapa duniani ni kazi ya maumbile." Imamu akamjibu: **"Waulize kama maumbile hufanya kazi zake zote zilizokadiriwa kwa usahihi kwa mujibu wa elimu, mawazo na uwezo wake yenyewe. Kama watasema kwamba maumbile yana elimu na uwezo, kuna kitu gani kinachozuia wao kupinga lile chimbuko la milele la ki-ungu na wakakiri kuwepo kwa hiyo kanuni kuu? Endapo kwa upande mwingine watasema kwamba maumbile hufanya kazi zake kwa kawaida na kwa usahihi bila matumizi ya ujuzi na utashi basi kinachofuata ni kwamba shughuli zote za hekima na zilizo sahihi, sheria zilizopangwa vizuri ni kazi ya muumbaji mjuzi na mwenye hekima. Kile ambacho wao wanakiita maumbile, kwa kweli, ni sheria na kawaida zilizowekwa na mkono wa uwezo wa ki-mungu ili zitawale maumbile."**[1] Ustadi wa maumbile.

Mfikirie mbu wa malaria. Hakuna haja ya kutumia darubini; unaweza kutambua mpangilio sahihi na changamano uliomo kwenye kiumbe kile kisicho na thamani kwa matumizi ya kawaida ya jicho tupu. Ndani ya kiumbe hiki dhaifu mnakuwemo na seti kamili ya viungo na milango ya fahamu, ya kipekee kwa usahihi wao: mfumo wa kusaga chakula tumboni, mfumo wa mzunguko wa damu, mfumo wa neva, mfumo wa kupumua. Mbu anayo maabara iliyoandaliwa kwa vifaa: kwa usahihi na kasi ya ajabu, itengeneza vitu vyote anavyovihitaji. Mlinganishe mbu na maabara ya kisayansi: pamoja na nguvu zote za kibinadamu na kiuchumi zilizomwagwa juu yake, maabara hiyo haiwezi kamwe kupata kasi, umakini na usahihi wa maabara inayodharaulika ya mbu. Ni muda kiasi gani, tafakuri na akili vinavyohitajika, kwa mfano, kutengeneza tiba kwa ajili ya ule uumaji wa mbu tu!

Wakati ambapo upangaji mwingi, mawazo na usahihi vinahitajika kwa mtu kufanya kazi kama hii, hivi huu ustadi, usahihi na utaratibu unaoonekana duniani, sio uthibitisho wa chimbuko linalotokana na akili, maandalizi bunifu na busara ya kiwango cha juu ya huyo muumbaji? Hivi

1. Biharul Anwar, Juz. II, uk. 21.

inawezekana hata kidogo kufikiria jometri yote sahihi, utendaji wa mwendo wa ulimwengu kuwa ni matokeo ya mata, na kukosa elimu kwake? Tunatamka kwa dhati kabisa kwamba jambo la maumbile linaonyesha mpangilio na utaratibu; haya hayatangazi kutokuwa na lengo, vurugu na machafuko.

Endapo nyakati fulani tunaona dalili za dosari katika maumbile hii haina maana ya kuwepo kwa upungufu au kasoro kwenye kitabu kikubwa cha uumbaji. Fikira na utambuzi wetu haviwezi kupaa na kuruka angani na uwezo wa akili zetu ni mfupi mno kuweza kuelewa miujiza na vitendawili vyote vya ulimwengu. Akili zetu haziwezi kuvumbua azma na malengo yote ya uhai. Kama hatuwezi kuelewa kazi ya skrubu ndogo kwenye mashine kubwa, sasa basi, hali hii inatupatia sisi haki ya kumshutumu na kumlaani mbunifu kwamba ni mbumbumbu? Au ni kwamba upeo wetu wa kukodoa macho ni mfinyu mno kuweza kuelewa lengo na madhumuni halisi ya mashine hiyo?

Bahatisho haliwezi kufanya kazi ya elimu, elimu, ambayo zaidi ya hayo, haikuchanganyika na ujinga kwa hali yoyote ile. Ikiwa, kama wayakinifu wanavyodhani, dunia ya maumbile haikutokana na elimu na utashi (licha ya dalili za uumbaji na ubunifu unaoonekana wazi katika kila kiumbe) halafu, mwanadamu pia ili aweze kufanikisha malengo yake atalazimika kuacha maendeleo yake kwenye mkondo wa elimu na kujifunga mwenyewe kwenye ujinga ili aweze kutenda kufuatana na kule kutokujitambua kwa maumbile yenyewe. Ile hali halisi inayoongoza na kuelekeza utendaji wa dunia kwa utaratibu na mpangilio wa namna hiyo una lengo, madhumuni na dhamira, mambo ambayo hayawezi kukanushwa. Haiwezi kudhaniwa kwamba mlolongo wa utendaji usiokatika na athari zake huendelea kuelekea upande maalum bila uingiliaji na uangalizi wa akili fulani.

Baada ya miaka mingi ya maandalizi yaliyofanywa kwa uangalifu na kazi ya kuchosha mabingwa wa sayansi ya biokemia wamefaulu katika kugundua mfumo fulani wa majaribio katika kiwango cha kawaida na cha chini ambao kutoka humo dalili zote za uhai zinakosekana. Ushindi huu wa kisayansi ulionekana kuwa na manufaa sana na ulipokelewa kwa shauku kubwa katika duru za kisayansi, na hakuna mtu aliyedai kwamba uumbaji huu wa maabara wenye upungufu mkubwa na wa kiwango cha chini sana uliotokeza kuwepo kama matokeo ya bahati, bila ya mwelekeo, maandalizi na usahihi.

Hali ikiwa ni hivi, wale wanaohusisha viumbe vyote viliyomo kwenye mfumo mpana wa ulimwengu, pamoja na sifa zake changamani na za kimwujiza kwenye nguvu povu na zisizo na fahamu za mata, kwa kweli wanaifanyia vurugu na udhalimu mantiki na akili ya binadamu na kuendesha vita vya wazi dhidi ya ukweli. Weka mazingatio yako kwa dakika moja tu juu ya mtayarishaji wa chapa kwenye kiwanda cha uchapishaji. Yeye anachukua hadhari na uangalifu mkubwa anapozipanga herufi zinazotakiwa kwa ajili ya ukurasa mmoja wa kitabu, lakini anapoirudia kazi yake, anakutana na makosa madogo madogo yatokanayo na kukosa umakini kidogo tu. Mtayarishaji wa chapa angekuwa achukue herufi chache kiganjani na kuzisambaza kwenye bamba badala ya kuzipanga kwa uangalifu katika mistari, je, itawezekana kwa vyovyote vile kwamba

ukurasa utakaotokea uweze kuwa sahihi katika maudhui na kutokuwa na kosa lolote?

Itakuwa bado ni upumbavu zaidi kudai kwamba kila mia moja za risasi iliyoyeyushwa, ikashindiliwa kwenye tyubu, itatokeza katika hali ya herufi ambazo zimetengenezwa tayari; na kwamba dhoruba kali iweze kuzichukua herufi hizo na kuzipanga kwenye mpangilio na utaratibu maalum unaokubalika, kwenye maelfu ya mabamba ya chuma, na kwamba mabamba haya yaishie kwenye kuchapishwa kitabu chenye kurasa elfu moja chenye maudhui nyingi sahihi za kisayansi na maelezo ya kuvutia na kushawishi, yote haya yafanyike bila hata kosa dogo kutokea. Kuna mtu yoyote anayeweza kuiunga mkono nadharia hii?

Wayakinifu ambao hukanusha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu wana nini cha kusema kuhusu kutokeza kwa maumbo tofauti ya herufi za maumbile na uhusiano ulio sahihi na changamani ambao hudhibiti viumbe vya mbinguni, maumbile asilia na vitu vyote vya kimaada? Je, herufi za maumbile (yaani atomu na chembechembe zinazoziunda) zinaweza kuwa hazina maana kuliko herufi zitumikazo katika uchapishaji? Inawezekana kukubalika kwa namna yoyote ile kwamba hizi herufi zenye mpangilio na maana, jometri hii iliyo sahihi na iliyoandaliwa vizuri maumbo ya kushangaza yanayofafanuliwa kwenye kitabu cha uumbaji, iwe ni kazi ya kijinga na isiyo na malengo? Kwamba nguvu kuu na yenye hekima, kanuni ya mpangilio ya kimwujiza, isiwepo kwenye muonekano wenyewe wa dunia? Je, mambo yote sio kwamba yanachipukia kutokana kudhihiri kwa ufahamu, utambuzi na uwezo?

Endapo uwezo uliofichika kwenye vina vya mata hautokani na akili ya fani zote, ni jambo gani linauongozo kwenye ufafanuzi wa maumbile, kwenye utaratibu na uwiano wa kushangaza? Ikiwa uwezo huo ni wakala asiye na akili na fahamu, kwa nini basi haujaangukia kamwe kwenye vurugu, na kwa nini mchanganyiko wake wa mata kamwe hausababishi mgongano na maangamizi? Hapa ndipo ambapo imani ya kuwepo kwa muumbaji inaleta maana juu ya maada yote na hujaalia dunia kuwa na maana na kutosheka. Wale wenye mtazamo wa mbali na fikra safi za wazi hutambua dhahiri kwamba uwezo usio na ukomo ndio unaohakikisha utunzaji wa mpangilio wa dunia kwa njia ya usimamizi ulio madhubuti na mamlaka kamili.

Zamani, kila mtu alikuwa akimwongoza na kumdhibiti mnyama wake wa kipando, na vile vile alikuwa na desturi, katika zama zote, ya kumuona mmiliki au msimamizi anayesimamia sehemu ya rasilimali, kila kipande cha ardhi isiyotumika, kila kundi au chama. Sasa mambo yamebadilika. Mwanadamu wa kisasa anaweza kutengeneza setilaiti inayoendeshwa toka mbali, ala za elektroni na ndege zisizo na rubani, vyote hivi vikiwa vimetayarishwa kwa vifaa vinavyojiendesha vyenyewe. Kila mtu anajua kwamba inawezekana kutengeneza mashine yenye vifaa vyote ambayo inaweza kufanya kazi kwa namna nyingi zinazofaa kwenye hali yoyote itakayojitokeza, bila mtengenezaji wa chombo hicho kuwepo au kuonekana. Kwa hiyo, hatuna tena haki ya kukataa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kwa ukaidi tu kwa sababu mkono Wake hauonekani haufanyi kazi kwa

kuonekana katika mambo ya uumbaji - kwa kuonekana, yaani kwa uelewa na elimu yetu yenye upungufu.

Kwa kweli, ungekuwa ni ufananishaji wenye upungufu mkubwa endapo tungemlinganisha mtengenezaji setilaiti au roketi bandia, ambaye ameketi kwenye kituo chenye vifaa vyote hapa ardhini na kwa msaada wa vifaa changamani anaongoza na kudhibiti njia na mwendo wa chombo cha angani. Lakini kama uingiliaji kati wa mkono wa Mwenyezi Mungu kwenye mpangilio wa maumbile hauonekani kwa jicho letu la kawaida na utambuzi wetu (ingawaje tunaweza kuona dalili na ishara ambazo zinafanana na mwale unaoendelea kutoka kwenye fahari ya utukufu wake) tunaweza kwa sababu hiyo kutotilia maanani kuwepo kwa mpangaji na mwendeshaji ambaye peke yake ndiye elimu ya dhati, uwezo na utashi halisi, kwa sababu tu kwamba hawezi kudhibitiwa ndani ya mfumo finyu wa muda na nafasi.

Ni kweli kwamba uwezo wetu wa kuelewa nafsi ambayo haifanani wala haina mfano na chochote katika himaya ya hisia na ambayo lugha ya kibinadamu haiwezi kuieleza kikamilifu na kwa usahihi ni mfinyu sana. Taa ya akili zetu hutoa mwanga mdogo kwenye uwanda huu usio na ukomo, au - kwa lugha nyingine tofauti - unakabiliana na kuta za mipaka. Wakati huo huo uhusiano wetu katika dunia hii upo juu ya matukio; lile ambalo litajiingiza lenyewe kwenye akili zetu linakuwa na miali ambayo hugunduliwa na kaida za dunia yenye busara. Lakini katika kuitambua dunia hiyo, tatizo la kuidhania linaondolewa kwetu; hakuna kipingamizi kilichopo baina ya fikira zetu na kile kiasi muhimu cha ufahamu.

Hata hivyo, watu fulani wenye kushuku ambao wameutelekeza mtindo thabiti wa fikra ambao unatokana na asili ya msingi ya mwanadamu na ambao wamekuwa, kimipaka kabisa, na mazoea ya uhai wenyewe hasa wa maumbile wakati wote wakingojea kutokea muujiza kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambao utavunja utaratibu uliopo wa muumbo ili kufanya zawadi kwao ya itikadi na imani, na kufanya kuwepo Kwake (Mwenyezi Mungu) kueleweka na kukubalika bila kusita. Hata hivyo, watu hao hawatilii maanani kwamba dalili na ishara zozote mpya za Mwenyezi Mungu zinazoweza kutokea zitasababisha msisimko mashaka ya muda tu, na kwa kupita muda, yatakuwa mambo ya 'kawaida' na hayatavuta nadhari tena.

Ingawa mambo yote sasa yamejumuishwa kwenye muundo wa mpangilio wa maumbile, yalianza kwa kuvunja mpango wa asilia, na kwa kuwa viumbe vyote vimerudiwa katika hatua za dunia tangu kudhihiri kwa mara ya kwanza, sasa vinaonekana kuwa vya kawaida na kuzoeleka. Kinyume chake, kiumbe kisichoweza kutambulika kihisia - kiumbe, ambacho zaidi ya hayo kimejaa fahari na utukufu na kilichojaa utakatifu na ukuu - kila mara kitavutia roho za wanadamu. Mazingatio yao kwa kiumbe kama hicho, kwa kweli kila wakati utaongezeka na wakati wote watakiangalia kwa kuhitajia.

Ni kutawaliwa na nafsi ya ukaidi, ya uamuzi uliotengenezwa kwenye mantiki isiyopatana, ambayo huifungia fikira ya kibinadamu kwa mipaka. Kwa kila kiumbe katika mpangilio wa kuwepo ni uthibitisho unaotosha kwa ajili ya wale wanaobana na kuweka tupu akili zao za ukaidi na sababu za ukanushaji.

6

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA SITA

### HAJA YA ULIMWENGU KUMHITAJI YULE ASIYEHITAJI CHOCHOTE

Kanuni ya usababisho ni ya kawaida na fani zote na msingi wa juhudi zote za mwanadamu, katika kutafuta elimu na katika shughuli zake za kawaida vilevile. Jitihada za wanazuoni kuvumbua sababu za kila jambo, ama liwe la kimaumbile au la kijamii, hutokana na imani kwamba hakuna kitu kinachojianzisha ndani yake, au chenyewe tu bila sababu na asili kuingilia kati.

Utafiti wa wanafikra duniani pote umewapa wao uwezo wa kufahamu vizuri zaidi mpangilio wenye nguvu sana wa maumbile; jinsi wanavyozidi kusonga mbele kwenye mkondo wa maarifa ndivyo wanavyozidi kujifunga kwenye kanuni ya usababisho. Kiungo baina ya sababu na athari, na kanuni kwamba hakuna kitu kitakachotokea chenyewe kwenye uwanja wa uwepo bila sababu, ni miongoni mwa maamuzi yenye nguvu sana ambayo yamepata kufanywa na mwanadamu na kuthaminiwa kama sharti la kimsingi kwa shughuli za kitaalamu. Yanawakilisha kitu ambacho ni kawaida na cha asili, kinachofyonzwa na akili zetu moja kwa moja bila kukwepa.

Hata mwanadamu aliyeishi kabla ya historia kuanza kuandikwa alielekea kugundua sababu za mambo, na kwa kweli, wanafalsafa waliipata dhana hai ya uhusiaino kati ya sababu na athari kutoka kwenye asili yenyewe na silika ya mwanadamu kabla ya kuiweka katika kalibu (chungu) ya kifalsafa. Kufungiwa kama tulivyo kwenye kuta nne mata, hatukabiliani kamwe na kitu chochote cha kutuka chenyewe kwenye uhai, na kwa kweli, hakuna hata mtu mmoja aliyewahi kamwe kukabiliana, katika historia ya ulimwengu, na kutuka kwa jambo ambalo halitokani na sababu. Kama hali isingekuwa hivyo, tungeweza labda kuwa kisingizio cha kuufikiria ulimwengu kuwa ni kitu cha kutuka chenyewe katika asili yake. Itakuwa ni aina gani ya kutuka kiajali ambako tangu mwanzo wa kuwepo kwa uhai hadi sasa, kumeongoza muingilano huo usiopimika wa vitu vyote, katika mfumo na mtindo wa kushangaza kiasi hicho? Je, inawezekana mpangilio huu tunaoufahamu ukawa ni kuakisi kwa jambo la kutuka na sadifa ya hivi hivi tu?

Kitu chochote kinachoweza kudhaniwa hapa ulimwenguni kilikuwa kimezamishwa kwenye giza la kutokuwepo kabla hakijapata umbile la kiumbe. Hakiwezi kupenya giza la kutokuwepo na kujitokeza kwenye uwanja wa uhai kama kitu kilichopo hadi mkono wa kisababisho wenye uwezo mkubwa uingie kazini.

Uhusianao baina ya chanzo na athari ni uhusiano baina ya vitu viwili vilivyopo, kwa maana kwamba kuwepo kwa kimoja chao kunategemea juu ya kuwepo kwa kile kingine. Kila athari ina uhusiano wa mvuto na uwiano na chanzo chake, kwa kuwa athari hupata kuwepo kwake kutoka kwenye

chanzo. Uhusiano huu maalum hauwezi kuharibiwa au kubadilishwa na mwingine.

Wakati wowote unapofikiria asili ya kitu chenye uhusiano wenye kufanana kwa kiumbe hai na kisichokuwa hai, na vyote vikiwa hakuna ambacho ni muhimu kimsingi kwa ajili ya kitu hicho, kitu hicho huitwa 'dharura' kwa maana kwamba hakuna chochote katika asili yake kinachosababisha ama uhai au kutokuwa hai. Kama kitu katika asili yake kinahitaji kutokuwa hai kwake, basi kuwa hai kwake hakuwezekani. Hatimaye, endapo uhai utajitokeza kutoka ndani ya asili ya kitu kwa namna ambayo kwamba akili haiwezi kukiona kwamba ni tegemezi kwa kitu kingine chochote, uhai wa kitu hicho unafanywa kuwa muhimu. Ni kiumbe hai kinachojitegemea, kisichohitaji chochote na kinajikimu kwa njia za asili yake binafsi, kuwepo kwake ndicho chanzo cha viumbe vingine vyote ambapo chenyewe hakitawaliwi na haja au hali yoyote.

Inapaswa kuongezwa hapa kwamba kuwepo kwa maada hakuwezi kupata sifa ya "muhimu" kwa sababu kuwepo kwa kitu chochote cha mchanganyiko wa maada kunategemea kuwepo kwa sehemu zinazokiunda kitu hicho; kinakuwa ni tegemezi juu ya sehemu zake chenyewe kwa ajili ya chanzo na kuendelea kwa uhai wake. Mata ina mielekeo tofauti na ukubwa mbalimbali; yenyewe imetumbukizwa kwenye kiasi na kuongezeka, na inapata ukubwa wake mbali mbali kwa namna ya sifa na tabia. Kiumbe muhimu, kwa kinyume chake, hakihitajii tabia zote hizi.

Vitu vyote ambavyo wakati fulani havikuwepo halafu vikajakuwepo, wakati mmoja vilitawaliwa na dhana ya kufikirika ya uhai na kutokuwa hai. P ale vilipokimbilia kwenye hatua ya uhai, hii ilikuwa ni matokeo ya chanzo ambacho kilivilazimisha mwelekeo huo, kilikuwa ni kichocheo, kipengele cha nje ambacho kilivisukuma vyote kwenye mwelekeo mmoja badala ya ule mwingine. Kwa mneno mengine, kuwepo kwa chanzo ilikuwa ni wakala wa kiumbehai, kama vile kutokuwepo, au kukosekana sababu ni asili ya kutokuwepo kiumbe.

Kwa kawaida, kitu ambacho kinakuja kuwepo kama matokeo ya kuwepo kwa chanzo kamwe hakipotezi asili yake ya kuhitaji, wakati wote kitabia kiumbe chenye kuainishwa na kuhitaji. Kwa sababu hii, haja ya kitu juu ya kuwepo chanzo ni ya kudumu na isiyotanguka, uhusiano wake na chanzo hicho hautakatika japo mara moja. Endapo uhusiano huo ungekatishwa, uhai wa kitu hicho ungesalimu amri mara moja na kutokuwepo, kwa namna ile ile ambayo kwamba, mara jenereta ya umeme inapoacha kufanya kazi, taa zote angavu zilizounganishwa hapo hizimika. Ni kwa sababu hii kwamba chanzo na athari, uhuru kutokana kuhitaji na kutawaliwa na mahitaji ni hali ambazo zinahusiana wakati wote, endapo uhusiano huo ungekatizwa, kusingebakia chochote isipokuwa giza na kutokuwepo uhai.

Hivyo, hakuna jambo linaloweza kuonekana dhahiri hapa duniani mpaka uwezo maalum uwe umewekwa juu yake na kimoja ambacho asili yake iko huru kutokana na kuhitaji na chenyewe ndio chanzo haswa ambacho uhai hububujika kutoka humo. Kama uhai ungekuwa ni sehemu ya asili za vitu, kamwe usingefuata mkondo wa kukoma na kutoweka. Lakini ni ile tabia ya kuhitaji ndio tabia ya msingi kwenye asili zao, ili hata baada ya uhai wao kuanzishwa kwenye mpangilio wa viumbe, sifa yao ya kuhitaji huendelea

kuwepo kwa hali yoyote ile. Haviko huru kamwe na kutohitaji chanzo; haiwezekani kwamba athari iweze kupata uhai kwa uhuru kabisa au iendelee kuwepo japo kwa nukta moja bila kutegemea juu ya chanzo. Kwa hiyo inakuwa dhahiri juu yetu kwamba vitu vyote - viumbe hai vyote vinavyoweza kutokea - vinapata wakati wote na kwa kila mara kutoka kwenye asili isiyo na ukomo ambayo ndio hugawa uhai - yaani, ile Nafsi Muhimu, ya Pekee na Muumbaji Muweza - ule uwezo na uhai unaoviruhusu kuwa hai na kubakia kuwepo hai.

Qur'anii Tukufu inasema:

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ أَنتُمُ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّـهِ ۖ وَاللَّـهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿١٥﴾

"Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kujitosha, Msifiwa (Fatir:35:15).

Na tuzingatie pia wito huu wa Qur'ani:

﴿أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ ﴿٣٥﴾

"Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji?" ( Tur: 52:35).

﴿أَمْ خَلَقُوا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ۚ بَل لَّا يُوقِنُونَ ﴿٣٦﴾

"Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana na yakini" (Tur: 52:36).

﴿أَمْ لَهُمْ إِلَـٰهٌ غَيْرُ اللَّـهِ ۚ سُبْحَانَ اللَّـهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٤٣﴾

"Au wanae mungu mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu? Subhanallah! Ametakasika Mwenyezi Mwenyezi Mungu na hao wanao washirikisha naye." (Tur: 52:43).

﴿تَبَارَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾

"Ametukuka ambaye mkononi mwake umo Ufalme wote; na Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu." (Almulku: 67:1).

Chanzo cha viumbe vyote chenyewe hakihitajii kuwa na Asili Wafuasi wa uyakinifu wanatoa uangalifu wa ukosoaji sana kwenye kanuni ya kwamba Mwenyezi Mungu hahitaji kuwa na Asili. Wao wanasema endapo tutadhani Muumbaji ndiye chimbuko la ulimwengu na ndiye anayeweka uhai juu yake, viumbe vyote vikipata vyanzo vyao na uhai wa kuendelea kutoka kwake, ni sababu gani imemuondolea yeye haja ya kuwa na muumbaji, ni kiwakilishi gani kilichosababisha yeye mpaka kuja kuwepo? Katika hotuba iliyotolewa kwenye jumuiya ya 'Londoni Atheist Sosiety,' mwandishi maarufu, Betrand Russell, alisema; "Siku moja, nilipokuwa na umri wa miaka kumi na nane, nilikuwa ninasoma wasifu wa John Stuart Mill. Sentenso moja mahsusi ilinivutia sana: Mill aliandika kwamba siku moja alimuuliza baba yake, ni nani aliyemleta yeye kwenye uhai duniani, na baba yake hakuweza kumjibu." Sababu yake ni kwamba papo hapo aliuliza swali la ni nani aliyesababisha Mwenyezi Mungu kuwepo?

Halafu Russell anaongeza: "Bado ninasadiki kwamba sentenso ile rahisi inadhihirisha ile ghiliba ya chanzo cha msingi. Kwani kama kila kitu lazima kiwe na sababu na chanzo, hali hiyo lazima itumike juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Kama, kinyume chake, kitu kinaweza kuwepo bila ya sababu au chanzo, kitu hicho inawezekana kiwe ama Mwenyezi Mungu au

ulimwengu, na mjadala wote unakuwa hauna maana."[1] Kwa bahati mbaya, wanafalsafa fulani wa nchi za Magharibi ambao wanakubali kuwepo kwa Mwenyezi Mungu wameshindwa kufumbua tatizo hili. Mwana falsafa wa Uingereza Herbet Spencer amesema yafuatayo

kuhusiana na suala hili: Tatizo ni kwamba, kwa upande mmoja, akili ya binadamu hufuata sababu ya kila kitu na, kwa upande mwingine, hukataa fhana zote zisizo na mantiki (kwa vile ukweli wa dhana hizo hauwezi kuthibitishwa bila kurejea kwenye hitimisho). Haitambui wala kuelewa chanzo kisichosababishwa. Mchungaji anapomwambia mtoto kwamba Mwenyezi Mungu ameumba ulimwengu, mtoto huuliza nani aliyemuumba Mwenyezi Mungu?[2] Mahali pengine mwanafalsafa huyu anasema: "Myakinifu hujaribu kujisadikishia mwenyewe kuhusu dunia ambayo ipo na imetokana na yenyewe, milele bila ya kisababisho. Hata hivyo, hatuwezi kukiamini kitu ambacho hakina mwanzo wala asili. Mwanatheolojia huyo anayapeleka mambo haya hatua moja zaidi nyuma kwa kusema kwamba Mwenyezi Mungu aliuumba ulimwengu. Lakini mtoto anamuuliza swali lisilojibika: Nani aliyemuumba Mwenyezi Mungu?[3].

Tunaweza kuleta hasa upinzani kama huo huo dhidi ya wayakinifu na kuwauliza, endapo tukifuata mlolongo wa usababishaji kinyumenyume, hatimaye tutafika penye chanzo cha msingi. Natuseme kwamba chanzo si Mwenyezi Mungu, bali ni mata. Sasa hebu tuambieni ni nani aliyeiumba mata ya msingi. Ninyi mnaoamini katika kanuni ya usababisho, tujibuni sisi swali hili. Kama mata ndio chanzo halisi cha vitu vyote, ni nini chanzo cha mata? Mnasema kwamba asili ya vitu vyote ni nguvu ya mata, ni nini sababu na asili ya nguvu ya mata? Kwa kuwa mlolongo wa usababisho hauwezi kurudi kwenye kutokuwa na ukomo, jibu pekee wanaloweza kutoa ni kwamba mata ni kitu kisicho na wakati na chenye umilele ambacho hakiwezi kuwekewa mwanzo: mata ni kitu kisichoumbwa, hakina mwanzo wala mwisho, kuwepo kwake hutukia ndani ya asili yake yenyewe.

Hii ina maana kwamba wayakinifu wanakiri kuwepo kwa kanuni ya umilele na kukosa chimbuko; wanaamini kwamba vitu vyote vilitukia kwenye maada ya milele na kwamba uhai unatukia kutoka ndani ya asili yenyewe hasa ya maada, bila ya haja yoyote ya muumbaji. Russell anelezea wazi imani hii kwenye hotuba iliyonukuliwa hapo juu. Yeye anasema; "Hakuna uthibitisho kwamba dunia ilipata kuwa na mwanzo kamwe. Hii fikira ya kwamba vitu lazima wakati fulani vilikuwa vina mwanzo inatokana na ufinyu wa fikra zetu."[4].

Kwa namna ile ile ambayo Russell anafikiria mata kuwa ni ya milele, wanaomwamini Mwenyezi Mungu wanahusisha sifa ya umilele kwa Mwenyezi Mungu. Imani katika kitu chenye umilele kwa hiyo ni ya shirika, ya kawaida kwa wanafalsafa wa kiyakinifu na kidini. Makundi yote mawili yanaafiki kwamba kuna chanzo cha msingi, lakini wanaomwamini Mwenyezi Mungu wanakiachukulia chanzo cha msingi kama ni chenye hekima, ujuzi wote, na chenye kumiliki uwezo wa kuamua na utashi,

---

1. Russell, Why I am not a Christian, uk. 9.
2. Imenukuliwa katika Furughi, Sayr-I Hikmat dar Urupa, III, uk. 162.
3. Will Durant, History of Philosophy, II, uk. 497.
4. Russell, Why I am not a Christian, uk. 20.

ambapo kwa maoni ya wayakinifu, hicho chanzo cha msingi hakina busara wala akili, utambuzi ama uwezo wa maamuzi. Hivyo, kumwondoa Mwenyezi Mungu, kwa hali yoyote ile hakuleti ufumbuzi wa tatizo linaloletwa na suala la kiumbe cha milele.

Zaidi ya hayo, maada ni kituo cha mwendo na mabadiliko, na mwendo wake ni wenye nguvu na imewekwa ndani ya asili yake yenyewe. Sasa, mwendo muhimu hauendani na umilele, na mata na utulivu muhimu ni jinsi mbili ambazo zote ni za kipekee ambazo haziwezi kuunganishwa kwenye kituo kimoja. Chochote kile ambacho kimetulia na hakibadiliki katika asili yake hakiwezi kupokea mwendo na mabadiliko katika asili hiyo.

Ni vipi wenye fikira za ki-Marx, ambao wanaamini kwamba mata inaandamana na tamathali yake yenye dhana ya kutofautiana (tabaini), wanavyoweza kuthibitisha umilele wa maada? Umilele maana yake ni umadhubuti na kutobadilika kwa asili, kutowezekana kwa ukomo, lakini maada katika asili yake ni ufupisho makini wa nguvu na uwezekano; inawiana yenyewe, ikiwa imenasa kabisa katika kuishi na kufariki. Umilele hauendani na mtindo wa uhai uliomo kwenye mata na vipengele na sifa zilizolazimishwa na asili yake. Itikadi ya wale walio na imani juu ya Mwenyezi Mungu kuhusu kanuni isiyobadilika na ya dhahiri inahusika kwa kiumbe ambacho ndani, na, kwa asili yake kinaweza kukubali utulivu na kutobadilika; asili yake hainazo kabisa - na iko mbali nazo - sifa za maada. Asili yenyewe hasa ya maada inakataa kudumu, umilele na uendelevu, kwani kamwe haiwezi kujitenga yenyewe na mwendo, kuwiana na inakataa kuwa chanzo cha msingi au kisichobadilika.

Itakuwa na manufaa hapa kusimulia mazungumzo baina ya Imamu Sadiq (a.s) na mmoja wa wayakinifu wa wakati wake. Myakinifu: "Viumbe viliumbwa kutokana na nini? Imamu: "Havikuumbwa kutokana na kitu chochote (yaani kiasili havikuwa viumbe)." Myakinifu: "Sasa vinakua vipi na kujitokeza kutoka kwenye kutokuwa kiumbe?"

Imamu: "Je, sikusema kwamba vitu vyote duniani havikuumbwa kutokana na chochote? Maana yangu ni hii, kwamba viumbe vyote ki-asili havikuwa viumbe, na halafu vikaja kuwepo. Unataka kusema kwamba dunia ni ya milele, lakini fhana hii si sahihi kwa sababu zifuatazo:

"Kwanza, kama dunia hii ya maada ni ya milele, ina maana kwamba kitu chenye umilele lazima kipatwe na kubadilika na ukomo, jambo ambalo haliwezekani.

"Pili: endapo elementi zinazotengeneza dunia ni vya milele kwa sababu ya asili yao, inawezekanaje basi ziingie kwenye mkumbo wa kifo na kutoweka? Na kama, katika kinyume chake, zinakuwa hazina uhai katika asili zao, ni namna gani uhai unavyoweza kuchomoza kutoka ndani yao? Endapo utasema kwamba viumbe hai hutokana na elementi hai na viumbe visivyo hai hutokana na elementi zisizo hai, tunajibu kwamba asili isiyona uhai ndani mwake na utokanao ndani mwake haiwezi kuwa ya milele na haiwezi kuwa chanzo cha uhai." Myakinifu: "Kama maada iko kama vile usemavyo, kwa nini viumbe vinasemekana kuwa na umilele?" Imamu: "Imani katika umilele wa ulimwengu inashikiliwa na wale wanaokanusha kuwepo kwa mtawala na mpangaji wa maumbile, wanawakataa mitume wa

Mwenyezi Mungu, wanafikiria vitabu wanavyokuja navyo wajumbe ni ngano za kale, na kubuni itikadi zinazowaridhisha wao wenyewe."[1].

Sasa tunasema kwamba, kuwepo kwa kitu hakuwezekani bila ya chanzo cha kitu chenye upungufu, yaani, ambacho majaaliwa yake yamo mikononi mwa chanzo chake na ambacho kudumu kwake kunategemea kuwepo hai kwa chanzo chake. Hali hii haiwezi kutumika kwa kitu ambacho, kinafahamu uhalisi wake na hakioneshi dalili yoyote ya upungufu na ukomo.

Chanzo cha msingi ni chanzo msingi kwa sababu ya kuwa na uhai kamilifu na usiokuwa na kikomo; bila kutawaliwa na asili yoyote, kimeepukana na kuhitaji, mazingira na utegemezi, na hakina dalili ya kugeuka au kubadilika.

Tunapozungumzia kuhusu sababu ya mwanzo na wakati huo huo tunasema kwamba Mwenyezi Mungu ameepukana na haja yote ya kuwa na chanzo, hatuna maana ya kwamba Yeye kwa ujumla anashirikiana na viumbe vilivyoumbwa ile haja ya kuwa na chanzo lakini wakati fulani alikuwa, kama ilivyokuwa, aliondokana na kanuni ya usababisho. Mwenyezi Mungu sio athari kwamba ahitaji chanzo; Yeye si kiumbe kwamba ahitajie muumbaji. Kinyume chake, dalili zote na maajabu ya uhai vinatokana na Yeye, chanzo cha milele cha uhai. Kanuni ya usababisho hutumika kipekee kwenye mazingira ya vile vitu ambavyo kutokuwepo kwao kulitangulia - kabla ya kuwepo kwao.

Vivyo hivyo, maana ya sababu ya mwanzo si kwamba Mwenyezi Mungu alijibuni Mwenyewe, kwamba Yeye alikuwa ndio chanzo chake mwenyewe. Mahitaji ya athari kwa ajili ya chanzo yamo kwenye aina ya uhai ambao kile kilichotangulia kinao; kinakuwepo sio kwa sababu kina uhai kimsingi bali ni kama matokeo ya uhai utokanao na kitu kingine na ulio tegemezi kinaoupata kutoka kwenye chanzo. Lakini kiumbe ambacho asili yake haitawaliwi na hali yoyote na kinaonyesha kutokuwepo kabisa kwa utegemezi na uhusiano umeondolewa kabisa kutoka kwenye mazingira ambamo ile kanuni ya usababisho inafanya kazi.

Endapo kiumbe kwa sababu ya ukamilifu na kutokuhitaji kwa asili yake, kinakuwa hakihitaji chanzo, maana yake ni kwamba hakuna chanzo kilichokiweka katika kiwango maalumu cha uhai na kwamba hakuna sababu inayoweza kuingilia ndani yake. Mlolongo wa kisababisho hauwezi kurefushwa kurudi nyuma bila kikomo, na kukosekana kwa uhusiano ni kwa asili katika dhana yenyewe hasa ya chanzo cha awali. Swali kama: "Hicho chanzo cha awali kilijitokeza lini?" kwa hiyo, huwa halijitokezi; hivyo maswali kama haya hutumika tu juu ya vyanzo vya vitu na tabia zao za kutegemea.

Kuwepo kwa chanzo cha kwanza kunatambulika kwa dhati yake; kuwa kwake chanzo cha kwanza chenyewe, kwa hakika pia kunattmbulikana kwa dhati yake. Tabia zote hizi zinaashiria kujitosheleza, ambapo vitu ambavyo kuwepo kwao kumetokana na vitu vingine huwa vinahitaji chanzo, kwa sababu vinajulikana kwa tabia za kubadilik na kugeuka, kwa kuchipukia kutoka kwenye kutokuwepo na kuingia kwenye kuwepo. Inawezekanaje

1. Biharul Anwar, Juz. I, uk. 166.

kudhaniwa kwamba imani katika kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ni kukiri kuwepo kwa kuhitilafiana, ambapo imani juu ya asili isiyoanzishwa ya athari kama vile maada iwe haipingani?

Tunaishi kwenye dunia ambayo vitu vyote vimeachwa wazi kwenye kubadilika na kuharibika; ipo dalili ya kutokudumu, kutawaliwa na kufadhiliwa kulikochapwa kwenye kila chembechembe yake. Kuhitaji na kutegemeana kumeota mizizi imara katika uhai wetu na ule wa kila kitu kilichomo duniani na mbinguni. Uhai wetu sio wa kudumu na haukuzuka kutoka ndani ya asili yetu wenyewe; hatukuwa, na halafu tulifunikwa kwenye joho la kuwepo na tukaja kuwa hai. Ili kuweza kuja kwenye uhai, viumbe kama vile sisi lazima tuwe wenye kuomba sana kumfikia mwenye kutoa uhai.

Lakini Yeye Ambaye ni wa milele nawa kudumu, ambaye kuwepo kwake kunatokana ndani ya asili Yake Mwenyewe, na Ambaye kuonekana kwake kuko nje ya wakati, ni wazi kabisas hana haja ya chanzo. Maana ya chanzo katika falsafa ni kile kinacholeta athari kutoka kwenye kutokuwepo kitu hadi kuwepo kwake na kukifunika na vazi la uhai. Uumbaji huu hauwezi kutolewa hoja kwa ajili ya vyanzo vya kimaada, na jukumu moja tu la mata ni kuacha umbile moja ili kuweza kupokea umbo lingine.

Ni kweli kwamba kila kiumbe cha kimaada hupata tabia mpya na iliyo tofauti katika kila nukta kama matokeo ya maendeleo ya ndani kwa ndani. Hata hivyo, usogevu wa kimaumbile wa dunia na mifuatano ya uletaji na uchafuzi inadai mahitaji kudumu ya msaada kwa yule ambaye huumba mwendo, msaada ambao hulea msafara wa haraka wa uhai na kuusukuma kwenda mbele.

7

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA SABA

### UKOMO WA NYORORO YA USABABISHO

Wayakinifu wanaweza kung'ang'ania kwa ukaidi kabisa katika kukanusha ukweli na kuleta hoja nyingine yenye kuonekana kama ni nzuri. Wanaweza wakasema, "Hatuikatishi nyororo ya usababisho lakini, kinyume chake tunaiendeleza isiwe na mwisho; tunatetea kanuni ya asili isiyo na ukomo ya kiungo sababishi."

Kama ni hivyo, wanapaswa kujibiwa kama ifuatavyo: Kuchambua dunia ya maumbile kwa namna hii kunasimama kwenye kufikiria juu ya nyororo ya visababisho na athari na mkunjuko wa kudumu wa mfuatano wa vyanzo usio na ukomo. Hata hivyo, kwa vile kila chanzo pia ni athari, kinakosa chenyewe kuwa kwenye asili yake; kinakuwa hakiwezi kuchukua sehemu ya uhai, mbali na chanzo bora zaidi na kilichokitangulia kabla.

Kwa hiyo, ni jinsi gani kila sehemu ya nyororo hiyo, ambayo imetawaliwa na tabia ya kuhitaji kutoka mwisho mmoja hadi mwingine, ilivyoibuka kutoka kwenye hali ya kutokuwa kiumbe? Kuwepo kwa kila sehemu ya nyororo hiyo huonyesha upungufu, kutokuwa na nguvu na chimbuko ndani ya muda uliowekwa, kuwepo kwake kulianza lini? Inawezekanaje vitu vikubwa na vyenye vijisehemu kuibuka kutoka viunganisho vya vitu visivyokuwepo? Je, uhai hububujika kutoka kwenye muungano wa vipengele vingi ambavyo husababisha kifo?

Hata kwa umbali kiasi gani nyororo hii isiyo na ukomo ingerefushwa, bado itakuwa na zile sifa za uhitaji, utegemezi na uibukaji kwa wakati. Nyororo kutoka kwenye ile asili hasa ambayo kwamba kujitawala na uhuru kutokana na kuhitaji hakujitokezi kamwe haiwezi kuchukua sura ya kuwepo hadi itakapoungana na yule ambaye katika asili yake yuko huru kabisa kutokana na kuhitaji - na kiumbe ambaye anazo sifa za utakatifu na ambaye yeye ni kisababisho tu na sio athari. Bila ya kuwepo kwa kitu kama hicho kisichotawaliwa na masharti yoyote, chanzo cha sababu zote na msingi wa uhai wote, mpangilio wa maumbile hauwezi kuelezeka.

Tuseme kwamba kwenye uwanja wa kivita, kikosi cha wapiganaji kinaazimia kumshambulia adui lakini hakuna hata mmoja wao ambaye yupo tayari kuanza vita kwa kurukia katikati ya jeshi la adui. Yeyote anayepewa amri kufanya hivyo jibu lake ni: "Sitashambulia hadi fulani wa fulani aanze kupigana." Kila mpiganaji anajibu hivyo; hapana hata mmoja wao ambaye yupo tayari kushambulia bila kuweka sharti.

Je, katika hali kama hiyo, shambulizi litaweza kutokea kamwe? Kwa vyovyote vile halitatokea, kwa sababu kupigana kwa kila askari ni kwa masharti juu ya kupigana kwa mwenzake. Ni dhahiri kwamba mfululizo wote wa mashambulizi ya masharti hautatokea bila kutimizwa kwa sharti lenyewe, kitu kisichowezekana chini ya mazingira hayo, na matokeo yake, shambulizi halitafanyika.

Kama tukiiendeleza nyororo ya chanzo na athari milele, kuwepo kwa kila kiunganishi kwenye nyororo hiyo kutakuwa kwa sharti la kiunganishi

kilichotangulia ambacho nacho baadaye kitakuwa kwa sharti la kuwepo kwa kiunganishi kilichotangulia. Inakuwa kana kwamba kila kiunganishi kwenye nyororo hiyo ya usababishaji kingekuwa kitangaze kwa sauti kubwa kutoka vina vya nafsi zao: "Sitachukua sura ya kuwepo hadi hapo yule mwingine atakapokuwa amekanyaga uwanja wa viumbe." Kila kiunganishi kinategemea juu ya sharti ambalo halijatimizwa, na kila kimojawapo, kwa hiyo, kikiwa kimezuiwa kupata baraka za kuwepo.

Kwa kuwa tunauona ulimwengu wote ukiwa umetapakaa aina tofauti za viumbe, lazima duniani pawepo na chanzo ambacho sio athari, sharti ambalo halitawaliwi na sharti jingine; vinginevyo uso wa dunia usingekuwa umefunikwa hivi na vitu vingi. Chanzo cha msingi ni mmoja, ambaye katika asili yake yu huru na kuhitajia chochote, ambaye anaweza kujiweka mbali na vipengele vyote tofauti vya uhai, na ambaye anaweza kusababisha kutokea mambo ya maajabu kabisa na dalili za asili kabisa. Ni muumbaji ambaye hupanga yote haya na halafu huyaweka kwenye utekelezaji, ambaye huunganisha maumbile yote kwenye utaratibu wa dunia, ambaye wakati wote hutawanyisha uzuri wa uhai juu ya dunia, na ambaye huisukuma mbele ile mandhari kubwa ya maumbile kuelekea kwenye kutimiza lengo la mpangilio wa uhai. Kwa kuifanya dunia si yenye kuumbwa na ya milele, wayakinifu wanajaribu kukanusha haja ya kudumu ya dunia juu ya muumbaji na hapo kuweka uhai wa kujitegemea juu ya dunia. Utaratibu wao, hata hivyo, hauleti matokeo ya kuridhisha.

Wayakinifu wanadhani kwamba dunia inahitaji muumbaji pale wakati wa mwanzo wa uumbaji tu; mara lengo hilo likitimizwa, Mwenyezi Mungu na ulimwengu hawategemeani na hawana kiunganisho baina yao. Kwa matokeo ya itikadi hii, wayakinifu wanaendelea kukanusha hata ule wakati wa mwanzo wa haja, na kwa kukataa wazo la kuwepo mwanzo wa uumbaji, wanadhani wamepata ufumbuzi wa suala la Mwenyezi Mungu na maumbile na wameikomboa dunia kutokana na haja juu ya muumbaji. Hii ni kwa sababu wanadhani kwamba mahitaji juu ya dunia, kuwa ni ya muda na ya mpito tu, ambapo mahitaji hayo ni ya msingi katika asili ya dunia - dunia si chochote bali ni mwendo, muundo wa mwendo wenye ukomo na utegemezi.

Kwa kweli, kila nukta ni mwanzo wa uumbaji; kila muda; kila atomu hapa duniani inajishughulisha na uanzilishi. Ina maana kwamba kitu kizima ambacho hizo atomu ni kama sehemu yake, hivyo hivyo kimeanzika katika muda; hakina asili na nafsi ambayo imejitenga na huru kutokana na ile ya atomu ambazo zinakijenga. Kwa hiyo dunia bado inayo haja ile ile juu ya kuwepo muumbaji ambayo ilikuwa nayo muda uumbaji ulipoanza. Hata kwa kudhaniwa dunia kuwa ya milele, bado isingepata kujitawala kwa uhai. Jibu la wanasayansi juu ya hoja ya Umilele wa dunia.

Kama vile ambavyo binadamu hupoteza uwezo wa kiakili kadiri muda unavyopita hivyo kwamba siku moja taa ya uhai wake inazimika; viivyo hivyo pia ulimwengu nao wakati wote unaelekea kwenye kuporomoka na kukoma. Kwani nishati zilizopo duniani zinaendelea kufifia pole pole; atomu zimegeuka kuwa nishati na nishati hai inazima na kutulia. Mara tu atomu zinapogawanyika kwa ulinganifu na usawa, hakuna kinachobakia isipokuwa ukimya na kutosogea kwa dhahiri. Kwa hiyo, haiwezekani kuichukulia mata kama ni asili ya milele au maudhui ya uhai, na hakuna

jinsi nyingine isipokuwa kuiona dunia kama ni kitu kilichoumbwa. Kanuni ya pili ya mwendojoto, kipimo cha ukosekanaji wa nguvu ya joto katika mfumo (entropy) au kupungua kwa nishati ya joto, inatufundisha kwamba ingawaje hatuwezi kuweka tarehe maalum ya kutokeza kwa dunia, kwa hakika dunia ilikuwa na mwanzo. Joto hapa duniani linapungua polepole na kuanguka, kama kipande cha chuma kilichoyeyushwa ambacho hutawanya joto lake hewani hadi mwishowe joto la chuma hicho litakuwa sawa na lile la vitu na hewa inayokizunguka.

Kama ingekuwa hakuna mwanzo au mahali pa kuondokea kwa ajili ya dunia, Atomu zote zilizopo zingemumunyuka na kugeuzwa kuwa nishati kipindi cha miaka isiyokikomo iliyopita nyuma. Katika kipindi cha muda mrefu uliopita joto la dunia lingeweza kufikia kuisha kabisa, kwani kuhusu mata, katika mkondo wa mabadiliko ya mfululizo muendelezo, hatimaye hubadilika kuwa nishati yenye kuharibika. Haiwezekani kwa nishati yote iliyosambaa kugeuka kuwa mata na bonge lenye starehe kwa dunia ya uhai.

Kufuatana na kanuni ambayo imetajwa hapo juu, mara tu nishati itumikayo ikimalizika nguvu yake, utendaji na hisia za kikemikali haziwezi kuendelea kutokea. Lakini kama ilivyo bayana kwamba utendaji na hisia za kemikali vinatokea, kwamba maisha yanawezekana duniani, na kwamba kitu kikubwa sana kama jua hugawanyika kila siku mchana na usiku kwenye tani milioni mia tatu elfu, ni dhahiri kwamba dunia ilianza wakati fulani. Kuangamia kwa sayari na nyota na kutokuweka majua ni uthibitisho wa kifo na mabadiliko katika mpangilio uliopo; vinaonyesha kwamba dunia inaelekea kwenye kutoweka na hatima isiyoepukika.

Halafu tunaona kwamba, sayansi asilia zimeiondoa mata kwenye ngome ya umilele. Sayansi si tu kwamba inathibitisha kuumbwa kwa dunia lakini pia hushuhudia kwamba dunia ilikuja kuwepo katika wakati maalum. Wakati wa kuumbwa kwake, dunia ilijikuta inahitaji nguvu zisizo za kawaida kwani mwanzoni, vitu vyote havikuwa na umbile na havikutofautiana. Ilikuwa muhimu kwa cheche asili ya mwendo na uhai kutua juu ya ulimwengu wa maumbile. Ingewezekanaje mazingira yasiyokuwa na nishati hai, yanayoainishwa na ukimya kabisa na ukosa maumbile, yangekuwa ndio chanzo cha usongevu na uhai?

Umakanika unatuambia kwamba kitu kisichosogezeka wakati wowote kinakuwa kimetulia isipokuwa kinapopatwa na nguvu ya nje yake. Kanuni hii inawakilisha kanuni isiyoweza kukiukwa katika dunia yetu ya maada, na kwa hiyo, hatuwezi kuamini nadharia ya uwezekano au kubahatisha.

Hakuna kitu kisichosogezeka hata kimoja hadi sasa ambacho kimeingia katika mwendo bila ya kusukumwa na nguvu ya nje yake. Hivyo kwa msingi wa kanuni hii ya kimakanika, lazima pawepo na nguvu ambayo ikiwa ni nyingine mbali na dunia hii ya kimaada, inayoumba dunia hiyo na kuipatia nguvu hivyo kwamba inachukua maumbile, inayojitofautisha yenyewe, na inayojipatia sifa mbali mbali. Mwanasayansi mashuhuri Frank Allen, anapendekeza hoja ya kuvutia ifuatayo yenye msimamo wa kukubali kuumbwa kwa dunia na Mwenyezi Mungu: "Watu wengi wamejaribu kuonyesha kwamba dunia hii ya kimaada haihitaji kuwa na muumbaji. Kilicho juu zaidi ya mashaka yote ni kwamba dunia ipo na maelezo ya aina nne yanaweza kupendekezwa kuhusu chanzo chake: "Kwanza, ni kwamba

licha ya hayo ambayo tumeyasema hivi punde, tunaiona dunia kama ndoto na madanganyo (kiini-macho) tupu. Ya pili ni kwamba dunia imechomoza kutoka kwenye hali ya utupu kabisa, yenyewe tu hivihivi. Ya tatu ni kwamba dunia haikuwa na mwanzo na kwamba imekuwepo daima. Ya nne ni kwamba dunia imeumbwa.

"Nadharia tete ya kwanza inategemea katika kukubali kwamba hakuna, kiukweli, tatizo linalotakiwa kupatiwa ufumbuzi mbali na tatizo la metafizikia la utambuzi wa mwandamu juu ya nafsi, ambalo pia linaweza kupuuzwa kama ndoto, njozi na kiini macho. Inawezekana kwamba mtu anaweza kusema kwamba treni za kubuniwa, zilizojaa watu wa kubuniwa zinavuka mito hewa ya kubuniwa kupitia kwenye madaraja yasiyo ya kimaada.

"Nadharia tete ya pili, kwamba dunia ya mata na nishati iliyojitokeza na kuwepo yenyewe tu hivihivi, haina maana na ya kipumbavu kama ile ya kwanza, haifai hata kufikiriwa kwa mazungumzo. "Nadharia tete ya tatu, kwamba dunia imekuwepo wakati wote ina ele - menti moja inayofanana na ile dhana ya kuumbwa, kwani ama mata isiyokuwa na uhai, na hiyo nishati vilichanganika nayo au amekuwepo muumbaji wakati wote. Wala uhusishaji wa umilele hauleti tatizo lolote maalum ndani yake yenyewe. Hata hivyo, mwendojoto umethibitisha kwamba dunia inasogea kuelekea kwenye hali ambayo joto la vitu vyote litakuwa kwenye kiwango cha chini kinachofanana na nishati ya kutumika itakuwa haipatikani tena. Kwa hiyo, uhai utakuwa hauwezekani.

"Kama dunia haingekuwa na chimbuko na ilikuwepo tangu milele yote, hali kama ya kifo na kutokuwepo uhai tayari ingekwishatokea. Jua ling'aralo na lenye joto, nyota na dunia iliyojaa uhai vinabeba ushahidi wa kuaminika wa dunia kuanzilika katika wakati; muda maalum katika wakati ulianisha mwanzo wa uumbaji. Hapo basi, dunia haiwezi kuwa vinginevyo mbali na kuwa imeumbwa; lazima ilikuwa kisababisho kikubwa, cha tangu dahari, muumba wa milele, mwenye ujuzi wa kila kitu na kudra, ambaye ndiye aliyeileta dunia kwenye kuwepo."[1]

Kama mwanadamu atafikiria kwa kina japo kidogo na akatafakari kuhusu ukweli kwa mtazamo mpana, ataelewa kwamba akiwa amekabiliwa na maeneo mapana sana ya kijiografia ya maisha na haja ya namna fulani ya kuyatambua, hawezi hata kidogo kuuona uwezo wake binafsi kama wenye kugetosha kwa kazi hiyo. Elimu juu ya mpango wa maumbile iliokusanywa na mwanadamu kupitia juhudi zake zisizochokesha zinakuwa kama ni bure kabisa. Ingawa sayansi imepiga hatua kubwa sana mbele, kuna hitilafu kabisa baina ya wanadamu, ni nini mwanadamu amejifunza, na ni yapi ambayo bado hayajui.

Kwa kiasi ambacho vile vipindi vilivyopita vinahusika ambavyo vimefunikwa na giza nene, kwa jinsi tujuavyo, maelfu au hata mamilioni ya jamii za wanadamu zilizo bora zaidi ya hii iliopo sasa zinaweza kuwa zilikuwepo. Jamii kama hizo bado zinaweza kuja kuwepo tena hapo baadaye. Kile kinachoitwa sayansi na wale wanaoabudu sayansi wa zama hizi za sasa na wao wakaziona kuwa sawa na jumla yote ya ukweli, ni

1. Isbat-I Vujud-I Khuda, uk. 17.

mkusanyiko tu wa sheria zinazotumika kwa upande mmoja tu wa dunia. Matokeo ya bidii zote za binadamu na majaribio ni sehemu ya ujuzi inayohusu nukta moja ndogo ing'arayo - inayoweza kulinganishwa na mwanga hafifu wa mshumaa - uliozungukwa na usiku wa giza uliofunika jangwa pana sana la ukubwa usio na mpaka.

Kama tukirudi nyuma mamilioni ya miaka vumbi la vurugu litafunika njia yetu ikiwa kama moja ya dalili ya nguvu ya udhaifu na ujinga wa mwanadamu anapokabiliwa na utukufu na ukubwa wa maumbile. Inaweza kuwa kwamba kipindi ambamo mwanadamu amekuwepo si chochote zaidi ya muda kidogo tu katika uhai wa dunia; ni hakika kwamba palikuwepo na bahari nyeusi isiyokuwa na uhai ambamo hamkuwepo na dalili ya mwanadamu. Kwa ufupi tunajua kiasi kidogo sana cha mwanzo wa safari yetu na hatujui chochote kuhusu mustakabali wake. Wakati huo huo, ni vigumu kuamini kwamba mazingira muhimu kwa ajili ya uhai yapo kwenye sayari hii ndogo pekee tu. Wanasayansi wengi wa kipindi hiki wanaona eneo la maisha ni kubwa na pana mno; wanawasilisha mamilioni yasiyo na idadi ya sayari kwenye kukodoa macho kwetu na tunazitazama kwa namna mbalimbali. Lakini kile tunachowezeshwa kuona si chochote zaidi ya umbali wa maono ya mdudu mchwa pale inapolinganishwa na ukubwa wa ulimwengu.

Kuelezea safari ya kufikirika tu kwenye dunia isiyo na ukomo, mwanasayansi mashuhuri; Camille Flammarion, anasema yafuatayo katika kitabu chake cha elimu ya nyota: "Tunaendelea kusonga mbele kwa miaka elfu moja, kwa miaka elfu kumi, kwa miaka mia moja elfu, kwa kasi ile ile, bila kutetereka, bila kupunguza kasi ya mwendo wa gari yetu, wakati wote tukienda mbele katika msitari ulionyooka. Tunasonga mbele kwa kasi ya kilomita mia tatu elfu kwa sekunde. Tunadhani kwamba baada ya kusafiri kwa kasi hiyo kwa miaka milioni moja tutakuwa tumefika kwenye mipaka ya ulimwengu huu unaoonekana?

"Hapana, zipo anga kubwa mno za mbali zaidi zenye giza nene ambazo lazima zipitiwe, na huko pia, nyota mpya zinazoonekana katika mipaka ya mbingu. Tunaziendelea hizo, lakini je, tutazifikia kamwe? "Mamilioni zaidi ya miaka, uvumbuzi mpya zaidi, fahari na ukubwa zaidi, ardhi na dunia nyingine zaidi mpya, viumbe vipya vingine zaidi na vitu vya kiroho vinginevyo - je, kavitakwisha kamwe? Upeo haujifungi kamwe; mbingu daima hazizuii njia yetu; anga yenye kuendelea, pengo inayoendelea. Tupo wapi sisi? Ni njia gani ambayo sisi tumepita? Bado tungalipo katikati ya ile nukta - sehemu ya katikati ya duara ipo kila mahali, mzingo wake hauonekani popote.

Hiyo ndio dunia isiyo na mwisho ambayo inaonekana kukaa wazi mbele yetu na ambayo uchunguzi wake ndio kwanza umeanza. Bado hatujaona chochote, na tunageuka nyuma kwa woga, tukianguka kwa kuchoka kutokana na safari hii isiyo na mafanikio. Lakini tutaangukia wapi? Tunaweza kuangukia kwenye umilele kwenye madimbwi yasiyo na kikomo ambamo kina chake hatukifikii kamwe, kama vile ambavyo, hatuwezi kuvifikia vilele vyao. Kaskazini inakuwa kusini; hakuna mashariki wala magharibi, hakuna juu wala chini, hakuna kushoto wala kulia.

Kokote kule tutakapotazama hatuoni mwisho, na ndani ya eneo hili lisilokuwa na mwisho, ulimwengu wetu si chochote zaidi ya kisiwa kidogo kwenye mkusanyiko mkubwa wa visiwa vilivyoenea kwenye bahari isiyo na mwisho. Maisha yote ya mwanadamu, kwa fahari yote ambayo mwanadamu anajigamba nayo katika historia yake kisiasa na kidini, au hata uhai wote wa sayari yetu pamoja na ufahari wake wote, ni sawa na ndoto ya kitambo kinachopita kwa kasi kubwa.

Kama tungependa kuandika tena kazi zote za utafiti ambazo zimeandikwa na mamilioni ya wasomi kwenye mamilioni ya vitabu, wino ambao unahitajika kwa kazi hiyo ni sawa na ujazo ambao hautazidi ujazo wa tenki moja dogo. Lakini kuelezea na kupanga kwa mtindo wa utaratibu, ile miundo ya vitu vyote vilivyopo duniani na mbinguni, katika vipindi visivyoonekana vilivyopita na kwenye mustakabali usiopimika - kuandika, kwa ufupi, miujiza yote ya maumbile - inaweza kuhitaji wino mwingi zaidi kuliko bahari kuwa na maji."[1].

Kama asemavyo Profesa Ravaillat; "Ili kuwa na utambuzi uliokamilika wa dunia, inatosha kujua kwamba idadi ya kundi la nyota na sayari kwenye anga pana isiyopimika ya ulimwengu ni kuwa zaidi kuliko ile ya chembechembe za mchanga katika pwani zote za dunia hii."[2] Fikra za aina hiyo kuhusu yale tunayoyajua na tusiyoyajua zinatuwezesha kuepuka kifungo katika kifukofuko cha maisha yetu finyu; ili tuweze kutambua kwa unyonge kuhusu tupo wadogo kiasi gani; kwenda zaidi ya haya maisha yetu yenye ukomo, kwa kiwango ambacho tunaweza na kutafakari ukweli kwa uangalifu mkubwa na kwa kuzama zaidi.

1. Hii ni kwa kumbukumbu ya Ayah za Qur'anii zinazozungumzia kuhusu miti yote kuwa kalamu na bahari zote kuwa wino na bado zisiweze kuyamaliza maneno ya Mwenyezi Mungu, (18: 109; 31 :27).

2. Dau Hazar Danishman dar Justuju-yi Khuda-yi Buzurg, uk. 13.

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA NANE

### FITINA BANDIA ZA KISAYANSI

Watu wa maada wanasema kwamba kuasisiwa kwa kitivo chao cha fikra mnamo karne ya 18 na 19 kulihusiana moja kwa moja na maendeleo ya sayansi na kwamba ile mbinu pembuzi ilikuwa ni tunda ambalo lilichumwa kutoka kwenye mti uliostawi vizuri wa sayansi.

Wanaonyesha kila falsafa mbali na uyakinifu kama aina ya udhanifu, unaopingana na mbinu ya fikra ya kisayansi, na wanasisitiza kwamba msimamo wao ni wa kisayansi na endelevu. Kwa mujibu wa msimamo wao, uhalisia unategemea katika kukengeuka kutoka kwenye ukweli wa metafizikia; kila mtu anapaswa ategemeze falsafa yake ya maisha juu mantiki ya fahamu na majaribio na kuchagua uyakinifu. Lakini madai haya si lolote zaidi ya ndoto za kishabiki ambazo zimetegemezwa kwenye nadharia zisizothibitishwa. Mawazo kama haya yanakuja moja kwa moja kutoka kwenye mfumo wa fikra uliolenga kwenye uyakinifu; ambamo ndani yake, kila kitu kimeainishwa na kuwekewa mipaka kwa mujibu wa uyakinifu.

Imani kuhusu kitu cha kuabudu bila shaka ni mojawapo ya vyanzo vikuu vya utamaduni na elimu ya mwanadamu. Kupendekeza imani juu ya Mwenyezi Mungu kama msingi wa falsafa ya maisha kumesababisha mabadiliko makubwa katika misingi ya jamii na fikra katika historia yote ya binadamu. Sasa, pia, katika zama za sayansi na teknolojia, ambapo mwanadamu amekwishagundua kwenda angani, idadi kubwa ya wanasayansi wanao mtazamo wa kidini kama sehemu ya mfumo wa kisomi; wamekuja kuamini juu ya kuwepo kwa muumbaji, chanzo cha viumbe vyote, sio tu kwa njia ya moyo na dhamira, bali pia kupitia maamuzi na mantiki.

Kama uthibitisho wa wayakinifu juu ya falsafa yao ya maisha ungekuwa wa kweli, badala ya kutegemea kwenye ujuzi pungufu wa historia ya fikra za uyakinifu, panapaswa pawepo na uhusiano maalumu baina ya sayansi na mwelekeo kwenye uyakinifu; ni mawazo ya kiyakinifu tu yangewakilishwa kwenye nyanja ya kisayansi. Hivi kila mwana falsafa na msomi, katika kila kipindi, alishikilia falsafa ya maisha ya ukana-Mungu na akawa mtu wa kambi ya wayakinifu. Uchunguzi wa kisomi wa maisha na kazi za wanafikra wakubwa zitatosha kuonesha kwamba fulan kwamba kambi ya kidini kwa hali yoyote haina wanasayansi wa kweli, lakini pia kwamba wanafikra wa kisayansi wakubwa na watu wengine maarufu, wakiwa ni pamoja na waasisi wa nyingi ya sayansi ya wakati huu, wamekuwa na imani juu ya mungu mmoja.

Kwa nyongeza, itikadi za kiyakinifu na ukana-mungu kwa namna yoyote zimewekewa mipaka kwenye kipindi cha mageuzi na mendeleo ya sayansi, tangu nyakati za kale na kwa kweli wakati wote wa historia, wayakinifu wamebaki katika upinzani dhidi ya muungano wa umoja wa waumini. Leo hii hasa zaidi ni katika muundo wa Umarx uliorahisishwa kwamba bidhaa

za sayansi zimegeuzwa kuwa chombo cha udanganyifu. Wale ambao mathalan wangekuwa wapange njia yao kwenye mwanga angavu wa elimu na kutathmini mambo yote kwa utambuzi na uchunguzi wa kina na wa kimantiki, katika hali ya kutokutawaliwa kabisa na ushabiki na ubaguzi wa haraka haraka - watu hawa hasa wamenaswa katika mtego wa kuvia na kuiga kijinga. Wamekataa kwa kuonyesha kiburi tu, maadili yote yaliyo bora zaidi kuliko akili na fikra, na hata wanajivunia ukanushaji wao wa kijinga.

Madai yao kwamba kuja kwa sayansi kumeondoa ile dhana ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ni ufasaha wa usemaji tu na hauhusiani chochote na utaratibu wa kimantiki, kwa sababu hata maelfu ya majaribio ya kisayansi yasingeweza kwa hali yoyote ile kutosheleza kuonyesha kwam- ba hakipatikani kuwepo kiumbe au kitu chochote kisichokuwa cha kimaada. Uyakinifu ni itikadi ya ki-metafizikia, na kwa hiyo, lazima ithibitishwe au ikanushwe kwa mujibu wa utaratibu wa kifalsafa. Kwa sababu hii haswa, ukubalikaji wa uyakinifu hauwezi kufanywa kuwa ndio msingi kwa ajili ya ukanushwaji wa metafizikia. Kutafsiri uyakinifu kwa maana kama hiyo, ni katika uchambuzi wa mwisho utakuwa hauna maana kabisa; itakuwa ni dhana ya kishirikina ikihusisha upotoshaji ukweli, na kuifikiria kama ni ya kisayansi, kwa kweli itakuwa ni uhaini kwa sayansi.

Ni kweli kwamba mpaka hivi karibuni mwanadamu alikuwa kwa kiasi kikubwa hajui vyanzo vya asili na vipengele vinavyosababisha mambo na kwamba alikuwa na utambuzi mdogo sana wa matukio yaliyojitokeza karibu yake. Lakini imani yake haikutokana na ujinga, kwani endapo ingekuwa hivyo, ile misingi juu ya kumwamini Mwenyezi Mungu ingeporomoka pale mambo fulani yahusuyo dunia yalipovumbuliwa. Kinyume chake, tunaona katika zama hizi kwamba pamoja na uvumbuzi wa miujiza mingi kuhusu maumbile, imani juu ya Mwenyezi Mungu imepanuka zaidi. Sasa sayansi inanururisha eneo finyu sana; falsafa ya maisha ya kisayansi ni ujuzi wa sehemu moja, sio ujuzi wa kitu kizima.

Sayansi inashindwa kuonyesha hali na muundo wa maumbile yote. Lakini wakati huo huo, kwa vile mtindo wa utambuzi wa kisayansi ni sahihi na wa dhahiri, imani juu ya Mwenyezi Mungu inapata asili ya kisayansi zaidi na aina mpya ya mantiki kupitia maendeleo ya sayansi. Utambuzi wa mwanadamu hupatikana kupitia uelewa wake juu ya kisababisho na athari, na mtu anayeamini katika kisababisho kilichoko chini ya kitu haiwezekani kupuuza kirahisi wajibu wa jambo la msingi ambalo linafanya kazi juu, na kuzidi visababishi vingine vyote.

Hadi hivi karibuni, mwanadamu alidhani kuwepo kwake kulikuwa ni muundo tu wenye sehemu mbili na zinazowiana vizuri sana; alikuwa haitambui miujiza yenye utata iliyokuwemo kwenye maumbile yake. Leo hii amegundua ukweli wa kustajabisha sana na wenye athari nyingi kuhusu sehemu ya ndani ya mwili wake mdogo, akitambua kwamba kuna makumi ya mamilioni ya mabilioni ya chembe chembe hai mwilini mwake. Hali hii inawezesha kuwepo mazingatio maalum juu ya utukufu wa muumba anayehusika na matokeo-sanifu haya ambayo hayakuwezekana kufanyika zamani.

Je, kuna mantiki kusema kwamba imani ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ni ya kipekee kwa wale wasiojua chochote kuhusu kubuniwa na kuumbwa kwa mwanadamu, na kwamba kinyume chake, mwana sayansi ambaye anatambua sheria za maumbile na mambo yanayohusiana na kukua na kuendelea kwa mwanadamu, ambaye anatambua kwamba sheria na mahesabu sahihi ndio yanaongoza hatua zote za uhai wa mwanadamu, analazimika kuamini kwamba mata, pamoja na kukosa utambuzi wote na fahamu, ndio chanzo cha sheria za kustaajabisha za maumbile? Hivi ugunduzi na ujuzi wa kisayansi unasababisha mwana sayansi kama huyo kuhitimisha kwamba mata ambayo haina utambuzi na ujuzi, ndiye muumbaji wa yeye na wa viumbe vingine vyote? Uyakinifu unaitazama dunia huku jicho moja likiwa limefumbwa na, matokeo yake ni kwamba, hauwezi kutoa majibu kwa mengi ya maswali.

Pia, sayansi haitoi jibu kwa lile swali la kama dunia inaweza kugawanyika katika sehemu mbili, ya kimaada na isiyo ya kimaada, au kwa swali la kama dunia ina lengo la kimaumbile. Maswali haya hayapo kwenye nyanja ya sayansi, elimu ya kisayansi inaweza kutufahamisha sisi - kwa kiwango fulani - kwamba ni nini, lakini haitaweza kutuonyesha mwelekeo katika uhai au kutuzindua na njia ya kufuatwa. Falsafa ya maisha, ya kisayansi, kwa hiyo, haiwezi kuwa msingi wa itika- di ya mwanadamu.

Tathmini ya ujuzi wa kisayansi zaidi ya yote ni ya kimatendo, kwa vile inamfanya mwanadamu aweze kutawala maumbile. Ni mifano na tathmini ya kinadharia ndio ambayo inahitajika kama msingi wa imani. Zaidi ya hayo, sayansi imeegemea kwenye majaribio na uchunguzi, na sheria zenye kuwa na majaribio juu ya msingi wao hulazimika kubadilika na kuyumba. Imani inahitaji msingi wenye umilele, ikiwa na kinga dhidi ya mabadiliko, na iwe na uwezo wa kujibu maswali kama vile asili na umbo la dunia kwa ujumla katika namna ya kuaminika na ya kudumu. Ni hapo tu ambapo mahitaji ya mwanadamu ya tafsiri na uchambuzi wa kina wa kuwa hai unaweza kutimia.

Kadiri anavyoelekea kwenye ukamilifu, mwanadamu anahitaji uwiano wa kiroho na kiakili; bila kuwa na lengo, atapotea na kwenye njia zisizo sahihi na kujihatarishia mabalaa. Mtu asiyeweza kupata lengo lake katika dini, atafuata lengo analolielewa yeye mwenyewe ambalo halitakuwa chochote isipokuwa maasi dhidi ya matakwa ya maumbile, halitahusiana na uendelevu au ukomavu wa akili.

Sababu za ukanushaji na kutoamini Vitabu juu ya historia ya dini hujaribu kufafanua kinaga ubaga mambo ambayo yamewavuta watu kwenye dini. Lakini majaribio kama hayo wanayoyafanya hayana maana yeyote na hayawezi kufichua ukweli wenyewe wa mambo. Ni muhimu kushabahia kwenye muelekeo wa asili wa mwanadamu kwenye imani ya mungu mmoja, ile sifa ya kiuhai ya jamii za wanadamu ambayo humpa mwanadamu - pamoja na tofauti zake zote ndani yake, fikira na matamanio yake - sehemu maalumu katika maumbile. Hapo ndipo inapowezekana kugundua mambo ambayo humwongoza mwanadamu kuikanyaga asili yake mwenyewe kwa kukataa dini, kwa viapo kabisa.

Mahusiano ya kidini ya mwanadamu ni matokeo ya asili yake, na uyakinifu ni kitu kinachopingana na maumbile yake. Kwa kulingana na

tabia yake ya dhahiri, binadamu atajiumbia mungu wake mwenyewe kama hatamgundua Mungu wa kweli, na mungu anayemgundua yeye anaweza kuwa ni maumbile au mambo ya kihistoria yasiyoepukika. Na mungu huyu wa uwongo anachukua nafasi ya Mwenyezi Mungu wa kweli kwa kuzingatia ufahamu na mamlaka, kufaa kwa maagizo, na uwezo wa kumwongoza mtu kwenye njia fulani na kumsogeza mbele, bila kuzuiwa na matakwa ya mtu yeyote.

Huu ndio mwanzo wa kubadilishana miungu wa uwongo, ufuasi kwenye uabudu masanamu upya, ambao ungemtoa kafara Mwenyezi Mungu kikatili kwenye historia na kubadilisha lulu kwa shanga. Inasikitisha kwamba, watu wengi waliojiangamiza kwa unyonge waliojiingiza wenyewe wakawa wameinama chini mbele ya sanamu ambalo wameliunda wenyewe na kulifanya kuwa mungu! Wamempa kisogo muumba asiye na kifani na kwa hiari yao wakakubali fedheha inayochafua ya ibada iliyoongozwa vibaya kama hiyo.

Kama tukilichunguza jambo hili kwa ukaribu zaidi, tunaona kwamba kujitokeza kwa uyakinifu huko Ulaya kama kitivo cha fikra, ukatwaji wa uhusiano wa binadamu na kanuni ilioyo tukufu, kufungwa kwao kwenye nyororo za maada, kuchagua kuendekeza sayansi mahali pa dini - yote haya yalisababishwa na mlolongo wa mambo ya kijamii na kihistoria yaliyojitokeza katika nchi za magharibi.

Mojawapo ya mambo yaliyoamsha upingaji wa mabadiliko ulioenea katika Ulaya yote na kusababisha kutokeza kwa fikra zisizofuata dini na propaganda dhidi ya dini, ilikuwa shinikizo baya mno lililowekwa na mamlaka za kikanisa mwanzoni mwa kipindi cha mwamko-sanaa juu ya wasomi waliokuwa wanaleta mawazo mapya ya kisayansi. Kwa kuongezea kwenye mafundisho maalum ya kidini, kanisa pia liliwiwa shukrani kwa ajili ya kanuni fulani za kisayansi kuhusu mwanadamu na dunia ambazo lilizirithi kutoka kwa wanafalsafa wa kale - hasa wa Kigiriki - na ambazo ziliwekwa katika ulinganifu sawa na imani za dini. Nadharia yoyote iliyojitokeza kupingana na Biblia na hizi kanuni zilizorithiwa zilifikiriwa kama za uasi, na yeyote aliyezitetea angeadhibiwa vikali.

Upinganaji wa dhahiri baina ya dini na sayansi ulianzisha uadui wa pamoja katika pande hizi mbili. Wasomi na wanasayansi waliona kwamba Kanisa la Kikristo lilikuwa linazifunga akili na fikra, na kuzuia maendeleo huru ya mawazo; kupitia kwenye ufuasi wake wa mfumo unaoogofya wa fikra na desturi ya kwenda kinyume na akili, lilikuwa linatengeneza mazingira yenye kusonga kwa ajili ya mwanadamu wa zama hizo mpya. Hivyo, mabingwa walikimbilia kwenye kujitenga kunakohuzunisha kutoka kwenye dini.

Mashinikizo haya yaliyokuwa yakilimbikizana kwa siku nyingi, hatimaye yalisababisha majibu ya vurugu zilizoikumba Ulaya yote. Hapo ndipo nguvu na utawala wa Kanisa ulididimia na uonevu wake ulikoma, uhuru wa fikira za kimagharibi ulipatikana tena na ulionyesha hisia kali dhidi ya mipaka iliyokuwa imewekwa hapo mwanzoni. Wasomi waliondoa nyororo zote za taratibu za kizamani toka kwenye shingo zao na wakatoka kwenye dini. Maumivu na hasira zote walizokuwa wamezipata zilidhihiri kwenye wimbi kubwa la uadui dhidi ya dini. Hali ya wasi wasi mkubwa wa

kiroho ilianza ambayo ilifikia kilele katika kutenganishwa sayansi na dini. Tamaa ya kisasi kisicho na mantiki dhidi ya dini kilisababisha kukanushwa kwa ukweli mwingi wa ki-Mungu na wa imani ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.

Ni kweli kwamba baadhi ya mafundisho yaliyounganishwa na dini hayakuwa na mantiki au hata msingi, yakiwa hayana uhusiano na ujuzi wa kidini uliothabiti. Lakini kulipiza kisasi juu ya Kanisa ni jambo moja na kuangukia kwenye chuki haraka na kwa makosa dhidi ya dini, kama hivyo, ni kitu kingine tofauti. Ni dhahiri kwamba kulipa kisasi, kukiwa ni jambo ambalo linatokana na hisia, halina uhusiano wowote na ufasaha wa kisomi.

Umasikini wa kiroho wa mwanadamu uliongezeka kwa kiwango kinacholingana na utajiri wake wa kisayansi na kiteknolojia. Jinsi alivyoendelea katika viwanda vingi, ndivyo maadili na nguvu yake ya kiroho vinazidi kupungua, hadi kufikia kiwango ambapo alikosa uwezo wa kimaadili wa kuweza kutumia inavyostahili ujuzi wake mpya alioupata. Ujuzi wa kisayansi haujishughulishi na maadili, mtu hawezi kuamua kazi za mwanadamu mwenye kuwajibika kwa kutumia kigezo cha sayansi. Sayansi hata ifike mbali vipi, bado haina uwezo wa kuona hata hatua moja mbele yake. Ujuzi wa kibinadamu hauwezi kufika kwenye chimbuko la dunia na kutambua kwa ufasaha yaliyomo, wala hauwezi kutabiri mustakabali wa baadaye wa mwanadamu.

Ni falsafa ya maisha ya Mungu Mmoja tu ambayo haijaribu kumfungia mwanadamu kwenye vipengele vya kimaada vya maisha yake. Kinyume chake kupitia kwenye ishara na dalili ambazo mwanadamu amepewa ili zimwongoze katika njia yake, imani ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, inaonyesha utukufu wa asili na mustakabali kwa ajili ya mwanadamu.

Mara tu mwanadamu anapoingia kwenye njia ya kumwamini Mwenyezi Mungu, hupata falsafa ya maisha pana ndani ya mfumo ambamo huweza kupata majibu kuhusu swali lake la msingi la ki-uchunguzi. Mara akishafikia hatua hii ya imani pana na yenye vipimo vingi, maisha yake mwanadamu huchukua juhudi mpya na maadili ambayo ndio matunda mazuri ya hiyo falsafa ya maisha huja kuwa kweli. Mapambano na kanisa yalikuwa kwa hiyo, kipengele kimoja katika kutenganisha sayansi na dini. Kundi lingine liliitekeleza dini na kukimbilia kwenye uyakinifu kwa sababu mawazo yaliyoshauriwa na Kanisa hayakuwa sahihi na hayaku- tosheleza, yaliyokosa na maadili yaliyo nje ya uwezo wa mwanadamu.

Mawazo haya kwa kawaida yalionekana kutokubalika na yasiyovutia kwa watu wenye akili. Kanisa lingemwonyesha Mwenyezi Mungu katika hali ya maada na kibinadamu kwa maana ambayo ilipingana na haja ya mwanadamu juu ya maadili kamili na kule kujitahidi kupenya na kuvuka mifumo yote yenye kuweka mipaka. Hapawezi kuwa na shaka kwamba endapo ukweli usiopingika unaingizwa kwenye ubongo wa mtu katika muundo wa hekaya wenye dosari, mtu huyo atakwenda kinyume nao mara tu atakapofika ukomavu wa kiakili.

Wakikabiliwa na taswira ya Mungu mwenye kupachikwa umbo la kibinadamu, iliyotengenezwa katika theolojia ya Ukristo, kutukuza imani zaidi kuliko matumizi ya akili na msisitizo kwamba imani lazima itangulie akili, watu walioelimika walitambua kwamba jitihada hizi zitokanazo na

akili finyu, kwa lengo la kuzuia matumizi ya busara na sayansi katika ukiritimba wa theolojia ya Kikristo hazikuendana na kigezo cha mantiki na mbinu ya kisayansi. Kwa vile hazikuwa na chanzo thabiti ambacho kutokana nacho wangejifunza mafundisho ya kweli kuhusu Mwenyezi Mungu, yote yakiwa huru kabisa kutokana na taasisi za Kanisa na vitabu vyake vipotovu, na kwa kuwa hawakuwa na njia ya kuwafikisha kwenye mfumo ulio bora zaidi ambao ungeweza kutosheleza mahitaji yao ya kiroho na kimwili na kuwapa muundo unaofaa kwa ajili ya kuunganisha vipengele vyote muhimu vya maisha, vya kimwili na kiroho, hisia na kiakili, falsafa ya maisha ya uyakinifu iliota mizizi ndani yao, na kuwaelekeza kukana maadili yote yaliyo nje ya uwezo wa kibinadamu na yaliyo zaidi kinyume cha ubinadamu.

Walikuwa hawatambui kwamba ingawa kosa hupotosha dini wakati linapofuata njia ya ujinga, dini ya ukweli, isiyokuwa na uwongo wowote, ushirikina na upotovu inaweza kumkomboa mwanadamu kutoka kwenye utumwa wa visasili na ushirikina, na kumshikilia kwa umadhubuti kwenye mhimili wa imani ya kweli na kumpatia uelewa sahihi wa mafundisho yahusuyo Mwenyezi Mungu, ambayo hutosheleza akili yenye udadisi. Badala yake, wasomi wa nchi za Magharibi walitambua upande moja tu wa ushirikiana wa dini ya uwongo na jinsi mfumo ulioundwa wa imani wa dini, usio na kuswali, ulivyokosa kuwa na msingi wa kimantiki, kwa hiyo hawakusita kushutumu dini kwamba haina msingi wowote. Uamuzi wao uliegemezwa kwenye ile hali halisi ya kukatisha tamaa iliyomo kwenye dini yao wenyewe, na uamuzi huo haukuweza kushindwa kuwa wa haraka, usio wa kweli, usio na busara na mantiki.

Haya yamefafanuliwa ifuatavyo na msomi wa fiziolojia na biokemia: "Ukweli kwamba wasomi fulani hawakuongozwa, katika njia ya utafiti wao, kwenye utambuzi wa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, una sababu nyingi sana. Hapa tunataja mbili miongoni mwa hizo. Kwanza; hali ya kisiasa iliyotengenezwa na udikteta, pamoja na hali zinazoambatana na mambo ya kijamii na kiutawala, zilielekea kumsababisha mwanadamu kukana kuwepo kwa Muumbaji. Pili, mawazo ya mwanadamu wakati wote yamekuwa yakivutiwa na njozi fulani na uwongo, na ingawa mwanadamu anaweza kuwa hana woga wa maumivu makali ya kiroho na kimwili, bado hana uhuru kamili wa kuchagua njia iliyonyooka.

"Katika familia za Kikristo, watoto wengi huamini kuwepo kwa Mwenyezi Mungu afananaye na mwanadamu, kana kwamba mwanadamu aliumbwa katika umbo la Mwenyezi Mungu. Wanapoanza kuingia kwenye nyanja ya sayansi na kujifunza na kutekeleza fikira za kisayansi, hawawezi tena kupatanisha dhana yao dhaifu ya kumpa Mwenyezi Mungu viungo vya mwanadamu na ushahidi wa kimantiki na mbinu za sayansi. Kwa hiyo baada ya muda fulani, wakati ambapo matumaini yote ya kupatanisha imani na sayansi yanatoweka, wanaitelekeza kabisa fikira yote ya Mwenyezi Mungu na kuifuta kabisa kwenye akili zao. "Sababu yake kubwa ni kwamba ushahidi wa mantiki na aina za sayansi hazirekebishi hisia na imani zao za mwanzoni, lakini badala yake, huwafanya wahisi kwamba walikosea katika imani yao ya mwanzo kuhusu Mwenyezi Mungu. Kwa mvuto wa hisia hizi, ikiunganishwa na mambo mengine ya kisaikolojia, wanashangazwa na

upungufu wa fikra zao na huachana kabisa na majaribio ya namna yoyote ya kumjua Mwenyezi Mungu.[1].

Kwa hiyo, wanasayansi, walijaribu, kwa kufafanua aina zote za sheria na fomyula na kutoacha nafasi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na dini katika kutafuta ufumbuzi wa maswali yanayogusa kuwepo uhai na maumbile. Walijaribu kukatisha matumaini ya wanadamu kutoka kwenye dini na kumweka kando Mwenyezi Mungu katika kuwa na wajibu wowote katika utendaji wa ulimwengu na mpango wa maumbile.

Kila walipofikia kukwama walijaribu kutafuta ufumbuzi wa tatizo kwa kutumia nadharia tete mbali mbali au kuahirisha ufumbuzi bayana wa tatizo hadi hapo utafiti mkubwa zaidi utakapokuwa umefanywa. Walidhani kwamba kwa njia hii walikuwa wanaepuka kujisalimisha kwenye fomyula isiyo ya kisayansi na ushirikina. Hivyo, ingawa waliepuka hatari ya kukubali ushirikina, kwa masikitiko walianza kupiga vita upagani na ukana-Mungu.

Ingawa imani juu ya Mwenyezi Mungu na kuamini katika kanuni ya uasilishaji ni jambo la kawaida na msingi kwa mwanadamu, haliwezi kulinganishwa na mahitaji ya kimaada ambayo mwanadamu wakati wote anajitahidi kuyapata. Liko tofauti kabisa na maisha ya kimaada, na kwa kuwa ni hitajio la ndani ya mwanadamu, linahusiana na namna tofauti kabisa. Zaidi ya haya, ni rahisi kukanusha kitu kisichoonekana kwa macho kuliko ilivyo kwa kukithibitisha, tukichukulia kutoweza kwetu kukielezea vya kutosha. Watu wanaokosa uwezo wa kiakili, kwa hiyo, huchagua njia rahisi na isiyo na usumbufu ya kukataa badala ya kujitahidi kutumia akili. Njia ya kukanusha aidha, haihusishi madhara yoyote yaliyodhahiri. Kwa kugeukia mbali na Mwenyezi Mungu, watu pole pole hujenga msimamo wa ukaidi na uadui kwenye dini, ulioathiriwa na ushabiki. Athari kubwa za msimamo kama huo zinaweza kuonekana kwa urahisi kwenye hoja zenye uovu za wale ambao wameipa mgongo dini.

Pia ni rahisi zaidi kukana kitu kisichoonekana kwa sababu kukithibitisha kuwepo kwake kutamaanisha wajibu mbali mbali kwa mwanadamu, wale wanaotaka kuzitupilia mbali wajibati hizo, kwa urahisi hukataa kuwepo kwa kanuni ya uanzishaji. Qur'anii inasema:

بَلْ يُرِيدُ الْإِنسَانُ لِيَفْجُرَ أَمَامَهُ ﴿٥﴾ يَسْأَلُ أَيَّانَ يَوْمُ الْقِيَامَةِ ﴿٦﴾ فَإِذَا بَرِقَ الْبَصَرُ ﴿٧﴾

"Lakini mtu anataka tu kuendelea na maasi kwa siku zilizioko mbele yake. Anauliza: Lini itakuwa hiyo Siku ya Kiyama? Basi jicho litapoduwaa." ( Qiyama:75: 5-7).

Mafundisho ya wale wataalamu wa kujihini, wajinga na wasio na mantiki pia hayawezi kutoonekana kama kipengele kinachosukuma vikundi fulani vya watu kuelekea kwenye uyakinifu. Zile silika zinazokuja kuwepo pamoja na maisha ya kawaida ya mtu ambazo zimefungamanishwa na uhai wake, si tu kwamba hazikosi maana na lengo; zenyewe pia ni nguvu ya kuumua na kuandaa takdiri, kipengele cha maendeleo na msogeo, ambacho ndio humsukuma mtu na kusonga mbele kuelekea kwenye lengo lililozingatiwa katika kuumbwa kwake. Ni kweli kwamba, mtu hatakiwi kuwa mtumwa

1. Isbat-i Vujud-i Khuda, Uk. 60.

aliyefunikwa macho kwenye silika zake kama mfungwa ambaye uhai wake wote na nyendo vinadhibitiwa na mwangalizi wa jela. Lakini, pia hapaswi kupigana vita na ukweli wa uhai wake mwenyewe na kutafuta kuzuia shughuli zote na nyendo kwa upande wa silika zake. Uhai wa mwanadamu wenye matunda mazuri, kwa kweli hutegemea juu ya kuwepo hai katika maisha yake kwa silika zake, zilizoenea kwa uwiano unaofaa; kuzuia silika kunasababisha utata na uharibifu wa haiba ya mtu.

Falsafa ya maisha iliyokuwepo kwenye Ukristo katika kipindi cha kati ilikuwa kwenye msingi wa maelekezo ya mazingira pekee ya Akhera ambayo yaliingiza na ushushaji thamani wa dunia ya kimaada. Sasa, matokeo yatakuwaje endapo mtu anakanusha uhalali wote wa nguvu za silika, kwa jina la Mwenyezi Mungu na dini, akajaribu hata kuziharibu kabisa; kama mtu anatukuza useja na maisha ya utawa na akakanusha hadharani ndoa na kuzaana kama ni uchafu, shughuli yenyewe hasa ambayo ndiyo inayolinda uhai wa spishi mbali mbali; na kama mtu anaona umasikini na kutojiweza kama ndio uhakikisho wa furaha ya hali ya juu? Je, kwa hiyo, itawezekana kutegemea dini kuchukua jukumu mashughuli na endelevu?

Jukumu halisi na kazi ya dini ni kusafisha, kuongoza na kudhibiti silika, kuwekea mpaka wa eneo la ushughulikaji wao, na kuzitakasa na upotofu na uovu wote. Sio kuziharibu na kuziondoa kabisa. Kwa kuzidhibiti silika na kujitahidi wakati wote kujinasua mwenyewe kutoka kwenye mtego unaoweza kuwepo, mwanadamu hujitengenezea hatima yake yenye lengo. Endapo mwanadamu anashindwa kufanya hivi, mgongano mkubwa wa silika ndani mwake ni mkubwa mno hivyo kwamba hawezi kuwa mdhibiti wa nafsi yake mwenyewe kwa urahisi. Kwa hiyo, anahitaji mfumo wenye maarifa mengi juu ya elimu ya maadili. Kwa upande moja binadamu anapatwa na mvuto wa shauku ya kidini, hali hii, humtiisha kwa siri na huzikusanya pamoja zile nguvu zake zilizotawanyika, kwenye mshiko wa uwezo wake, na kuzielekeza kwenye kupata maadili na manufaa. Kwa upande mwingine binadamu pia anapatwa na mvuto wa silika zake.

Katika jamii yoyote ambamo watu wakati wote wanaambiwa, kwa jina la Mwenyezi Mungu na dini, kwamba njia ya kwenye furaha ipo katika kuzikataa zawadi za dunia hii, mwanya unajitengeneza wenyewe kwa ajili ya maendeleo ya uyakinifu na umakinifu zaidi juu ya thamani ya vitu vya kimaada, ili kwamba zile fikra tukufu za dini, pamoja na athari zake zenye kufika mbali, zitoweke kwenye mazingira.

Lakini, hii haiwakilishi mantiki halisi ya dini. Dini za kweli huelekeza mazingatio ya mwanadamu kwenye maadili thabiti ya kiroho, yakijiegemeza katika imani juu ya muumbaji na kumpatia mtu mafundisho mapana na kanuni kwa ajili ya maisha yake. Maadili haya hupanua uwanja wa uoni wake hadi kwenye mipaka ya eneo la ki-mbingu, na kumtoa kutoka kwenye utumwa wa kuabudu matamanio yake mwenyewe na anasa za kidunia (uyakinifu), na wakati huo huo, yanamruhusu afurahie starehe za kidunia kwa kiasi cha kutosheleza tu.

Baadhi ya watu wanadhani kwamba starehe holela juu ya vitu fulani ambavyo vimepigwa marufuku na dini itawahakikishia kudumu furaha yao. Wanafikiri kwamba dini inapigana kwa ukaidi dhidi ya starehe zote na

haiko tayari kukubaliana raha za dunia hii, kana kwamba Mwenyezi Mungu anamlazimisha mwanadamu kuchagua kati ya furaha ya hapa duniani na furaha ya Akhera. Mwelekeo huu kwenye dini ni wa unapotoshaji kabisa usiowezekana kuwa kweli. Ikiwa dini kuwajibika katika jitihada za binadamu na uchaguzi wake wa mwelekeo, ni kwa sababu kujiendekeza kusikozuilika kwenye matamanio, kujisalimisha bila masharti kwenye silika na hamu, na utiifu kwenye amri za umimi, hutia giza maisha ya mtu na humpeleka kwenye hali ya utumwa wa kutojitambua. Licha ya asili yake safi kimsingi, anaanguka kutoka kwenye daraja lake halisi na kukengeuka kutoka kwenye njia yake ya kweli. Kama kule kujiendekeza kiholela kwenye silika za matamanio kungekuwa sio sababu ya mateso ya milele na kujivunjia hadhi kuchungu, kusingeweza kukatazwa.

Ni fikira kama hizi ambazo zinafanya iwezekane kuelewa ni kwa nini dini imekataza mambo fulani na ni jinsi gani starehe ya dunia ilivyo na ulinganifu na furaha ya Akhera. Fikira kama hizi hutumika katika kumlazimisha wajibu fulani juu ya mwanadamu. Jaribio ya kutekeleza matendo ya faradhi ya ibada, kwa uaminifu na bila unafiki, huleta mabadiliko ya ndani kabisa mwa mtu, lengo la matendo haya kwa namna yoyote sio kupunguza furaha ya mtu ya kidunia.

Kuabudu ni sawa na tufani kali kwenye dimbwi (wangwa) tulivu la moyo, inayobadilisha tabia ya ndani ya mwanadamu na kigezo chake cha maamuzi. Ndiyo jiwe la pembeni ambapo msingi wa dini huimarishwa, mazoezi ya kuelimisha yenye manufaa yanayopenya kwenye vina virefu vya nafsi. Upanga wake mkali hukata fundo la upotofu na udhalili ndani ya binadamu na kumwezesha yeye kukimbilia eneo pana na safi, lisilo na mipaka. Kwa ufupi humwezesha mwanadamu kukua na kufikia ukomavu halisi.

Si tu kwamba hakuna mikinzano kati ya mambo ya maisha na yale ya kiroho; mambo ya kiroho yanafaa sana kwenye maisha ya furaha kubwa zaidi hapa duniani. Inaweza kuwa labda kwamba mafundisho yasiyoaminika na yasiyo na mantiki ya Ukristo yameathiri mielekeo ya kinyume na dini ya watu kama Betrand Russell. Kwa dhahiri aliamini kwamba kumwamini Mwenyezi Mungu ni kujitakia huzuni, kama inavyodhihirika katik a maneno yafuatayo: "Mafundisho ya Kanisa yamefanya binadamu achague baina ya aina mbili ya mateso na umasikini. Ama mateso ya hapa duniani na kukosa starehe zake au mateso ya maisha ya akhera na kukosa furaha ya peponi.

Kuhusu Kanisa, mojawapo ya aina hizi mbili za mateso lazima na muhimu ivumiliwe. Ama mtu lazima ajisalimishe kwenye mateso ya hapa duniani na kuteseka kwa umasikini na upweke ili aweze kufurahia starehe za akhera, au, ikiwa mtu anataka kufurahia starehe za dunia hii lazima akubali kwamba atanyimwa starehe za akhera." Ueneaji wa maoni kama haya, ambayo yanadhihirisha ujinga mkubwa sana na wa kina falsafa ya maisha kidini, kunaweza kuamua hatima ya dini iliopo katika jamii fulani. Athari za maoni haya kwa itikadi na matendo ya binadamu ni nzito sana kuweza kupimwa vizuri, kwa mtazamo wa mpito wa juu juu. Muundo huu wa fikira umesababisha mazingatio ya mwanadamu kuelekezwa kipekee kwenye nyanja ya kimaada - awe anatambua au hatambui. Umakinifu

unaojitokeza juu ya starehe na anasa umesababisha kudhoofika kwa mambo ya kiroho na maadili.

Dini haimshutumu mtu kuvumilia mojawapo ya aina mbili hizi za mateso. Inawezekana kabisa kuunganisha furaha ya dunia hii na ya Akhera. Kwa nini, Mwenyezi Mungu Ambaye hazina yake ya huruma na neema haipungui, asitake waja Wake wapate furaha kamili ambayo inakusanya dunia hii na Akhera? Hivi ndivyo kwa usahihi hasa anavyopenda Yeye.

Jambo lingine katika kuenea kwa fikira za kiyakinifu limekuwa ni uendekezaji wa tamaa na kuzama kwenye shimo la ashiki. Kila utambuzi wa kiakili na mawazo hufanya msingi wa baadhi ya matendo ya nje; njia ya matendo ya mwanadamu huchukua umbo la njia ya mvuto wa itikadi zake. Kinyume chake matendo na maadili ya mwanadamu pia huleta mabadiliko yenye ubora katika tabia yake ya kiakili na muundo wa fikira. Mtu anayeabudu matamanio yake polepole atapoteza mawazo yote matukufu kuhusu Mwenyezi Mungu. Mara tu anapochagua mhimili wa uhai wake kinyume na Mwenyezi Mungu na kudhania kwamba chochote kilichopo katika dunia hii, kimetupwa hivi hivi tu juu yake, bila madhumuni yoyote, hivyo kwamba wazo la kuwa na lengo katika maisha linakuwa halina maana kabisa, huanza kutoa uwezo wake wote wa kiakili katika kufanya starehe kwa wingi zaidi. Kutumbukia huku kunakofedhehesha, kwenye kiwango cha chini cha maisha, kunanyausha mizizi ya matumaini yote kwa ajili ya makuzi na maendeleo.

Mawazo ya kumwamini Mwenyezi Mungu; kwa kulinganisha, ni kama mbegu ambayo inahitaji udongo unaofaa ambamo inaweza kumea. Mbegu hiyo inaweza tu kustawi kwenye mazingira safi, mazingira ambamo mwanadamu anaweza kupata kwa haraka na urahisi kiwango cha ubora ambao ni wa kipekee kwake, kwa sababu ya muundo ambamo kanuni za maisha yake zimewekwa. Imani ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, haiwezi kustawi kwenye mazingira yaliyo jaa uovu.

Mojawapo ya vipingamizi vinavyo mzuia mtu asipate kumjua Mwenyezi Mungu na sababu za mwanadamu kukanusha kuweko huku, pamoja na kuwepo dalili zilizowazi na ushahidi wenye maamuzi ambao upo, kwa hiyo, ni kujisalimisha kwenye dhambi na kuendekeza matamanio. Imam Jafar as-Sadiq (a.s) alisema alipomjibu Mufadh'dhal ndani ya Risalah-yi Ahlija: "Ninaapa kwa nafsi yangu mwenyewe kwamba Mwenyezi Mungu hajashindwa kujijulisha Yeye kwa wasiomjua, kwani wanaona ushahidi dhahiri na ishara zisizo na shaka za Muumba katika mumbile Yake na wanatazama mambo ya ajabu katika Ufalme wa angani na duniani ambayo yanaelekeza kwa Muumba wao.

"Watu wajinga ni wale ambao wamefungua milango ya dhambi mbele yao na wakafuata njia ya kujiendekeza kwenye tamaa na ashiki. Matamanio ya nafsi zao yametawala nyoyo zao, na kwa sababu ya dhulma zao juu ya nafsi zao wenyewe shetani amechukua mamlaka juu yao. Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri nyoyo za waovu."[1]

Tamaa ya starehe, ushindani, ubadhirifu, mantiki dhaifu ya waumini fulani wasio na elimu - hawa pia ni miongoni mwa vipengele

---

1. Biharul-Anwaar, Juz. III, uk.152.

vinayomlazimisha mwanadamu kukimbilia uyakinifu. Ghasia na mchafuko wa maisha, wingi wa bidhaa zinazozalishwa, utajiri na mamlaka, mielekeo ya maisha ya kisasa inayozuzua na kushughulisha, kuenea haraka kwa vitu vya anasa na starehe - yote haya yanawafunikiza kabisa watu walafi. Watu hawa wanajaribu kabisa kujitoa kwenye mazingira ya masuala ya kidini na hukataa kukubali mamlaka ya madaraka yoyote makubwa zaidi, kwani si tu kwamba hii isingewaletea manufaa yoyote ya kidunia, bali pia ingeshika hatamu kwenye mawimbi ya matamanio yao yaliyokomaa.

Kwenye mazingira ambayo watu wamezama kwenye dhambi, ufujaji, na uovu, na wakakataa kukubali mipaka yoyote inayotawala matendo yao, dini itabakia jina tu. Watu wanaojiendekeza na wayakinifu hawawezi kuwa wenye kumtafuta na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Wakati ambapo mojawapo ya kanuni mbili zinazopingana; kanuni ya kusaka anasa na ile ya kumwamini Mwenyezi Mungu, inapokuwa imetawala nafasi ya akili ya mhusika, kanuni nyingine lazima iondoke humo. Mara tu moyo wa kuabudu unapokuwa katika maisha ya mwanadamu, huiondoa mielekeo yote ya kiyakinifu kwa kuzikata pingu imara za matamanio duni na wakati wote hutia msukumo juhudi ya mtu kupanda kuelekea kwenye lengo lake. Hivyo, muundo kamili wa uhuru wa binadamu wa kutoka kwenye utumwa na kuingia kwenye hali ya asilihujitokeza.

Jinsi lengo analojiwekea mtu mwenyewe linavyokuwa la juu na la mbali zaidi, ndivyo mwelekeo wa kuliendea utakavyo kuwa mkali zaidi na ndivyo jitihada inayohitajika ili kulifikia itakavyozidi kuwa kubwa zaidi na ya muda mrefu zaidi. Kwa hiyo, kama tunamchagua Mwenyezi Mungu kama lengo letu, tutakuwa tumechagua lengo la hali ya juu lisilo na ukomo, na njia inayoelekea kwenye mafanikio ya lengo hilo vivyo hivyo itakuwa haina ukomo, ingawa njia hiyo ni wazi na iliyonyooka wakti huo huo.

Ni lengo ambalo litajibu matatizo na maswali mengi, na kwa kuwa litatulazimisha kukataa udhalimu wa nafsi, utatupatia uhuru kamili juu yetu. Kama tukimkubali Mwenyezi Mungu kama ndio lengo letu, uhuru utapatanishwa na makuzi na maendeleo yetu. Juhudi zetu za kujiendeleza na kupiga hatua zitakuwa na maudhui na maana, kwa msaada wa silika za kiungu na tamaa ya uzima wa milele. Kwa ufupi, tamaa ya kupiga hatua na maendeleo, mara tu inaporekebishwa na ibada ya Mwenyezi Mungu, ama kwa hakika haipingani na uhuru wa binadamu wala haiishii kwenye yeye kuwa mtumwa.

Tunaweza kudai kuwa tumepata uhuru hapo tu tunapokuwa tunakwenda sambamba na kusonga mbele kwa ujumla kwa dunia yote kuelekea kwenye ukamilifu, kwa akili, na utambuzi kamili wa manufaa yatakayoletwa na hatua hii. Kufanya matendo kwa kutii hali ya asili au kwa kutoepukika kwa historia sio uhuru, kwani wakati mwanadamu anapoacha kujali ustawi wake mwenyewe kwa kufuata maamuru ya maumbile, hili si jingine mbali na utumwa au utii wa kijinga.

9

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA TISA

### QUR'ANII INAMUWASILISHAJE MWENYEZI MUNGU

Tunapotaka kutathmini tabia na ujuzi wa kisayansi wa msomi, tunapima kazi zake na kuzichunguza kwa karibu zaidi. Vivyo hivyo, ili tuweze kupima kipaji, ubunifu na uwezo wa msanii wa kuvumbua michoro bunifu, tunafanya uchunguzi wa bidhaa zake za kisanii.

Kwa njia hiyo hiyo, tunaweza pia kutambua sifa na tabia za nafsi halisi ya Muumba kutokana na sifa na mpangilio ulioenea katika maumbile yote, pamoja na ustadi na utaratibu wake. Hapo, ndani ya mipaka iliyowekwa na uwezo wetu wa kujua na kutambua, tunaweza kufahamu ujuzi wa Mwenyezi Mungu, hekima, uhai na uwezo.

Endapo likiwa ni suala la ujuzi kamili na mpana juu ya Mwenyezi Mungu basi, kwa kweli, lazima tukubali kwamba uwezo wa mwanadamu wa kujua haufikii kiwango hicho. Sifa za Mwenyezi Mungu haziwezi kuwekwa ndani ya mipaka yoyote inayofahamika, na ulinganisho wowote au mfanano tunaoutoa juu ya sifa hizo hauna budi uwe wa uwongo, kwani chochote kinachoweza kuchunguzwa na sayansi na fikira katika nyanja ya maumbile ni kazi ya Mwenyezi Mungu na matokeo ya utashi na amri yake, ambapo dhati yake sio sehemu ya maumbile na haitokani na aina ya vitu vilivyoumbwa. Hivyo, dhati ya Mwenyezi Mungu haiwezi kueleweka kwa mwanadamu kwa njia ya ulinganisho na analojia - mfanano na kilichotangulia kuwepo.

Kwa ufupi, Yeye ni nafsi Ambaye kwa elimu ya dhati Yake hakuna kipimo au kigezo chochote kilichopo na kwa ukadiriaji wa uwezo Wake, mamlaka na ujuzi Wake, hatunazo tarakimu wala takwimu zake. Hivi, mwanadamu ni duni sana na asiye na uwezo wa kutambua kitu chochote cha dhati na sifa za ukweli wenye kutokeza kiasi hiki? Kukubali udhaifu wa uwezo wetu na kutoweza kwetu kupata elimu kamili, ya kina na pana ya Mwenyezi Mungu haimaanishi kwamba tumenyimwa kila aina ya ujuzi, uwe mdogo kiasi gani.

Mpangilio wa utaratibu wa ulimwengu unatangaza kwa sauti kubwa sifa Zake kwetu, na tunaweza kuuelewa uwezo na ubunifu usio na mipaka wa Mola Mlezi kutoka kwenye uzuri na manufaa ya maumbile. Maajabu yanayoonekana, kwetu sisi ni dalili ya Dhati Yake ya kipekee.

Mazingatio ya utashi, utambuzi ujuzi na upatanifu wa asili katika mpangilio wa maumbile na mambo yote mbalimbali ya maisha, hufanya iwezekane kwetu kutambua kwamba sifa zote hizi - pamoja na vipengele vingine vyote vinavyozungumzia lengo, mwelekeo na madhumuni ni muhimu vitoke kwenye utashi wa Muumbaji Ambaye Yeye Mwenyewe anazo sifa hizi kabla hazijaakisiwa katika kioo cha maumbile.

Kile kinachokuja kumjua Mwenyezi Mungu na kugusa nafsi Yake ni uwezo usio kifani wa fikra - mwanga wa ghafla ambao kutokea kwenye kile chanzo cha kabla ya umilele ukamulika juu ya mata na kuipatia uwezo wa kupata ujuzi na kusonga mbele kuelekea kwenye ukweli. Ni kutoka ndani ya

zawadi hii kuu ya ki-Mungu ambamo elimu ya Mwenyezi Mungu inadhihirishwa.

Uislamu hushughulika na elimu ya Mwenyezi Mungu kwa njia ya wazi na ya simulizi. Qur'ani, chanzo cha msingi wa kujifunzia falsafa ya maisha ya Kiislamu, inatumia mbinu ya kukana na kuthibitisha kwenye swali hili. Kwanza ilikana, kwa njia ya ushahidi wa kusadikika na dalili, kuwepo kwa miungu ya uwongo, kwa sababu katika kuyaendea mafundisho ya juu sana ya upweke, kwanza ni lazima kukana aina zote za miungu ya uwongo na ibada ya mwingine mbali na Allah. Hii ndio hatua ya kwanza muhimu katika njia ya kuuelekea upweke.

Qur'ani inasema:

أَمِ اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ آلِهَةً ۖ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ ۖ هَـٰذَا ذِكْرُ مَن مَّعِيَ وَذِكْرُ مَن قَبْلِي ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ الْحَقَّ ۖ فَهُم مُّعْرِضُونَ ﴿٢٤﴾

"Au wanawaabudu miungu mingine badala yake? Sema: Leteni ushahidi wenu! Huu ni ukumbusho wa hawa walio nami, na ukumbusho wa walio kabla yangu. Lakini wengi wao hawaijui kweli, na kwa hiyo wanapuuza." (Anbiya:21:24).

قُلْ أَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا ۚ وَاللَّـهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٧٦﴾

"Sema: Je! Mnawaabudu, badala ya Mwenyezi Mungu, wale ambao hawawezi kukudhuruni wala kukufaeni? Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kujua." (Maida:5:76).

Yule ambaye amevunja uhusiano wake na upweke wa Mwenyezi Mungu husahau pia, nafasi yake halisi kuhusiana na dunia na uhai na nafasi hiyo inakuwa imetenganishwa na yeye mwenyewe. Kwani namna mbaya kabisa ya mfaraka binafsi ni kukata viunganisho vyake vyote na hali yake ya asili kama mwanadamu. Kinyume chake, pindi mtu anapotenganishwa na asili yake mwenyewe, kwa athari ya mambo ya ndani na ya nje, pia atatengwa na Mungu wake na kufanywa mtumwa na asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

Kujiweka chini ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ndipo basi huchukua nafasi ya fikira yote ya kimantiki. Hii inawakilisha kugeuka na kuanza kuabudu maada, kwani kuabudu sanamu na kuweka ubora kwenye maada, zote ni aina za muanguko ambao unamnyang'anya mwanadamu uwezo wake wa asili wa ukuaji.

Tauhiid (Upweke wa Mungu mmoja) tu, ndio nguvu inayomwezesha mwanadamu kukamata tena uumbwaji wa maadili ya binadamu. Kwa kuirudisha tena hadhi yake halisi, mtu huingia katika hali ya uelewano na asili yake mwenyewe ya kibinadamu na asili ya msingi ya viumbe wote, hivyo kufikia muundo kamilifu zaidi wa uhai ukiwa wazi kwa ajili yake. Katika historia yote, miito yote na vuguvugu za kidini zilianza kwa kutangaza upweke wa ki-ungu na utukufu pekee wa Mwenyezi Mungu.

Hakuna fikra ambayo imepata kutokea kwa mwanadamu ambayo ni yenye kuleta matunda zaidi ya utambuzi wa ubunifu na wenye kuhusika zaidi kwenye maeneo mbalimbali ya maisha ya binadamu, kizuizi chenye nguvu zaidi katika upotovu wa mwanadamu, kuliko dhana ya upweke wa Mwenyezi Mungu. Kwa kutumia ushahidi wa wazi kabisa, Qur'ani

inamwonyesha mtu njia ya kupata elimu juu ya Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ ﴿٣٥﴾ أَمْ خَلَقُوا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ بَل لَّا يُوقِنُونَ ﴿٣٦﴾

"Ama wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji? Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini." (52:35-36).

Qur'ani inamwachia mwanadamu atumie fikira na akili yake ya kawaida ili atambue uwongo wa nadharia mbili hizi - kama mwanadamu ametokea kuwepo mwenyewe tu vivi hivyi, au kama alikuwa amejiumba yeye mwenyewe - kwa kuzifanyia majaribio na kuzichanganua kwenye maabara ya akili yake. Kwa kutafakari juu ya dalili na ishara za Mwenyezi Mungu, atatambua kwa uhakika uliowazi na dhahiri kabisa kile chanzo cha maumbile yote na kuelewa kwamba hakuna tathmini yoyote inayoweza kutolewa juu ya mtindo wowote wa ulimwengu isipokuwa pawepo na akili inayopanga na yenye uwezo inayofanya kazi nyuma yake.

Kwenye Aya zingine, mazingatio ya mwanadamu yameelekezwa kwenye jinsi alivyoumbwa na kutokeza kwake pole pole kutokea kwenye hali ya kutokuwepo kabla. Hivyo, anakuja kutambua kwamba uumbwaji wake wa kipekee, pamoja na maajabu yote uliyonayo, ni dalili na ishara za utashi wa ki-ungu usiyo na ukomo, miale inayopenyeza na kugusa viumbe vingine vyote. Qur'ani inasema:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ مِن سُلَالَةٍ مِّن طِينٍ ﴿١٢﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَّكِينٍ ﴿١٣﴾ ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ عِظَامًا فَكَسَوْنَا الْعِظَامَ لَحْمًا ثُمَّ أَنشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ فَتَبَارَكَ اللَّـهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ ﴿١٤﴾

"Na kwa yakini tumemuumba mwanadamu kutokana na asili ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaliumba tone kuwa damu iliyoganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa na mifupa tukaifunika na nyama. Kisha tukamfanya kiumbe kamili. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu, Mbora wa waumbaji." (23:12-14).

Wakati ambapo kijusi (mimba) kinapokuwa tayari kuanza kupata mwili na umbo, chembehai zote za macho, masikio, ubongo na viungo vingine, huanza kufanya kazi na huanza utendaji wao usiyo na ukomo. Huu ndio ukweli ambao Qur'ani inaelekeza mazingatii ya mwanadamu. Halafu, Qur'ani inamuuliza mwanadamu swali la kwamba kama maajabu yote haya yanaendana na ile nadharia ya kwamba hakuna Mungu.

Wala sio suala la kwamba mambo kama haya yanathibitisha na kuonesha, kwa msisitizo mkubwa, kuwepo na haja ya mpango, usanifu, mkono unaoongoza ukisukumwa na utashi makini? Hivi inawezekana kwamba chembe hai za mwili ziweze kujifunza kazi zao, zifuatilie malengo yao kwa mtindo sahihi na mpangilio, na kujidhihirisha kimuujiza kiasi hicho katika ulimwengu wa viumbe, bila ya kuwepo nafsi yenye utambuzi na uwezo mkubwa na ambayo inatoa maelekezo?

Qur'ani inajibu swali hili ifuatavyo:

هُوَ اللَّـهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ ۖ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۚ يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٤﴾

"Yeye ndiye Muumbaji, Mtengenezaji, Mtiaji sura, Mwenye majina mazuri kabisa. Kila kilichoko katika mbingu na ardhi kinamtakasa, naye ni Mwenye kushinda, Mwenye hikima." (Hashir:59:24).

Qur'ani inaelezea kila jambo la hisia ambalo mtu analiona karibu yake kama ni kitu kinachohitaji kutafakari na kupata hitimisho lake:

وَإِلَـٰهُكُمْ إِلَـٰهٌ وَاحِدٌ ۖ لَّا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَـٰنُ الرَّحِيمُ ﴿١٦٣﴾ إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنفَعُ النَّاسَ وَمَا أَنزَلَ اللَّـهُ مِنَ السَّمَاءِ مِن مَّاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِن كُلِّ دَابَّةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيَاحِ وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٦٤﴾

"Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hapanaa Mungu ila Yeye. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na kuhitilafiana usiku na mchana, na marikebu ambazo hupita baharini kwa viwafaavyo watu, na maji anayoyateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na akaeneza kila aina ya wanyama; na katika mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayoamrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi, bila shaka humo zimo Ishara kwa watu wanaozingatia" (Baqarah :2:163-164.

قُلِ انظُرُوا مَاذَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ وَالنُّذُرُ عَن قَوْمٍ لَّا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠١﴾

"Sema: Angalieni kwa makini yaliyomo mbinguni na kwenye ardhi! Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasioamini". (Yunus: 10:101).

Qur'anii pia inataja uchunguzi wa historia ya mwanadamu na watu wa kale pamoja na mabadiliko yote ambayo yamefanyika kama chanzo maalum cha elimu. Qur'ani inamlingania binadamu kuzingatia, ili aweze kugundua ukweli, kwenye ushindi na kushindwa, utukufu na udhalili, bahati na misiba ya watu mbali mbali wa zama za kale, hivyo kwamba kwa kujifunza mpangilio na sheria sahihi za historia, ataweza kunufaika yeye na jamii yake kwa kulinganisha historia ya wakati wake mwenyewe na sheria hizo.

Kwa hiyo Qur'ani inatangaza:

وَكَمْ قَصَمْنَا مِن قَرْيَةٍ كَانَتْ ظَالِمَةً وَأَنشَأْنَا بَعْدَهَا قَوْمًا آخَرِينَ ﴿١١﴾

"Na mingapi katika miji iliyokuwa ikidhulumu tumeiteketeza na tukawasimamisha baada yake watu wengine." (21:11).

قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِكُمْ سُنَنٌ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ ﴿١٣٧﴾

"Kabla yenu zimepita nyendo nyingi; basi tembeeni katika ulimwengu muangalie vipi ulikuwa mwisho wa wanaokanusha" (Imran: 3:137).

Qur'ani pia inatambua dunia ya ndani ya mwanadamu, ambayo inaielezea kwa neno anfus (nafsi) kama chanzo cha tafakari yenye kutoa matunda mazuri na ugunduzi wa ukweli. Inaonyesha umuhimu wake kama ifuatavyo:

سَنُرِيهِمْ آيَاتِنَا فِي الْآفَاقِ وَفِي أَنفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُ الْحَقُّ ۗ أَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ أَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٥٣﴾

Tutawaonyesha ishara zetu kwa dhahiri kabisa katika dunia na ndani ya nafsi zao, mpaka iwabainikie kwamba Mwenyezi Mungu ni Haki." (Fussilat: 41:53)

وَفِي الْأَرْضِ آيَاتٌ لِّلْمُوقِنِينَ ﴿٢٠﴾ وَفِي أَنفُسِكُمْ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٢١﴾

"Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini. Na pia katika nafsi zenu. Je! Hamwoni? ( Zariyat: 51:20-21).

Kwa maneno mengine ni kwamba kipo chanzo kikubwa cha elimu katika uzuri na mpachano wa mwili wa binadamu, pamoja na viungo vyake vyote na uwezo, matendo yake na athari zake, taratibu zake zilizo sahihi na stadi, nishati zake mbali mbali na silika zake, utambuzi wake, hisia na misisimko yake, yote, ya kinyama na kibinadamu, na hasa zaidi katika uwezo wa kushangaza wa akili na utambuzi ambao mtu amepewa - uwezo ambao bado unabakia kwa kiadi kikubwa haujajulikana, kwani mwanadamu amechukua hatua chache tu katika kuichunguza nguvu hii isiyoonekana na uhusiano wake na umbile la mwili wake.

Qur'ani inatangaza kwamba inatosha kutafakari na kuipima nafsi yako mwenyewe ili uweze kuongozwa kwenye chanzo cha milele na kisichokuwa na ukomo kisichohitajia kitu chochote, chenye ujuzi usio na mipaka, ustadi na uwezo, na ule mfano dhaifu ambao unaonekana katika utu wako. Hapo ndipo utakapojua kwamba ni huo ukweli usio na ukomo ambao umezikusanya mahali pamoja mchanganyiko wenye manufaa kiasi hicho wa vitu asili na kuutokeza kwenye uwanja wa uhai.

Kujulikan kwa dalili za wazi kama hizo na uthibitisho wenye maamuzi, ambao umewekwa wazi mikononi mwako na ndani ya mwili wako mwenyewe ili uweze kutafuta elimu ya Mwenyezi Mungu, hakuna kisingizio kitakachokubaliwa kutoka kwako kwa upotofu na ukanusho. Qur'ani pia inatumia mbinu ya ukanushaji na uthibitisho kwenye suala la sifa za Mwenyezi Mungu. Hivyo, inatoa maelezo ya sifa ambazo kwamba dhati ya Muumbaji inakuwa nazo kama 'sifa za kukubali.' Miongoni mwa hizo ni ujuzi, uwezo, utashi, ukweli kwamba kuwepo Kwake hakukutanguliwa na kutokuwepo na kwamba dhati Yake haina mwanzo, na ukweli kwamba misogeo yote ya dunia inapatikana kutokana na utashi Wake na uwezo Wake.

Qur'ani inasema:

هُوَ اللَّـهُ الَّذِي لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ هُوَ الرَّحْمَـٰنُ الرَّحِيمُ ﴿٢٢﴾ هُوَ اللَّـهُ الَّذِي لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ سُبْحَانَ اللَّـهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٢٣﴾

"Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, ambaye hapana Mungu isipokuwa Yeye tu. Mwenye kuyajua yaliyofichikana na yanayoonekana. Yeye ndiye Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana aabudiwaye isipokuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwenye nguvu, Anayefanya analolitaka, Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayomshirikisha nayo." (Hashir: 59:22-23).

'Sifa za ukanushaji' ni zile ambazo Mwenyezi Mungu yupo huru nazo. Ni pamoja na ukweli kwamba Mwenyezi Mungu hana mwili na hana mahali;

dhati yake takatifu haina mshirika wala wakufanana nayo; Yeye si mfungwa kwenye mipaka iliyowekwa na ukomo wa hisia; Hakuzaa wala hakuzaliwa; wala hakuna mabadiliko wala msogeo katika dhati Yake, kwani Yeye ni mkamilifu kabisa, na Yeye haikabidhi kazi ya uumbaji kwa yeyote.

Qur'ani inasema:

﴿قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ اللَّهُ الصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ ﴿٤﴾

"Sema; Yeye Mwenyezi Mungu ni Mmoja. Mwenyezi Mungu ndiye anayekusudiwa kwa haja. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anayefanana naye hata mmoja." (Iklas: 112:1-4).

﴿سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿١٨٠﴾

"Ameepukana Mola Wako, Mola Mwenye enzi na yale wanayomsifu nayo." (37: 180).

Mantiki ya kibinadamu, ambayo bila kupingwa hufikiria kwa namna yenye ukomo, hana uwezo wa kuketi katika kuhukumu utakatifu, kwa sababu lazima tukubali kwamba si rahisi kutambua msingi halisi wa nafsi hiyo ambayo juu yake hakuna kifanani au kilingano cha kuonekana au kufahamika kinachopatikana katika ulimwengu wa maumbile. Madhehebu kubwa sana na mbinu kubwa sana za tafakuri hapa zinaangukia kuwa mawindo ya utatanishi.

Kama vile ambavyo viumbe vyote hai lazima virudi nyuma kwenye asili ambayo kwayo uhai unafanana, kwa nafsi huru ambayo juu yake viumbe vyote vingine vinategemea, hivyo pia, lazima vitokane na chanzo cha uhai, uwezo na ujuzi, kutoka kwenye ile nafsi ambamo humo ndimo sifa hizi na ubora zinamochipukia.

10

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI

### MASHARTI YA LENGO BORA LA IBADA

Mola wa ulimwengu, kama anavyowasilishwa ndani ya Qur'ani, anayo masharti yote muhimu ya lengo bora la ibada. Yeye ndiye muumba wa upendo na aina zote za uzuri, mwanzilishi wa aina zote za uwezo na nguvu. Yeye ni bahari pana ambamo kwenye uso wa wimbi lake dogo sana muogeleaji wa kutafuta elimu na akili yake anasukwasukwa huku na huko kama kitu cha kuchezea. Ni yeye ambaye anayezilinda mbingu zisianguke na dunia isiporomoke. Endapo kwa sekunde moja tu, Atafumba jicho lake la huruma au kuligeuzia mbali na dunia, ulimwengu wote utatoweka na kuvurumishwa kuelekea kwenye kutokuwepo katika hali ya mavumbi. Kule kuwepo na ule uhai wa kila chembehai katika ulimwengu, kwa hiyo kunamtegemea Yeye.

Ni yeye ndiye Anayegawa neema na furaha zote; anayetumiliki sisi na anaweza kutuondoa sote kwa hiari atakavyo. Wakati anapoamuru, agizo hutoka na kuendelea, mara anaposema, "Kuwa!" kiumbe kinatokea kuwepo. Ukweli na uhakika hupata nguvu kutoka kwenye dhati Yake, na uhuru haki na sifa na sifa nyinginezo za ukamilifu zinapatikana kutoka kwenye miale ya sifa Zake. Kukimbia kuelekea Kwake, kutafuta uwezekano wa kuwa karibu na lango lake tukufu, ni kupata mahitaji yenye kufikirika kwa kiwango cha juu sana. Yeyote anayeusalimisha moyo wake kwa Mwenyezi Mungu, hupata mwenzi mwenye upendo na rafiki ampendaye; mtu anayemtegemea Yeye ameyaweka matumaini yake kwenye msingi imara, ambapo yule anayeambatanisha moyo wake kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni windo la njozi za uwongo na anajenga msingi kwenye upepo.

Yeye ambaye anautambua ule msogeo ulio mdogo zaidi unatokea katika maumbile pia anaweza kutuamulia njia inayoelekea kwenye furaha na kuweka njia ya maisha na mfumo wa uhusiano wa kibinadamu unaotenda kufuatana na kanuni ambazo Ameziweka katika mpango wa uumbaji. Yeye, hata hivyo anayatambua manufaa yetu halisi, na vile vile ni haki Yake kuweka njia kwa ajili yetu kama matokeo ya kimantiki na ni matokeo ya asili la utakatifu Wake. Kutenda kwa mujibu wa mpango ambao Ameuweka ndio uhakika maalum tu kwa ajili yetu sisi kupanda kuelekea Kwake. Inawezekanaje kwamba mtu awe na mapenzi juu ya ukweli na uadilifu na kwamba yuko tayari hata kujitolea mhanga uhai wake kwa sababu hiyo, alimradi tu awe anajua chanzo asili yake?

Kama kitu kinastahili kuabudiwa haiwezekani kiwe kingine isipokuwa Muumba ambaye ndiye mhimili wa viumbe vyote. Hakuna kitu au mtu yeyote mwenye daraja kama hilo na akastahili kusifiwa na kutumikiwa na mwanadamu. Malengo mengine yote isipokuwa Mwenyezi Mungu hayana uhakika na ubora na hayajitoshelezi ndani yake, na yenyewe tu; ni viwakilishi na hutumika tu kama njia ya kupata viwango vya juu zaidi kuliko yenyewe.

Sifa kuu ambazo zinashawishi ibada ya mwanadamu zinakuwa ndio watoaji wa neema zote na kuwa watambuzi wa kila uwezekano, mahitaji, uwezo na nguvu zilizomo kwenye mwili na roho wa binadamu. Sifa hizi ni zake Mwenyezi Mungu pekee; viumbe vyote vinakuwa vyenye kuhitajia na hutegemea juu ya nafsi hiyo ambayo Ipo kwa uwezo wa dhati Yake Yenyewe. Msafara wa uhai wakati wote unaosonga mbele kuelekea Kwake kwa njia ya msaada Wake, amri zake huteremka bila ukomo za kila kitu (japo chembe ndogo) hapa ulimwenguni. Kujisalimisha halisi na ibada ni vyake, tena pekee chini ya Dhati Yake Tukufu Kabisa. Kuwepo Kwake kutukufu, kusikoingiliwa kati na hata sekunde moja ya kutokuwepo, kunahisiwa kwenye moyo wa kila kiini cha chembe ya uhai. Vitu vyote isipokuwa Mwenyezi Mungu hufanana na sisi kwa kuwa udhaifu na upungufu vinakuwepo juu yao. Kwa hiyo, havistahili sisi kujisalimisha kwavyo na havistahili kutwaa mamlaka juu ya sehemu yoyote ya milki ya Mwenyezi Mungu ambayo ni uwanda wote mpanawa uhai. Mwanadamu pia ni kiumbe bora na chenye thamani mno kuweza kutawaliwa na kudhalilishwa na kitu kingine chochote mbali na Mwenyezi Mungu.

Katika uwanda wote mzima wa uhai, ni Mwenyezi Mungu pekee Anayestahiki kusifiwa na mwanadamu. Mwanadamu lazima atoe kwenye mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu, kwenye jitihada zake za kujisogeza karibu Naye na kupata radhi Zake, kipaumbele juu ya viumbe na malengo mengine ya upendo. Hali hii itasababisha kumboresha mwanadamu na kuzidisha thamani yake, kwani mwanadamu ni tone dogo sana na kama hakuungana na bahari (maumbile yote) ataangamizwa na wimbi la uovu, na kukaushwa na joto la machafuko. Mwanadamu hupata utu wake halisi na kuwa wa milele pale anapojiambatanisha na kile chanzo chenye kutia nuru, ambapo Mwenyezi Mungu hutoa maana ya dunia yake naye anakuwa mfasiri wa matukio yote yahusuyo maisha yake. Ni kwa maana hii kuwa dunia za wanadamu zinaweza kuwa ama ni pana na kubwa sana au finyu na zinazobana.

Amirul-Mu'minin Ali (a.s) anasema anapozungumzia udhaifu wa mwanadamu na uwezo wake pungufu:

**"Mambo ya mwanadamu ni mageni na ya ajabu ilioje! Kama anakuwa na matumaini kuhusu tamaa fulani, ulafi utamfanya adharauliwe; tamaa itamletea choyo, na choyo kitamuangamiza. Kama atashikwa na kukosa matumaini, huzuni na masikitiko vitamuua. Kama akipata furaha na bahati njema, atashindwa kuvihifadhi. Endapo atashikwa na hofu na woga vitamfanya achanganyikiwe. Endapo atapewa usalama wa kutosha, atakuwa mzembe. Kama atarudishiwa neema zake, anakuwa kiburi na muasi. Kama anapatwa na balaa, atafedheheka kwa masikitiko na huzuni. Endapo mwanadamu anapata utajiri, anakithirisha majivuno. Endapo anakumbwa na ufukara, atatumbukizwa kwenye mateso. Endapo anadhoofishwa na njaa, atashindwa kunyanyuka kutoka ardhini. Endapo anakula kupita kiasi, ghasia tumboni mwake itamkosesha raha. Kwa hiyo upungufu wote katika maisha ya mwanadamu una**

**madhara kwake, na ziada zote ile zinasababisha uovu na maangamizo."**[1]

Kuzungumzia kwa ujumla, uadilifu, ubora, wema na sifa zingine zinazobeba heshima na utukufu ama lazima ziwe za uwongo na za kudhania au lazima tuyaone maadili haya kuwa ni ya kweli na muhimu, yenye kutokana na msingi wa utambuzi wa dhamira na silika. Katika suala hili la pili, lazima tukubali kwa unyeyekevu kwenye maumbile ya kilimwengu na ukamilifu wa dhahiri unaoenea pamoja na faida (manufaa), uhai na uwezo, na ambamo maadili yote yanatokana namo.

Tunapoliangalia jambo lenyewe kwa uangalifu, tunaona kwamba viumbe vyote visivyo na idadi ambavyo vinaishi ulimwenguni, pamoja na upendo na tamaa ambayo imeota mizizi ndani ya nafsi zetu, vyote hukusanyika mahali pamoja, vyote vinarudi kwenye chanzo kimoja - Mwenyezi Mungu. Asili yenyewe hasa na uhalisi wa dunia inafanana na uwiano wake, uhusiano na mwambatano kwa Mwenyezi Mungu. Kiumbe hupanda tena kwa kufuata njia tofauti hadi kwenye sehemu kilipoanzia na ambayo kiliteremkia, na sehemu hiyo pekee ndio inastahili mapenzi na kujitoa kwa mwanadamu. Pindi binadamu anapogundua sehemu hii, huvutiwa sana na uzuri wake halisi na ukamilifu kiasi kwamba anasahau vingine vyote.

Tunanona kwamba vitu vyote vimejitokeza kwenye kutokuwepo na kuja katika hali ya kuwepo na kwamba katika kipindi chote wakati cha kuwepo kwao, imma kipindi kifupi au kirefu, vinategemea kwenye chanzo cha nje yao vyenyewe juu ya misaada na riziki; vitu hivi vimewekwa alama ya utegemezi usiofutika na kukosa kujitawala.

Ikiwa lengo bora la ibada tunalotafuta na ambalo tunajaribu kuliendea lingekuwa halitambui matatizo tunayoyapata na hali ya dunia; kama lingekuwa haliwezi kutosheleza matakwa na tamaa zetu, likawa lenye udhaifu na mapungufu tele kama vile sisi tu na likawa katika kundi moja kama lile tulimo sisi - lisiingeweza kuwa kusudio letu la mwisho na lengo letu la mwisho kabisa au kuwa na thamani kamili.

Tunapotafuta utimilizaji wa matakwa yetu kwa njia ya ibada, ni Mwenyezi Mungu peke yake Anayeweza kutujibu. Qur'ani inasema:

إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ عِبَادٌ أَمْثَالُكُمْ فَادْعُوهُمْ فَلْيَسْتَجِيبُوا لَكُمْ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٩٤﴾

"Hakika wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu ni waja mfano wenu nyingi. Basi hebu waombeni, nao wakuitikieni; kama mnasema kweli." (7:194).

**Amirul-Mu'minin (a.s) alipokuwa anaomba dua kwa Mola Wake kwenye msikiti wa Kufah alisema: "Ewe Mola Wangu, Ewe Mola Wangu! Wewe ni Mwenyezi Mungu na Mkuu na mimi ni mtumwa wako duni nisiye na thamani. Nani awezaye kuonyesha huruma kwa mtumwa wake asiye na thamani isipokuwa Mwenyezi Mungu Mkuu? Ewe Mola Wangu, Ewe Mola Wangu! Wewe unazo nguvu na uwezo mimi ni mnyonge na dhaifu; nisiyekuwa na nguvu na uwezo, ni nani ambaye anaweza kuonyesha huruma kwa wanyonge?**

1. Sheikh al-Mufid, Irshad, uk.142.

**Ewe Mola Wangu, Ewe Mola Wangu! Ni Wewe Ambye humkirimu mwombaji, na mimi ni mwombaji kwenye lango lako. Nani atakayeonyesha huruma kwa mwombaji isipokuwa yule aliye mpaji na mkarimu mno? Ewe Mola Wangu, Ewe Mola Wangu! Wewe ni uzima wa milele na mimi ni kiumbe niliyekadiriwa kutoweka. Nani atakayemhurumia yule mtu aliyekadiriwa kuangamia isipokuwa ile dhati ya milele, na ya kudumu? Ewe Mola Wangu, Ewe Mola Wangu! Wewe ndiye mwongozaji unayeelekeza njia, na mimi nimepotea na kukanganyikiwa. Nani atakuwa na huruma na yule aliyepotea na kukanganyikiwa kama siye yule mwongozaji anayeelekeza njia?**

**Ewe Mola Wangu, Ewe Mola Wangu! Nihurumie kwa huruma zako zisizo na ukomo, nikubali na utosheleke na mimi katika ukarimu Wako, upendeleo, na wema wako, Ewe Mwenyezi Mungu, mmiliki wa ukarimu, upendeleo na wema, na katika huruma zako zote, Ewe mwenye huruma zaidi ya wenye huruma!"**[1]

Kwa hiyo kuonyesha heshima kuu kwa yeyote asiye Mwenyezi Mungu, kujielekeza mwenyewe kwa mwingine mbali na dhati Yake halisi, si njia iliyo halali; mbali na Mwenyezi Mungu, hapana chochote kinachoweza kuwa na athari hata kwa kiwango kidogo tu juu ya mustakabali wetu halisi. Kama lengo la kuabudiwa kinastahili utii na upendo wa mwanadamu na lina uwezo wa kumnyanyua yeye kwenye vilele vya furaha kuu, lengo hilo la ibada lazima lisiwe na dosari na upungufu wowote ule. Miale yake ya umilele lazima iguse viumbe vyote kwa kuruzuku na maisha, na uzuri wake lazima usababishe kila mtu mwenye umaizi kupiga magoti chini mbele yake. Kwa kule kuwa na uwezo usio na ukomo, hukata kiu kali ya nafsi zetu, na kuipata elimu yake, si vinginevyo mbali na kupata chanzo cha msingi cha asili yetu halisi.

Kama tunachagua lengo la upendo na ibada mbali ya Mwenyezi Mungu, linaweza kuwa na uwezo fulani na kuweza kukamilisha matamanio yetu hadi kiwango fulani, lakini pindi tufikapo kwenye kiwango hicho, halitakuwa lengo la upendo na ibada tena kwetu sisi. Halitaweza tena kutushawishi na kutuvutia, kinyume chake, litasababisha sisi tukwame hapo hapo. Kwani sio tu kwamba kitashindwa kutosheleza silika zetu za tamaa ya ibada, litatuzuia kutafakari kuhusu manufaa mengine yoyote ya juu zaidi na kutufungia kwenye mduara mfinyu, kwa jinsi ambavyo tunawa

hatuna dhamira yoyote tena ya kusonga mbele au kunyanyuka. Ikiwa lengo tunalochagua kuabudu na kulipenda ni duni kwetu, kamwe halitaweza kutufanya sisi tunyanyuke na kutakasa nafsi zetu. Mwelekeo wetu kwenye lengo hilo, kinyume chake, utatuburuza na kuturudisha nyuma, na tutakuwa kama mshale wa dira ambao umeelekezwa pembeni mwa nguzo kwa nguvu ya athari ya eneo geni kabisa la sumaku. Matokeo yake yatakuwa ni kupoteza kabisa mwelekeo; mateso ya milele yatakuwa ndio mustakabali wa mwanadamu usiokwepeka.

## IBADA, NJIA BORA YA BINADAMU YA KUONYESHA SHUKRANI

1. Mafatih al-Jinan, uk.400.

Lengo la kuabudiwa linaweza kutoa maelekezo kwa mwenendo wa mwanadamu na kumuondolea giza lake kwa mng'aro wake wakati linapoweza kumpatia mifano bora, linapokuwa limejaaliwa uhai wa hakika na ulionyanyuliwa kwa daraja, na kuwa ni chanzo cha athari, na kuwa asili hasa ya uimara na hali ya kudumu. Halafu, lengo hilo la kuabudiwa hutoa athari za ndani zaidi kwa mwanadamu na kumwongoza katika fikra na matendo yake. Linarahisishia asili ya mwanadamu, ile sehemu yake inayolelewa na hekima ya ki-Mungu katika utafutaji wa ukamilifu wake.

Jitihada yoyote au msogeo kwa upande wa binadamu kujichagulia mwelekeo mbaya, kufuata njia isiyo sahihi katika maisha, matokeo yake yatakuwa kutenganishwa na nafsi yake, kupoteza kuridhika kwake, na kubadilisha utu wake. Mwanadamu hataweza kujitambua kwa usahihi kama atakuwa amejitenga na Muumba wake. Kumsahau Mwenyezi Mungu maana yake ni kujisahau mwenyewe, kutokuyaelewa malengo ya jumla ya maisha ya binadamu na dunia inayomzunguka, na kushindwa kutafakari kuhusu aina yoyote ya maadili ya juu zaidi.

Kama vile kujiambatanisha na mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu kunavyomtenga binadamu na nafsi yake mwenyewe na kumgeuza kuwa kama mashine fulani ya kibaiolojia inayotembea, hivyo, pia ndivyo ilivyo kwa mtu anayemtegemea Mwenyezi Mungu na kuomba dua mbele ya lango lake kunavyomchukua mtu asiyekuwa na uelekeo wowote, ambaye hana kabisa maisha ya kiroho, kutoka kwenye kina kirefu cha bahari ya kutojali, kumhuisha na kumrudisha kwenye utu wake tena. Kwa kumwabudu Mwenyezi Mungu, uwezo wa kiroho na nguvu za kimbinguni ndani ya mwanadamu zinastawishwa. Mwanadamu huelewa hali ya uduni wa umbile lake lisilo na thamani, matumaini na tamaa na kuyaona mapungufu na udhaifu bila ya utu wake mwenyewe. Kwa ufupi, hujigundua mwenyewe kama alivyo hasa.

Kumtambua Mwenyezi Mungu na kukimbilia kwenye kile chanzo kisichoonekana cha viumbe vyote huwa kunatia nuru na kuuamsha moyo. Inafurahisha sana, furaha ambayo haiwezi kulinganishwa na furaha ya ile dunia ya kimaada ya pande tatu. Ni kupitia kwa mtu kujielekeza mwenyewe kwenye nadharia hiyo, yaani, ukweli wa kitu kisicho cha kimaada, kwamba fikira huchukua nafasi ya juu sana na maadili hugeuzwa. Amirul-Mu'minin, Ali (a.s) anazungumzia kuhusu athari ya ajabu ya utambuzi wa Mwenyezi Mungu katika nyoyo za watu kama ifuatavyo:

**"Muumba Mwenye Nguvu zote ameufanya umtambuzi juu Yake kuwa ni njia ya kutakasa moyo. Ni kupitia kumtambua Mwenyezi Mungu ambapo nyoyo zilizokufa masikio huanza kusikia, nyoyo zilizopofuka huanza kuona, nyoyo zenye uasi hulainika na kuwa tiifu."**[1].

Pia anasema: **"Ee Mola Wangu! Wewe ni mwenza mzuri zaidi kwa wale wanaokupenda Wewe na ni chanzo kizuri zaidi cha kuponya kwa wote wanaoweka mategemeo yao juu Yako. Unawaona wao katika hali zao za ndani na matendo yao ya nje na unatambua undani wa nyoyo zao. Unajua kiwango cha utambuzi na ujuzi wao, na siri zao zipo wazi**

1. Nahj al-Balaghah, Hotuba ya 220.

**Kwako. Nyoyo zao hutetemeka zinapotenganishwa na Wewe, na kama upweke wao unawasababishia woga na wasi wasi, utambuzi wao juu Yako huwapa faraja, na kama wanakumbwa na shida na matatizo, ni Kwako pekee ndiko yaliko makimbilio yao."**[1]

Imam Sajjad [(a.s)], yule aliye mfano bora wa usafi na uadilifu ambaye alikuwa na dhamana isiyovunjika na Mola Wake, anatuonyesha katika dua zake za maombi, udhihirisho wa hali ya juu sana wa upendo. Huu ulikuwa upendo uliotakasika ambao uliuwasha moto utu wake wote, na ingawa nafsi yake ilikandamizwa sana na huzuni ya kibinadamu ya kutenganishwa, ubawa wa upendo wenye nguvu kubwa ulimwezesha kupaa juu kwenye mbingu zisizo na ukomo, kwa hiyo, kwa utiifu na unyenyekevu usioelezeka, yeye aliomba kwenye lango la Mwenyezi Mungu, wa milele:

"Ee Mola Wangu! Nimehamia kwenye msamaha wako na nimetoka kuiendea huruma Yako. Kwa shauku kubwa ninahitaji msamaha wako na ninategemea juu ya ukarimu wako, kwani hakuna chochote katika tabia yangu cha kuweza kunifanya mimi nistahiki kusamehewa, na upole Wako tu ndio matumaini yangu pekee. "Ewe Mwenyezi Mungu, niongoze kwenye njia iliyo nzuri zaidi na ujaalie kwamba nifariki nikiwa muumini katika dini Yako na nifufuliwe kama muumini katika dini Yako.

"Ewe Mola Wangu Ninayekuabudu! Oh, Ewe ambaye msaada wako, walio watenda dhambi wanauomba kupitia huruma Yako! Oh, Ewe ambaye katika kukumbuka ukarimu wako, wanyonge hutafuta kimbilio! Oh, Ewe Ambaye kwa kukuogopa Wewe, wenye dhambi hulia kwa uchungu!

"Ewe chanzo cha utulivu juu ya nyoyo za wale ambao wamehamishwa makwao kwa hofu! Ewe mliwazaji wa wale ambao wanahuzunika kwa nyoyo zilizovunjika! Ewe unayewasaidia wenye upweke, msaidizi wa waliotupwa na wenye kuhitaji! Mimi ni yule mja ambaye nimeitika kwa utiifu pale ulipowaamuru watu waje Kwako. "Ewe Mola Wangu! Mimi hapa nimesujudu juu ya udongo kwenye lango Lako. Ewe Mwenyezi Mungu, ikiwa unaonyesha huruma kwa yeyote anayekuja Kwako kwa maombi na dua basi naomba nifanye niwe na bidii ya dhati katika dua zangu, au ikiwa unamsamehe kila mwenye kulia mbele Yako, basi naomba unifanye niharakishe kulia.

"Ewe Mwenyezi Mungu, usimkatishe tamaa yule ambaye haoni mpaji isipokuwa Wewe; usinisukumie mbali kwa mkono wa kukataa, kwa sasa ambapo nimesimama hapa kwenye lango Lako."[2] Yeyote anayetaka kuelewa maana ya kina ya dua lazima atambue kwamba maelezo ya busara na maamuzi ya kimantiki hayawezi kutoa uelewa wa kina juu ya maswali yanayogusa nuru ya kiroho.

Qur'ani tukufu inaeleza tabia na njia ya maisha ya wasioamini na wayakinifu kama ifuatavyo:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَالُهُمْ كَسَرَابٍ بِقِيعَةٍ يَحْسَبُهُ الظَّمْآنُ مَاءً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُ لَمْ يَجِدْهُ ﴿٣٩﴾

"Na waliokufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji. Hata ayafikiapo hapati chochote."( 24:39),

1. Nahj al-Balaghah, Hotuba ya 225.
2. Sahifayi Sajadiya, uk. 163-198.

لَهُ دَعْوَةُ الْحَقِّ ۖ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِهِ لَا يَسْتَجِيبُونَ لَهُم بِشَيْءٍ إِلَّا كَبَاسِطِ كَفَّيْهِ إِلَى الْمَاءِ
لِيَبْلُغَ فَاهُ وَمَا هُوَ بِبَالِغِهِ ۚ وَمَا دُعَاءُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿١٤﴾

"Maombi ya haki ni Kwake Yeye tu. Na hao wanaowaomba badala yake hawawajibu chochote; bali ni kama mwenye kunyoosha viganja vyake kwenye maji ili yafike kinywani mwake lakini hayafiki. Na maombi ya makafiri hayako ila katika upotovu." (13:14).

مَثَلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ كَمَثَلِ الْعَنكَبُوتِ اتَّخَذَتْ بَيْتًا ۖ وَإِنَّ أَوْهَنَ الْبُيُوتِ لَبَيْتُ
الْعَنكَبُوتِ ۖ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾

"Mfano wa wale waliochukua miungu badala ya Mwenyezi Mungu, ni mfano wa buibui ajitandiaye nyumba. Na hakika nyumba mbovu mno kuliko zote ni nyumba ya buibui, laiti wangelijua" (29:41).

مَّثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ ۖ أَعْمَالُهُمْ كَرَمَادٍ اشْتَدَّتْ بِهِ الرِّيحُ فِي يَوْمٍ عَاصِفٍ ۖ لَّا يَقْدِرُونَ مِمَّا
كَسَبُوا عَلَىٰ شَيْءٍ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الضَّلَالُ الْبَعِيدُ ﴿١٨﴾

"Mfano wa waliomkufuru Mola wao vitendo vyao ni kama majivu yanayopeperushwa kwa nguvu za upepo katika siku ya kimbunga. Hawawezi kupata chochote katika waliyoyafanya. Huo ndio upotovu wa mbali" (14:18).

Udhihirisho wa kiwango cha juu sana wa hali ya shukurani ambao mwanadamu anaweza kufanya kwenye lango la lengo lake la ibada ni dua, kule kutangaza imani ya mapenzi juu ya ukamilifu Wake halisi na bidii juu yake. Anafanya hivi kwa ulingano na maumbile yote, kwa sababu viumbe vyote humsifu na kumtukuza Mwenyezi Mungu. Qur'ani inasema:

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَاوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَن فِيهِنَّ ۚ وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَٰكِن لَّا
تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ ۗ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٤٤﴾

Zinamtukuza mbingu saba na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Na hapana chochote ila kinamtukuza kwa sifa zake njema. Lakini ninyi hamfahamu kutukuza kwao. Hakika Yeye ni Mpole, na Mwingi wa maghfira." (17:44).

Kwa kawaida ibada hii na utukuzaji ni vitendo ambavyo havimletei Mwenyezi Mungu manufaa japo madogo, kwani Yeye anao ukamilifu wote kwa kiwango kisicho na ukomo na wala sio dunia ama binadamu anayeweza kuongeza kitu chochote Kwake au kuchukua chochote kutoka Kwake. Hivi inaingia akilini kwa hali yoyote ile kwamba, Angemuumba mwanadamu kwa sababu ya kunufaika kutokana na ibada na kumtukuza kwake. Kinyume chake, ni mwanadamu ndiye ambaye, kwa kupata elimu juu ya Dhati ya hali ya juu sana na kumwabudu Yeye katika utukufu Wake, hufikia lengo lake la mwisho na ukamilifu halisi.

Profesa Ravaillet, mwanafalsafa maarufu na bingwa wa fizikia, anayo haya machache yafuatayo ya kusema kuhusu utambuzi wa ulimwengu: "Kosmolojia mpya inasema kwamba atomu na molekuli zinatambua zinafanya nini; katika maana ya kawaida ya usemi huo; vitu hivi vina utambuzi wa kazi zinazofanya na mwenendo wa maisha yao. Utambuzi wao huu ni bora zaidi ya ujuzi wa bingwa wa fizikia, kwa sababu chote

anachofahamu bingwa wa fizikia juu ya atomu ni kwamba kama isingekuwa inagusika na kutambulika, hakuna mtu ambaye angejua chochote kuihusu hiyo.

"Miili, msogeo, kasi, mawazo ya hapa na pale, mnururisho, ulingano, nafasi, anga, umbali pamoja na vitu vingine vingi - vyote vilikuja kuwepo kwa sababu ya atomu. Endapo atomu haingekuwepo, chanzo cha viumbe vyote vya kustaajabisha kingekuwa nini? Upo uhusiano huo huo baina ya utambuzi na mwili kama ilivyo baina ya msogeo na mtuamo, au vipengele chanya na hasi vya mwendo.

"Sasa, angahewa, ikichukuliwa kama ilivyo kwa ujumla wake, sio pofu. Kama unakumbuka tulionyesha, tulipokuwa tunachunguza eneo la uoni, kwamba jicho sio kile kipengele cha msingi na uamuzi. Kwa kuwa limepangiwa mahali maalum katika dunia, kwa mujibu wa mazingira yenye mipaka, ya jamii ya binadamu na viumbe vingine vya dunia, lina eneo maalum finyu la kimwili ambamo hufanya kazi ndani yake. Lakini kuhusu angahewa baina ya dunia na jua, baina ya jua na kundi la nyota, na baina ya kundi la nyota na sayari kubwa sana za mbali, ambamo nguvu kubwa zenye masafa marefu mno zinashughulika katika kubadilishana nishati - huko, kiungo kama jicho cha viumbe vya duniani halina fursa kujionyesha lenyewe au kudhihirisha jinsi linavyo fanya kazi.

"Lakini hasa kwa sababu hii hutuwezi kuamini kwamba kunakuweko na ukosefu wa utambuzi na ufahamu kwenye nyanja hiyo kwa ajili ya kubadilishana nishati kubwa sana na nguvu inayotawaliwa na kununi ya mvutano, ulingano, msogeo, mwanga na nguvu ya mzunguko wa kati. Upofu unakuwa haupo kwenye vitu hivi vya ajabu, na hata chembechembe za mwanga haziwezi kufikiriwa kama kitu kinachofanana na msambaza barua asiye na elimu, ambaye kazi ni ile tu ya kuwasilisha barua ambazo hawezi kuzisoma."[1].

1. Dau Hazar Danishmand dar Justuju-yi Khuda-yi Buzury, uk. 61 & 99.

11

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA MOJA

### KUTOLINGANISHIKAKWA SIFA ZA KI-MUNGU

Katika jitihada zetu za kumwelezea alivyo Muumba na kupata kujua sifa zake, tunahitaji kwa ukamilifu kuwa na dhana na maelezo ambayo yako nje ya uwezo wetu. Yale maneno tunayotumia hayatatuwezesha kufikia lengo letu, maelezo halisi juu ya Mwenyezi Mungu, kwani uchache wa kuelewa kwetu hauwezi kuzingatia utambuzi wa asili hasa ya sifa za Mwenyezi Mungu zisizo na ukomo. Ametukuka juu ya dhana na fikra zote zinazobuniwa na kuundwa na akili ya binadamu.

Mwanadamu, ambaye ameumbwa na kuwekewa mipaka katika kila hali, asitumainie kuwa na uwezo wa kukadiria na kuelezea kitu kisicho cha kimaumbile kwa njia ya sifa na tabia za kimaumbile. Uhakika ambao ni kinyume na viumbe vinavyoweza kutokea na vile vya kawaida, ambao mamlaka yake kamili na elimu isiyo na ukomo vinafunika vitu vyote, ambao kwa maneno ya Qur'ani:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١١﴾

"Hakuna kitu chochote mfano Wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona." (42:11).

Dhati ya aina hii kwa kawaida haiwezi kujadiliwa kwa haraka kama mada zingine za kawaida. Ali (a.s) Bwana wa wacha-Mungu, alisema: "Yeyote anayemlinganisha na kumchanganya Mwenyezi Mungu na kitu au anakihusisha kwenye asili yake takatifu atakuwa kwa uhakika bado hajamuona Yeye. Chochote anachokijua mwanadamu kuwa ni msingi wa asili Yake ni lazima kiwe kimeumbwa. Mwenyezi Mungu ndiye Muumbaji na Mtengenezaji. Chochote kinachotegemea kitu kingine zaidi ya chenyewe hicho kimesababishwa na kimeumbwa. Ni Mwenyezi Mungu peke Yake tu ambaye ndiye sababu pekee (na sio athari).

Yeye anashughulikia uumbaji bila ya kutumia namna yoyote ya vitendea kazi. Hupima bila msaada wa fikira na tafakuri. Yeye si mhitaji na hapati manufaa kutokana na kitu chochote. Wakati na nafasi haviandamani Naye. Vyombo na vifaa havimsaidii Yeye. Kuwepo kwake hutangulia nyakati zote na ukabla wa umilele Wake ulitangulia mwanzo wote.

"Yeye habanwi na mipaka, kwani ni viumbe ndivyo huwekea mipaka maumbile yao kwa njia ambazo ni maalum kwao, na miili yao ndio inayoonyesha aina zao. Dhati Yake takatifu haikubali dhana ya mwendo na ile ya kutokuwa na mwendo, inawezekanaje kwamba kitu kilichoumbwa ndani ya kiumbe pia kiwepo ndani ya Dhati Yake? Kama pangekuwepo mwendo na kutuama kimya katika Dhati Yake, Angelazimika kukumbwa na mabadiliko na marekebisho; angeweza kugawanyika na kutokuwa na mwanzo kwake kungekanushwa. Yeye ni chanzo cha nguvu zote, kwa hiyo hakuna kiumbe ambacho kingeweza kumwathiri.Mwisho kabisa, Yeye ni

Muumba Ambaye habadiliki au kutoweka na Ambaye kamwe hafichikani kwa watu wa ujuzi na umaizi."[1]

Ukweli kwamba sifa za Mwenyezi Mungu zimejitenga kabisa na zile za kwetu na haziwezi kupimwa kwa kulinganishwa na sifa zetu ni kwa sababu sifa za hicho chanzo cha viumbe ni tofauti na sifa za viumbe vingine vyote. Mathalani, sisi tunao uwezo wa kufanya kazi fulani, lakini hii sio sawa na ule uwezo wa Mwenyezi Mungu; kwa upande wetu, sifa ni kitu kimoja na kitu hasa kinachozungumziwa ni kingine. Tunapojivunia elimu zetu, hatuko kitu kimoja na kufanana na elimu zetu. Wakati wa utoto wetu hapakuwapo na dalili ya ujuzi au elimu katika utu wetu, lakini baadaye tulianza polepole kupata kiasi fulani cha elimu kwa kujifunza. Elimu na uwezo vinaunda pembe mbili tofauti za utu wetu, pembe hizi hazifanani na asili yetu na wala kuunganishwa pamoja katika maisha yetu. Sifa ni matokeo ya bahati na asili yetu ndio kiini; kila kimoja hakitemgemei mwenzie.

Lakini suala la sifa za ki-Mungu kimsingi ni tofauti: tunaposema kwamba Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa yote na ni Muweza wa yote, tunachokimaanisha ni kwamba Yeye ndiye chanzo cha elimu na uwezo. Sifa hizo sio kitu kingine mbali na kile inachokielezea ingawaje kifikra vinatofautiana. Kwa hali halisi, sifa Zake zinafanana na Dhati Yake; kwani Dhati Yake haiundwi na kitu ambamo mambo ya kubahatisha yanaweza kushikilia. Yeye ni Dhati halisi, yenye kufanana na elimu, uwezo, uhai, uthabiti na utambuzi; Yeye hatawaliwi na mipaka yoyote ya kiakili au ya kutoka nje au kizuizi.

Kwa kuwa tunalelewa katika kiini hasa cha maumbile, na kwa hiyo tuna uzoefu nayo wakati wote, na kwa kuwa chochote tunachokiona kina kipimo na umbo maalumu, wakati na mahali na sifa zingine zote za miili - kwa ufupi, kwa sababu ya mazoea ya akili zetu kwenye maumbile ya kawaida - tunajaribu kupima vitu vyote kwa kigezo cha maumbile, hata dhana za kiakili na kihekima. Kigezo cha maumbile kwa hiyo, kinakuwa kituo cha kuanza kuondokea cha uchunguzi wote wa kisayansi na kifalsafa. Kuidhania nafsi ambayo haina hata sifa moja ya kimaada na ambayo ni tofauti kabisa ni vile akili zetu zinavyoweza kutambua na kuelewa sifa ambazo hazitenganishiki na dhati hiyo, sio tu kunahitaji usahihi lakini pia kunatutaka tusafishe kabisa akili zetu na mambo ya maumbile.

Ali [(a.s)] amesema kwa ufasaha kabisa, kwa kina na kwa umuhimu mkubwa kuhusu jambo hili. Anasisitiza kwamba mwanadamu hawezi kumfunga Mwenyezi Mungu katika maelezo, akisema: "Upwekeshaji halisi wa Mwenyezi Mungu (Tawhiid) na imani halisi vinategemea katika kuacha, kukana na kuondoa kabisa kutoka kwenye asili Yake tukufu, sifa zote za viumbe vilivyoumbwa. Mwenyezi Mungu apishie mbali kwamba Angeweza kuelezwa kwa sifa zozote kama hizo, kwa sababu akielezewa hivyo, itaonekana kama vile kila sifa imejitenga na mwenye sifa hiyo na ni mgeni nayo. Kwa hiyo mtu anayesema chochote katika kumuelezea Muumbaji akimdhania Yeye kuwanazo sifa fulani ambazo zimeongezwa na kukithirishwa kwenye ile dhati, tayari zimemfanya Yeye kuwa mshirika wa kitu fulani na kushauri kwamba anazo sehemu mbili. Jaribio la namna hii la

1. Nahjul-Balaghah, Hutuba ya 181.

kumwelezea Mwenyezi Mungu husababishwa na kutokujua na kutokutambua."[1]

Dhana za kiakili haziwezi kumwelezea Mwenyezi Mungu kwa kukimbilia sifa zenye ukomo, kwa kuwa na mipaka kwao, basi hazifai kumwelezea Mwenyezi Mungu. Kila sifa, kwa kuhusiana na ile maana maalum inayoiwasilisha, iko tofauti na sifa zingine zote. Kwa mfano; sifa ya uhai ni tofauti kabisa na sifa ya uwezo; hazibadilishaniki. Inawezekana kwamba mifano fulani huenda ikakusanya sifa zote hizi mahali pamoja, lakini kila moja ina maana yake kimsamiati.

Wakati akili ya mwanadamu inapotaka kukipatia sifa kitu fulani, lengo lake ni kuanzisha, katika mfano maalum, aina ya ushirikiano baina ya sifa na kitu inachokielezea. Lakini kwa kuwa sifa kimawazo inatofautiana na kitu chenyewe, akili bila kukwepa inaamuru kwamba vibakie mbali mbali. Njia moja tu ya kujua vitu ni kuvieleza kwa kutumia fikra za kiakili, ambazo kimawazo kila moja imetengana na mwenziwe, na kwa hiyo lazima viwe na ukomo. Dhana hizo haziwezi kwa hiyo, kutumiwa kupatia elimu juu ya ule Uhakika wa Hali ya Juu zaidi. Yeye ametukuka juu ya uwezekano na kujulikana kwa maelezo, na yeyote anayemwekea mipaka Mwenyezi Mungu kwa kutumia sifa fulani, huyo ameshindwa kupata

Kwa kutaja mifano michache tunaweza kuelewa kwa kiwango fulani jinsi ambavyo sifa hazikithirishwi kwenye dhati hiyo. Hebu zingatia kwamba miale ya joto inayotoka kwenye moto inafikisha joto kwenye kila kitu, hivyo kwamba mojawapo ya tabia na sifa ya moto ni kuwaka na kusambaza joto. Je, tabia hii imekalia pembe moja katika mwili wa umbile la moto? Kwa kweli, jibu ni hapana; uhai wote wa moto kwa jumla una sifa ya uwakaji na ugawaji wa joto. Imam Jafar as-Sadiq (a.s) alisema katika kumjibu mtu ambaye alimuuliza kuhusu hali halisi ya Mwenyezi Mungu: "Mwenyezi Mungu ni kitu tofauti kabisa na vitu vingie vyote; ni Yeye peke yake ndiye anayelingana na dhati halisi ya asili ya uhai wote. Yeye si mwili na wala hana umbile. Milango ya fahamu haiwezi kumtambua Yeye na hawezi kutafutwa. Yeye ameepukana na utambuzi aina yoyote wa milango mitano ya fahamu; njozi na dhana havimtambui Yeye. Kupita kwa wakati na kupishana kwa zama havimpunguzi Yeye kwa hali yoyote, na ameepukana na mabadiliko na kigeugeu cha aina yoyote."[2]

### UPWEKE WA MWENYEZI MUNGU (TAWHIID)

Wakati suala la upweke wa Mwenyezi Mungu linapojitokeza kwenye mazungumzo ya kidini, linachukuliwa kujumuisha mada nyingi, ikiwemo pamoja na imani ya upweke wa hiyo dhati, hivyo pia mkusanyiko wa sifa na tofauti baina ya dhati na sifa imewekwa pembeni kabisa kuhusiana na umoja wa sifa. Upambanuzi na utofautishaji unatokana na uwekaji mipaka. Kama tunatanguliza tofauti miongoni mwa sifa za ki-Ungu, inakuwa ni halali tu kwa mtazamo wa mawazo na tafakuri zetu za kawaida; ongezeko la mielekeo na sifa zilizokithirishwa haziwezi kuathiri hiyo dhati tukufu

Endapo katika ulimwengu wa maumbile tutatazama kiwiliwili kwa kutumia vipande vya kioo vyenye rangi tofauti; kiwiliwili hicho kitaonekana

1. Nahj al-Balaghah, toleo la Fuyz al-Islam, uk. 14. elimu yoyote juu Yake.
2. Usul al-Kafi, Kitab at-Tauhid,uk.. 150 kama hivyo.

katika mfululizo wa rangi tofauti. Hivyo hivyo, tunapotafakari dhati tukufu ya kipekee kwa busara zetu, wakati mwingine tunaihusisha elimu na hiyo dhati isiyokuwa na ukomo kwa kuzingatia ukweli kwamba viumbe vyote wakati wote vipo mbele yake; halafu tunasema Yeye ni Mjuzi wa Yote. Wakati mwingine tunatambua uwezo wake wa kuumba vitu vyote, na halafu tunazungumzia juu ya Yeye kuwa Mwenye Nguvu zote. Kwa hiyo, pale tunapotambua kupitia kwenye vipenyo hivi mbali mbali, zile sifa tofauti zinazoonekana kufanana na uhai wetu wenye ukomo, tunajaribu kuzitenga kutoka kwenye dhati Yake isiyo na ukomo. Hata hivyo, bila upendeleo, dhana zote zilizowasilishwa na sifa hizo tofauti zinakuwepo mahali pamoja na unawasilisha ukweli moja, ukweli ambao hauna dosari na upungufu wowote, wenye ukamilifu wote kama vile uwezo, huruma, ujuzi, neema, hekima na ufahari.

Amirul-Muminin Ali (a.s) anasema katika hotuba ya kwanza ya Nahjul-Balagha, **"Mwanzo wa dini ni kumtambua, na ukamilifu wa kumtambua ni kumsadiki. Imani ukamilifu wa kumsadiki ni kumpwekesha, na ukamilifu wa kumpwekesha ni kuwa na Ikhlasi Naye, na ukamilifu wa kuwa na Ikhlasi Naye ni kumuondolea sifa, kwa ushuhuda wa kila sifa ni si chenye kusifiwa, na ushuhuda wa kuwa kila chenye kusifiwa sio sifa. Hivyo basi mwenye kumsifu Mungu swt. Amemfanyia mwenzi, na mwenye kumfanyia mwenzi amemfanya kuwa wawili, na mwenye kumfanya wawili amemfanya kuwa mwenye sehemu sehemu, na mwenye kumfanya kuwa mwenye sehemu sehemu anakuwa hamjui, na ambaye hamjui anakuwa amemuashiria, na mwenye kumuonyesha amemuwekea mpaka, na mwenye kumwekea mpaka amemfanya wa idadi. Na mwenye kusema yuko ndani ya nini amemfanya yuko ndani ya; na mwenye kusema yuko juu ya nini amemtoa humo."**

Kwa hiyo, kila sifa haina ukomo na inakuwa na uhai mrefu wa pamoja na umilele wa dhati yenyewe. Mwenyezi Mungu ametakasika na kuondokana na sifa zinazoweza kuwa tofauti na nyingine na kutenganishwa na dhati yenyewe. Pindi tutakapotambua kwamba dhati ya Mwenyezi Mungu inatokana na Yeye mwenyewe, hiyo ina maana kwamba kuna nafsi kamilifu isiyopimika katika namna zote. Kama kiumbe hai na kisichokuwa na uhai vyote vinaweza kufikiriwa sawa kwa ajili ya maisha, lazima kipate uhai kutoka kwenye kitu kingine ili kiweze kuwa hai; kitu kujianzisha chenyewe, hata hivyo, haiwezekani. Kwa hiyo, ni dhati kamilifu tu ndio inayoweza kutokana na yenyewe; hali halisi nyingine zote ziko chini yake na zinajulikana tu kwa njia yake. Pindi dhati itakapofanana na uhai wake, inakuwa isiyopimika kuhusu ujuzi, uwezo, kutojianzisha na hali ya kudumu milele, kwani zote hizi ni aina za viumbe na chimbuko ambalo linafanana na asili yake kwa hali yoyote ni lazima kuwa na ukamilifu wote huu kwenye kiwango kikubwa sana.

Upweke wa Mwenyezi Mungu (Tauhiid) ni mojawapo ya sifa Zake za mwanzo kabisa. Dini zote za mbinguni, katika mafundisho yao ya asili na yasiyopotoshwa, yamemlingania mwanadamu kwenye uthibitisho halisi wa upweke wa Mwenyezi Mungu, usiotiwa dosari na kushirikishwa na miungu wenza. Kupachikwa washirika huko, kwa namna zote za miundo na

mielekeo ndio kosa baya sana ambalo mwanadamu anawajibika kwalo kisheria. Imetokea katika historia yote kama matokeo ya ujinga, kutokutambua, na kukengeuka toka kwenye mwongozo wa akili na mafundisho ya Mitume.

Kama mwanadamu alimwamini Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa fikra sahihi, uthibitisho wa akili na mwongozo wa mitume, isingewezekana kwa wao kukubali vitu vyovyote vya kubahatisha au vitu vilivyoumbwa, kusimama mahali Pake, na kudhani kwamba kiumbe kingine chochote kinaweza kuwa mshirika wake au kuwa sawa katika kuamuru na kuthibiti hali za dunia, au hata kuwa na sehemu katika uendeshaji wa mpango wa ulimwengu. Kama miungu wengi wangeitawala dunia na kila mmoja wa miungu hawa angefanya anavyotaka na kutoa amri kufuatana na utashi wake, mpangilio wa ulimwengu ungetambukia kwenye uawala huria. Qur'ani inasema:

وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ آتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٢٢﴾

"Na (Yusuf) alipofikilia utu uzima, tulimpa hukumu na elimu na hivyo ndivyo tunavyo walipa watendao mema." (12:22)

Kama tunasema kwamba Mwenyezi Mungu ni mmoja, ni kwa sababu Yeye sio mwili. Kuimbe ni mkusanyiko wa mlolongo wa elementi, ambazo kuunganika kwao husababisha kiumbe kuwepo. Kuchanganyika, mgawanyiko na kuzaana zote hizi ni sifa za viumbe na miili inayotegemewa kuweko au kutokea; kwa hiyo tunaiondoa kwenye mfano wa Mwenyezi Mungu na tunathibitisha kwamba chochote ambacho kimekuwepo, kama matokeo ya uchanganyikaji na uzaanaji, wala hakiwezi kuwa Mwenyezi Mungu ama kufanana Naye.

Inawezekana kufikiria juu ya u-wingi ndani ya namna fulani maalum pindi tunapozungumzia mipaka kama vile wingi, ubora na muda. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu habanwi kimipaka na lolote kati ya haya, na kwa hiyo haiwezekani kumfikiria Yeye kuwa na wa kufanana Naye au mwenza. Kama tunajaribu kudhania asili ya maji, bila sifa yoyote ya ukomo au mpaka, na tukalirudia zoezi hili mara kadhaa, hakuna kitakachoongeka kwenye dhana yetu ya awali. Kwa sababu mwanzoni tuliyafikiria maji katika maana yake halisi, bila kuweka ufinyu wowote katika hali, wingi au ubora, haiwezekani kwamba katika majaribio yetu yatayofuata ya kutafakari juu yake, nadharia mpya itajitokeza kwetu sisi.

Lakini tunapoongeza kwenye asili ya maji sifa fulani zenye ukomo ambazo sio za msingi juu yake, aina tofauti na mifano ya maji itatokea na pamoja nayo, ni uwingi. Mifano ya hili ingekuwa maji ya mvua, maji ya chemchem, maji ya mto, maji ya bahari, yote haya yakionekana nyakati na sehemu tofauti hapa na pale. Kama tukiondoa masharti yote haya na kuangalia tena asili ya msingi ya maji, tutaona kwamba yameondokana na aina zote za uwili mchanganyiko na sasa ni asili moja tu.

Lazima tutambue kwamba kiumbe chochote ambacho kinaweza kuwekwa na kuenea kwenye sehemu fulani, basi kwa lazima sana kinaihitaji sehemu hiyo, na kitu chochote ambacho kitakuwa ndani ya wakati fulani, uhai wake yenyewe unategemea mazingira bainifu ya wakati huo: uhai wake utatambuliwa tu ndani ya muundo maalum wa kiwakati ambamo mazingira hayo yanaupata.

Kwa hiyo, tunapokuja kuitambua nafsi ambayo ipo wakati wote na kila mahali na ambayo ina kiwango cha juu sana cha ukamilifu wa kueleweka, na ambayo mbali na hiyo hakuna kitu kingine ambacho ni kikamilifu au halisi na kisicho na walakini, lazima tuelewe kwamba kupachika uwili juu ya dhati ya juu kiasi hicho ni kukifanya kiwe chenye mwisho na ukomo. Hakika Mwenyezi Mungu si mmoja kwa maana ya kimahesabu, hivyo kwamba tunaweza kudhania kwamba Yeye ni wa kwanza wa aina ambayo anafuatiwa na wa pili. Upweke wake ni kiasi kwamba kama tukidhania kuwepo wa pili pamoja Naye, yule wa pili lazima afanane na yule wa kwanza.

Kwa kuwa uongezekaji wa vitu hutokana na mazingira yenye kuweka mipaka ambayo huvitofautisha kimoja na kingine, itakuwa haina mantiki kabisa kuleta nadharia ya wa pili juu ya kiumbe kisichokuwa na mipaka na vifungo. Kuwepo kwa wa pili itamaanisha kwamba wa kwanza alikuwa na mipaka na vifungo, na endapo mipaka na vifungo vikiondolewa, hatuwezi kuwa na viumbe viwili; dhana yetu ya kiumbe cha pili itakuwa ni marudio ya kile cha kwanza.

Mafundisho ya upweke wa Mwenyezi Mungu yana maana kwamba kama tukimchukulia Mwenyezi Mungu peke yake bila kuvihusisha viumbe vingine vyote vinavyotambulika, dhati yake tukufu inathibitika kikamilifu. Vivyo hivyo, endapo tunafikiria kuwepo kwake, pamoja na kuvihusisha viumbe vingine vyote, hapo tena, kuwepo kwake kutakuwa kumethibitika kikamilifu. Lakini kama, kwa kinyume chake, tunaviangalia vitu vinavyotokea bila kutarajiwa bila kumhusisha Mwenyezi Mungu basi vitu hivyo haviwezi kusemekana kwa njia yoyote ile kwamba vipo, kwa sababu kuwepo kwao kunategemea juu ya Muumba kwa ajili ya chimbuko lao na kuongezeka kwao.

Kwa hiyo wakati wowote tunapomwekea Mwenyezi Mungu mipaka na masharti, maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu atakoma kuwepo wakati wowote ambapo mpaka na sharti hilo litakoma kuwepo. Hata hivyo, kuwepo kwa Mwenyezi Mungu hakutawaliwi na sharti au wingi, na kwa hiyo akili haiwezi kuleta nadharia ya wa pili katika namna yake. Hebu natutoe mfano mmoja: Tuchukulie kwamba dunia haina ukomo; haina mipaka na katika upande wowote tutakaoelekea kamwe hatufikii mwisho wake. Kwa fikra kama hii kuhusu dunia ya maumbo, mipanuko yake yote ikiwa haina mwisho, tunaweza kudhania kuwepo kwa dunia nyingine zaidi yake, imma yenye ukomo au isiyo na ukomo. Hakika hatuwezi, kwa sababu dhana ya dunia ya viumbe isiyo na mwisho inalazima kuondoa kuwepo kwa dunia nyingine kama hiyo. Endapo tunajaribu kufikiria dunia nyingine kama hii, ama itafanana na ile ya kwanza au iwe ni sehemu yake.

Kwa hivyo, kufikiri kwamba asili tukufu ni kiumbe kilicho kamilika, kudhania kuwepo kwa kiumbe cha pili kinachofanana na Yeye ni sawa kabisa na kudhani dunia ya pili ya viumbe kuwepo kwa wakati mmoja huohuo na dunia ya viumbe isiyo na mwisho. Kwa maneno mengine, hiyo haiwezekani. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba maana ya Mwenyezi Mungu kuwa Mmoja sio kwamba Yeye sio wawili; ni kwamba, wa pili hafikiriki kuwepo na kwamba umiliki pekee wa utukufu unalazimishwa na asili Yake. Anakuwa tofauti na mwingine asiyekuwa Yeye Mwenyewe, sio kwa namna

ya mpaka wowote bali kwa namna ya asili Yake yenyewe ambayo inaweza kutofautishwa wazi wazi na zingine zote. Viumbe vingine vyote, vinapolinganishwa, hupata ubainishwaji wao, sio kutoka kwenye asili zao bali hasa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Tunaona dhahiri kwamba uhusiano na upatanifu mkubwa unakuwepo miongoni mwa vijenzi vyote vya dunia. Binadamu huzalisha gesi ya asidi ya kaboni ambayo huiwezesha mimea kuvuta hewa hiyo, na miti na mimea, kwa kubadilishana hurudisha hewa ya oksijeni ambayo humwezesha binadamu kuivuta. Kwa matokeo ya kubadilishana hivi baina ya binadamu na mimea, kiasi cha hewa ya oksijeni huhifadhiwa wakati wote; kama isingekuwa hivyo, hakuna dalili za maisha ya mwanadamu yangebaki juu ya duniani.

Kiasi cha joto kinachopokelewa na dunia kutoka kwenye jua huwa kinakubaliana na mahitaji ya viumbe hai kwa ajili ya kupata joto. Kasi ya mbiringiko wa dunia kuzunguuka jua na umbali inaouweka kutoka kwenye chanzo hicho cha nishati na joto vimekadiriwa katika kiwango kinachofanya uhai wa binadamu juu ya dunia uwezekane. Umbali wa dunia kutoka kwenye jua ndio unaoamua kiwango cha nyuzi joto ambacho hasa ndicho kinachokubaliana na mahitaji ya uhai juu ya ardhi. Kama kasi sya mbiringiko wa dunia kuzunguka jua ingekuwa maili 100 kwa saa badala ya maili 1000 kwa saa, kama ilivyo sasa, vipimo vya usiku na mchana wetu vingekuwa mara kumi zaidi kwa urefu, na ukali wa joto la jua ungepanda na kufika kiwango ambacho uhai wote wa mimea ungeunguzwa na usiku wa baridi wa kila siku ya majira ya kipupwe ungegandisha machipu yote mapya ardhini.

Endapo, kwa upande mmoja, miale ya jua ingepunguzwa kwa nusu, viumbe hai vyote vingegandishwa pale vilipo na baridi iliyokithiri sana. Endapo, kwa upande mwingine, miale ya jua ingeongezwa na kuwa maradufu, mbegu ya uhai kamwe isingeweza kufanikisha matunda yake. Kama mwezi ungekuwa mbali sana kutoka duniani, mawimbi ya bahari yangekuwa na nguvu na makali kiasi cha kutosha kuweza kung'oa milima. Inapooonekana kwa mtazamo huu, dunia huonekana kama msafara ambao wasafiri wake wote wameungana pamoja kama viungo katika mnyororo. Sehemu zake zote, kubwa na ndogo zinajitahidi kwa pamoja kusonga mbele kwenye muelekeo mmoja. Katika mfumo wote huu, kila kitu kinatimiza kazi yake mahsusi na vitu vyote husaidiana na kukamilishana. Kiungo kikubwa na kisichoonekana huunganisha kila atomu moja na atomu zingine zote.

Dunia ambayo imejaa umoja kiasi hicho lazima iwe imeunganishwa na chimbuko na kanuni moja. Uhai unatokana na chanzo kimoja, kama ujumla wote wa ulimwengu ni mmoja, muumbaji wake pia lazima awe mmoja. Ule ukweli kwamba muumbaji ameleta umoja katika uwingi wa dunia iliyoumbwa, huo peke yake ni uthibitisho wa kutosha wa Upweke wake, uwezo na hekima Yake.

Qur'ani inasema:

قُلْ أَرَأَيْتُمْ شُرَكَاءَكُمُ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ أَرُونِي مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَاوَاتِ أَمْ آتَيْنَاهُمْ كِتَابًا فَهُمْ عَلَىٰ بَيِّنَتٍ مِّنْهُ بَلْ إِن يَعِدُ الظَّالِمُونَ بَعْضُهُم بَعْضًا إِلَّا غُرُورًا ﴿٤٠﴾

"Sema: mmewaona washirika wenu mnaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu? Nionyesheni ni sehemu gain ya ardhi waliyoiumba au wanayo shirika katiaka mbingu? Au tumewapa kitabu na wao ambacho kwacho wakawa na dalili za wazi? Lakini madhalimu hawaahidiani wao kwa wao ila udanganyifu tu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu huzuia mbingu na ardhi zisiondoke, na kama zikiondoka hakuna yeyote wa kuzizuia baada yake. Bila shaka yeye ni Mpole, Mwingi wa kusamehe." (35:40-41).

Asili yetu ya kimaumbile, ambayo ni kipimo cha msingi wa maisha yetu pia inathibitisha upweke wa Mwenyezi Mungu. Katika nyakati za hali mbaya sana na taabu, matakwa yetu yote huelekezwa mahali pamoja; tunageukia upande mmoja na kukabidhi nyoyo zetu Kwake. Mmojawapo wa wanafunzi wa Imamu Jafar as-Sadiq (a.s) alimwuliza, "Kuna uthibitisho gani juu ya upweke wa Mwenyezi Mungu?" Imamu alimjibu: "Uthibitisho wa upweke Wake ni uhusianaji mwendelezo wa maumbile yote, mpangilio muhimu wa uhai ambao unatawala juu ya kila kitu. Mwenyezi Mungu anasema kwenye Qur'ani:

"Angekuwepo muumba mbinguni na katika ardhi, mbali na yule Mungu Mmoja, mpango wao ungetoweka na dunia ingeangamia."[1] Kwa hiyo, utaratibu na uelewekaji wa mpangilio uliotawala vitu vyote unaikanusha ile nadharia ya kuwa panaweza kuwepo na miungu wengine kadhaa, wanaotawala maeneo yale au maeneo mengine tofauti.

Ingawa Qur'ani inasisitiza upweke wa Mwenyezi Mungu katika uumbaji na hekima, pia inatamka wajibu wa visababisho na njia ambazo zinatekeleza amri ya Mwenyezi Mungu. Inasema:

وَاللَّهُ أَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٦٥﴾

"Na Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mbinguni na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, kwa hakika katika hayo mna mazingatio kwa watu wanaosikia." (16:65)

Pindi tunapofikia kwenye hitimisho kwamba Mwenyezi Mungu peke Yake ndiye anayeshughulika na uumbaji, upangaji na uendeshaji wa ulimwengu wote, na kwamba vyanzo vyote vya athari na uhusiano baina yao viko chini ya utashi na amri Yake, kila kimoja kikiwa na kazi yake maalum ilichopangiwa na Mwenyezi Mungu - pindi tunapofikia uamuzi huo, tunawezaje kudhania kiumbe kingine chochote kuwa katika daraja sawa na Mwenyezi Mungu na kuinama katika kukiabudia mbele yake?

Qur'ani inasema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّهِ أَندَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَشَدُّ حُبًّا لِّلَّهِ وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا وَأَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعَذَابِ ﴿١٦٥﴾

1. Usul al-Kafi, Kitab at-Tauhid.

"Na miongoni mwa watu wako ambao huwafanya miungu wasiokuwa Mwenyezi Mungu, wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini wale walioamini wanampenda sana Mwenyezi Mungu zaidi. (2: 165)

وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّـهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾

"Na miongoni mwa ishara zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi. Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu aliyeviumba, ikiwa ninyi mnamuabudu Yeye tu." (41:37).

12

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA MBILI

### UWEZO WA MWENYEZI MUNGU USIOPIMIKA

Uwezo wa Mwenyezi Mungu Usiopimika,haun uthibitisho wa wazi zaidi kuliko ule unaopatikana kwa njia ya uchunguzi na kuhoji maumbile ya ulimwengu ulioumbwa na mifumo mingi ya mpangilio wa rangi za maumbile ambazo kamwe haziwezi kuelezewa kukamilifu.

Tunapo tazama viumbe wa Mwenyezi Mungu tunajikuta tunakabiliwa na nguvu kubwa mno hivyo kwamba hapana ukomo unaoweza kufikiriwa juu yake. Kutazama uumbaji na mamilioni ya ukweli yaliofichika kwenye maajabu ya maumbile na vina vya ndani vya utu wake mwanadamu mwenyewe kunatoa dalili za wazi kabisa za kipimo cha uwezo wa yule Mmoja Aliyeuumba huo, kwani mpangilio mzito wa uhai na mgumu kuelezeka haukubali maelezo mengine.

Ni uwezo wa Mwenyezi Mungu usiolinganishika ambao humlazimisha binadamu kuinama kwa unyenyekevu mbele ya Muumbaji wa mpango huu mkubwa. Hakuna neno la kuweza kuelezea kadiri ya vipimo vya uwezo Wake, dhati hiyo ya pekee ina uwezo mkubwa mno ambao kwamba wakati wowote Anapolitaka jambo, hutosha kwa ile amri, 'Kuwa' itoke kwake na kitu kilichoambiwa hivyo, kitakuwa. Qur'ani inasema:

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَن يَقُولَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾

"Hakika amri yake, anapolitaka jambo lolote ni kuliambia tu: 'KUWA' na linakuwa. (36:82).

Sheria iliyofafanuliwa katika Aya hii ni ishara nzuri zaidi ya uwezo Wake usio na mpaka na udhihirisho wa mamlaka wa utukufu Wake usio na mwisho. Inabatilisha mpaka wowote ambao unaweza kuwekwa juu ya uwezo wa Mwenyezi Mungu na kutangaza kutotoshekeza kwa vigezo vyote na vipimo, vinapokabiliwa na sheria hii tukufu.

Mabingwa wa sayansi ya viumbe, watu wa maabara, licha ya maendeleo yote ambayo wamepata, hawajapata elimu kamili ya siri za ndani kabisa za kiumbe mmoja pekee miongoni mwa viumbe vingi na vyenye kutofautiana vya ulimwengu ulioumbwa. Hata hivyo, ile sehemu ya elimu na yenye dosari ambayo mwanadamu ameipata kuhusu viumbe vichache vilivyopo hapa ulimwenguni inamtosha yeye kutambua kwa nafsi yake yote kwamba ile nguvu kubwa ambayo imeumba aina mbalimbali na nyingi kama hizi hapa duniani lazima iwe haina ukomo.

Fikiria wingi wa viumbe Vyake: viumbe vidogo sana na madubwana yenye sura za ajabu kwa pamoja wakiishi katika vina vya baharini; ndege wanaopendeza wenye sauti za kuvutia wenye mabawa yenye rangi mbalimbali, ambao uzuri wao, wasanii stadi huiga, kama mapambo ya kazi yao; nyota zing'arazo mbinguni na jua lichomozalo na kuzama; alfajiri na mwanga wa mwezi; sayari, galaksi na jamii ya nyota nyingi za mbali sana kila moja yao wakati mwingine kwenye kiini chake huwa na mamilioni ya nyota kubwa sana zing'arazo na kufanya maruweruwe ukosa ukomo wake wa dhahiri.

hivi maumbile kama haya, yanayoshangaza kwa utukufu wake, hayaashirii uwezo usio na ukomo wa mtengenezaji wake? Je, mtu anaweza kudharau uwezo wa Muumbaji Ambaye anatoa mabadiliko mbali mbali kama haya kwenye maisha, akafanya miundo dhahiri, ya mabadiliko hayo, yenye ukomo kujitokeza kwenye mpango wote huu mpana wa matukio. Sasa baada ya ukweli kwamba aina zote hizi za viumbe za kuvutia hatimaye zinachipukia kutoka kwenye atomu, suala la uhai haliwezi kuelezewa isipokuwa kwa kurejea kwenye mamlaka yenye muongozo na yasiyo na ukomo. Ni Yeye Ambaye huvichochea vitu vyote kuelekea kwenye dhana ya muundo wenye kuleta uhai na anao uwezo na akili ya kupanga na kubuni mpango huu mpana na sahihi.

Kubwa na ndogo, ngumu na rahisi ni tabia zinayofungamana na viumbe vyenye ukomo; katika ufalme wa milele wa dhati na sifa za Mwenyezi Mungu, hakuna suala la ukubwa na udogo, nyingi na chache. Unyonge na udhaifu husababishwa na ukomo wa nishati katika haki ya utumiaji wa wakala, kwa kuwepo kipingamizi katika njia yake, au kwa kukosekana njia na vifaa, hayo ni yasiyowazika katika suala la uwezo usio na ukomo. Qur'ani inasema:

وَمَا كَانَ اللَّـهُ لِيُعْجِزَهُ مِن شَيْءٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ ۚ إِنَّهُ كَانَ عَلِيمًا قَدِيرًا ﴿٤٤﴾

"... Na hakuna kitu kiwezacho kumshinda Mwenyezi Mungu mbinguni wala ardhini, Bila shaka yeye ni Mwenye kujua, Mwenye uwezo." (Fatir: 35:44).

Ingawa Mwenyezi Mungu anaweza kufanya vitu vyote, Ameumba ulimwengu kulingana na mpango usahihi na maalum katika mfumo ambao kwamba jukumu lililopangwa maalum, limewekwa juu ya viumbe fulani katika uanzishaji wa vingine. Viumbe hivyo, moja kwa moja na bila shaka yoyote viko chini ya amri Yake wakati vinapotimiza jukumu hilo na kamwe havikiuki amri Zake japo kidogo. Qur'ani inasema:

وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّـهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾

"Na jua na mwezi na nyota vimetiishwa kwa amri Yake. Fahamuni kuumba na amri zote na Zake. Amebarikiwa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote. (A'aaraf: 7:54).

Kusema kweli, hapana kiumbe katika mpango wa ulimwengu kinachoweza kuwa udhihirisho wa mamlaka au kuwa na fungu lolote katika utashi na amri Yake, kwani kama vile ambavyo Mwenyezi Mungu hana mshirika katika dhati Yake, vivyo hivyo, pia, hana mshirika katika uwakala Wake. Kama vile ambavyo viumbe vyote duniani vinavyokosa uhuru katika asili zao na vikawa vinamtegemea Yeye, pia vinaukosa vilevile katika kutoa vitendo na athari. Kila kiwakilishi na kisababishi hupata dhati ya uhai wake kutoka kwa Mwenyezi Mungu na pia uwezo wake wa kutenda na kutoa athari.

Kila anapotaka na kukilazimisha, amri ambayo inahusu viumbe vyote hutelekeza wajibu wake, kwani utaratibu huo wenyewe upo chini ya utashi Wake, hata kama uwe wenye thamani na imara vipi. Muumbaji Ambaye ameweka athari mahsusi kwa kila kitu na chanzo, anaweza kuitangua na

kuahirisha athari hiyo wakati wowote. Kama vile ambavyo amri moja ilivyosababisha utaratibu wa ulimwengu kuwepo, amri nyingine hunyang'anya maumbile athari zao za desturi.

Hivyo, Qur'ani inasema:

قَالُوا حَرِّقُوهُ وَانصُرُوا آلِهَتَكُمْ إِن كُنتُمْ فَاعِلِينَ ﴿٦٨﴾ قُلْنَا يَا نَارُ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿٦٩﴾

"Wakasema; mchomeni (Ibrahim) na muiokoe miungu yenu, ikiwa ninyi ni watu wenye kutenda. Tukasema; Ewe moto! Kuwa baridi na salama juu ya Ibrahim. (21:68-69).

Ingawaje ule mvuto wenye nguvu sana utolewao na jua na ardhi unaenea kwenye nafasi kubwa mno, bado maumbo yote hayo yako chini ya utashi Wake. Mara tu Anapompa ndege mdogo nguvu za lazima, ndege huyo anakuwa na uwezo wa kuzuia mvuto wa ardhi na akaruka zake. Qur'an inasema:

أَلَمْ يَرَوْا إِلَى الطَّيْرِ مُسَخَّرَاتٍ فِي جَوِّ السَّمَاءِ مَا يُمْسِكُهُنَّ إِلَّا اللَّـهُ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٧٩﴾

"Je, hawawaoni ndege waliotiishwa katika anga la mbingu? Hakuna awazuiaye (wasianguke) isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika katika hayo mna mazingatio kwa watu wanaoamini. (16:79).

Kiumbe chochote kinachoweza kufikiriwa kuwepo katika dunia ya maumbile kinakuta mahitaji yake ya riziki na maisha yanatimizwa na Muumbaji. Kwa hiyo, uwezo wowote na nafasi inayoonekana kwenye mpango wa maumbile inabidi lazima kurudi kwenye uwezo usio na kikomo wa Mwenyezi Mungu. Amirul-Mu'minin Ali (a.s) anasema kwenye hotuba iliyoandikwa kwenye Nahju al-Balagha:

**"Ee Mwenyezi Mungu, hatuwezi kupenya vina vya ubora utukufu wako. Tunajua kwamba Wewe uko hai daima na unajitosheleza, kwamba wewe huhitajii kula wala kulala usingizi. Hakuna akili inayoweza kukutambua Wewe na hakuna jicho linaloweza kukuona wewe. Bali Wewe unayaona macho yote, Unajua kipindi cha uhai wa kila kiumbe, na Wewe ni Muweza wa kila kitu.**

**"Ingawa hatujatambua lolote katika uumbaji Wako, tunashangazwa na uwezo Wako na tunakutukuza sana Wewe. Kile kilichofichika kwetu na macho yetu hayawezi kukiona wala fikra na akili haviwezi kukipata, ambacho kimefichwa kwetu kwa mapazia ya ghaib (yasiyoonekana) ni kikubwa zaidi kuliko kile tunachokiona."**[1] Mtu anapoamua kujenga kitu - mfano hospitali - hukusanya vitendea kazi muhimu na vifaa vingine ambavyo havina uhusiano wowote muhimu kati ya kimoja na kingine, na halafu anaviunganisha kwa kutumia mlolongo wa uhusiano wa bandia ili kutimiza lengo lake.

Ili aweze kutengeneza uhusianao wa bandia kama huo, hutumia nguvu tofauti tofauti na vitu vingine ambavyo anavikuta tayari vipo. Kazi na shughuli ya mtu huyu ni sehemu ya mfumo wa maumbile, sio shughuli ya ubunifu kwa kusema kweli, bali ni namna ya msogeo tu ambao unafanyika

1. Nahj al-Balaghah, Hotuba ya 159.

ndani ya vitu vilivyopo. Uumbaji wa ki-Mungu unakuwa na aina tofauti kabisa na ule uzalishaji wa uhusiano wa bandia baina ya vitu visivyo husiana. Mwenyezi Mungu huanzisha vitu vikiwa na tabia zao zote, nguvu, nishati na sifa bainifu.

Tunaposema Mwenyezi Mungu ni mweza wa yote, lazima tuelewe kwamba uwezo wake unavutika au kuitikia tu kwenye vitu vinavyowezekana. Vitu ambavyo haviwezekani kimantiki vipo nje ya nyanja (fani) ya uwezo Wake na kutumia neno 'Uwezo' kuhusiana na vitu ambavyo haviwezekani sio sahihi na haina maana yoyote. Ingawa uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa kweli hauna ukomo, uwezo wa mapokezi wa vitu na uwezo wao wa kutumika kama kituo maalum kwa ajili ya udhihirishaji wa uwezo wa ki- Mungu lazima ufikiriwe. Utekelezaji wa utashi wa Mwenyezi Mungu unasokotana na uhusiano baina ya chanzo na athari, na mfumo mgumu wa sababu na vyanzo usioelezeka kwa urahisi. Ili kitu kiweze kuwa lengo la utashi wa ki-Mungu, lazima kisiwe ni kisichowezekana na lazima, katika asili yake, kiwe na uwezo wa kupokea; utashi wa ki-Mungu unatimizwa kwa njia ya wepesi wa upokeaji vitu vyenyewe. Ni kweli, kwamba nuru ya ki-ungu haina ukomo na wakati wote inazidi kufurika, lakini sehemu inayotakiwa kuipokea nuru hiyo inaweza kuwa na dosari na kwa hiyo inashindwa kufyonza mgawo huo wa kudumu ambao unatolewa na chanzo hicho chenye ukwasi tele.

Bahari ni chanzo kikubwa sana cha maji, chenye maji mengi sana, lakini meli ya kubebea vimiminika ina nafasi ndogo tu ya kuchukua maji yake; kwa kweli ni kiasi kidogo sana cha maji hayo kitakachoweza kupakiwa kwenye meli hiyo. Kwa uwazi wa kutosha kabisa ni kwamba chenye mpaka na kikomo katika mfano huu ni nafasi ya meli, sio maji katika bahari hiyo.

Mtu mmoja wakati fulani alimuuliza Ali, Amirul-Mu'minin (a.s): "Je, Mola wako anaweza kuijaza dunia yote kwenye yai la kuku?"

Akajibu: **Mwenyezi Mungu Mweza wa Yote, kwa hakika anaweza kufanya chochote, lakini kile ulichouliza ni kitu kisichowezekana.**"[1] Kwa hiyo ingawa dhati tukufu ya Mwenyezi Mungu ipo huru kabisa kutokana na kutokuwa na nguvu na uwezo, haina maana na mantiki kuuliza kama Mwenyezi Mungu anaweza kufanya jambo ambalo kwa asili haliwezekani.

Mtu ambaye moyo wake hudunda kwa kumpenda Mwenyezi Mungu na ukawa umejawa na imani juu ya Muumbaji wa vitu vyote kamwe hatokata tamaa, kujihisi mpweke na asiye na matumaini hata katikati ya matatizo magumu sana. Tendo lolote analolifanya, anafanya huku akitambua kwamba yupo kwenye kivuli cha ulinzi cha nguvu kubwa ambayo inaweza kumfanya yeye aweze kupata ushindi juu ya matatizo yote. Mtu anayemtambua Mwenyezi Mungu na anajua kwamba anafaidi msaada Wake anaweza kujizuia na kustahamili matatizo ya kila aina. Kwake yeye mtu huyo matatizo ni kama sehemu ya povu iliyomo kwenye povu linalotoweka haraka juu ya uso wa maji. Moto unaowaka ndani mwake huendelea kuwaka na kuangaza zaidi na anatokea kuwa na nguvu zaidi kuliko mwanzo kutoka kwenye kalibu (kikaango) ya mateso.

1. Bihar al-Anwar, Juz. iv, uk. 143.

Wakati wote binadamu wa kazi ngumu anazostahimilia, analiwazwa na kutiwa nguvu na huruma na upendeleo wa Mwenyezi Mungu, hali hii ndiyo inayo tengeneza nguvu ya shughuli yake. Kushindwa hakumzibii njia yake na kusababisha asalimu amri badala yake, kwa nia njema na juhudi za uchapakazi, huendelea kufanya bidii kwake hadi mwishowe anapopata ushindi.

Anaelewa vema kabisa kwamba juhudi zake haziwezi kukosa kuleta matokeo mazuri na kwamba ushindi huenda kwa yule anayestahili. Kila anaporidhia, Mwenyezi Mungu humshika mkono yule aliyeanguka na mwenye kudhulumiwa ambao hawana kimbilio jingine mbali na Kwake na kuwanyanyua na kuwafikisha kwenye kilele cha uwezo. Pia wakati mwingine Mwenyezi Mungu, huzipaka vumbi la udhalilishaji na mabalaa, zile pua za wenye uwezo na madhalimu wenye kiburi ambao huamini kwenye vurugu tu na mantiki ya mabavu na kuwatendea watu kama vile hawana thamani.

Ni madikteta wangapi wenye kiburi wametupwa chini na mabalaa katika historia ya mwanadamu, wakazama na kutoweka katika wimbi la aibu. Mfululizo wa kisa cha mitume wa Mwenyezi Mungu unawakilisha mfano kamili na bora wa maadili mema ya binadamu. Sote tunajua jinsi mitume walivyosimama peke yao dhidi ya nguvu za dhuluma za wakati wao ili waweze kuwaongoza wanadamu kwenye ukombozi, kuibadili jamii yao, na kuwafundisha maadili ya kiwango cha juu. Kwa kufanya hivyo, waliwasha cheche ya kwanza ambayo hatimaye iliangamiza ushirikina.

Majibu yaliyoamshwa na imani zao yalisababisha vurugu ya uhakika hivyo, kiasi kwamba waliweza kubadili sura na mwelekeo wa historia. Waliweka misingi ya ibada ya Mungu mmoja (Tawhiid) na waliasisi kanuni za maadili kwa njia pana zaidi. Ni nani anayeweza kukanusha wajibu waliofanya kwa kujitolea kwao na imani zao katika mapambano yasiyochokesha waliyoyafanya? Ni umbali gani nguvu ya utashi peke yake inaweza kumfikisha wanadamu na kwa kiasi gani itamwezesha kustahamili na kujitolea mhanga?

Uchambuzi wa haraka wa historia ya kujivunia ya maisha ya Mitume unatuwezesha sisi sote kutazama, kwa namna ya dhahiri kiasi iwezekanavyo, ule uaminifu na utiifu waliouonyesha, huruma zao na uvumilivu wao na tamaa yao kubwa ya kuwaongoza na na kuwabadilisha wanaadamu.

Siri yao kuu juu ya mafanikio yao ni ukweli kwamba kamwe hawakujifiria wao wenyewe binafsi hata mara moja, kwa uaminifu walizikana nafsi zao, na kuzifanya wakfu katika njia ya Mwenyezi Mungu. Halafu Mwenyezi Mungu akajibu kwa kuwajaalia Mitume uhai na umaarufu wa milele daima.

13

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA TATU

### ELIMU YA MWENYEZI MUNGU ISIYO NA MIPAKA

Muumbaji ambaye hawezi kuzingirwa na mahali, Ambaye Dhati yake haiwezi kuwekewa ukomo, Ambaye uhai wake umeenea kila sehemu ya mbingu na dunia - Muumbaji kama huyu kwa kawaida anatambua vitu vyote, hapana kitu kilichomo katika mpangilio wote wa maumbile ambamo miale yenye nuru kali ya elimu yake haikiangazii.

Matukio yanayotokea sehemu za mbali sana za ulimwengu, matukio yaliyotokea mabilioni ya miaka iliyopita au ambayo yatatokea mabilioni ya miaka ya wakati ujao baadaye - yote yamo ndani katika ujuzi wake, na majaribio makubwa, mapana sana katika kuitafsiri elimu yake, hayana budi kwa hiyo kutofanikiwa.

Ili kuweza kuuelewa upeo mkubwa wa elimu Yake, tunapanua wigo wa fikra zetu, tunatumia akili zetu kutafakari na kutafiti, na kujaribu kusonga mbele kuelekea lengo letu tukiwa na akili nzuri. Mambo mengine yote yakishindikana, hata hivyo, chombo chetu cha kiakili hupungukiwa ustadi unaohitajika kufikia lengo hilo. Kama tungekuwa tuwepo kila mahali kwa namna ile ile ambayo tunaishi mahali maalum kwa muda uliopangwa, ili kwamba hakungekuwa na mahali ambapo panakoseshwa kuwepo kwetu sisi, hakuna kitu kingefichikana kwetu na tungetambua kila kitu.

Kwetu sisi, dunia ya maumbile imegawanywa katika sehemu mbili: sehemu tunayoiona dhahiri na ile tusiyoiona. Vitu "vimefichikana" kwa maana kwamba, ukweli fulani, ambao hauna ukomo na usio na umbile, hauwezi kutambuliwa na milango ya fahamu za nje. Ni muhimu kukumbuka kwamba mfumo wote wa uhai hauwi na mambo yaliyomo kwenye upeo wa sayansi za kutegemea majaribio. Ili kuzielewa siri na miujiza ya maumbile, tunahijati, kama ilivyo kuwa, jukwaa la kujiinulia (kielimu). Muinuko tunaoweza kufika unategemea nguvu ya akili yetu tuliyonayo na kiwango cha uelewa wetu unaosukuma mbele mwinuko wetu. Pindi tunapokuwa na jukwaa linalofaa, ukweli mwingi utakuwa ni wenye kujulikana kwetu.

Kwa kupitia matumizi ya neno ghaibu (fichwa) Qur'ani Tukufu inamfunulia mwanadamu mwonekano mpana wa ukweli halisi. Mitumbe wa Mwenyezi Mungu pia wamejitahidi kuunyanyua utambuzi wa mwanadamu juu ya ulimwengu ulioumbwa hadi kwenye kiwango kinachojumuisha visivyo na ukomo na vyenye ukomo na mipaka ya visivyoonekana na vipimo vya vinavyoonekana. Kwa upande wa Mwenyezi Mungu, hayo "yaliyofichika" hayapatikani kamwe; kwake Yeye, ulimwengu wote 'unaonekana.'.Qur'ani inasema:

هُوَ اللَّـهُ الَّذِي لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ هُوَ الرَّحْمَـٰنُ الرَّحِيمُ ﴿٢٢﴾

"..Mwenye kuyajua yaliyofichikana na yanayoonekana. Yeye ni Mwingi wa rehema, Mwingi wa kurehemu." (59:22).

Chochote kilichotengenezwa na binadamu kinatokana na ustadi, akili na ujuzi wa mtu aliyekitengeneza. Jinsi kitu hicho kitakavyokuwa kigumu kiufundi na kisafi zaidi, ndivyo kitakavyoonyesha wazi wazi ukubwa na

upana wa elimu ya mtengenezaji wake, na ndivyo kwa ukamilifu zaidi kitakavyozidi kuthibitisha uwezo wake wa kubuni na kuunda. Kazi za mikono za mwanadamu haziwezi kulinganishwa kwa hali yoyote na ule mwujiza na utukufu ya maumbile. Hata hivyo, kwa upande wetu inatuashiria kwamba ule utaratibu wa ulinganifu na mpangilio wa ulimwengu, na kuonekana kwa akili nyingi kwenye mtindo huu ulio mpana, mzuri na wa kustaajabisha mno wa maumbile, lazima uwe unaonyesha kwa umuhimu kwamba mtayarishaji mwenye kuupanga lazima awe na elimu kubwa isiyo na mipaka. Mpangilio wa ulimwengu ndio uthibitisho wenye nguvu zaidi juu ya kuwepo kwa dhati ambayo inafurika kwa elimu, utashi, utambuzi na hekima na imebuni maajabu ya maumbile kwa mujibu wa mpango uliokadiriwa kwa ufasaha na usahihi. Dalili za ujuzi Wake usio na ukomo unaonekana wazi kwenye kila sehemu ya kila kiumbe.

Majaribio na nadharia za wanasayansi yanatoa uthibitisho kwa yeyote anayeutaka kuhusu ujuzi wa Mwenyezi Mungu usio na mipaka na kujidhihirisha kwake kwenye wadudu, wanyama na katika nyanja ya mimea. Mwenyezi Mungu ana utambuzi wa njia zipitamo nyota angani, dunia ya nyota nyingi za mbali sana iliyojaa ghasia na mzunguko wa makundi makubwa ya nyota; wa vitu vyote vya kabla ya umilele na baada ya umilele; wa jumla ya idadi yote ya chembechembe ndani ya maumbile yote ya mbinguni; wa miondoko ya mabilioni ya viumbe, vikubwa na vidogo, vile vinavyotembea kwenye mgongo wa dunia na ndani ya vina vya bahari; wa desturi na kanuni zinazodhibiti maumbile bila ya kukosea; wa vipengele vya mambo yote, vilivyofichika na vya dhahiri. Yeye anaijua pia ile mikanganyiko yenye kufadhaisha, vizuri zaidi kuliko wanavyoijua wao wenyewe.

Sikiliza tena Qur'ani inasema nini:

أَلَا يَعْلَمُ مَنْ خَلَقَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ ﴿١٤﴾

"Je! Hivi asijue Yeye aliyeumba? Naye ndiye mjuzi wa ya siri Mwenye habari? (67:14).

إِنَّ اللَّـهَ لَا يَخْفَىٰ عَلَيْهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ ﴿٥﴾

"Hakika hakifichiki Kwake Mwenyezi Mungu kitu chochote kilichomo ardhini au mbinguni."(3:5).

Wataalam wa sayansi ya viumbe wanafahamu vema zaidi kuliko wengine kuhusu miujiza yenye kutatiza na ya sahihi ambayo imepandikizwa kwenye kila chembe ya maumbile; wanatambua kutokana na uchunguzi na utafiti wao wa mahesabu mbalimbali ambayo yamewekwa ndani ya viumbe vyote, vile vyenye uhai na visivyo na uhai, kwenye seli na matone; wa aina mbali mbali ya matendo na matokeo, ya nje na ya ndani, yale yanayofanyika ndani mwao, na athari za vitu na maudhui zao.

Hivyo, wanashuhudia ishara za hekima ya kushangaza ya Mwenyezi Mungu na ujuzi usio na ukomo katika maumbile au kama Qur'ani inavyoliweka, "..katika upeo wa mbali." (41:53).

Zaidi ya wengine, wanasayansi hao wamepata fununu ya sifa za Mwenyezi Mungu na ukamilifu Wake, ikiwa ni pamoja na ujuzi Wake usio na mipaka, na endapo hawakatai wito wa dhamira zao, pia watatambua kuwepo kwa Muumbaji kwa uwazi zaidi. Mwanafikra fulani alisema;

"Dunia yetu inafanana na dhana kubwa kuliko inavyofanana na mashine kubwa. Kama nadharia au ufasiri wa kisayansi, inaweza kusemekana kwamba dunia ni matokeo ya dhana kubwa, udhihiri wa fikira na dhana iliyo kubwa kuliko yetu. Fikra ya kisayansi inaelekea kusonga kuelekea upande wa nadharia hii."

Ujuzi wa Mwenyezi Mungu haukomeshei kwenye mambo yalivyopita au matukio na mambo ya sasa; ujuzi Wake wa wakati ujao ni sawa kabisa na ule ujuzi wa wakati huu. Ujuzi wa Mwenyezi Mungu, ni kusema kwamba ni wa "papo hapo" katika maana kamili ya neno lenyewe. Sio muhimu kwanza kabisa kwamba pawepo na kitu cha kielimu ambamo ujuzi Wake upasike kujiambatanisha nacho. Vitu vyote vinabakia wazi mbele Yake, kwani kwa wakati huo huo dhati Yake tukufu ingawa ni nyingine tofauti kabisa na viumbe na vitu vyote, pia haikutengana mbali navyo; vitu vyote, vilivyopita na vya wakati ujao; vyote viko kwenye hadhira Yake ya moja kwa moja bila kuingiliwa.

Ali (a.s) Amirul-Mu'minin, anasema: **"Yeye Anajua vitu vyote, lakini si kwa kutumia njia au vifaa; ambavyo kutokuwepo kwao kungeweka ukomo wa elimu Yake. Hakuna kitu kilichoongezwa kiitwacho elimu kilichoingilia kati baina Yake na vitu vya ujuzi Wake; hakuna kitu chochote isipokuwa dhati Yake pekee."**[1] Hapa, Ali (a.s) anazungumzia kanuni ya kiteolojia kwamba utambuzi wa mambo wa Mwenyezi Mungu ni wa moja kwa moja na wa papo hapo. Katika ujuzi wake wa vitu, Mwenyezi Mungu hana haja ya mifumo ya kiakili ambayo ndio msingi wa elimu inayopatikana. Angekuwa apate ujuzi Wake kwa kutumia mifumo hiyo, hali ya kuhitaji ingejitokeza ndani Yake, ambapo Yeye ameepukana na kuhitaji kabisa.

Yule ambaye kutoka Kwake dunia na vilivyomo humo vimepatikana, ambaye anaweza kutimiza kila mahitaji yanayofikirika, ambaye hutoa kila ukamilifu na neema - hivi inaweza kufikirika kwamba yeye mwenyewe awe wa kufungwa na kuhitaji? Mifumo ya kiakili inabakia akili mwetu tu almradi tunataka idumu humo; inatoweka pindi tu tunapoindolea nadhari zetu kwa sababu zinabuniwa na kutengenezwa na sisi wenyewe. Namna hii ya elimu sio ya moja kwa moja na isiyoingiliwa kati, na kwa hiyo inaitwa "ujuzi wa kupatikana," kwa kutofautisha na "ujuzi wa papo hapo", ambao hauna haja ya njia. Tofauti baina yetu, sisi ambao tunatengeneza mifumo yetu wenyewe ya akili na Muumba aliyeanzisha maumbile yote ipo hapa, kwamba sisi kuwepo kwetu kwenyewe hasa kunatokana na Yeye, na kwa hiyo sisi tunakuwa ni wenye kumhitaji Yeye, ambapo yeye ndiye Muumba wa kweli na mhuishaji wa vitu vyote, si muhitaji, na hana haja ya zoezi la kutazama ili apate ujuzi.

Ufafanuzi wa matukio yaliyopita na yajayo ambayo hutokea katika upeo nafsi na fikra zetu ni lazima una ukomo, kwani tunatumia muda na nafasi maalum ambao nje ya hapo sisi hatuna kuwepo tena. Sisi ni viumbe vya maada tu; na dutu, kwa mujibu wa kanuni za fizikia na nadharia ya uwiano, inahitaji muda na mahali katika maendeleo ya polepole endelevu ya kukua na kubadilika. Yaliyopita na yajayo hayana maana kwa nafsi ambayo

1. Saduq, Tauhid, uk. 73.

imekuwepo kabla na baada ya umilele, kila mahali na wakati wote na iliyoepukana ufungiwaji wa maada na athari zake.

Kwa kuwa kila kiumbe kinategemea juu ya uwepo wa milele wa Muumba kwa ya asili yake na uhai wake, hakuna pazia au kizuizi ambacho kinaweza kuwepo kati ya Mwenyezi Mungu na kiumbe hicho; Mwenyezi Mungu anazienea sehemu zake za ndani na nje na anao uwezo mkubwa kabisa juu ya kiumbe hicho. Mtu mmoja alimuuliza Amirul-Mu'minin Ali (a.s), "Hivi! Mwenyezi Mungu yupo wapi?" Ali alimjibu: "Sio sahihi kuuliza Mwenyezi Mungu yuko wapi kwa sababu ni Mwenyezi Mungu ndiye Aliyeumba nafasi. Wala si sahihi kuuliza Mwenyezi Mungu alivyo, na ni wa asili gani, kwani ni Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba kila asili. Zaidi ya hayo, si sahihi kuuliza Mwenyezi Mungu ni nini kwa sababu ni Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba vyanzo (vinavyofanya kitu kiwe kitu - quiddity) vya vitu vyote.

"Atukuzwe Mwenyezi Mungu Mweza wa yote ambaye kwenye mawimbi ya utukufu Wake wenye hekima hushindwa kuogelea, ukumbukaji wa umilele Wake husimamisha fikra zote katika mkondo wake, na Ambaye katika mbingu yake pana ya utakatifu akili hupotea njia!"[1].

Qur'ani inasema:

وَعِندَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ ۚ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۚ وَمَا تَسْقُطُ مِن وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلُمَاتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٥٩﴾

"Na ziko kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye anajua kilichoko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinachobainisha." (6:59)

Hebu tufikirie kwamba tumo katika chumba kinachoelekea mtaani na tunatazama kupitia dirisha dogo msururu mkubwa wa magari ambayo yanapita kwa kasi mtaani hapo. Ni wazi kwamba hatuwezi kuyaona magari yote kwa wakati mmoja; bali tunayaona moja moja yanapopita mbele ya dirisha hilo, halafu yanatoweka machoni. Kama tungekuwa hatujui lolote kuhusu magari, tungeweza kudhani kwamba yanakuja kuwepo pole pole upande moja wa dirisha halafu yanakoma kuwepo ule upande mwingine wa dirisha.

Sasa dirisha hili dogo linashabihiana kabisa na nyanja yetu ya kuona, linathibitisha wakati uliopita na unaokuja wa magari hayo. Wale walioko nje ya chumba hicho wakiwa wamesimama kando kwenye nia ya migu wanayaona magari yote yakipita kwa pamoja. Hali yetu kuhusiana na muda uliuopita na ujao wa dunia hii ni kama ile ya mtu yule anayetazama magari kupitia kwenye dirisha dogo. Pindi tutakapotambua kwamba Mwenyezi Mungu yuko juu ya muda na nafasi, tunaelewa kwamba matukio yote yaliyopita na yajayo wakati wote huwa yanakuwepo na yanaendelea kuwepo mbele Yake, kama mchoro.

Kwa hiyo, tunatakiwa kuwa na hisia ya wajibu kwa Mumba Ambaye anatambua hata chembe ndogo sana ya shughuli na kitendo cha maumbile - kama isemavyo Qur'ani: "..Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yale

1. Bihar al-Anwar, Juz. III, uk. 297.

mnayoyatenda." (2:283) - na tuepuke dhambi au kosa lolote ambalo linaweza kusababisha sisi kuwa mbali na Yeye. Tunapaswa kumuabudu Mwenyezi Mungu, Mmiliki wa elimu yote Ambaye ametufanya sisi kupita kwenye hatua zote hizi mbali mbali na kupata uwezo tulio nao sasa. Hatupaswi kutozitii amri Zake ambazo hutufungulia njia yetu kuelekea kwenye furaha ya kweli na shabaha ya mwisho ya mwanadamu na tusikubali lengo jingine mbali na Yeye.

Ili tuweze kumfikia Mwenyezi Mungu lazima tujipambe sifa takatifu na tujiandae, katika muda wetu mfupi hapa duniani, kwa ajili ya kukutana Naye. Halafu tuweze kurejea Kwake, ambaye ni chanzo, chimbuko na mwanzo wa kuwepo kwetu. Jambo hili linahitaji bidii ya utendaji yenye kulenga katika utakasaji wa nafsi, kwani wajibu wa kutekeleza busara hii umewekwa juu ya mwanadamu kama dhamana tukufu.

14

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA NNE

### MAONI KUHUSU UADILIFU WA MWENYEZI MUNGU

Tatizo la uadilifu kama mojawapo ya sifa za Mwenyezi Mungu limekuwa na historia yake iliyo dhahiri. Madhehebu mbali mbali za Kiislamu zimeshikilia maoni tofauti kuhusu suala hili, wakilitafsiri kwa mujibu wa kanuni zao bainishi. Baadhi ya Sunni ambao hufuata maoni ya mwanateolojia Abul-Hasan Ash'ari hawaamini katika uadilifu wa Mwenyezi Mungu kuwa ni suala la imani na wanakanusha kwamba uadilifu unatimizwa na matendo ya ki-Mungu.

Hata hivyo, kwa maoni yao, Mwenyezi Mungu humtendea mtu fulani, na adhabu yoyote au thawabu Anazompa, bila kuzingatia ni nini angeonekana kustahili kupewa, itawakilisha uadilifu na wema kamili, hata kama itaweza kuonekana si haki ikipimwa katika viwango vya kibinadamu. Hawa Ash'ari, kwa hiyo hutofautisha sifa ya Mwenyezi Mungu ya uadilifu mbali na matendo Yake na kwa hiyo, wanafikiri chochote kinachohusishwa na Mwenyezi Mungu kuwa ni haki. Kama anampa thawabu muadilifu na kumwadhibu mkosaji, huu ni uadilifu, na ndivyo itakavyo kuwa kwa kinyume chake; bado ingekuwa kwenye nyanja yake pana ya uadilifu Wake.

Madai yao kwamba maneno yenyewe hasa 'uadilifu' na 'udhalimu' hayana maana yanapotumiwa kwa Mwenyezi Mungu, bila shaka yanakusudiwa kunyanyua dhati ya Mwenyezi Mungu takatifu hasa kufikia upeo wakuvuka mipaka. Lakini hakuna mtu mwenye mawazo kamili atakayeziona dhana hizi za juu juu na pungufu kuwa na uhusiano wowote na uvuka mipaka wa Mwenyezi Mungu. Kwa kweli, wanahusisha ukanusho wa mpango hapa duniani, wa kanuni ya uababishaji katika mpango wa jumla wa dunia na katika tabia na matendo ya watu binafsi.

Wafuasi wa al-Ash'aria wanaamini hata hivyo, kwamba taa ya akili yenye mwanga mkali, huzimika wakati wowote inapokabiliwa na utambuzi na matatizo ya dini, kwamba haiwezi kumnufaisha mwanadamu au kuangaza njia yake. Madai haya wala hayaendani na mafundisho ya Qur'ani wala maudhui ya Sunna. Qur'ani inaona kupuuza akili ni namna ya upotovu na inarudia kuwataka watu watafakari na kuzingatia ili waweze kujifunza elimu bora zaidi na imani za kidini. Wale wanaoshindwa kunufaika kutokana na taa hii angavu iliyomo ndani mwao wanalinganishwa na hayawani. Qur'ani inasema:

إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِندَ اللَّـهِ الصُّمُّ الْبُكْمُ الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٢٢﴾

"Hakika ya viumbe wabaya zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu ni wale viziwi na mabubu ambao hawatafakari." (8:22)

Mtume wa Uislamu anasema: **"Mwenyezi Mungu amemwekea kila mtu walinzi wawili: mmoja ni wa nje yake, wajumbe wa Mwenyezi Mungu, na mwingine wa ndani, uwezo wake mwenyewe wa akili".**

Wafuasi wa Mutazilite na Shia wanapingana na al-Ashari na madhehebu yake. Kati ya sifa zote za Mwenyezi Mungu, wao wamechagua uadilifu kuwa kama kanuni ya imani yao. Kwa kutegemea uthibitisho wa mapokezi

au wa kihekima, pia wamepinga na kukataa kama isiyoendana na kanuni ya uadilifu, mafundisho ya athari za hatima ya ki-Mungu na kudra ya matendo ya mtu (kabla hajayafanya). Wanaamini kwamba uadilifu ndio msingi wa matendo ya Mwenyezi Mungu, katika mpangilio wa ulimwengu na katika kuanzisha sheria. Kama vile ambavyo matendo ya mtu yanavyoweza kupimwa kwa mujibu wa kigezo cha wema na uovu, matendo ya Muumbaji pia yanatakiwa kupitishwa kwenye kigezo cha namna hiyo hiyo. Kwa kuwa mantiki ya akili huamua kwamba uadilifu ni wa kutukuzwa kiasili na udhalimu kiasili ni wa kulaumiwa, basi lengo la kuabudiwa ambalo sifa zake ni pamoja na akili isiyo na ukomo na mawazo hakiwezi kamwe kufanya kitendo ambacho mantiki inakiona hakiruhusiwi.

Tunaposema kwamba Mwenyezi Mungu ni mwadilifu, ina maana kwamba dhati Yake yenye kujua kila kitu na bunifu haifanyi kitu ambacho ni kinyume cha busara na manufaa. Dhana ya hekima, inapotumiwa kwa Muumbaji haimaanishi kwamba Yeye huchagua njia bora ya kufikia malengo Yake au kurekebisha mapungufu Yake, kwani ni mwanadamu tu ambaye anayetakiwa kutoka kwenye upungufu kuelekea kwenye ukamilifu. Anachotaka Mwenyezi Mungu kuwafanya viumbe waondoke kutoka kwenye mapungufu na kuwasukuma kwenda kwenye ukamilifu na malengo ya asili ya dhati zao. Hekima ya Mwenyezi Mungu ni pamoja na hili; kwamba kwanza hupandikiza aina ya upendeleo wake kwenye kila kiumbe, na halafu baada ya kukipa uhai juu yake, hukisukuma kuelekea kwenye ukamilifu wa uwezo wake kupitia utekelezaji zaidi wa ukarimu Wake.

Halafu, uadilifu una maana pana, ambayo kwa kawaida inajumuisha kuepuka ukandamizaji na matendo yote ya kipumbavu. Imamu Jafar as-Sadiq (a.s) anasema katika kuelezea uadilifu wa Mwenyezi Mungu: **"Uadilifu katika suala la Mwenyezi Mungu maana yake ni kwamba usihusishe jambo lolote kwa Mwenyezi Mungu ambalo kwamba kama ungelifanya wewe lingekusababishia kulawamiwa na kukosolewa."**[1] Kwa mwanadamu, ukandamizaji na aina zote za shughuli za kidhalimu ambazo huzifanya, bila shaka, hutokana na ujinga na upungufu katika umtambuzi na kuhitaji kulikoungana na uduni wa hulka, pia wakati mwingine ni kuakisi kwa chuki na uadui, kunakochomoza kutoka kwenye nafsi ya ndani kabisa ya mwanadamu kama cheche.

Ni watu wengi sana ambao huchukizwa na ukandamizaji na uovu wao wenyewe. Hata hivyo, kwa sababu ya kutokujua kuhusu matokeo ya mwisho ya matendo yao, wanaendelea mara kwa mara, kufanya udhalimu na kujichafua wenywe kwa aina zote za matendo ya fedheha na uovu. Wakati mwingine mwanadamu anahisi kwamba anataka kupata kitu ambacho yeye mwenyewe hana njia au uwezo wa kukipata. Hii ndio sababu ya msingi ya maovu mengi. Hisia za kuhitaji, njaa na ulafi, mtu kuwa na tamaa ya kuumiza au kutawala - yote haya ni mambo ambayo huongozea kwenye tabia ya ugomvi.

Chini ya ushawishi wao, wanadamu hukosa udhibiti wa kujizuia. Huweka juhudi zake zote katika kutimiza matakwa yake na kukiuka masharti yote ya kimaadili, huanza kukaba makoo ya wanaogandamizwa.

1. Kifayat al- Muwahhidin, I, uk. 442.

Dhati ya kipekee ya Mwenyezi Mungu, ile nafsi isiyo na ukomo, imeepukana na tabia na mipaka ya aina hiyo, kwani hakuna kinachofichikana kwenye elimu Yake bila ya mipaka, na haiingii akilini kwamba apatwe na udhaifu wa kutokuwa na uwezo kuhusiana na kitu chochote -Yeye, wa Tangu na Tangu, ambaye nuru Yake ya milele inagawa uhai na riziki kwa vitu vyote na Ambaye anawahakikishia mwenendo wao, namna zao mbalimbali na maendeleo.

Dhati stadi ambayo inakusanya viwango vyote vya ukamilifu haina haja ya kitu chochote ambacho kwamba kama hakipo kitatia hali ya wasiwasi ndani Yake Anapopatwa na kukihitajia. Nguvu na uwezo wake bila shaka hazina mipaka na hazipungukiwi na chochote hivyo kwamba anaweza kusababishiwa kupotoka kutoka kwenye njia ya uadilifu na kumfanyia uovu mtu au kulipiza kisasi ili kutuliza moyo wake au kufanya kitendo kisichostahili na kiovu. Hakuna hamasa yoyote ya tabia ya udhalimu inayoweza kupatikana kwa Mwenyezi Mungu, na kwa kweli dhana za ukandamizaji na udhalimu hasa hazitumiki kwa dhati, Ambayo ukarimu na huruma yake vinavienea vitu vyote na Ambaye utakatifu wa dhati yake unaonekana dhahiri katika maumbile yote.

Qur'ani inakanusha mara nyingi mawazo yote ya udhalimu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kumchukulia Yeye katika utukufu Wake kwamba ameondokana kabisa na matendo yote mabaya. Qur'ani inasema:

إِنَّ اللَّـهَ لَا يَظْلِمُ النَّاسَ شَيْئًا وَلَـٰكِنَّ النَّاسَ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤٤﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu kitu chochote; lakini watu wenyewe wanajidhulumu nafsi zao." (10:44).

Katika Aya hii, Mwenyezi Mungu Anajitenga Mwenyewe na fikra yoyote ya udhalimu, jambo linachukiza kwa wanadamu, na badala yake analirudisha kwao wenyewe.

Kwa nyongeza, inawezekanaje kwamba Mwenyezi Mungu awaite wanadamu kwenye uadilifu na usawa ambapo wakati huo huo achafue mikono Yake kwa matendo ya kidhalimu? Qur'ani inasea:

إِنَّ اللَّـهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنكَرِ وَالْبَ غْيِ
يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٩٠﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu na hisani, na kuwapa jamaa, na anakataza uchafu na uovu na dhulma. Anakuwaihidhini ili mpate kukumbuka." (16:90).

Uislamu unathamini sana uadilifu hivyo kwamba endapo kundi moja la Waislamu linataka kupotoka kwenye njia ya uadilifu na kuanza kujihusisha na ukandamizaji, lazima wazuiwe, hata kama hili litahusisha vita. Haya ndio maagizo ya Qur'ani:

وَإِن طَائِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا فَإِن بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَىٰ فَقَا تِلُوا
الَّتِي تَبْغِي حَتَّىٰ تَفِيءَ إِلَىٰ أَمْرِ اللَّـهِ فَإِن فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا إِنَّ اللَّـهَ يُحِبُّ
الْمُقْسِطِينَ ﴿٩﴾

"Na ikiwa makundi mawili katika waumini yanapingana, basi yapatanisheni. Na ikiwa moja kati yao linamdhulumu mwenzie, basi lipigeni linalodhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu. Na likirudi

basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaohukumu kwa haki." (49:9).

Jambo la kuvutia linalojitokeza kutoka kwenye Aya hii ni kwamba mpatanishi amepewa maagizo kumuelekeza kuhakikisha, pale anapofanya usuluhishi, ugomvi uishe kwa mujibu wa uadilifu, bila kuonyesha huruma kwa yule mchokozi. Inaweza kutokea, katika hali ambapo vita vimeanzishwa kwa malengo ya uchokozi, kwamba mpatanishi anajaribu kumaliza ugomvi kwa kusisitiza juu ya huruma na kutoyaangalia makosa, na hatimaye, anashawishi upande mmojawapo wa wagomvi kuacha madai yake kwa manufaa ya upande wa pili. Utaratibu huu wa huruma, ingawa una uhalali ndani yake, unaweza kuzidisha moyo wa uchokozi ulikuwepo tayari kwa wale walionufaika kwa kuanzisha vita. Kwa kweli ni jambo la kawaida kumridhisha mchokozi katika hali kama hizi kwa kumpatia tahafifu.

Ingawa kusamehe madai kwa hiari, lenyewe ni jambo la kupendeza, katika hali kama hiyo, linaweza kuwa na athari mbaya katika fikra za mchokozi. Lengo la Uislamu ni kung'oa matumizi ya nguvu na udhalimu kutoka kwenye jamii ya Ki-Islamu na kuwahakikishia Watu wake kwamba hakuna mtu anayeweza kupata kitu chochote kwa uchokozi na mabavu.

Kama tukitazama utaratibu wa maumbile, tunaweza kuona kwamba upo uwiano mkubwa na mpana mno miongoni kwa viumbe vyote vya kimaada. Hali hii, inadhihiri kwenye ukawaida wa Atomu, haraka ya elektroniki, mzunguko wa sayari, na kusogea kwa viumbe vyote. Inaonekana kwenye madini na kwenye nyanja ya mimea na chanikiwiti, kwenye uhusiano sahihi uliopo baina ya viungo vya kiumbe hai, katika ulingano miongoni mwa vijenzi vya ndani ya atomu, katika uwiano miongoni mwa maumbo makubwa ya angani na nguvu zao za mvutano zilizokokotolewa vizuri.

Aina zote hizi za ulingano na uwiano, pamoja na kanuni zingine sahihi ambazo sayansi bado inatafuta, kuzigundua, zinatoa ushahidi wa kuwepo kwa mpangilio usiokanika katika ulimwengu, ambao unathibitishwa kwa mlinganyo wa kimahesabu. Mtume wetu mkweli ameuelezea kuhusu uadilifu huu wa jumla na uwiano mpana - ukweli kwamba hakuna kisicho sawa au kilichoko nje ya sehemu yake - kwenye tamko hili fupi na fasaha: "Ni uwiano halisi na mpachano ambao unaendesha dunia na mbingu."

Qur'ani inayahusisha maneno yafuatayo na Musa (a.s) na Mtume wetu: **"Akasema: Mola wetu Mtukufuni yule aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha akakiongoa."** (20:50).

Katika sentensi hii fupi, Musa anamfafanulia Firauni jinsi dunia ilivyoumbwa pamoja na mpangilio na uzuri wake, ambavyo ni miongoni mwa ishara za Mwenyezi Mungu. Lengo lake Musa lilikuwa ni kumkomboa Firauni kutoka kwenye fikra zake potofu na kumsaidia kutambua kuwepo kwa mpango wa adilifu na mtukufu uliowekwa ulimwenguni.

Mojawapo ya kanuni zinazotawala maumbile bila kuzuilika, kwa hiyo ni mpangilio na uadilifu, na vitu vyote, kwa sababu ya kuwa chini ya kanuni na taratibu za maumbile, vipo katika mlolongo wa mageuzi kuelekea kwenye ukamilifu ambao ni mahsusi kwa kila kimoja chao. Ukengeukaji wowote kutoka kwenye mkondo huu wa jumla wa mpangilio na uhusiano ulioandaliwa juu yake utasababisha utatanishi na ghasia. Wakati wowote panapotokeza hali isiyo ya kawaida kwenye maumbile, vitu vyenyewe

huonyesha athari, na vitu vya ndani au nje hujitokeza kuondoa vikwazo vya maendeleo na kuanzisha upya ule utaratibu unaohitajika kuendelea kwenye njia ya kwenye ukamilifu.

Mwili unaposhambuliwa na viini na mambo mengine ya maradhi, chembechembe za damu nyeupe huanza kuvidhoofisha, kwa mujibu wa kawaida isiyozuilika. Dawa yoyote itakayoagizwa na daktari ni kipengele cha nje ambacho kinazisaidia chembe chembe nyeupe katika kazi ya kudhoofisha viini vya maradhi na kuanzisha upya uwiano mwilini. Mwisho kabisa, haiwezekani kwamba Mwenyezi Mungu, Ambaye upendo Wake niwa milele na Ambaye kwa ukarimu hutoa fadhila Zake kwa waja wake, afanye kosa lolote dogo sana la kidhalimu au tendo lisilofaa. Jambo hili ndilo ambalo hakika Qur'ani inaelezea ifuatavyo:

اللَّـهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ قَرَارًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُوَرَكُمْ وَرَزَقَكُم مِّنَ الطَّيِّبَاتِ ذَٰلِكُمُ اللَّـهُ رَبُّكُمْ فَتَبَارَكَ اللَّـهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٤﴾

"Ni Mwenyezi Mungu aliyekufanyieni ardhi kuwa ni mahala pa kukaa, na mbingu kuwa dari. Na akakutieni sura, na akazifanya nzuri sura zenu, na akakuruzukuni vitu vizuri. Huyo ndio Mwenyezi Mungu, Mola Wenu. Na ametukuka Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote." (40:64).

15

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA TANO

### UCHAMBUZI KUHUSU BALAA NA DHIKI

Suala la uadilifu wa Mwenyezi Mungu linahusisha matatizo fulani, kama vile kuwepo kwa maafa, hasara na uovu katika mpangilio wa asili, na kutokuwepo usawa katika mpango wa kijamii. Suala hili, kwa kweli, linazua wimbi kubwa la maswali na ugumu kwenye akili za watu wengi. Matatizo wanayokabiliana nayo ni ya msingi mno hivyo kwamba kinachoanza kama mashaka na kusita, hatimaye huwa tatizo sugu.

Watu kama hao, wanahoji kwamba inawezekanaje katika dunia iliyoumbwa kwa misingi ya akili na hekima, iwe inakumbwa na mateso mengi sana, maumivu na uovu, mara nyingi ipatwe na misukosuko ya dhiki na mabalaa yasiyokwisha; pamoja na hasara na upungufu kuongezeka kila mara. Kwa nini kwamba katika sehemu mbali mbali za dunia, matukio ya kuogofya na kugharikisha yanashambulia wanadamu, na kusababisha hasara na maangamizi yasiyosemekana? Kwa nini mtu huyu ana sura mbaya na mwingine ana sura nzuri, huyu ana afya nzuri na yule mgonjwa? Kwa nini watu wote hawakuumbwa sawa na je, kutokuwa sawa kwao hakuonyeshi kukosekana kwa uadilifu duniani?

Uadilifu katika utaratibu wa mambo unategemea juu ya kuwa kwake huru kutokana na dhulma, ubaguzi na maafa, au kutokuwepo ndani yake dosari, maradhi na umasikini, hii peke yake, wao wanasema, ingesababisha matokeo ya ukamilifu na uadilifu.

Lazima tuanze kwa kukubali kwamba tathmini yetu juu ya mambo ya ulimwengu haiturusu sisi kupenya vile vina hasa vya mambo; haitoshelezi kwa ajili ya uchambuzi wa matokeo na malengo ya vitu. Uelewa wetu wa mwanzo wa matukio yasiyopendeza na maafa una uhakika wa kuwa wajuu juu; hatupo tayari kutambua ukweli wowote ulioko nje ya maoni yetu ya mwanzo. Hatuwezi pale mwanzoni kabisa, kufafanua yale malengo ya juu kabisa ya matukio hayo, na kwa hiyo, sisi tunayachukulia kama dalili za udhalimu. Hisia zetu huamshwa na hutuongoza kwenye uchunguzi usio wa kimantiki kabisa.

Lakini endapo tutatafakari kwa kina zaidi, tutaona kwamba tathmini hii ya matukio ya upande moja ambayo tunaiita udhalimu inatokana na kuzifanya nadhari zetu, au zile za watu ambao tuna uhusiano nao wa moja kwa moja au wa mzunguko, kuwa ndio mfano au kigezo chetu. Chochote kitakachosalimisha maslahi yetu ni kizuri na kile kinachotuumiza tutakiona kibaya. Kwa maneno mengine, uamuzi wetu wa uzuri na ubaya umeegemea kwenye utambuzi dhaifu, upeo mfinyu wa fikra, na kutokuwa na ujuzi sahihi kuhusu kanuni za maumbile.

Kuwepo kwetu tu ndio jambo linalohusika katika kila tukio? Je, tunaweza kupata faida na hasara zetu kuwa mfano wa wema na ubaya? Dunia yetu hii ya kimaada siku zote inashughulika katika kuzalisha mabadiliko. Matukio ambayo hayakuwepo leo yatatokea kesho; baadhi ya vitu vitatoweka na vingine vitaziba nafasi yao. Ni dhahiri kwamba kile

chenye faida na manufaa leo kwa baadhi ya watu, kesho kitakoma kuwepo. Lakini kwetu sisi ambao ni binadamu na tulioambatana na uhai wetu wenyewe vitu vya dunia, upatikanaji wa vitu ni mzuri na kukosekana kwao ni kubaya. Lakini licha ya binadamu na viambatanishi vyake, asili inayobadilika ya dunia inatoa vitu vinavyobadilika siku zote. Kama dunia haikutambua uwezekano wa mabadiliko, viumbe vyenyewe visingekuwepo, na kwa hiyo, pia kusingekuwepo na suala la wema na uovu.

Katika dunia ya kinadharia na isiyobadilika kama hiyo wala kisingekuwepo na hasarana upungufu ama kustawi na kuendelea, hakuna kinyume wala utofautishaji, aina mbali mbali au wingi, uachanishaji au mwendo. Kwenye dunia isiyokuwa na dosari au hasara, pia kusingekuwepo na binadamu, kigezo cha maadili au kijamii, mipaka au sheria. Maendeleo na mabadiliko ni matokeo ya mwendo na mzunguko wa sayari; kama zingekoma kuwepo, kusingekuwepo na ardhi, mwezi, jua, siku, hakuna mwezi na hakuna mwaka.

Mtazamo mpana kiasi wa dunia utaturuhusu kutambua kwamba jambo tunaloliona kuwa baya kwetu leo, au linaweza kuwa hivyo siku za usoni, ni lenye manufaa kwa wengine. Dunia kwa ujumla husogea kuelekea kwenye upande ambao ulioamriwa na kusudio la jumla la kuwepo kwake na manufaa ya kuwepo kwake; mtu mmoja mmoja wanaweza kupata madhara katika utaratibu huu; na inaweza hata ikawa kwamba binadamu wote kwa ujumla hawafaidiki.

Endapo tungeweza kutumbukia kwenye kina kirefu zaidi cha bahari ya elimu na tupekuwe kurasa za kitabu chake kilichojaa miujiza kwa kidole chetu cha uelewa, lengo la mwisho na matokeo ya matukio yote na mambo yote yatajionyesha kwetu. Hata hivyo, uwezo wetu wa maamuzi si mpana vya kutosha kuweza kushughulika na mtandao tata unaotukabili: wala hatujui mlolongo wa sababu zilizotangulia ambazo zimezaa haya matukio ya leo, wala mlolongo wa athari za siku za usoni ambazo baadae matukio haya yatazaisha.

Kama ingekuwa inawezekana sisi kutazama chini kutoka juu ya uwanda mpana wa dunia, namna ambayo tungeweza kuona vipengele vyote vya dhahiri na hasi ya kila kitu, miujiza yote ya kila kitu inayotokea hapa duniani; kama ingewezekana sisi kutathmini athari na matokeo ya kila tukio katika historia, iliyopita, ya sasa na ijayo na kila kitu kinachotokea baina ya kabla ya mwanzo na baada ya umilele, na kama, jambo hili lingewezekana kwetu sisi, tungeweza kusema kwamba madhara ya tukio lililotajwa yamezidi uzito manufaa yake na kuyaita uovu.

Lakini je, binadamu anao utambuzi mpana kiasi hicho wa minyororo iliyonyyka na iliyosimama ya visababishi? Binadamu anaweza kujiweka kwenye muhimili unaosogea wa dunia? Kwa kuwa hatuthibiti uwezo wa aina hiyo, kwa kuwa hatutaweza kamwe kusafiri mwendo mrefu hivyo, hata kama hatua zetu zingekuwa ndefu kiasi gani, kwa kuwa hatutaweza kufunua pazia kutoka kwenye changamano zote hizi na kuchukua vipimo vya vinavyostahili, ni vema tujizuie kufanya uamuzi ulioegemezwa upande moja na wa haraka ambao msingi wake ni uoni wa upeo mfupi. Lazima tutambue kwamba tusifanye manufaa yetu wenyewe kuwa ndio tu kigezo pekee cha kuitambua dunia hii pana. Uchunguzi kiasi tunaofanya katika mfumo wa

takwimu chache tulizonazo na mazingira maalum ambayo yanatutawala hayawezi kamwe kutoa na kigezo cha kutuwezesha kutoa uamuzi wa uhakika.

Mara nyingi asili inaweza kuwa inafanya kazi kuelekea kwenye ukamilishaji wa lengo maalum ambalo mwanadamu hawezi kulifikiria, kama ilivyoelezewa hali yake ya kawaida. Kwa nini isidhaniwe kwamba matukio mabaya ni matokeo ya jitihada zinazolenga kutayarisha uwanja wa vitu vingi na vipya ambavyo vitakuwa zana ya utashi wa Mwenyezi Mungu juu ya duniani? Inawezekana kwamba hali na mazingira ya zama hizi yanalazimisha utaratibu kama huo.

Kama mabadiliko na mageuzi yote yanayotuogofya hayakutokea katika mpango na ubunifu unaotakiwa na kwa sababu ya lengo maalum, kama yangeongezwa wakati wote bila kutoa matokeo yoyote mazuri au ya yenye kusaidia, kusingekuwepo na dalili yoyote ya kiumbe hai hapa duniani, pamoja na mwanadamu. Kwa nini tuilaumu dunia kwa kutotenda haki, kwa yenye vurugu na kuyumba, kwa sababu tu ya matukio machache ya ajabu na mambo ya asili? Je, tuanze kukataa kwa sababu ya kiasi cha ubaya; kikubwa na kidogo, na kusahau udhihiri wa usahihi wote na busara, maajabu yote tunayoyaona kwenye dunia na viumbe vyake, ambavyo vinashahidilia utashi na akili ya dhati tukufu?

Kwa kuwa mwanadamu huwa anaona ushahidi mwingi sana wa upangaji makini katika ulimwengu wote, lazima akiri kwamba dunia kwa ujumla ni kitu kizima chenye lengo, utaratibu unaosogea kuelekea kwenye ukamilifu. Kila jambo ndani humo linatawaliwa na kigezo chake maalum, na kama jambo linaonekana halielezeki au lisiloweza kutetewa, hii ni kwa sababu ya kutoona mbali kwa binadamu. Mwanadamu lazima aelewe kwamba katika ukomo wake, anakosa uwezo wa kuelewa malengo ya mambo yote na maudhui zao; si kwamba maumbile yana dosari yoyote.

Msimamo wetu kwenye matukio yenye uchungu yasiyopendeza ya dunia hii hufanana na uamuzi uliofanywa na mwenyeji wa jangwani anapokwenda mjini na kuona mabuldoza yenye nguvu yanavyovunja nyumba za zamani. Yeye anauona uvunjaji huu kama ni kitendo cha kipumbavu cha maangamizi, lakini ni busara kwake kufikiri kwamba uvunjaji huo haukupangwa na hauna malengo? Kama mambo yalivyo, hivyo sivyo, kwa sababu yeye anaona ule utaratibu wa uvunjaji tu, sio mahesabu na mipango ya wasanifu ujenzi na mengineyo yanayohusika. Kama alivyosema mwanasayansi mmoja: "Hali yetu ni kama ile ya watoto wanao tazama vifaa vya sarakasi vinafungashwa na kujiandaa kuondoka. Hili ni muhimu kwa kundi la wanasarakasi kuondoka na kwenda mahali pengine na kuendelea na maisha yake ya msisimko, lakini wale watoto wasioona mbali wanaona mahema yanavyokunjwa na kule kuja na kuondoka kwa watu na wanyama, hakuna kingine chochote isipokuwa kuvunjwa na kuhamishwa kwa sarakasi hizo."

Endapo tutaangalia kwa undani zaidi na kwa ubunifu zaidi matatizo na mabalaa yanayomkera binadamu na kuzitafsiri kwa usahihi, tutatambua kwamba kwa kweli, matukio hayo ni neema, sio balaa. Neema kuwa neema, na balaa kuwa balaa inategemea na jinsi binadamu atakavyolichukulia tukio hilo; tukio moja linaweza kuhisiwa tofauti na watu wawili tofauti. Matatizo

na usumbufu ni sawa na kengele ya inayomtahadharisha mwanadamu ili arekebishe dosari zake na makosa yake; yamekuwa kama mfumo wa kinga ya asili au utaratibu wa urekebishaji wa kiasili kwa binadamu.

Kama utajiri huelekeza kwenye kupenda anasa na starehe, hayo ni matatizo na balaa, na kama umaskini na ufakara huelekeza kwenye utakaso na maendeleo ya nafsi ya mwanadamu hizo ni neema. Hivyo, utajiri hauwezi kuhesabiwa kama ni wema moja kwa moja wala umaskini kuwa balaa hasa. Kanuni kama hiyo inajumuisha neema yoyote ya asili anayoweza kuwa nayo binadamu.

Mataifa ambayo yanakabiliwa na makundi mbali mbali yenye uhasama na kulazimishwa kupigania kudumu kwao huimarishwa hapo. Pindi tunapochukulia juhudi na mpambano kuwa ni jitihada za uhakika na zinazosaidia, hatuwezi kuacha kutilia maanani majukumu yanayofanywa na shida, katika kukuza uwezo wa utambuzi wa ndani zaidi na kumsukuma kwenye maendeleo. Watu ambao hawalazimiki kupambana na ambao huishi kwenye mazingira yasiyo na mikanganyiko yoyote kwa urahisi sana watatumbukia kwenye ustawi wa mali katika starehe na anasa zao.

Ni mara ngapi hutokea ambapo mtu hustahamili dhiki na matatizo kwa hiari yake mwenyewe, kwa sababu ya lengo kubwa! Isingekuwa dhiki na matatizo hayo, lengo hilo lisingeonekana la kutamanika kwake! Njia nyepesi ambayo hupita mtu bila kuangalia na bila kufikiria haifai kwa maendeleo na ustawi, na jitihada ya binadamu ambamo dalili ya utashi wa nafsi imeondolewa, haiwezi kuleta mabadiliko ya msingi kwa mwanadamu.

Mapambano na kuhitilafiana ni kama mateso yanayomsukuma mwanadamu mbele. Vitu vigumu huvunjika kwa shinikizo la kipigo cha kurudia tena na tena, lakini binadamu huundwa na kuimarishwa na matatizo wanayoyastahimilia. Hujitupa baharini na kuanza kujifunza jinsi ya kuogelea, ni kwenye hali ngumu ya matatizo ambapo kipaji hujitokeza. Mambo yaliyokithiri bila vikwazo, mapenzi juu ya dunia, kutafuta starehe bila vipingamizi, kutokujali malengo ya juu zaidi - yote haya ni dalili za upotofu na kutokutambua. Kwa kweli, watu mafedhuli kabisa ni wale waliokulia kwenye raha na starehe, ambao kamwe hawajawahi kupitia kwenye matatizo mengi ya maisha au kuonja siku zake chungu sambamba na zile za furaha; jua la maisha yao huchomoza na kuchwa ndani yao bila kuonekana na mtu yeyote.

Kufuata mwelekeo wa mtu na kuambatana na matakwa yake haviendani na uimara na kunyanyuliwa roho kwa juhudi zenye malengo na kujitahidi. Utafutaji wa starehe na uovu, kwa upande mmoja, na nguvu na dhamira na kuwa na lengo kwa upande mwingine, zinadhihirisha mielekeo ya pande mbili tofauti inayopingana kwa binadamu. Kwa vile hakuna unaoweza ama kukanushwa au kukubaliwa ukiacha nyingine, mtu lazima ajitahidi kupunguza tamaa ya starehe na kuimarisha ile nguvu pinzani ndani ya muelekeo mmoja.

Wale ambao wamepewa malezi ya starehe, ambao hawajaonja siku za uchungu na utamu wa hapa duniani, ambao wakati wote wamekuwa wakifurahia neema na kamwe hawajadumu na njaa - kamwe hawawezi kuelewa ladha ya chakula kitamu wala furaha ya maisha kwa ujumla na hawana uwezo wa kuuelewa uzuri hasa. Starehe za maisha zinaweza

kufurahikiwa tu hasa na wale ambao wamepitia maisha ya dhiki na kushindwa katika maisha yao, ambao wana uwezo wa kuhimili matatizo na kuzivumilia dhiki hizo zinazomngojea katika kila hatua ya njia ya mwanadamu. Raha ya kidunia na kiroho huwa na thamani kwa binadamu hapo baada tu ya kuyaona mema na mabaya ya maisha na mashinikizo ya matukio yake yachukizayo.

Pale mwanadamu anaposhughulishwa zaidi maisha yakinifu, vipimo vyote vya maisha yake hufungwa minyororo na hupoteza tamaa na hoja. Bila kukwepa, pia atatelekeza maisha yake ya milele na utakaso wa ndani. Almuradi matamanio yanazingira maisha yake na roho yake inakamatwa na giza, atakuwa kama doa dogo linalotupwa huku na kule kwenye mawimbi ya mata. Atatafuta kimbilio kila mahali isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, anahitaji kitu cha kumwamsha na kudukiza ukomavu katika fikra zake, kumkumbusha yeye kuhusu mpito wa dunia hii ya muda mfupi na kumsaidia kupata madhumuni ya mafundisho yote ya ki-mbinguni - uhuru wa Mnafsi yake kutoka kwenye vikwazo vyote na njia zinazomzuia mtu kupata ukamilifu wa kiwango cha juu.

Mazoezi na utakasaji wa nafsi sio vya kupatikana kirahisi; inahitaji ukanushajiwa raha na starehe mbali mbali, na utaratibu wa kujitoa humo ni mchungu na mgumu.

Ni kweli kwamba jitihada kama hizo zitakuwa kwa ajili ya kutakasa nafsi ya ndani ya mwanadamu na kuruhusu uwezo wake uliojificha kutokeza. Hata hivyo uvumilivu wa kujizuia kutenda dhambi na kutafuta starehe siku zote ni mchungu kwa utashi wa binadamu na ni kwa upinzani wa kikaidi wa kushusha msukumo kwamba anaweza kutimiza kazi yake ya kuvunja vizuizi ambavyo vinamkabili na hivyo kupanda juu kwenye uwanda wa maadili ya juu.

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA SITA

### MATATIZO, SABABU YA KUAMKA

Watu waliolewa kiburi cha madaraka na mafanikio na ambao wamesahau kabisa maadili ya kibinadamu kwa sababu ya upotofu wa roho na hisia zao, wakati fulani wataona kwenye pembe mbali mbali za dunia, kwamba matokeo ya matukio yasiyopendeza huwafanya wakubali mabadiliko ya msingi na maendeleo ambayo huwafungulia mapazia ya usahaulifu. Wanaweza hata kuongozwa kwenye njia inayoelekea kwenye kiwango fulani cha ukamilifu wa maadili na maisha yao ya siku za usoni ambayo ni mazuri zaidi kuliko ya wakati huo. Hawa ni watu ambao matatizo yamedukiza mabadiliko makubwa kwao.

Tukizingatia athari zenye madhara za uzembe na ulevi wa kiburi kwa upande mmoja, na masomo mengi ya maadili yanayofundishwa tokana na matatizo kwa upande mwingine, inaweza kusemekana kwamba kutofaulu na matatizo ni hali zinazowiana kwa kadiri ambavyo zinakuwa na baraka kubwa; zinatoa mchango mzuri katika ujenzi wa utambuzi na utashi wa mwanadamu.

Matatizo basi, ni kitangulizi cha hali za juu zaidi na zilizoendelea za maisha; humtayarisha mwanadamu kwa ajili ya malipo yanayomngojea yeye, na kutoka kwenye witikio wake kuhusu jambo hili, inakuwa wazi kama amefikia kiwango cha juu cha uaminifu na kujitolea au amezama kwenye uoza. Qur'ani inasema:

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ فِي كَبَدٍ ﴿٤﴾

"Hakika tumemuumba mtu katika kupambana na taabu." (90:4)

Au inasema tena:

وَلَنَبْلُوَنَّكُم بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنفُسِ وَالثَّمَرَاتِ وَبَشِّرِ
الصَّابِرِينَ ﴿١٥٥﴾ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُم مُّصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّـهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٦﴾ أُولَـٰئِكَ
عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ وَأُولَـٰئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٧﴾

"Hapana shaka tutakujaribui kwa chembe ya hofu, na njaa, na upungufu wamali na nafsi na matunda. Na wabashirie wenye subira. Wale ambao ukiwafika msiba wao husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea. Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola Wao na rehama. Nao ndio wenye kuongoka." (2:155-157).

Bila shaka Mwenyezi Mungu angeweza kuumba dunia isiyo na matatizo, magumu na maafa, lakini hiyo ingemaanisha kumnyang'anya binadamu uhuru na fursa ya kuchagua; binadamu angekuwa ameachwa katika dunia vivi hivi tu kama kiumbe kisicho na utashi au uwezo wa kuamua, kama vile kiumbe kingine chochote kisichokuwa na fikra na utambuzi.

Baada ya kupata hasara kubwa kabisa ya kupoteza uwezo wake wote wa asili na uhuru, ambao ndio rasilimali yake ya thamani sana, je, binadamu angeweza kuendelea kuelekea kwenye ukamilifu, au angeoza na kuanguka? Dunia je, pia isingepoteza ubora na uzuri wake wote, haya yakiwa

yanaeleweka tu katika tofauti zao? Ni wazi kwamba uwezo wa kutofautisha na kuainisha huwezesha kuwepo kwa wema na uovu, uzuri na ubaya. Kwa kumpa binadamu neema isiyokadirika ya hiari na uwezo wa kuchagua, Mwenyezi Mungu ambaye hekima yake inadhihiri kwenye maumbile yote, alitaka kuonyesha kikamilifu uwezo wake wa kuumba viumbe vyenye kushuhudia hekima na nguvu zake.

Aliweka kwenye uhai wa mwanadamu uwezekano wa kutenda yote mema na mabaya, na ingawa hamlazimishi kutenda lolote kati ya hayo, wakati wote Mwenyezi Mungu anamtegemea mwanadamu kutenda wema. Mwenyezi Mungu haafiki uovu; ni tabia njema ndio inayopata ridhaa Yake, na kwa badala yake Yeye hutoa thawabu nyingi sana zisizo na kifani. Mwenyezi Mungu humwonya binadamu dhidi kufuata njia ya uovu na humhofisha na adhabu na mateso kama akifanya hivyo.

Hivyo, kwa kutumia uwezo wa hiari yake, ambayo Mwenyezi Mungu amempa, mwanadamu anaweza kufanya kama awezavyo, kwa kufuata mwongozo wa ki-Mungu na dhamira yake mwenyewe. Lakini, endapo wakati fulani atateleza na kufanya dhambi, njia inabaki wazi kwake kurudi kwenye utakaso na nuru, kwenye neema na huruma ya Mwenyezi Mungu. Hili peke yake ni udhibitisho zaidi wa ukarimu wa Mwenyezi Mungu na uadilifu unaovienea vyote, neema mojawapo nyingine ambayo amewapa waja wake.

Kama Mwenyezi Mungu angekuwa atoe thawabu haraka kwa waja wake wema kwa ajili ya tabia zao adilifu na matendo yao mema, wasingekuwa bora zaidi kwa namna yoyote kulinganishwa na watu waovu na wenye dhambi. Na kama watu waovu kiakili na kimatendo wakati wote wangepewa adhabu na mapatilizo ya papo hapo, maadili mema na utakatifu visingeweza kupata ubora wowote hapa duniani dhidi ya uovu na ukware.

Kanuni ya hitilafu, kwa kweli, ndio msingi wa dunia iliyoumbwa; ndio inayowezesha vitu kubadilika na kugeuka ili kwamba neema ya Mwenyezi Mungu ienee duniani. Kama maada ingekuwa isichukue maumbo tofauti kama matokeo ya migongano na viumbe vingine na maisha yasingekuwa na uwezo wa kuchukua miundo mengine, utofautishaji na maendeleo ya maisha hayangewezekana. Dunia isiyoyumba na kubadilika itafanana na mtaji usiotumika ambao hauzalishi faida yoyote. Kwa maumbile, mabadiliko ni mtaji unaozalisha faida. Kama mambo yalivyo ni kwamba inawezekana kwamba uwekezaji wa kiasi fulani cha mtaji uishie kwenye hasara, lakini usongevu wa wakati wote wa maada kwa ujumla haswa husababisha matokeo yenye faida. Hitilafu inayotokea katika miundo ya maada huishia kwenye maendeleo ya utaratibu wa maisha kuelekea kwenye ukamilifu.

Kuna swali fulani kuhusu kama uovu upo hapa duniani kwa maana halisi ya neno lenyewe. Endapo tutatazama kwa uangalifu, tutaona kwamba uovu wa vitu si sifa halisi; ni sifa ya uhusiano. Silaha zilizoko mikononi mwa adui yangu ni mbaya kwangu, na silaha iliyoko mikononi mwangu ni mbaya kwa adui yangu. Mimi na adui yangu tukiwekwa pembeni, silaha zenyewe zote ima sio mbaya au nzuri. Uelekeo wa maumbile unaweza kusemekana kuwa ni wa kimahesabu, yaani ni kwamba, mfumo wake umewekwa kwa namna ambayo hauwezi kutosheleza mahitaji yetu yote. Hata hivyo,

tunataka kutimiza matakwa yetu yasiyo na idadi bila kukabiliana na kipingamizi chochote, na nguvu za asili hazitimizi matakwa yetu mengi tunayoyathamini, matakwa ambayo kwa hali yoyote ile hayana faida kwa mtazamo wa asili yetu muhimu ya kimaumbile. Maumbile hayazingatii matakwa yetu na hukataa kukubali mahitajio yetu. Kwa hiyo, tunapokutana na mambo yasiyo pendeza katika maisha yetu, tunakasirika bila uhalali wowote na tunaziita sababu hizo za kusumbuka kwetu kuwa ni "uovu."

Endapo mtu anataka kuwasha taa yake ambapo haina mafuta, hataanza kushusha pumzi na kulalamika au kulaani dunia yote! Wakati wote maumbile huelekea kwenye lenyo lililodhahiri, kupita juhudi na mapambano. Sababu maalum huamua kila hatua inayochukuliwa, na mabadiliko na maendeleo yanayofanyika hayakubuniwa kukidhi uthibitisho wa mwanadamu au kutosheleza matakwa yao. Lazima ikubalike kwamba baadhi ya matukio ya ulimwengu huu hayawezi kuendana na matakwa yetu, na si lazima tuvifikirie vitu visivyotupendeza kuwa ni udhalimu.

Ali [(a.s)] Amirul-Mu'minin anaielezea dunia kama makazi ya mashaka, lakini hata hivyo, ni mahali pazuri kwa mtu anayeijua dunia sawa sawa. Ingawa yeye mwenyewe alikukabiliana na aina zote za matatizo na maudhi, kila wakati alikuwa anawatahadharisha wanadamu kuhusu uadilifu kamili ya Mwenyezi Mungu.38 Jambo lingine la muhimu ambalo ni lazima tusilisahau ni kwamba wema na ubaya haviwakilishi namna mbili pamoja za kipekee au sanjari katika mpango wa maumbile. Wema ni sawa na uhai, na uovu ni sawa na kutokuwepo uhai; popote kiumbe chenye uhai kinapotokea, kutokuwepo na uhai pia kunajiashiria.

Tunapozungumzia umaskini, ufukara na ujinga au maradhi tusidhani kwamba kila moja kina uhalisi wake peke yake; umasikini kwa kifupi ni 38 Nahju al-Balaghah, kilichohaririwa na Subhi Salh, uk. 493. kutokuwa na mali, ujinga ni kukosekana kwa elimu na maradhi ni kutokuwa na afya. Mali na elimu ni mambo halisi, lakini umaskini si kingine zaidi ya kuwa na mkononi na mifuko mitupu, na ujinga ni ukosefu wa elimu. Hivyo, umaskini na ujinga havina uhalisi wa kugusika; vinaelezeka kwa kupitia kutokuwepo kwa vitu vingine.

Ni vivyo hivyo kuhusu majanga na mabalaa ambayo huwa tunayafikiria kuwa ni uovu na chanzo cha mateso. Mambo haya ni aina ya hasara au kutokuwepo kitu, na yanakuwa mabaya kwa maana ya kwamba husababisha kuharibika au kutokuwepo kwa kitu kingine mbali na yenyewe. Mbali na haya, hakuna kitu kingine kwa kadiri kinavyoweza kuwepo kinachoweza kwa hali yoyote kuitwa kiovu au kibaya. Kama majanga yasingefuatana na magonjwa na kifo, kupotea na kuharibika kwa viumbe fulani, hivyo kuzuia uwezo wao wa kusambaa, yasingekuwa mabaya. Ni kupotea na kuharibika kunakotokana na maafa yenye asili ya ubaya. Chochote kilichopo duniani ni chema; uovu unafungamana na kutokuwepo kwa kitu, na kwa kuwa kutokuwapo kitu hakufanyi jamii juu ya maisha, hakikuumbwa kwa hiyo hakipo.

Kiumbe na kisicho kiumbe ni sawa na jua na kivuli chake. Wakati umbile likielekezwa kwenye jua linatupa kivuli. Kivuli ni nini? Kivuli hakijaumbwa na kitu chochote; kinategemea pale jua linapokuwa halifikishi

miale yake mahali fulani kwa sababu ya kuwepo kizuizi; hakina chanzo au asili yake chenyewe binafsi.

Vitu vina uhai halisi kwa sababu ya kuwa vimeumbwa bila ya kuhusisha vitu vingine mbali na vyenyewe; kwa maana hii, vitu hivi sio viovu. Kwa falsafa ya maisha itokanayo na imani ya kuwepo Mwenyezi Mungu, ulimwenguni sawasawa na wema. Kila kiumbe kwa asili ni chema; kama ni kiovu, kinakuwa hivyo tu katika maana ya ulinganisho tu katika kukiunganisha na vitu vingine visivyokuwa hicho chenyewe. Uhai wa kila kiumbe sio wa kweli kwa kitu kingine mbali na chenyewe, na kisichoguswa na viumbe.

Mbu wa malaria mwenyewe tu sio mwovu. Kama akielezewa kwa namna hiyo, ni kwa sababu ana madhara kwa mwanadamu na anasababisha ugonjwa. Ambacho kimeumbwa ni uhai wa kitu ndani yake na kwa chenyewe, ambacho ni uhai wa kweli; kuwepo kwa kitu kwa kubahatisha au wa kimasharti hakuna nafasi katika mpangilio wa maisha na sio kweli. Kwa hiyo, hatuwezi kuuliza kwa nini Mwenyezi Mungu ameumba vitu vyenye kuhusiana au vya kutegemea hali - masharti. Vitu vya kutegemea hali au vitu vya kufikirika havitenganishiki na vitu halisi vinavyotokana navyo; ni viambatani visivyoepukika na havichukui sehemu ya uhai wao. Mtu hawezi kuzungumzia vitu vya kutegemea hali (au shuruti ya kuwepo vitu vingine) kuwa vimeumbwa.

Kiumbe ambacho ni halisi kina umuhimu wa lazima wa kupata uhai wake kutoka kwa Muumbaji. Ni vitu vile tu na sifa zile ambazo ni halisi ambavyo vinapatikana nje ya akili. Sifa za kuhusiana hutengenezwa na akili na hazipatikani kuwepo nje yake, hivyo mtu hawezi kumtafuta muumbaji. Zaidi ya hayo, kitu chenye uwezekano wa kuwepo ni ulimwengu wote kwa ujumla, pamoja na vitu vyote vilivyomo humo na sifa ambazo hazitenganishiki nao; ulimwengu uwakilisha kitu kisichogawanyika. Kutokana na sehemu ya inayofaa kutazamia hekima ya Mwenyezi Mungu, ama ulimwengu lazima uwepo katika mfumo ambao ni wa pekee juu yake, au usiwepo kabisa.

Ulimwengu usio na utaratibu au kanuni ya kisababishi, dunia ambayo wema na uovu havikuachanishwa, ingekuwa ni kitu kisichowezekana na ni njozi. Si rahisi kudhania kwamba sehemu moja ya dunia inaweza kuwepo na nyingine isiwepo. Maumbile ni kitu kizima kamili, kama muundo na umbo la mtu, na viungo vyake havitenganishiki.

Mwenyezi Mungu si muhitaji wa chochote na moja ya matokeo ya hili ni kwamba huweka viumbe kwa uhuru kabisa, kama mtu karimu ambaye ukarimu wake mkubwa hautazamii shukrani, au kama fundi stadi ambaye wakati wote hushughulika na kutengeneza vitu vipya. Ukarimu mkubwa kama huo na ubunifu unafafanua dhati ya Mola Mtukufu ambaye ishara zake zinaonekana na ziko wazi kwenye kila kiumbe.

17

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA SABA

### BAADHI YA VIPENGELE VYA TOFAUTI

Tuchukulie kwamba mwenye kiwanda ameajiri wafayakazi wenye ujuzi na wasio na ujuzi kukiendesha na kukisimamia kiwanda chake. Wakati wa kuwalipa mishahara yao unapofika, anawalipa wale wajuzi na wenye sifa ambao kazi yao ni ya kiwango cha juu, malipo makubwa zaidi ya yale ya wafanyakazi wasio na ujuzi. Sasa je, tofauti hii katika mishahara ni haki au sio haki? Mmiliki wa kiwanda anatenda kwa usawa au kwa upendeleo? Bila shaka kuna tofauti iliyoingia hapa, lakini hatuwezi kuiita ubaguzi. Uadilifu haumtaki mmiliki wa kiwanda kuwalipa wafanyakazi wasio na ufundi mshahara sawa na wale wenye ujuzi. Ina maana badala yake kwamba anapaswa kulilipa kila kundi kile linachostahili kupata. Kanuni ya aina hii itafafanua kwa uwazi kabisa kadirio linalolingano kwa kila kazi na kuchangia kwenye ustawi wa mahali hapo pa kazi.

Kutofautisha katika masuala kama haya ni aina ya uadilifu yenye kujieleza vizuri na ya kivitendo, bila kufanya hivyo ingekuwa sawa na ukandamizaji, ubaguzi na dhuluma; ingekuwa ni matokeo ya tathmini pungufu ya thamani wakilishi ya vitu katika kuvitofautisha kwake.

Tunapoitazama dunia kwa ujumla na kuchambua sehemu zake mbali mbali, tunaona kwamba kila sehemu ina nafasi na kazi yake maalum na imefunikwa na sifa ambazo zinafaa juu yake. Katika kutambua huku, tunaweza kuelewa umuhimu wa mabadiliko katika maisha ya binadamu, ya mwanga na giza, ya kufuzu na kushindwa, kwa ajili ya kudumisha ulinganifu wa dunia kwa ujumla.

Kama dunia ingekuwa inafanana, bila ya mabadiliko au tofauti, aina zenye tofauti na nyingi za viumbe zisingekuwepo. Ni katika aina mbali mbali hizi na wingi wake uliopo hasa ambamo tunaiona fahari na utukufu wa dunia. Uamuzi wetu juu ya vitu utakuwa na mantiki, sahihi na wa kukubalika wakati tutakapo zingatia ulingano uliopo ulimwenguni na uhusiano ambao kwa manufaa kabisa unaunganisha sehemu zake mbalimbali na kila moja yao, si pale tunapochunguza sehemu moja katika mtindo wa kuitenga yote kabisa.

Mpango wa maumbile umeegemezwa kwenye ulinganifu, juu ya upatikanaji na uwezo; kile kinachothibitika kabisa katika maumbile ni utofautishaji, si ubaguzi. Uzingatiaji huu unatuwezesha kuchunguza jambo hili kwa busara zaidi na kwa uhakika. Ubaguzi unamaanisha kutofautisha miongoni mwa vitu vyenye upatikanaji mmoja uleule na vilivyomo katika mazingira mamoja yaleyale. Utofautishaji unamaanisha kuonyesha tofauti miongoni mwa uwezo usio sawa na usiotawaliwa na mazingira mamoja.

Itakuwa si sahihi kama tutsema kwamba ingekuwa nzuri zaidi kwa kila kitu hapa duniani kuwa namna moja na isitofautiana, kwani mwendo wote, shughuli na ubadilikaji motomoto tunaouona duniani unawezeshwa na utofautishaji. Binadamu anazo njia nyingi za kutambua na kuzoea uzuri, pindi panapokuwepo ulinganisho baina ya uzuri na ubaya. Mvuto

unaowekwa na uzuri, kwa maana fulani, ni kuakisi kwa ubaya na uwezo wake wa kurudisha nyuma.

Kwa njia hiyo hiyo, kama binadamu asingejaribiwa na kutahiniwa katika maisha, uchamungu na maadili mema vingekuwa havina thamani, na kungekuwa hakuna sababu ya kutakasa roho ya mtu na hakuna kitu cha kumfanya mtu ajizuie matamanio yake. Kama turubai zima limekuwa katika hali moja ya kufanana, hatuwezi kusema hiyo ni picha, ni tofauti za rangi mbali mbali na mpangilio wake ndio ambao huonyesha ustadi wa msanii. Ili utambulisho wa kitu ujulikane, ni muhimu kitofautishwe na vitu vingine, kwani kipimo ambacho hutumika kutambua vitu au watu ni tofauti za ndani au nje zilizopo baina yao.

Moja ya ajabu za maumbile ni tofauti katika uwezo na vipaji ambavyo viumbe vimepewa. Ili kuhakikisha maisha ya jamii yanaendelea, maumbile yamempa kila mtu seti maalum ya muonjo na uwezo, ambavyo muingiliano wao unahakikisha nidhamu ya jamii, kila mtu hutimiza baadhi ya mahitaji ya jamii na anachangia katika kutatua baadhi ya matatizo yake.

Tofauti ya kawaida baina ya watu kuhusu uwezo wao huwa inasababisha wao kuhitajiana. Kila mmoja wao huchukua baadhi ya kazi za jamii kwa mujibu wa muonjo na uwezo wake, na maisha ya kijamii yanayohifadhiwa kwa njia hiyo humwezesha mtu kusonga mbele na kuendelea.

Hebu tuchukue jengo au ndege Ulaya kama mfano. Kila kimojawapo cha vitu hivi kina sehemu nyingi tofauti, visehemu vigumu na vilivyopangwa vinavyo tofautiana sana kwa ukubwa na maumbo, tofauti hii inatokana kwenye wajibu ambao kila sehemu inao kwenye kitu kizima hicho.

Kama tofauti hii isingekuwa iwepo kwenye umbile la ndege Ulaya, basi isingekuwa ndege Ulaya tena isipokuwa mchanganyiko wa vyuma mbali mbali. Kama utofautishaji ni dalili ya uadilifu wa kweli katika ndege Ulaya, lazima pia iwe ni ishara ya uadilifu wa ki-Mungu miongoni mwa viumbe vyote vya dunia pamoja na binadamu. Zaidi ya hayo, lazima tutambue kwamba upambanuzi miongoni mwa viumbe ni asili kwenye chimbuko lao. Mwenyezi Mungu haumbi kitu kwa matumizi ya pekee na tofauti ya utashi Wake; utashi Wake haitumiki kwa kitu kipekee. Ulimwengu wote tangu mwanzo hadi mwisho ulitokea kuwepo kwa zoezi moja la utashi Wake; ilikuwa ni hili ambalo limeviwezesha viumbe katika kuongezeka kwao kusiko na ukomo, kuja kuwepo.

Halafu, ipo sheria na utaratibu maalum ambao hudhibiti vipimo yote vya muumbo. Ndani ya mfumo wa visababishi, hutoa daraja na nafasi ya pekee kwa kila kitu. Matakwa ya Mwenyezi Mungu kuumba na kuutengemaza ulimwengu ni sawa na utaratibu Wake ulioko tayari ndani yake. Zipo thibitisho za kifalsafa za uhakika zinazounga mkono pendekezo hili, na pia imefafanuliwa kwenye Qur'ani:

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾ وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ﴿٥٠﴾

"Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo, na amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho." (54:49-50).

Itakuwa ni makosa kudhania kwamba utofautishaji na uhusiano uliowekwa na Mwenyezi Mungu katika uumbaji Wake ni sawa na uhusiano wa kidesturi uliopo katika jamii ya binadamu. Uhusiano wa Mwenyezi Mungu na viumbe vyake si jambo la kawaida au kutambulikana tu; ni

uhusiano utokanao kwenye lile tendo hasa la uumbaji wenyewe. Utaratibu ambao ameuweka kwenye vitu vyote ni matokeo ya Yeye kukiumba kitu hicho. Kila kiumbe hupokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu kiasi cha ukamilifu na uzuri ambao kina uwezo wa kuupokea.

Kama usingekuwepo utaratibu maalum wa kuudhibiti ulimwengu, kiumbe chochote kingeweza, katika uelekeo wa mwendo wake, kusababisha kutokeza kwa kiumbe kingine chochote, na sababu ya athari vingeweza kubadilishana nafasi zao. Lakini ni lazima ieleweke kwamba mahusiano muhimu miongoni mwa vitu yamekadiriwa na ni ya lazima; kituo na sifa iliyowekwa kwenye kitu huambatana bila kutengana nacho, kwa daraja lolote na kiwango chochote kitakachokuwa nacho. Hakuna kitu kinachoweza kwenda kinyume na kiwango ambacho kimekadiriwa kwa yake na kuchukua daraja ya kiumbe kingine. Utofautishaji ni kiambata cha viwango vya viumbe, kinachoviwekea vipimo vinavyotofautiana vya udhaifu na nguvu, upungufu na ukamilifu.

Ikatuwa ubaguzi kama vitu viwili vilikuwa na uwezo sawa wa kupokea ukamilifu lakini ukatolewa kwa kimojawapo tu na kingine kikanyimwa. Kiwango cha kiumbe ambacho kipo katika mpango wa maumbile hakiwezi kulinganishwa na madaraja ya kawaida ya jamii ya binadamu. Viwango hivyo ni halisi, si vya kawaida, na havihamishiki. Kwa mfano wanadamu na wanyama hawawezi kubadilishana nafasi kwa namna ile ile watu binafsi wanavyoweza kubadilishana kazi na vyeo wanavyokalia katika jamii.

Uhusiano unaounganishwa kila kisababisho na athari zake na kila athari na chanzo chake hutokana na asili ya chanzo na athari kwa mpango huo. Kama kitu ni chanzo, ni hivyo kwa sababu ya sifa fulani ambayo haiwezi kuachanishwa nacho, na kama kitu ni athari, ni hivyo kwa sababu ya sifa ya kimsingi juu yake, ambayo si nyingine mbali na namna ya kuwepo kwake. Halafu, upo utaratibu muhimu na mzito sana unaounganisha viumbe vyote, na kiwango cha kila kiumbe ndani ya mpango huo unafanana na asili yake. Kwa kadiri utofautishaji unavyohusika kwenye upungufu uliopo kwenye asili, si ubaguzi, kwa sababu mmiminiko wa neema za Mwenyezi Mungu hautoshelezi kwa ukweli kujitokeza na kuwepo; upokeaji wa chombo kinachotakiwa kupokea neema hiyo pia ni muhimu. Ni kwa sababu hii kwamba viumbe fulani hupatwa na kutojiweza na havipati viwango vya juu; haiwezekani kwamba kitu kipate uwezo wa kuwa kiumbe au ukamilifu mwingine na kwamba Mwenyezi Mungu asikipatie sifa hiyo.

Suala la namba (numerali) unafanana hasa; kila tarakimu ina nafasi yake iliyokadiriwa. Mbili huja baada ya moja na haiziwezi kubadilishana nafasi hiyo. Kama tutabadilisha nafasi ya tarakimu, tutakuwa wakati huo tumebadilisha asili yake. Ni wazi kwa hiyo, kwamba viumbe vyote vinamiliki madaraja yaliyokadiriwa na visaidizi na huwa chini ya mlolongo wa sheria imara na zisizobadilika. sheria ya Ki-Mungu kwa kawaida haifanyi kuwa kitu tofauti kilichoumbwa, bali fikra ya kinadharia iliyochukuliwa kutoka kwenye hali ile ambayo vitu huonekana kuwepo. Kile ambacho kina uhai wa nje kinakuwa na viwango na daraja ya kiumbe, kwa upande mmoja, na mfumo wa chanzo na athari, kwa upande mwingine. Hakuna kinachotokea nje ya mpango huu, ambacho si kingine mbali na ile

desturi ambayo imetajwa na Qur'ani: "Na hutakuta mabadiliko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu." (35:43).

Mpango wa maumbile umekuwa kwenye mlolongo wa sheria zilizo sehemu ya asili yake. Nafasi ya kila kiumbe kilichomo humo imebainishwa wazi wazi, na kuwepo kwa viwango na daraja mbalimbali za uhai ni matokeo ya lazima ya hali ya utaratibu wa muumbile, ambao bila kuepuka husababisha kutokeza jamii mbali mbali na utofautishaji. Mabadiliko na utofautishaji ni vitu ambavyo vyenyewe havikuumbwa; ni sifa zisizotenganishika za viumbe vyote. Kila chembe ulimwenguni imepokea kila chochote ilichokuwa na uwezo wa kukipokea; hakuna dhulma au ubaguzi uliokiadhibu, na ukamilifu wa ulimwengu - unaofanana na jedwali la kuzidisha katika uamrishaji wake sahihi na usiobadilika - hapo umehakikishwa.

Wayakinifu ambao wanachukulia kuwepo kwa mabadiliko na utofautishaji kwenye utaratibu wa asili kama ushahidi wa ukandamizaji na udhalimu na hudhani kwamba ulimwengu hautawaliwi na uadilifu, bila shaka watahisi maisha kama ni magumu, yanayochukiza na kuchosha. Uamuzi huo wa haraka haraka wa wayakinifu unaokabiliwa na dhiki na matatizo ni sawa na uamuzi wa mtoto anayemtazama mwenye bustani anayepogowa matawi ya mti ya kijani yanayostawi vizuri wakati wa msimu wa kuchipua. Bila kutambua makusudi na umuhimu wa kupogowa huko, mtoto huyo atafikiri kwamba mwenye bustani ni mharibifu na mjinga. Kama neema zote za dunia zingewekwa chini ya mamlaka ya myakinifu, bado asingetosheka. Kwani, pindi dunia inapoonekana haina lengo na ikiwa juu ya msingi wa udhalimu, haina maana kwa binadamu kutafuta haki, na katika dunia ambayo inakosa lengo, ni upumbavu kwa mwanadamu kujiwekea lengo.

Ikiwa chimbuko na hatima ya binadamu ni kama wayakinifu wanavyoyaeleza, kana kwamba binadamu ni nyasi zinazojiotea zenyewe na halafu zikatoweka, basi mwanadamu lazima awe kiumbe dhalili kuliko viumbe vyote. Kwani angekuwa anaishi kwenye dunia ambayo imekosa mvuto wote, ulinganifu na utulivu. Mawazo, hisia na wasiwasi vingemsababishia huzuni, ikiwa si chochote zaidi ya mzaha mkali aliofanyiwa na maumbile ili kumwongezea mateso na unyonge na kumzidishia taabu.

Kama mtu mwenye uwezo na kipaji angekuwa ajitolee kuhudumia jamii ya binadamu, ingekuwa na faida juu yake? Ibada maadhimisho ya baada ya kifo chake na kutoa heshima inayofanyika kwenye kaburi lake, yasingemnufaisha hata kidogo; hayo yangekuwa kudumisha hadithi ama maelezo ya kinafiki, kwa sababu mtu anayehusika angekuwa si chochote zaidi ya umbile lililokusanywa na maumbile kwa ajili ya kiburudisho chake kama kitu cha kuchezea kwa muda wa siku chache kabla ya kugeuzwa kuwa ukufi wa vumbi.

Kama tukiangalia majaaliwa ya wengi wa watu ambao wakati wote wanapambana na aina mbalimbali za huzuni, wasiwasi, kuishiwa na kutofaulu, hali inaonekana kufifia zaidi. Kwa msimamo kama huo wa maisha ya mwanadamu, pepo pekee ambayo uyakinifu unaweza kumpa mwanadamu ni wingi wa hofu na mateso. Msimamo wa myakinifu kwamba

mwanadamu anakosa uhuru na hiari unamfanya awe kiumbe dhalili zaidi. Falsafa ya maisha ya mtazamo wa mwelekeo mmoja tu ya kiyakinifu ingekuwa na maoni kwamba binadamu ni kama roboti lenye mtambo na nguvu ya chembechembe zake zinazoendeshwa na maumbile. Je, akili na silika ya binadamu - bila kutaja hali halisi za maisha - vinaweza kukubali tafsiri ya kawaida na finyu ya binadamu kama hiyo, maisha yake na hatima yake?

Kama tafsiri hii ingekuwa ya kweli, mwanadamu angekuwa hana uwezo wa kuona furaha kama mwanasesere wa mtoto. Akiwa katika hali kama hiyo, binadamu angelazimika kufanya hisia zake na mielekeo kuwa ndio msingi wa maadili na kipimo cha tathmini, kuamua kila jambo kufuatana na faida na hasara binafsi. Angefanya kila juhudi kuharibu kila kipingamizi kwenye njia yake na kulegeza vizuizi vyote juu ya matamanio yake ya kimwili. Kama binadamu angekuwa afanye vinginevyo, angeonekana kama mtu wa nyuma na mjinga.

Mtu yoyote mwenye kiwango kidogo sana cha utambuzi na anaamua jambo kwa njia ya uadilifu na bila kupendelea ataziona hizi dhana zenye uoni mfinyu na za ajabu kuwa halali, hata kama zingepambwa kwa kiasi gani cha ghilba ya kifalsafa na kisayansi.

Binadamu mwenye falsafa ya maisha ya kidini, anaiona dunia kama mfumo wa utaratibu wenye utambuzi, dhamira, ufahamu na lengo. Hekima kuu ya Mwenyezi Mungu inayotoa uadilifu inatawala juu ya ulimwengu na kila chembe ya uhai na inaziangalia shughuli na matendo yote. Mtu wa kidini, kwa hiyo, anahisi hali ya kuwajibika kwa kuhusiana na ufahamu ambao unatawala ulimwengu, na anajua kwamba dunia iliyoumbwa na kusimamiwa na Mwenyezi Mungu ni muhimu kuwa ni dunia ya umoja, utulivu na nzuri. Anaelewa kwamba hitilafu na uovu vinakuwa vinapatikana kwa ufahamu wa ziada baada ya tafakari ya mwanzoni na kufanya wajibu wa msingi katika upatikanaji wa wema na kutokeza kwa umoja na utulivu.

Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa falsafa hii ya maisha ambayo inaweka kielelezo cha upeo mpana kwa ajili ya mwanadamu, maisha hayaishii kwenye dunia hii, na wala maisha ya dunia hii hayakufungwa kwenye hali nzuri ya kimali, utajiri au kuwa huru kutokana na kutofanya juhudi na kutopata matatizo. Muumini wa dini ataiona dunia kama njia ambayo lazima ipitwe, kama mahali pa mitihani, na kama uwanja wa juhudi. Ndani mwake uadilifu wa matendo ya wanadamu hupimwa. Mwanzoni mwa maisha yajayo, wema na uovu katika fikira, imani na matendo ya wanadamu yatapimwa katika mizani sahihi kabisa. Uadilifu wa Mwenyezi Mungu utadhihirika katika hali yake halisi, na kunyimwa kokote kunakoweza kuwa kumefika binadamu hapa duniani, iwe kuhusu mali au vinginevyo, kutafidiwa juu yake.

Kwa kuzingatia kuhusu hatima yake inayomngojea binadamu na kuelewa kubatilika kwa mambo mazuri ya dunia ya kiyakinifu, mtu anaelekeza ufahamu wake kwa kujitahidi kuelekea kwa Mwenyezi Mungu tu. Lengo lake linakuwa ni kuishi kwa ajili Yake na kufa kwa ajili Yake. Hayazingatii mabadiliko ya dunia hii tena. huviangalia vitu vya muda mfupi kwa thamani yake kama vilivyo tu, na haruhusu kitu chochote kushawishi moyo wake.

Kwani anajua kwamba nguvu za ushawishi zitasababisha ubinadamu wake kufifia na kumwangusha kwenye kimbunga cha upotofu wa uyakinifu.

Kwa kuhitimisha, tungeongezea kwamba hata ukiachilia mbali suala la uwazi, kuwepo kwa hitilafu hapa duniani haimaanishi udhalimu. Ukandamizaji na udhalimu una maana kwamba mtu fulani anafanyiwa ubaguzi ingawa naye anayo haki sawa na ya mwingine. Lakini viumbe havina "madai" yoyote kwa Mwenyezi Mungu wala kamwe hawakuwa nayo, hivyo basi, endapo baadhi ya vitu vinapata ubora juu ya vingine hii haihesabiki kama dhulima.

Hatuna chochote cha kwetu wenyewe: kila pumzi na kila pigo la moyo, kila fikira na wazo linalopita kwenye akili zetu, yanachukuliwa kwenye hazina ambayo sisi hatuimiliki na hatujafanya kitu katika kujenga. Hazina hiyo ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, aliyotuzawadia sisi wakati wa kuzaliwa.

Pindi tunapoelewa kwamba chochote tulicho nacho si chochote isipokuwa ni zawadi ya ki-Mungu, itadhihirika kwamba tofauti miongoni mwa zawadi anazowapatia wanadamu ziko kwenye msingi wa hekima Yake lakini hazihusiani na ama haki au udhalimu, kwa sababu hapakuwepo na suala la stahili yoyote au madai yoyote upande wetu.

Maisha haya yenye ukomo na ya muda mfupi ni zawadi kwetu, zawadi ya kutoka kwa Muumba; Anayo hiari kamili katika kuamua aina na kiasi cha zawadi Anayotoa, na hatuna dai lolote kwake. Kwa hiyo, hatuna haki ya kukataa hata kama zawadi tunayopewa bure kabisa, inaonekana ndogo na isiyo na maana sana.

18

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA NANE

### MTAZAMO WA JUMLAWA TATIZO HILO

Mojawapo ya maswali ambayo mara nyingi yamevutia wanafikra wanaojihusisha na asili ya maisha ya mwanadamu na ambalo limekuwa mada kuu yenye ubishani usio na ukomo ni kama binadamu anayo hiari ya kuchagua malengo yake na kutekeleza matakwa yake katika matendo na shughuli zake zote - katika mambo yote ya maisha yake, yawe ni mambo ya kimaada au vinginevyo. Matamanio yake, mielekeo yake na dhamira ndio tu kipengele kinachotafuta maamuzi yake?

Au matendo yake na mwenendo wake yamelazishwa yake? Analazimika kwa unyonge kabisa kufanya matendo fulani na kufanya uamuzi? Je, binadamu ni kifaa kisicho na hiari mikononi mwa mambo yaliyo nje yake? Ili kuweza kuelewa umuhimu wa suala hili lazima izingatiwe kwamba katika ufumbuzi wake inategemea uwezo wetu kunufaika kikamilifu kutokana na uchumi, sheria, dini, saikolojia na matawi mengine yote ya elimu ambayo yanamchukua mwanadamu kama somo lao. Hadi tutakapogundua kama binadamu anayo hiari au hapana, sheria yoyote itakayoshauriwa kwa ajili ya mwanadamu katika elimu yoyote ile, itakuwa inatumika kwa kiumbe ambacho asili yake hatuijui. Ni dhahiri kwamba hakuna matokeo yanayopendeza yatakayopatikana.

Suala la hiari dhidi ya majaaliwa si tatizo la kitaaluma au kifalsafa pekee. Pia, linawahusu wote wale wanaopendekeza kwa binadamu kwamba ana jukumu ambalo anawajibu wa kulikamilisha na wakamtia moyo wa kufanya hivyo. Kwani kama hawataamini, angalau kwa ukamilifu kabisa, juu ya utashi huru, hapatakuwepo na msingi wa kuwapa thawabu watu wanaotekeleza wajibu wao na kuwaadhibu wale ambao hawatekelezi. Baada ya kujitokeza kwa Uislamu, Waislamu pia walitoa mazingatio maalum juu ya suala hili, kwa sababu falsafa ya maisha ya Uislamu ilisababisha suala hili kuchunguzwa kwa undani zaidi kuliko ilivyokuwa kabla ya hapo na mashaka yote yafafanuliwe. Kwani, kwa upande moja, suala hilo liliunganishwa na upweke wa Mwenyezi Mungu na, upande mwingine, liliunganishwa na sifa Zake za uadilifu na mamlaka.

Mabingwa wa fikra wa zamani na sasa wanaweza kugawanyika katika makundi mawili kuhusu suala la utashi huru dhidi ya majaaliwa. Kundi la kwanza linakataa kwa ushupavu hiari ya mwanadamu katika matendo yake, na kama matendo yake yataonyesha kudhihirisha dalili za uchaguzi wa hiari, hii ni kwa sababu ya makosa na mapungufu ya namna ya utambuzi wa binadamu.

Kundi la pili linaamini katika utashi huru na kusema kwamba mwanadamu anapata uhuru kamili wa kutenda katika nyanja ya matendo ya hiari; uwezo wake wa kufikiri na kuamua una athari nyingi na uko huru kutokana na vipengele vyote vilivyopo nje yake. Kwa kawaida, binadamu anapata uzoefu wa athari za ulazimisho kuhusiana na kuzaliwa kwake, pia kutokana na mambo mbalimbali yanayomzunguka na matukio

anayokabiliana nayo wakati wa uhai wake. Matokeo ya hili yanaweza kuwa kwamba anaishia katika kuamini kwamba hakuna kitu kama utashi wa hiari. Aliingia dunia bila ya hiari na anaonekana kuwa anadhibitiwa kikamilifu na majaaliwa, akipeperushwa huko na huko kama kipande cha karatasi hadi mwishowe anaondoka hapa duniani.

Wakati huo huo, binadamu hutambua kwa wazi kabisa kwamba yuko huru na mwenye kujitegemea katika mambo mengi, bila ya aina yoyote ya ulazimishwaji au kuwekewa masharti. Mwanadamu anao uwezo na umahiri wa kupambana kikamilifu dhidi ya vikwazo na kuendeleza udhibiti wake wa maumbile kwa kutegemea uzoefu uliopita na ujuzi. Ukweli halisi na wenye madhumuni ambao hawezi kuukanusha ni kwamba kuna tofauti kubwa na halisi baina ya mishughuliko ya hiari ya mikono na miguu yake na utendajikazi wa moyo wake, ini na mapafu yake.

Hivyo, kwa kukubaliana na hiari, utambuzi na uwezo wake wa kuchagua, sifa ambazo ni ishara ya ubora wa ubinadamu wake na chimbuko la wajibu wake, binadamu anajua kwamba, ni kweli anao utashi huru katika mlolongo wote wa matendo yake na kwamba hakuna kipingamizi kinachozuia utekelezaji wa hiari yake au kutengeneza imani yake. Lakini, katika hali nyinginezo, mikono yake imefungwa na hana uwezo wa kuchagua: mambo yanaamuliwa na vitu vya kidunia au ulazimishwaji wa kisilika hali ambao unafanya thamani halisi ya maisha yake, na mengine ambayo yanalazimishwa juu yake na vipengele vilivyo nje yake.

Majaaliwa: Watetezi wa majaaliwa hawaamini kwamba binadamu yuko huru katika matendo ayafanyayo hapa duniani. Waamini majaaliwa wa kitheolojia kama ile madhehebu ya Kiislamu ijulikanayo kama Ashari ambalo linategemea maana ya nje ya Aya fulani za Qur'ani na hawasimami wakatulia na kutafakari kuhusu maana ya kweli ya Aya zote zinazohusika au namna ya mamlaka ya Mwenyezi Mungu ili kuazimia kabla, wamehitimisha kwamba mwanadamu hana hiari ya namna yoyote ile.

Wao pia wanakanusha kwamba vitu husababisha athari na hawakubali kwamba visababishi vina kazi ya kufanya kwenye maumbile na uchimbukiaji wa viumbe vya kawaida. Wanakiona kila kitu kuwa ni athari ya moja kwa moja na zisizopatanishika za utashi wa ki-Mungu, na wanasema kwamba ingawa mwanadamu ana kiasi fulani cha hiari na uwezo mikononi mwake, havina athari juu ya matendo yake. Matendo ya wanadamu hayasababishwi na uwezo wao na hiari yao lakini husababishwa na utashi wa Mwenyezi Mungu, ambao hutoa athari zote kipekee.

Binadamu anaweza kuchangia kiasi fulani kwenye matendo yake anayoyafanya kwa lengo na nia yake, na kuchangia huku kunaleta matokeo ya kuvuma kwa matendo kama ni mema au mabaya. Mbali na haya, mwanadamu si chochote isipokuwa ni kiini kwa ajili ya utekelezaji wa utashi na mamlaka ya Mwenyezi Mungu. Pia wanasema kwamba kama tukidhania kwamba mwanadamu anao utashi huru, tutakuwa tumepunguza uwanja wa mamlaka ya Mwenyezi Mungu na utawala wake. Uumbaji kamili wa Mwenyezi Mungu unahitajia kwamba hapana mtu atakayemkabili kama muumbaji, vivyo hivyo, imani katika misingi ya upweke wa Mwenyezi Mungu, kwa kufikiria mamlaka kamili tunayoyaweka juu Yake,

lazima imaanishe kwamba viumbe vyote vilivyoumbwa, pamoja na matendo ya wanadamu, yameingizwa kwenye uwanja wa utashi hiari ya ki-Mungu.

Kama tunakubali kwamba mtu anatengeneza matendo yake mwenyewe, tutakuwa tunakanusha mamlaka ya Mwenyezi Mungu juu ya maumbile yote, jambo ambalo haliendani, baadaye, na sifa ya Mwenyezi Mungu ya muumba, kwani tungekuwa tuna mamlaka kamili katika uwanja wa matendo na kusingekuwepo na kazi iliyobakia ya Mwenyezi Mungu. Hivyo, imani katika utashi huru inachukuliwa kama yenye kuelekeza bila huruma kwenye ushirikina au kuabudu miungu wawili.

Kwa nyongeza, baadhi ya watu waifanya kanuni ya majaaliwa - ima kwa utambuzi au kwa kutotambua - kuwa kisingizio cha kufanya matendo kinyume na dini na maadili, na kufungua njia ya kuelekea kwenye upotofu wa kila aina katika nyanja ya imani na matendo. Washairi fulani wa kundi linaloamini kwamba anasa ndio msingi wa maisha, wamo ndani ya kundi hili, wanadhania kwamba kuazimiwa kabla kuwa ni kisingizio tosha cha wao kufanya dhambi na kutumaini, kwa njia hii, kuweza kukwepa yote haya; mzingo wa dhamira na tabia mbaya.

Mtindo huu wa fikra ya majaaliwa ni kinyume na kanuni ya uadilifu, kuhusiana na Mwenyezi Mungu na jamii ya binadamu. Kwa wazi tunaona uadilifu wa ki-Mungu ukiwa umedhihirika katika mpanuko wote katika maumbile yote, na tunaitukuza dhati Yake tukufu kabisa kama yenye sifa hii. Qur'ani inasema:

شَهِدَ اللَّـهُ أَنَّهُ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ ۚ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٨﴾

"Mwenyezi Mungu, na Malaika, na Wenye elimu, wanameshuhudia kuwa hakuna aabudiwaye ila Yeye tu, ni Mwenye kusimamia uadilifu, Hakuna aabudiwaye isipokuwa Yeye tu, Mwenye nguvu, Mwenye hekima."(Imran:18)

Mwenyezi Mungu pia anaelezea usimamishaji wa uadilifu katika jamii ya wanadamu kuwa ni mojawapo ya madhumuni ya kuleta Mitume na anazungumzia kuhusu haja hii kwamba waja Wake wadumishe uadilifu:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ .. ﴿٢٥﴾

"Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani ili watu wasimamishe uadilifu.." (57:25). Katika Siku ya Kiyama, Mwenyezi Mungu atawatendea waja Wake kwa kufuata misingi ya uadilifu vilevile, na hakuna hata mmoja ambaye atafanyiwa dhulma japo kidogo. Qur'ani inasema:

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ... ﴿٤٧﴾

"Nasi tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote.." (21:47).

Sasa itakuwa haki kumlazimisha mtu kutenda jambo ambalo ni la dhambi na halafu kumwadhibu kwa hilo? Endapo mahakama yoyote ingetoa hukumu na kutoa adhabu chini ya hali kama hiyo, hakika hiyo ingekuwa ya kidhalimu. Kama tukikanusha kanuni ya uhuru na tusitoe kabisa kazi ya uhakika kwa hiari ya wanadamu, hakutakuwepo na tofauti yoyote baina ya binadamu na viumbe wengine wote waliobakia. Kwa mujibu wa

wanaoamini katika majaaliwa, matendo ya tabia ya mtu hufanana ya yale ya viumbe vingine kwa vile yanasababishwa na mlolongo wa vipengele vilivyoko nje ya udhibiti wao, hiari yetu haina kwa yenyewe haina uwezo wa kusababisha athari.

Lakini ikiwa Mwenyezi Mungu anaumba matendo ya matakwa ya binadamu, kama Yeye ndiye Muumbaji wa udhalimu na dhambi, hata wa kule kujiwekea washirika Yeye Mwenyewe, tunawezaje kuelezea tabia kama hiyo kwa upande wa Dhati Kamilifu na Iliyotukuka? Kuamini katika majaaliwa kunabatilisha na kufuta kanuni za Utume na wahyi; ile dhana ya ujumbe wa ki-Mungu ambao ndio utumike kama chanzo cha utambuzi wa binadamu; fikra ya maamrisho ya makatazo, ya kigezo cha kidini na amri, ya sheria na kanuni za imani, na mafundisho ya kulipia matendo ya mtu. Kwani, pindi tutakapoamini kwamba matendo yote ya wanadamu hufanyika bila kufikiri (kama mashine), bila ya hiari au chaguo juu ya mhusika, hakutakuwepo na wajibu uliobakia kwa ajilai ya ujumbe wa Mitume ambao wametumwa kuja kumsaidia mwanadamu katika jitihada zake.

Ikiwa wajibu uliowekwa juu ya mwanadamu na maelekezo yaliyoelekezwa kwake hayana uhusiano wowote na utashi huru wake na uwezo wa kutii na kuwajibika, yatakuwa na umuhimu gani? Kama hali ya kiroho ya mwanadamu na matendo ya nje yatakuwa yaa- muliwe kimashine bila yeye kufikiria, juhudi zote zisizo na ukomo za wenye kufundisha maadili, kuikomboa jamii ya binadamu na kuielekezea upande wa ubunifu na maadili ya kiwango cha juu zaidi hazitakuwa na athari yoyote kabisa.

Juhudi zao hazitafaa kitu; hakuna faida kutumaini kiumbe ambacho kila kitendo chake kimekwisha kuamuliwa kiweze kubadilika. Lakini binadamu anawajibika juu ya uongofu wake au maangamizi yake na vilevile juu ya ule wa wengine; uchaguzi wake ndio unaounda hatima yake, na pindi anapojua kwamba kila kitendo anachofanya kina umuhimu wake, atachagua njia yake kwa uangalifu sana. Tegemeo lake juu ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na radhi Zake litasababisha kufunguliwa kwa milango na madirisha ya uwezo kwa ajili yake.

Inawezekana kukanushwa kwamba kuchukulia imani katika ujuzi mkubwa wa Mwenyezi Mungu (Yeye amejua tangu mwanzo yale yote yanayofanyika hapa duniani, hakuna tukio lolote hapa duniani dogo au kubwa linalotokea bila Yeye kulijua kabla), Mwenyezi Mungu lazima ajue kabla juu ya ukatili, matendo maovu na dhambi ambazo binadamu hufanya, na kwa kuwa hutokea hata hivyo, nidhahiri wanadamu hawana uwezo wa kujizuia kufanya maovu hayo.

Tunajibu kama ifuatavyo: Ni kweli kwamba Mwenyezi Mungu anatambua viumbe vyote, vidigo na vikubwa lakini, ujuzi huu haumaanishi kwamba mwanadamu analazimishwa katika yote anayofanya. Ujuzi wa Mwenyezi Mungu upo kwenye msingi wa kanuni ya kisababishi; haitumiki kwa viumbe au kwa matendo ya mwanadamu ambayo yapo nje ya mfumo huo. Ujuzi unaofanya kazi kwa namna ya chanzo na athari haihusishi ulazimishaji. Mwenyezi Mungu alikuwa anatambua mwelekeo wa siku zijazo wa matukio hapa duniani na alitambua kwamba wanadamu wangefanya matendo fulani kwa mujibu wa hiari zao huru. Zoezi la hiari huru ni sehemu ya mfululizo wa usababisho ambao huwaelekeza kwenye

matendo yao, na ni wanadamu wenyewe ndio wanaoamua kufanya ama matendo mwema au maovu. Katika suala hili la mwisho, kwa kutumia vibaya utashi wao huru, wanasababisha uharibifu na ufisadi, hivyo endapo uovu na ukandamizaji unakuwepo katika jamii fulani, haya ni matokeo ya matendo ya wanadamu. Hayakuumbwa na Mwenyezi Mungu. Ujuzi wa Mwenyezi Mungu hauna athari juu ya chaguo la binadamu la wema au uovu.

Ni kweli kwamba katika upeo wa uhuru wa mwanadamu na uwezo wa kuamua, mambo fulani yanakuwepo - kama vile hali ya mazingira, hulka ya asili ya mtu, na mwongozo wa ki-Mungu - ambavyo huchukua wajibu mkubwa katika uchaguzi wake anaoufanya. Lakini wajibu huo umewekewa mipaka katika kuamsha matakwa, katika kutiwa nguvu na msaada wa hiari ya mwanadamu; haimlazimishi mtu kuchagua matakwa fulani. Kuwepo kwa vipengele hivi haimaanishi kwamba mwanadamu amefungiwa kwenye mfumbatio wao; kinyume chake, anao uwezo kamili ama wa kutii matakwa yaliyosababishwa na mambo ya nje au kuyakataa kwa kuyawekea mipaka au kuyabadilisha mwelekeo wao. Mtu anaweza kunufaika kutokana na mwongozo unaopatikana kwake kupitia umaizi na uoni wa dhahiri, unaotoa maumbo kwenye matakwa yake na kudhibiti au kuyarekebisha. Wingi wa misukumo ya kimaumbile mwanadamu aliyonayo ndani mwake kamwe haiwezi kuondolewa kabisa, lakini ni muhimu kuidhibiti na kuinyima fursa ya kwenda hovyo.

Natudhanie kwamba makanika mtaalamu anaikagua gari ndogo kabla haijatoka kuanza safari na anaona ya mbele kwamba motokaa hiyo haiwezi kwenda mbali zaidi ya kilomita chache kabla ya kusimama kwa sababu za dosari za kiufundi. Sasa, endapo motokaa hiyo itaanza safari na ikaharibika baada ya kwenda kilomita chache kama alivyotabiri fundi makenika, inaweza kusemekana kwamba yeye ndiye chanzo cha kuharibika huko kwa sababu amekutabiri hivyo? Ni dhahiri kwamba sivyo, kwa sababu hali duni ya matengenezo ya motokaa hiyo ndio ilikuwa sababu ya kuharibika, si ujuzi wa fundi makenika na utabiri aliofanya; hakuna mtu mwenye busara anayeweza kuuchukulia ujuzi wa fundi makenika kuwa ndio sababu ya kuharibika kwa gari hiyo.

Kwaw kutoa mfano mwingine: Mwalimu anajua maendeleo ya wanafunzi wake wanayoyafanya na anajua kwamba mwanafunzi mmoja hatafaulu katika mtihani wake wa mwisho kwa sababu ya uvivu wake na kukataa kujifunza. Pindi matokeo ya mtihani yatakapotolewa, ikadhihirika kwamba yule mwanafunzi mzembe kweli amefeli mtihani. Sasa, sababu ya matokeo kama hayo ni ujuzi wa mwalimu au uvivu wa mwanafunzi? Ni wazi kwamba ni uvivu wa mwanafunzi. Mifano hii imetuwezesha kuelewa, kwa kiwango fulani, kwa nini ujuzi wa Mwenyezi Mungu sio sababu ya matendo ya waja Wake.

Mojawapo ya athari zenye madhara za imani ya maqaadiru katika jamii ni kwamba inafanya kuwa rahisi zaidi kwa wakandamizaji wenye kiburi kuwakaba na kuwanyamazisha wanyonge na inakuwa vigumu zaidi kwa wanyonge kujitetea. Kutumia fikra ya majaaliwa kama kisingizio, mkandamizaji hukataa kuwajibika kwake na vurugu na matendo yake ya kikatili; anadai kwamba mkono wake ni mkono wa Mwenyezi Mungu na

anazihusisha dhambi zake zote kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi - Mungu Ambaye Yupo na lawama na vipingamizi vyote. Wanyonge hulazimika kustahamili na kukubali lolote wanalofanyiwa na mkandamizaji, kwa sababu kupambana dhidi ya udhalimu wake ni kazi bure na jitihada za kuleta mabadiliko bila shaka zingeshindwa.

Makabaila na wahalifu wengine wakubwa katika historia wakati fulani wametumia fikra ya majaaliwa kuendeleza ukatili wao na ukandamizaji. Wakati familia ya Amiri wa Mashahidi, Husein bin Ali (a.s) ilipofika mbele ya Ibn Ziyad, mhalifu huyo mwovu alimwambia Zainabul Kubraa, (a.s): "Umeona Mwenyezi Mungu alivyomfanya nduguyo na familia yake?" Zainab akajibu: **"Kutoka kwa Mwenyezi Mungu sijaona kitu isipokuwa huruma na wema. Wamefanya kile ambacho Mwenyezi Mungu aliwataka wafanye ili kunyanyua makazi yao na walitekeleza wajibu ambao ulikabidhiwa kwao. Baada ya muda si mrefu wote mtakusanywa mbele ya Mola wenu na kuhesabiwa matendo yenu; hapo ndipo utaelewa nani ameshinda na nani ameokolewa."**[1]

Kuhusu suala la hiari huru na majaaliwa wayakinifu wamenasa kwenye ukinzani. Kwa upande moja, wanamuona mwanadamu kama kiumbe cha kimaada, kinachopatwa, kama ilivyo kwa ulimwengu wote, mabadiliko ya kimetafizikia na kuwa hawezi kutoa athari yake yeye mwenyewe; akikabiliwa na mambo ya kimazingira, ulazima wa kihistoria na hali iliyokwisha kuazimiwa, anakosa hiari. Katika kuchagua njia yake ya maendeleo, mawazo na matendo yake, yupo katika kutegemea maumbile. Mageuzi au maendeleo ya kijamii yoyote ni matokeo halisi pekee ya hali fulani ya kimazingira, na mwanadamu hana wajibu wowote wa kufanya humo.

Kwa mujibu wa uhusiano wa kimajaaliwa baina ya chanzo na athari zake, hakuna jambo linalotokea bila sababu yake tangulizi na utashi wa mwanadamu pia, anapokabiliwa na vitu na matatizo ya kinyenzo na kiuchumi ya mazingira yake na vipengele vya kiakili, anategemea sheria zinazobadilika, zikiwa kwa kweli, ni zaidi kidogo kuliko 'athari' zinazoizalisha. Mwanadamu analazimika kuchagua njia ambayo imeshurutishwa juu yake na matakwa ya mazingira yake na maudhui yake ya kiakili.

Hivyo, hakuna nafasi kwa ajili ya utashi huru na uchanguzi wa mwanadamu kujieleza yenyewe, na hakuna nafasi kwa ajili ya hisia za wajibu wa kimaadili na utofautishaji. Lakini, wakati huo huo, wayakinifu wanamfikiria mwanadamu kuwa na uwezo wa kuathiri jamii na ulimwengu, na hata wanaweka msisitizo zaidi kuliko madhehebu mengine katika nidhamu ya uenezaji na Kiitikadi ndani ya chama chenye mpango. Wanawakusanya watu ambao wameonewa na ukabaila kusimama kidete na kufanya mapinduzi ya nguvu na kujaribu kuwafanya wanadamu wabadilishe imani zao na kuchukua dhima tofauti na ile walikuwanayo hapo kabla - yote haya kwa kutegemea juu ya nguvu ya uchaguzi huru. Uhusishaji huu wa dhima kwa binadamu unapingana na mpango mzima wa uyakinifu wa

1. A-Kafi, I, uk. 160 kutoka kwetu.

mabadiliko ya kimetafisikia kwa vile unatangaza kwamba utashi huru upo hata hivyo.

Endapo wayakinifu wanadai kwamba kuwaamsha watu wanaokandamizwa na kuimarisha makundi ya kimapinduzi huongeza kasi ya kuanzisha kwa mpango mwingine mpya kutoka kwenye chimbuko cha ule wa zamani, hii itakuwa haina mantiki kwa sababu hakuna mapinduzi au mabadiliko stahilifu yanaweza kufanyika kabla ya wakati wake au kwa wakati mwingine mbali na ule unaostahili. Maumbile hufanya kazi yake yenyewe vizuri zaidi kuliko mtu yeyote, kwa mujibu wa mbinu ya mabadiliko ya kimetafisikia, kujihusisha kwenye propaganda na kutafuta kuhamasisha maoni ni uingiliaji usio halali katika kazi ya nguvu asili.

Inaweza pia kusemwa na wayakinifu kwamba uhuru unategemea katika kujua kanuni za maumbile ili kuweza kuzitumia kwa ajili ya malengo na makusudio fulani, sio katika msimamo huru mkabala na kanuni za maumbile. Lakini hii pia inashindwa kupata ufumbuzi wa tatizo, kwa sababu hata hapo baada ya mtu atapokuwa amejifunza sheria hizo na kuamua, kimsingi, kuzitumia kwa malengo maalum, suala linabakia la kama ni nguvu za asili na mata ndizo zinazoamua malengo hayo na kuyashurutisha juu ya mwanadamu au binadamu anayachagua hayo kwa hiari yake.

Kama mtu anaweza kuchagua, je, maamuzi yake ni tafakuri ya matakwa na hali ya maumbile au yanaweza kwenda kinyume nayo? Wayakinifu wamemfikiria mwanadamu kama kiumbe cha sura moja tu hivyo kwamba hata itikadi zake na mawazo ni matokeo ya maendeleo ya uchumi na mali na yanapaswa kufanyiwa tabaka la madaraja na uhusiano wa uzalishaji ndani ya jamii - kwa ufupi, yanaakisi picha makhsusi ya hali inayotokana na mahitaji ya vitu ya wanadamu.

Kama mambo yalivyo, ni kweli kwamba binadamu ana ukiumbe wa kimaada na kwamba uhusiano wa kimaada wa jamii na hali ya kiwiliwili, kijogorafia na ya kimaumbile vyote vina athiri juu yake. Lakini, mambo mengine, yanayotokana na asili muhimu ya mwanadamu na nafsi yake ya ndani pia yameathiri majaaliwa ya mwanadamu wakati wote wa historia, na haiwezekani kuyachukulia maisha ya kiakili ya mwanadamu kuwa yametiwa msukumo na mata pekee na uhusiano wa uzalishaji. Mtu kamwe hawezi kudharau wajibu muhimu uliofanywa na mambo ya kidini na maadili, na silika za kiroho, uchaguzi wa mwanadamu wa njia ya kufuata, utashi wake ndio haswa kiunganishi kimoja katika nyororo ya visababishi vinavyomuongozea kufanya tendo fulani au kutolitenda.

Hapana anayetia shaka kwamba mwanadamu analazimika kupatwa na athari za matendo ya maumbile na hisia zake, na/au kwamba nguvu ya historia na vipengele vya uchumi hutayarisha uwanja kwa ajili ya kutokea matukio fulani. Lakini matukio hayo si kiamuzi pekee cha historia na hayana wajibu muhimu wa kimsingi katika kuamua hatima ya mwanadamu. Hayawezi kumnyang'anya mwanadamu uhuru na uwezo wake wa kuamua, kwa sababu amesonga mbele mpaka kiasi kwamba anayo thamani ambayo, ikiwa nje ya maumbile inamwezesha yeye kupata utambuzi na hisia ya wajibu.

Si tu kwamba mwanadamu si mfungwa wa mata na uhusiano wa uzalishaji, anao uwezo na mamlaka juu ya nguvu asili na anao uwezo wa kubadili uhusiano wa mata. Kama vile mabadiliko katika vitu vya kimaada yanategemea kwenye sababu za nje, sheria fulani na kanuni zinakuwepo katika jamii ya binadamu ambazo zinaamua kiwango cha maendeleo cha taifa na uwezo, au kushindwa na kuanguka kabisa. Matukio ya kihistoria wala hayategemei dhana pofu ya majaaliwa au ya bahati mbaya; yanakuwa sawa na kanuni na mipango ya maumbile, ambayo miongoni mwao utashi ya mwanadamu unashika nasafi ya muhimu sana.

Katika Aya nyingi za Qur'ani Tukufu, ukandamizaji, uonevu, dhambi, na uovu yanaonyeshwa kubadili historia ya watu fulani, hii ikiwa ni kanuni iliyozingatiwa na jamii zote za binadamu.

وَإِذَا أَرَدْنَا أَن نُّهْلِكَ قَرْيَةً أَمَرْنَا مُتْرَفِيهَا فَفَسَقُوا فِيهَا فَحَقَّ عَلَيْهَا الْقَوْلُ فَدَمَّرْنَاهَا تَدْمِيرًا ﴿١٦﴾

"Na pindi tukitaka kuuteketeza mji huwaamrisha wale wenye starehe na taanusi, lakini wao huendelea kutenda maovu humo. Basi hapo kauli huthibiti juu ya mji huo, nasi tukauangamiza kwa maangamizo makubwa." (17:16).

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦﴾ إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٧﴾ الَّتِي لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِي الْبِلَادِ ﴿٨﴾
وَثَمُودَ الَّذِينَ جَابُوا الصَّخْرَ بِالْوَادِ ﴿٩﴾ وَفِرْعَوْنَ ذِي الْأَوْتَادِ ﴿١٠﴾ الَّذِينَ طَغَوْا فِي الْبِلَادِ ﴿١١﴾
فَأَكْثَرُوا فِيهَا الْفَسَادَ ﴿١٢﴾ فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ﴿١٣﴾ إِنَّ رَبَّكَ لَبِالْمِرْصَادِ ﴿١٤﴾

"Kwani hukuona jinsi Mola wako alivyowafanya watu wa A'di? Na wa Iram wenye majumba marefu? Ambao haukuumbwa mfano wake katika nchi? Na Thamudi walichonga majabali huko bondeni? Na Firauni mwenye vigingi? Ambao walifanya jeuri katika nchi? Wakakithirisha humo ufisadi? Basi Mola Wako aliwapiga na mjeledi wa adhabu. Hakika Mola wako yupo kwenye mavizio anawavizia." (89:6-14).

Qur'ani pia inatukumbusha kwamba wanadamu wanaoabudu matakwa yao na kutii mielekeo yao ya upotofu, husababisha mengi ya majanga ya historia.

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضْعِفُ طَائِفَةً مِّنْهُمْ يُذَبِّحُ أَبْنَاءَهُمْ وَيَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ ۚ إِنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٤﴾

"Hakika Firauni alitakabari katika nchi, na akawagawa wananchi makundi mbalimbali. Akalidhoofisha taifa moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wanaume na akiwaacha watoto wao wa kike. Hakika yeye alikuwa katika mafisadi." (28:4).

فَاسْتَخَفَّ قَوْمَهُ فَأَطَاعُوهُ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَاسِقِينَ ﴿٥٤﴾

"Basi aliwapumbaza watu wake, na wakamtii. Kwa hakika wao walikuwa ni watu wapotovu." (43:54).

Kiasi gani cha umwagaji wa damu, vita, uharibifu na vurugu vimesababishwa na uabudu matamanio yenye shauku kali na uchu wa madaraka! Wanadamu ambao ni kijenzi muhimu katika jamii, wanazo akili na utashi wa asili katika nafsi zao wenyewe, kabla ya kujumuishwa katika

jamii, moyo binafsi haukukosa nguvu mkabala na moyo wa pamoja. Wale wanaodai kwamba mtu binafsi ameamuliwa kabisa katika matendo yake kikamilifu na mazingira ya kijamii wanadhania kwamba kompaundi achanishi ya uhakika ni muhimu ilazimike kuhusisha utengano wa sehemu katika umoja wa kitu kizima ili kuwezesha uhalisi mpya kutokeza. Njia mbadala pekee kwa hili, wao wanavyoamini, itakuwa ni imma kukanusha ukweli wa haki wa jamii kama mchanganyiko wa mtu mmoja mmoja na kukubali uhuru na kujitegemea wa mtu binafsi, au kukubali ukweli wa jamii kama mchanganyiko na kuacha kujitegemea na uhuru wa mtu binaf- si.

Haiwezekani kuunganisha matarajio haya mawili, wanashikilia hivyo. Sasa, ingawa jamii ina uwezo mkubwa zaidi kuliko mtu mmoja, hii haimaanishi kwamba huyo mtu mmoja analazimishwa katika shughuli zake zote za kijamii. Ubora wa maumbile muhimu ndani ya mwanadamu - matokeo ya maendeleo yake katika uwanda wa maumbile - yanampa yeye uwezekano wa kutenda kwa uhuru na kuasi dhidi ya udhia wa kijamii. Ingawa Uislamu unaweka mbele mwenendo na mamlaka kwa jamii, na vile vile kwa uhai na kifo, unamuona mtu binafsi kama mwenye uwezo wa kukataa na kupambana dhidi ya uovu uliopo katika mazingira ya jamii yake; hauoni kuwa katika hali za kitabaka yale mambo yenye kuamua, yanayoelekea kwenye kujitokeza imani zilizo na namna sawa miongoni mwa zile zilizoko chini yao.

Kazi ya kuamrisha mema na kukataza maovu yenyewe ni amri ya kuasi maagizo ya mazingira ya kijamii pale ambapo zinahusisha dhambi na uovu. Qur'ani inasema; 'Enyi mlioamini, kuweni imara katika imani zenu, kwa sababu upotovu wa watu wengine hauwezi kukulazimisheni kuingia kwenye upotvu.' Inaelezwa tena ndani ya Qur'ani Tukufu:

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنفُسِهِمْ قَالُوا فِيمَ كُنتُمْ ۖ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ
قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّـهِ وَاسِعَةً فَتُهَاجِرُوا فِيهَا ۚ فَأُولَـٰئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٩٧﴾

"Hakika wale ambao wametolewa roho na Malaika hali ya kuwa wamezidhulumu nafsi zao, Malaika watawauliza: Katika nini mlipoteza umri wenu? Watasema: Tulikuwa wanyonge ardhini. (Malaika) watasema: Je, ardhi ya Mwenyezi Mungu ilikuwa haina wasaa mkahamia humo? (ili mkayakimbia mazingira hayo; hivyo visingizio vyao havitakubaliwa) Basi hao makazi yao ni Jahannam, nayo ni marudio mabaya." (4:97).

Katika Aya hii, wale wanaojichukulia kama wamelazimishwa kuendana na hali ya jamii, wanalaumiwa sana na kisingizio chao cha kuwafanya washindwe kuwajibika kinakataliwa. Kwa binadamu kuendelea kimaadili na kiroho, kuwepo kwa utashi huru ndani mwake ni kwa lazima. Mwanadamu anayo maadili na maadili yanaweza kutegemewa kutoka kwake, hapo tu ambapo anakuwa huru. Tunapata uhuru wa binafsi na maadili pale tu tunapochagua njia inayoendana na haki na kukataa mwelekeo wa uovu ndani mwetu na mazingira yetu kwa njia ya jitihada zetu wenyewe. Kama tukienda kwa mujibu wa maendeleo ya kawaida au majaaliwa ya migongano ya kimantiki, tutakuwa tumepoteza maadili yote ya haiba.

Halafu, hakuna jambo linalomlazimisha mwanadamu kuchagua njia fulani katika maisha, wala nguvu ya kumshurutisha aache mojawapo. Mwanadamu anaweza kudai kutojitengeneza mwenyewe wakati

anapobahatisha muundo wake kwa mujibu wa sheria zilizopo katika jamii au malengo yaliyoandaliwa kabla, lakini pale tu anapochagua mwenyewe, anaamua na kuwekeza juhudi zake mwenyewe.

19

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA KUMI NA TISA

### HIARI

Watetezi wa kundi hili la kifikra wanasema kwamba mwanadamu anajitambua mwenyewe kwamba anao uhuru katika matendo yake; anaweza kuamua kama atakavyo na akaanzisha mtindo wa bahati yake kwa mujibu wa hiari yake mwenyewe na mwelekeo wake. Uhai ambao huamuru wajibu wa mwanadamu, majuto anayohisi mwanadamu kwa matendo yake fulani anayoyafanya, adhabu ambayo sheria hutoa kwa wahalifu, matendo wanayotekeleza binadamu ili kubadili mwelekeo wa historia, msingi wa sayansi na teknolojia - yote haya ni mambo yanayothibitisha kwamba mwanadamu anao uhuru katika matendo yake.

Vivyo hivyo, suala la wajibu wa kidini wa mwanadamu, kutumwa kwa mitume, ulinganiaji wa ujumbe mtukufu wa ki-Mungu, na kanuni ya ufufuo na hukumu - yote haya yapo mokononi mwa utashi huru na uchaguzi wa mwanadamu katika matendo ayafanyayo. Ingekuwa haina maana kabisa kama Mwenyezi Mungu kwa upande moja, awashurutishe watu kufanya mambo fulani na kwa upande mwingine awalipe thawabu au awaadhibu. Kwa hakika ingekuwa si uadilifu, kama Muumba wa dunia angetuamuru sisi kufuata njia yoyote aliyochagua Yeye, kwa njia ya uwezo Wake na utashi Wake, na halafu atuadhibu sisi kwa matendo ambayo tumeyafanya bila ya hiari zetu.

Endapo matendo ya watu, kwa kweli yangekuwa matendo ya Mwenyezi Mungu basi uovu wote, ufisadi na ukatili lazima ungechukuliwa kuwa ni matendo ya Yake, ambapo dhati Yake tukufu hasa imeepukana na uovu na udhalimu wote huo. Kama usingekuwapo na uchaguzi huru kwa mwanadamu, dhana yote ya uwajibikaji wa mtu kidini ingekuwa sio ya haki. Dikteta mkandamizaji asingestahili kulaumiwa na mwadilifu asingestahili kusifiwa, kwa sababu wajibu una maana pale tu ndani ya nyanja ya nini kinachowezekana na kinachowezekana mtu kukipata.

Binadamu anastahili shutuma au sifa hapo tu ambapo ana uwezo wa kuamua na kutenda kwa uhuru, vinginevyo, pasingekuwepo na suala la shutuma au sifa. Wale wanaoshikamana na msimamo huo hapo juu wamefikia kiwango katika kutetea kanuni ya hiari ya mtu kiasi kwamba wanamuona mtu kama kiumbe chenye hiari kamili isiyopingika katika matendo yake yote ya hiari. Wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hawezi kuendeleza mamlaka yake juu ya hiari na matakwa ya viumbe Vyake na kwamba matendo ya hiari ya wanadamu hayapo kwenye eneo la mamlaka Yake. Huu, kwa ufupi, ndio msimamo wa watetezi wa hiari kamili.

Wale wasemao kwamba ni kanuni za kawaida na hiari ya wanadamu ndivyo vinavyoumba dunia hii ya ajabu, na kwamba si mzunguuko wa dunia wala matendo ya wanaadamu ambavyo vina uhusiano wowote na Mwenyezi Mungu, wanapachika athari zote kwenye mhimili unaopingana na Mwenyezi Mungu. Angalau kidogo sana, wanavifanya viumbe vilivyoumbwa kama washirika wa Mwenyezi Mungu katika maumbile

Yake, au wanamweka mwumbaji kumpambanisha na Mwenyezi Mungu Muumba. Bila kujua wanachukulia kwamba asili za vitu vilivyoumbwa hazitegemei asili ya ki-Mungu.

Kujitegemea kwa kiumbe - kiwe binadamu au kinginecho mbali na mwanadamu - kunaingiza imani kwenye kiumbe hicho na kuwa mshirika wa Mwenyezi Mungu katika matendo Yake na kujitegemea Kwake, kunakomalizikia kwa wazi kabisa katika muundo wa uwili. Hivyo, binadamu anaondolewa kwenye kanuni ya juu sana ya umoja wa ki-Mungu na anatupwa kwenye mtego hatari wa ushirikina. Kukubali fikra za uhuru kamili wa binadamu ingekuwa kumwondolea Mwenyezi Mungu mamlaka Yake kwenye eneo fulani, ambapo kwa kweli, Yeye anaviene a viumbe vyote, kwani tungekuwa tunampa binadamu mamlaka yasiyo na vipingamizi na ya dhahiri kwenye nyanja ya matendo yake huru na ya hiari. Hakuna muumini wa kweli wa upweke wa Mwenyezi Mungu anayeweza kukubali kuwepo kwa uumbaji tofauti na ule wa Mwenyezi Mungu hata katika uwanja wenye mipaka wa matendo ya binadamu.

Wakati tunatambua uhalali wa sababu za asili na vipengele, lazima tuzingatie kuwa Mwenyezi Mungu ni chanzo cha kweli cha utaratibu na matukio yote na tutambue kwamba kama Mwenyezi Mungu angetaka, Angeweza kuutangua hata hapo penye eneo finyu linapotumika na kuufanya usiwe na kazi.

Kama ambavyo viumbe vyote hapa duniani vinavyokosa uhuru katika asili zao, viumbe vyote humtegemea Mwenyezi Mungu, pia vinakosa uhuru katika usababisho na utoaji wa athari. Kwa hiyo, tunayo kanuni ya umoja wa matendo, kwa kwa maana ya kutambua ukweli kwamba mpangilio wote wa maumbile, pamoja na vyanzo na athari zake, sheria na kanuni zake, ni kazi ya Mwenyezi Mungu na ni matokeo ya ridhaa Yake, kila jambo na chanzo linatokana Naye si tu asili ya uhai; lakini pia uwezo wa kutenda na kutoa athari.

Umoja wa matendo hautufanyi sisi tukanushe kanuni ya chanzo na athari na wajibu wake inaouchukua hapa duniani, au kuchukulia kila kitu kuwa kama ni matokeo ya moja kwa moja na yasiyopangwa ya utashi wa Mwenyezi Mungu, kwa namna ambayo kwamba kuwepo au kutokuwepo kwa mambo yasababishayo hakutaleta tofauti. Lakini tusihusishe usababisho huru kwenye mambo hayo, au kudhani kwamba uhusiano wa Mwenyezi Mungu na dunia ni kama ule wa msanii na kazi yake - mathalani, ule wa fundi rangi na kazi yake ya kupaka rangi. Kazi ya usanii inategemea msanii juu ya uanzilishwaji wake, lakini baada ya msanii kumaliza kazi yake, uzuri na mvuto wa kazi hiyo unakuwa huru na msanii huyo, kama msanii akitoweka hapa duniani, kazi yake nzuri sana bado itaendelea kuwepo.

Kudhania uhusiano wa Mwenyezi Mungu na dunia kuwa sawa na aina hiyo ni aina ya ushirikina. Yeyote anaye kanusha nafasi ya Mwenyezi Mungu ndani ya matukio na matendo ya wanadamu, hapo anafikiria kwamba uwezo wa Mwenyezi Mungu unasimama ghafla kwenye mipaka ya maumbile na utashi huru wa mwanadamu. Maoni kama hayo kimantiki hayakubaliki, kwa sababu inakuwa na maana ya kukanusha yote haya;

uwezo wote wa Mwenyezi Mungu, na uwekeaji mipaka ile dhati isiyo na mipaka na ukomo.

Mtu mwenye kuzingatia maoni kama hayo atajiona yeye kama asiye na haja yoyote na Mwenyezi Mungu, jambo ambalo litasababisha awe muasi dhidi Yake na kujiingiza kwenye kila namna ya uovu. Kinyume chake, hisia za kumhitaji Mwenyezi Mungu, za kumtegemea Yeye na kunyenyekea Kwake, zina athari za uhakika juu haiba, tabia na mwenendo wa mwanadamu. Kutotambua chanzo kingine cha amri mbali na Mwenyezi Mungu, kiwe cha ndani au cha nje, uchu wa matamanio na matakwa vitakakuwa haviwezi kumburuza huku na kule, na hakuna mtu mwingine atakayeweza kumtawala kabisa.

Qur'ani Tukufu inamkatalia mwanadamu ushiriki wowote na Mwenyezi Mungu katika kuendesha mambo ya dunia hii:

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّـهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَلَمْ يَكُن لَّهُ وَلِيٌّ مِّنَ الذُّلِّ وَكَبِّرْهُ تَكْبِيرًا ﴿١١١﴾

"Na sema sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye hana mwana, wala hana rafiki wa kumsaidia kwa sababu ya udhaifu wake. Na mtukuze kwa utukufu mkubwa." (17:111).

Aya nyingi sana kwa wazi zinatangaza uwezo kamili na nguvu za Mwenyezi Mungu. Mathalani:

لِلَّـهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا فِيهِنَّ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٢٠﴾

"Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo. Naye ni Muweza wa kila kitu." (5:120),

وَمَا كَانَ اللَّـهُ لِيُعْجِزَهُ مِن شَيْءٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ إِنَّهُ كَانَ عَلِيمًا قَدِيرًا ﴿٤٤﴾

"Hapana kitu kinachoweza kumshinda Mwenyezi Mungu mbinguni wala katika ardhi. Hakika Yeye ni Mwenye kujua, Mwenye uwezo." (35:44).

Viumbe vya dunia hii vinamuhitaji Mwenyezi Mungu kwa ajili ya uhai wao na kuendelea daima, sana kama vinavyohitaji uanzilizwaji wao. Ujumla wa maumbile yote lazima upokee haki ya kuweza kuendelea kuwepo upya kila dakika au kinyume chake ulimwengu wote ungeporomoka. Ubunifu wa nguvu zote hapa duniani unafanana na ubunifu wa Mwenyezi Mungu na ni mwendelezo wa shughuli Zake. Kiumbe ambacho katika dhati yake kinategemea utashi wa ki-Mungu hakina uamuzi huru juu yake chenyewe.

Kama vile ambavyo taa ya umeme zinavyopata mwanga wao kutoka kwenye kituo cha umeme ambacho huwashwa kwanza, hivyo, pia lazima ziendelee kupokea nishati kutoka chanzo kile kile ili ziweze kuendelea kuwaka.

Qur'ani Tukufu inatangaza kwa kuisisitiza wazi wazi:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ أَنتُمُ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّـهِ وَاللَّـهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿١٥﴾

"Enyi watu! Ninyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha, Msifiwa." (35:15).

Asili zote zinatokana na ridhaa Yake na zinamtegemea Yeye; matukio yote wakati wote yanaendelezwa Naye. Utaratibu wenye nguvu na mzuri kabisa wa ulimwengu umeelekezwa kwenye nguzo moja peke yake na huzunguka kwenye mhimili moja pekee. Imam Jafar as-Sadiq (a.s) alisema:

**"Uwezo na nguvu za Mwenyezi Mungu ni vitu vya juu sana kwa jambo lolote kutokea hapa duniani ambalo ni kinyume na ridhaa Yake."**[1]

Kama Mwenyezi Mungu asingetupatia kanuni ya utashi huru na kama kila sekunde Asingetupatia uhai, rasilimali na nishati, kamwe tusingeweza kufanya lolote. Kwani ni kwa sababu ya ridhaa Yake isiyobadilika ambayo imeamua kwamba tufanye matendo ya hiari kwa mujibu wa huru, na hapo kutimiza wajibu ambao Ametupangia. Yeye Ameridhia kwamba mwanadamu lazima ajenge maisha yake ya baadae mwenyewe, mazuri au mabaya, yang'aayo au ya giza, kwa mujibu wa utambuzi na matakwa yake mwenyewe.

Matendo yetu ya hiari halafu yanahusishwa na sisi wenyewe na Mwenyezi Mungu. Tunaweza kutumia rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu ametumilikisha kwa utambuzi kamili ama kwa kujiinua na kujiendeleza wenyewe kwa mujibu wa uchaguzi sahihi, au kujitumbukiza kwenye uovu, dhambi na mambo yaliyokithiri. Kama mambo yalivyo, ukweli unabaki pale pale kwamba upeo wa matendo yetu ya hiari umo nsdani ya mfumo uliokadiriwa; uwezo unatoka kwa Mwenyezi Mungu, na matumizi yake,

Chukulia kwamba mtu fulani ana moyo wa bandia, unaoendeshwa kwa nguvu ya betri ambayo tunaweza kuwasha na kuzima kutoka kwenye chumba cha udhibiti; wakati wowote tunapotaka, tunaweza kuzima swichi na kuusimamisha moyo kufanya kazi. Kile kilichopo ndani ya uwezo wetu ni mkondo wa umeme unaotoka kwenye betri kwenda kwenye moyo; tunaweza kuusimamisha wakati wowote. Lakini maadamu tunairuhusu betri kufanya kazi, huyo mtu ambaye moyo umepandikizwa ndani yake, ataendelea kuwa huru kufanya anavyotaka. Endapo atafanya tendo jema au ovu, bila shaka, itakuwa kwa mujibu wa hiari yake. Namna anavyotumia uwezo ambao tumempa hasa inategemea juu yake na sisi hatuhusiki kabisa.

Hali kadhalika, uwezo wetu unatoka kwa Mwenyezi Mungu na anaweza akatunyang'anya wakati wowote, lakini Ameweka namna amamo ambamo tunautumia uwezo huo hasa, kwa uchaguzi wetu wa moja kwa moja. Madhehebu ya Median. Viumbe vyote duniani vinakuwa na aina ya mwongozo maalum kwa hatua ya maendeleo ambayo vimefikia; aina zao mahsusi za mwongozo huendana na viwango tofauti vya maisha.

Inawezekana sisi kufafanua na kutambua nafasi yetu miongoni mwa viumbe tofauti katika ulimwengu huu. Tunajua kwamba mimea ni mateka mikononi mwa majaaliwa ya nguvu maumbile, wakati huo huo, ikionyesha matokeo fulani madogo ya kimaendeleo kuhusiana na mabadiliko katika mazingira yao.

Tunapo chambua tabia za wanyama, tunahisi kwamba wanazo sifa tofauti kabisa na zile za mimea. Ili waweze kupata lishe zao, wanyama wanapaswa kujiingiza kwenye eneo pana la mishughuliko, kwa kuwa maumbile hayawaaliki kwenye chakula ambapo mahitaji yao ya kilishe yamewekwa mbele yao. Wanyama wanahitaji nyenzo na vifaa fulani katika jitihada zao za kupata chakula, na vitu hivi maumbile yamekwishawapatia Ingawa wanyama wako chini ya mvuto wa nguvu wa silika, na kwa maana hii ni viumbe vinavyotiishwa, wanapata kiwango fulani cha uhuru kwa namna

1. Al-Kafi, I, uk. 160 kutoka kwetu.

ambazo wanaweza kujinasua, kwa kiasi fulani, kutoka kwenye kifungo kikali cha maumbile.

Wanasayansi wanayo maoni kwamba wanyama ambao ni wanyonge zaidi, wana uhusiano na maumbile yao na viungo vyao vya asili, jinsi wanavyokuwa na nguvu zaidi kufuatana na silika zao na jinsi wanapata msaada wa moja kwa moja ulinzi zaidi wa maumbile. Kinyume chake, jinsi walivyoandaliwa kwa unafuu zaidi kuhusiana na uwezo wa kihisia na utambuzi na jinsi kiwango chao cha kujitegemea kinavyozidi kuwa kikubwa, ndivyo ambavyo wanaongozwa na silika kwa kiasi kidogo. Wakati wa kipindi cha mwanzo cha maisha yake, mtoto anafunikwa moja kwa moja na ulinzi mkubwa wa baba na mama yake; jinsi anavyoendelea kukua, hujitoa taratibu kwenye uangalizi wao wa pamoja.

Mwanadamu ambaye amepata kiwango cha juu zaidi cha maendeleo kama kiumbe pekee mwenye uwezo wa utashi huru ya kujitegemea na upambanuzi anacho kiwango cha chini kiasi cha uwezo wa kisilika. Jinsi anavyopata uhuru wake polepole, ndivyo anavyoendelea kushambuliwa na udhaifu kiasi katika uwezo wake wa fahamu.

Maumbile hutosheleza kwa namna mbali mbali mahitaji yote tofauti ya mimea. Kwenye ufalme wa wanyama, ingawa mama analazimika kufanya jitihada fulani kumbeba, kumlea na kumlinda mtoto wake, silika hutokeza mapema kwa mtoto na mama hahitaji kujihusisha na kumzoesha na kumfundisha silika hizo. Lakini kwa upande wa binadamu, tunaona kwamba hana silika za asili zenye nguvu, na uwezo wake wa kukataa mambo yasiyofaa na ya kuchukiza ya kimazingira ni dhaifu sana kuliko ule wa wanya- ma. Hivyo utegemezi wake kwa wazazi wake unaendelea kwa miaka mingi hadi hatimaye anapopata kujitegemea na kujitosheleza na akaweza kusimama kwa miguu yake mwenyewe.

Qur'ani Tukufu inasema wazi wazi kuhusu unyonge na udhaifu wa mwanadamu:

يُرِيدُ اللَّـهُ أَن يُخَفِّفَ عَنكُمْ ۚ وَخُلِقَ الْإِنسَانُ ضَعِيفًا ﴿٢٨﴾

"Mwenyezi Mungu anataka kukupunguzieni taabu, na mwanadamu ameumbwa dhaifu." (4:28).

Maumbile yamemwachia mwanadamu kwenye mbinu zake zaidi sana kuliko wanyama. Kwa mwanadamu tunaona, kwa upande moja, kujifunua kwa uhuru na kujitokeza kwa uwezo wa kukua na kupata utambuzi, na kwa upande mwingine, ongezeko utegemezi na uhitaji. Wakati mwanadamu anapokuwa na uhuru kiasi fulani, huendelea kuvutwa kwa nguvu sana kuingizwa ndani na ndani zaidi kwenye utumwa wa kuhitaji.

Hali hizi zinazotofautiana ya mipango tofauti ya maumbile, kwa mtazamo wa mabingwa fulani huunda vipengele ambavyo vinavyochochea ukuaji na maendeleo. Jinsi kiumbe anavyosonga mbele kwenye ngazi ya maendeleo, ndivyo kinavyokaribia kwenye uhuru. Kwa usahihi, ni kuhitaji na kukosa uwiano wa kihulka ndiko ambako huwezesha kukua na maendeleo kufanyika.

Kuhusu hiari na fursa ya kujieleza wao wenyewe, kipengele kinachopinga silika ya asili lazima kiwepo. Halafu, mwanadamu atanasa kati ya mivuto miwili inayopingana, kila mmojawapo ukitafuta kupata utii wake, hivyo kwamba analazimika kuchagua njia aitakayo, kwa hiari yake,

akiwa anatambua, na kutegemea jitihada na maarifa yake. Akiwa huru kutokana na mambo yenye maamuzi na mawazo ya kabla ya kiakili, huanza kazi ya kujitengeneza na kujiendeleza mwenyewe katika misingi ya kanuni maalum na mifano.

Pindi anapokabiliwa na dalili hii ya hitilafu, mwanadamu hawezi kupata msimamo au kujichagulia njia yake sahihi kwa kujifanya kama mtambo unaojiendesha wenyewe au kuacha jitihada zote. Akibeba kama anavyofanya kwa mzigo wa dhamana ya ki-Mungu; ile zawadi kubwa ya ki-Mungu ambayo mbingu na ardhi havikustahili kupokea, mwanadamu pekee akithibitisha kustahili kuipokea, basi mwanadamu anakabiliwa na fursa mbili tu katika mgongano wake na harakati zake. Ama anakuwa mfungwa wa udikteta wa silika na matamanio yasiyodhibitika, hivyo kujijishusha hadhi na kujivunjia heshima, au kutoka kwenye uwezo wake mkubwa wa hiari, fikra na uamuzi, anaingia kwenye njia ya ukuaji na maendeleo na kuanza kupanda.

Wakati wowote kiumbe anapoachwa huru kutokana na utii wa kushurutishwa kwenye silika, hutupa minyororo ya utumwa, na kiumbe kutumia uwezo wa hulka na ule wa kutafuta; uelekevu wake wa fahamu unadhoofishwa na uwezo wake wa kiasili hupungua. Sababu ya hili ni kwamba kiungo chochote au uwezo ukiachwa umetulia na bila kutumika ndani ya kiumbe hai huwa kinadhoofika polepole. Kinyume chake jinsi kiungo au uwezo kitakavyotumika sana ndivyo kitakavyoendelea kukua na kujazwa nguvu.

Hivyo, pale mwanga wa utambuzi wa mwanadamu na hiari ya ubunifu, vinapotiwa msukumo na uwezo wa upambanuzi na akili, huangaza njia yake na kuamua matendo yake, uwezo wake wa utambuzi na fikra humwezesha kugundua ukweli na uhalisia mpya. Zaidi ya hayo, hali ya kutatizwa kwa binadamu na kusita kati kati ya nguzo mbili zinazopingana humwelekeza kutafakari na kuchambua, hivyo kwamba kwa kutumia busara anaweza kutofautisha kati ya njia iliyonyooka na njia potofu. Hii itamaamsha uwezo wake wa kiakili, itaimarisha uwezo wake wa tafakari, na kumpatia kiwango kikubwa zaidi cha nyendo na nguvu tele.

Umilikaji - tamaa ya uhuru, sayansi na ustaarabu - yote haya ni matokeo ya moja kwa moja ya mazoezi ya binadamu ya hiari yake. Pindi mtu anapopata uhuru na akaendeleza jitihada zake muhimu na za uhakika, anaweza kuendelea haraka katika hatua ya ukuaji na udhihirikaji wa vipengele vyote vya hulka yake, na tabia muhimu. Vipaji vyake na uwezo wake vitakapokomaa, atabadilishwa na kuwa chanzo cha manufaa na maadili katika jamii.

Tunaona matokeo ya hiari kila mahali, na mapambano yanayoendeshwa dhidi ya watetezi wake kutoka kwa wale ambao wanapinga jambo hili kwenyewe ni dalili ya wazi kwamba hawa wa mwisho, bila kutajwa bayana, wanalikubali hili.

Sasa, hebu tuone ni mipaka gani imewekwa kwenye uwezo wa kuchagua wa binadamu na ni uwezo gani anakuwa nao katika kutumia uelekevu huu. Fikra thabiti ya Shia, ambayo imechukuliwa kutoka kwenye Qur'ani na maneno ya Maimamu, inawakilisha madhehebu ya tatu, yaliyopo katikati ya wanaoitakidi majaaliwa na watetezi wa hiari kamilifu. Madhehebu haya

hayasumbuliwi na upungufu na udhaifu wa madhehebu ya kuamini majaaliwa, ambayo inapingana na akili, dhamira na mifano yote ya kimaadili na kijamii na hukanusha uadilifu wa Mwenyezi Mungu kwa kumhusisha Yeye na uovu na udhalimu wote unaotokea, wala kwa kushikilia msimamo wa hiari dhahiri sio kwamba kunakanusha upekee wa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kukataa upweke wa matendo ya Mwenyezi Mungu.

Ni dhahiri kwamba matendo yetu ya hiari hutofautiana na mienendo ya jua, mwezi na dunia, au nyendo wa mimea na wanyama. Uwezo wa hiari hutokea ndani mwetu na hutuwezesha kufanya au kutokufanya matendo fulani, hivyo kutupatia sisi uhuru wa kuchagua. Uwezo wetu wa kuchagua kwa hiari ama kufanya matendo mema au maovu hutokea kwenye uwezo wa kupambanua unaotumika kwa uhuru kamili. Lazima tutumie kipaji chetu cha uhuru wa kuchagua kwa makini sana; kwanza lazima tutafakari kiutu uzima na kwa uangalifu, tupime vitu kwa usahihi na halafu tufanye uchaguzi uliokusudiwa. Ni ridhaa ya Mwenyezi Mungu kwamba tutumie hiari yetu kwa njia hii katika dunia hii ambayo Ameiumba, kwa utambuzi na tahadhari.

Chochote tunachofanya ni wazi kwamba kimo kwenye upeo wa kitangulizi cha ujuzi na utashi wa Mwenyezi Mungu. Vipengele vyote vya maisha, vyote vinavyogusa hatima ya binadamu, kimewekewa mipaka na, pia na kwa masharti juu ya elimu Yake; kinafafanualiwa na mipaka ambayo tayari ipo kwenye ujuzi wa Mwenyezi Mungu. Zaidi ya hayo, sisi hatuko huru hata kwa sekunde moja kutokana na kuihitaji Dhati hiyo ambayo tumeunganishwa nayo, na matumizi ya uwezo wa asili katika maisha yetu hauwezekani bila ya msaada wa Mwenyezi Mungu wenye kuendelea. Kwa uwezo Wake mkuu kabisa, wenye kupita kiasi, Yeye anatuangalia kwa karibu sana, na kwa namna ambayo ipo nje ya udhaniaji wetu, Anao utambuzi kamili na mamlaka juu ya nia zetu zote na matendo yetu. Hatimaye, hiari zetu haziwezi kuvuka mipaka ya utaratibu ulioanzishwa na Mwenyezi Mungu katika maumbile haya, na kwa hiyo, hausababishi tatizo lolote kuhusu upweke wa matendo ya Mwenyezi Mungu.

Wakati akiwa anao uwezo wa kusababisha athari katika dunia hii kwa njia ya hiari yake, binadamu, yeye mwenyewe anatawaliwa na mlolongo wa sheria za asili. Anaingia duniani bila ya uchaguzi wowote kwa upande wake, na anafumba macho yake hapa duniani bila yeye mwenyewe kutaka kufanya hivyo. Maumbile yamemfunga kwa pingu za silika na mahitaji. Hata hivyo, binadamu anakuwa na nafasi na uwezo fulani; uhuru huzaa ubunifu ndani mwake ambao unamwezesha kutiisha maumbile na kuasisi utawala juu ya mazingira yake.

Imam Jafar as-Sadiq (a.s) alisema: **"Ukweli wa jambo haukai kati ya mambo haya mawili haya; wala si katika majaaliwa au hiari."**[1]

Kwa hiyo hiari inakuwepo, lakini haijumuishi kila kitu, kwa sababu kuweka fani tofauti kwa ajili ya binadamu itakuwa sawa na kumpa Mwenyezi Mungu mshirika katika matendo Yake. Hiari ambayo mwanadamu anakuwanayo imeridhiwa na Muumba wa asili, na amri ya

1. A-Kafi, 1, uk.160 Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu hudhihirika yenyewe katika muundo wa desturi na kanuni ambazo zinamtawala binadamu na maumbile yote, uhusiano wa asili, vyanzo na vipengele.

Kwa mtazamo wa Uislamu, binadamu wala si kiumbe cha kutengenezwa tayari, kinachokusudiwa kwenye kuamuliwa na majaaliwa, wala hakutupwa kwenye mazingira ya giza na yasiyo na malengo. Binadamu ni kiumbe kinachojawa na matumaini, vipaji, ustadi, ujuzi wa kubuni na mielekeo mbali mbali, ikiambatana na aina ya mwongozo uliojengeka mwilini. Kosa ambalo limefanywa na wenye kuamini katika majaaliwa na watetezi wa hiari isio na mipaka ni kwamba wamemdhani mwanadamu kuwa na njia mbili tu mbele yake: ama matendo yake yote lazima yahusishwe moja kwa moja kwa Mwenyezi Mungu, ili kwamba halafu apoteze uhuru wote na awe amekadiriwa katika matendo yake, au tunawajibika kukubali kwamba matendo yake ya hiari yanatokana na dhati inayojitegemea na isio na mipaka, maoni ambayo yanaingiza mipaka kwenye uwezo wa

Hata hivyo, ule ukweli kwamba tunayo hiari hauathiri upeo wa uwezo wa Mwenyezi Mungu, kwa sababu Ameridhia kwamba tufanya maamuzi yetu wenyewe kwa uhuru kabisa, kwa mujibu wa kanuni na desturi ambazo ameziweka. Kutoka kwenye mtazamo moja, matendo na kazi za binadamu yanaweza kuhusishwa naye mwenyewe, na kutoka kwenye mtazamo mwingine, yanahusishwa kwa Mwenyezi Mungu. Binadamu anao uhusiano wa moja kwa moja na wa haraka na matendo yake ambapo uhusiano wa Mwenyezi Mungu na matendo hayo sio wa moja kwa moja, lakini aina zote za uhusiano ni halisi na kweli. Imma hiari ya binadamu haiwezi kujiweka kwenye kupingana na utashi wa ki-Mungu, wala utashi wa binadamu hauko kinyume na kile anachokitaka Mwenyezi Mungu.

Watu wakaidi waioazimia kutokuamini, ambao wanapinga aina zote za mawaidha na maonyo, mwanzoni kabisa, wanachukua msimamo wao wa kimakosa kupitia matumizi ya hiari, halafu wanayaelewa matokeo ya ukaidi na upotofu wao wa moyo, kama adhabu, waliyoadhibiwa na Mwenyezi Mungu.

Kwa kutii matamanio ya nafsi zao duni, watu hawa madhalimu wanazuia nyoyo zao, macho yao na masikio yao kutokufanya kazi, na kama matokeo, huvuna hali ya kuteseka milele. Qur'ani inasema:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَأَنذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ خَتَمَ اللَّـهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَعَلَىٰ سَمْعِهِمْ ۖ وَعَلَىٰ أَبْصَارِهِمْ غِشَاوَةٌ ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٧﴾

"Hakika wale waliokufuru ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawataamini. Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao, na juu ya macho yao pana kifuniko. Basi watapata adhabu kubwa." (2:6-7).

Wakati mwingine uovu na dhambi sio vya ukubwa kiasi kwamba vinafunga njia ya kurejea kwa Mwenyezi Mungu na ukweli. Lakini katika nyakati zingine yanaweza kufika kiwango kwamba kurudi kwenye utambulisho wa kweli wa kibinadamu inakuwa haiwezekani; halafu muhuri wa ukaidi unapigwa kwenye nafsi za wasioamini zilizochafuliwa. Haya ni matokeo ya kawaida kabisa ya tabia yao, yaliyoamuliwa na utashi na matakwa ya Mwenyezi Mungu.

Kuwajibika kwa watu kama hao huazia matumizi ya hiari zao, na ukweli kwamba hawakupata baraka za mwongozo, haupunguzi kuwajibika kwao. Ipo kanuni imara na inayojidhihirisha yenyewe inayosema kuwa "chochote kinachoanzia kwenye hiari na kuishia kwenye lazima hakipingani na hiari." Imamu anasimuliwa kuwa amesema: **"Mwenyezi Mungu alitaka kwamba mambo yatokee kupitia vyanzo na njia za msaada, na hakuamuru chochote isipokuwa kwa msaada wa chanzo; kwa hiyo, akaumba chanzo cha vitu vyote."**[1]

Mojawapo ya vyanzo kilichotumiwa na Mwenyezi Mungu katika uumbaji Wake ni binadamu na utashi wake, kwa kuendana na kanuni kwamba vyanzo na njia maalum vimeanzishwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kutokea kila tukio hapa ulimwenguni: kutokea kwa tukio hulazimisha kuwepo kabla kwa vyanzo na njia husika, na kama isingekuwa kwa ajili ya hivyo, matukio hayo yasingetokea.

Hii ni kanuni ya jumla ambayo bila kipingamizi inatawala matendo yetu ya hiari vilevile. Fursa ya uchaguzi wetu na hiari vinakuja kufanya kiungo cha mwisho katika mnyororo wa vyanzo na njia ambavyo huishia utendaji wa kitendo kwa upande wetu.

Aya za Qur'ani ambazo zinahusisha vitu vyote kwa Mwenyezi Mungu na kuonyesha kama vinatokana Naye vinahusika na kutangaza utashi wa tangu kabla wa Mwumbaji kuwa ndio msanifu wa ulimwengu na kuelezea jinsi uwezo Wake unavyojumuisha na kupenya ndani ya mtiririko mzima wa uhai. Uwezo wake unaenea katika kila sehemu ya ulimwengu, bila kubakisha kitu, lakini nguvu za Mwenyezi Mungu zisizopingwa hazipunguzi utashi wa mwanadamu. Kwani ni Yeye ambaye anaifanya hiari hiyo kuwa sehemu ya mwanadamu, na ni Yeye anayeiweka juu ya mwanadamu huyo. Amemfanya binadamu kuwa huru kufuata njia anayochagua mwenyewe na hamuwajibishi mtu au watu kwa sababu ya dosari za mwingine.

Kama kuna lazima yoyote katika mambo ya binadamu, ni katika maana tu kwamba analazimika kuwa na hiari, kama matokeo ya utashi wa Mwenyezi Mungu, si kwa maana kwamba anahukumiwa kutenda kwa namna iliyoelekezwa. Kwa hiyo tunapofanya matendo mema bora zaidi, uwezo wa kuyatenda hayo unatoka kwa Mwenyezi Mungu, na fursa ya kutumia uwezo huo inatoka kwetu.

Aya nyingine za Qur'ani zinasisitiza kwa wazi kuhusu nafasi ya utashi wa binadamu na matendo, kwa dhahiri zikikataa kabisa maoni ya wenye kuamini majaaliwa. Inapotaka kuelekeza uzingativu wa binadamu kwa majanga na mateso anayoyavumilia katika dunia hii, huyaelezea kama ni matokeo ya matendo yake maovu. Kwenye Aya zote zinazohusu utashi wa Mwenyezi Mungu, hakuna hata moja inayoweza kupatikana kuhusisha matendo ya hiari ya binadamu kwenye utashi wa Mwenyezi Mungu. Hivyo Qur'ani inatangaza:

﴿فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٨﴾

1. Al-Kafi, 1, uk.183.

"Basi anayetenda lau chembe ndogo ya wema, ataiona! Na anayetenda chembe ya uovu atauona." (99 :7-8)

وَلَتُسْأَلُنَّ عَمَّا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾

"Na hakika mtaulizwa kwa yale mliyokuwa mkiyafanya." (16: 93).

سَيَقُولُ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَاءَ اللَّـهُ مَا أَشْرَكْنَا وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَّمْنَا مِن شَيْءٍ كَذَٰلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ حَتَّىٰ ذَاقُوا بَأْسَنَا قُلْ هَلْ عِندَكُم مِّنْ عِلْمٍ فَتُخْرِجُوهُ لَنَا إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ أَنتُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ ﴿١٤٨﴾

"Watasema wale walioshirikisha: Lau kuwa Mwenyezi Mungu angetaka tusingelishiriki sisi, wala baba zetu; wala tusingaliharamisha kitu chochote. Vivi hivi walikanusha waliokuwa kabla yao mpaka walipoonja adhabu yetu. Sema: Je, nyinyi mnayo ilimu mtutolee? Nyinyi hamfuati ila dhana. Wala hamsemi ila uwongo tu. (6:148).

Kama wokovu na upotofu wa binadamu ungekuwa utegemee ya utashi wa Mwenyezi Mungu, kusingekuwepo na dalili ya upotofu na udhalimu hapa duniani, wote wangefuata njia ya wokovu na haki, iwe wametaka au la. Wahalifu fulani wanaojitafutia visingizio vyao wamedai kwamba matendo yoyote ya dhambi watakayoyafanya yanaridhiwa na kupendelewa na Mwenyezi Mungu. Hivyo Qur'ani inasema:

وَإِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً قَالُوا وَجَدْنَا عَلَيْهَا آبَاءَنَا وَاللَّـهُ أَمَرَنَا بِهَا قُلْ إِنَّ اللَّـهَ لَا يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّـهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾

"Na wanapofanya mambo machafu husema: Tumewakuta nayo baba zetu, na Mwenyezi Mungu ametuamrisha hayo, Sema: Hakika Mwenyezi haamrishi mambo machafu. Mnamzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua?" (7:28).

Kwa namna ile ambayo Mwenyezi Mungu ameridhia thawabu kwa matendo mema, ndivyo, pia ambavyo Ameridhia adhabu dhidi ya dhambi na uovu, lakini katika mifano yote miwili, kuridhia matokeo ni tofauti na kuridhia kitendo kinachosababisha matokeo. Uhai wa binadamu na athari za kawaida za matendo yake ni kweli yanategemea ridhaa ya Mwenyezi Mungu, lakini matendo yake ya hiari hutegemea utashi wake mwenyewe.

Mtazamo wa Uislamu, kama unavyotambuliwa na Shia, ni kwamba mwanadamu hana hiari kamili kiasi hicho, hivyo kwamba anaweza kufanya matendo nje ya mfumo wa ridhaa ya Mwenyezi Mungu na utashi Wake, ambao unachukua ulimwengu wote katika miundo ya sheria na kanuni za kudumu, hivyo kumshusha Mwenyezi Mungu kuwa kitu dhaifu na kinyonge anapokabiliwa na utashi wa viumbe Vyake mwenyewe. Wakati huo huo, binadamu pia sio mfungwa wa utaratibu ambao unamzuia kuchagua njia yake mwenyewe katika maisha na kumlazimisha, kama wanyama, kuwa mtumwa wa silika zake.

Qur'ani Tukufu inasema wazi kwenye Aya zake kwamba Mwenyezi Mungu amemuonyesha binadamu njia ya wongovu, bali analazimika imma kukubali mwongozo na ukombozi ama kuangukia kwenye upotofu na uovu:

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

"Hakika sisi tumembainishia njia. Ama ni mwenye kushukuru, au ni mwenye kukufuru."(76:3).

Kwa hiyo, kuvihusisha vitendo vya hiari vya binadamu kwa Mwenyezi Mungu, kunakataliwa na Qur'ani Tukufu.

20

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA ISHIRINI

### MIUNDO YA RIDHAA ZA MWENYEZI MUNGU NA HIARI

Majaaliwa na hatima ni mojawapo ya hizo mada zinazoelekea kuleta ubishi na ambazo mara nyingi zinatafsiriwa vibaya kwa sababu ya kukosa kuelewa kwa usahihi au, wakati mwingine, kwa nia mbaya. Ili tuweze kuigundua mada hii, tutaifanyia uchambuzi hapa kwa muhtasari kwa kadiri iwezekanavyo.

Kila kitu hapa duniani kimeegemezwa kwenye mpango uliokadiriwa kwa usahihi, mantiki na kanuni. Kimewekwa mahali pake kwa mujibu wa kipimo sahihi, na kinapata tabia zake bainifu kutoka kwenye vyanzo na vipengele kinavyovitegemea. Kama vile ambavyo kila kiumbe hupata uhai wake muhimu kutoka kwenye chanzo chake maalum, pia hupata sifa zake zote za nje na ndani kutoka kwenye chanzo hicho hicho; kinapata umbo lake na ukubwa kutoka kwenye chanzo hicho. Kwa kuwa kuna hali ya ulinganifu baina ya chanzo na athari, hicho chanzo bila kipingamizi hupitisha kwenye athari tabia zile yenye uhusiano na asili yake chenyewe.

Filosofia ya maisha ya Uislamu, majaaliwa na hatima, ni mambo yenye maana ya amri ya Mwenyezi Mungu kuhusu kudhihiri kwa mambo ya dunia, ukubwa na mipaka yao. Matukio yote ambayo hutokea kwenye utaratibu wa maumbile, pamoja na matendo ya mwanadamu, yanakuwa yamepangwa na kuwa ya uhakika kwa njia ya vyanzo vyao; kuwa kwao ni matokeo ya uhalali ulimwenguni kote wa kanuni ya usababisho. Majaaliwa (qada') ina maana ya kitu kilichofikishwa mwisho wake na kisichogeuzika, na marejeo yake ni kwenye ubunifu na matendo ya Mwenyezi Mungu. Hatima (qadar) ina maana ya ukubwa au uwiano na inaashiria asili na sifa ya utaratibu wa maumbile, mwenendo wake wenye utaratibu; maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu ameupatia ulimwengu wa viumbe muundo uliopangwa wenye utaratibu. Kwa maneno mengine, hatima ni matokeo ya usanifu Wake kama inavyoacha athari zake kwenye vitu vyote vilivyoumbwa.

Kwa kuelezea kwa namna tofauti, maana ya hatima ni uwekaji mipaka na uwiano wa nje na ya busara ya kitu sio kiakili. Kabla hajatekeleza mpango wake, msanifu majengo atatayarisha kichwani mwake ubora na vipimo vya jengo analotaka kujenga. Qur'ani inasema kuhusu miundo hii iliyopangwa, tabia na uwiano wa vitu kama Qadar:

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾

"Kwa hakika sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo." (54:49),

قَدْ جَعَلَ اللَّـهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا ﴿٣﴾

"Mwenyezi Mungu amekijaalia kila kitu na kipimo chake." (65:3).

Neno, majaaliwa (qadar) kwenye Qur'ani maana yake ni mahitaji yenye uwiano na ya kawaida, sehemu zote za chanzo zinazoelekeza katika kutokeza kitu. Inamaanisha kwamba utashi wa Mwenyezi Mungu

utajitekeleza wenyewe pale tu ambapo kadiri, mazingira na vyanzo vya kitu vinafungamanishwa na kila kimoja chao.

Mwenyezi Mwenyezi Mungu anazingatia hali ya nafasi na muda ya matukio yote, pamoja na mipaka na uwiano wao, na halafu hutoa hukumu Yake katika misingi ya hayo. Jambo lolote lile au chanzo chochote kile kinachoonekana hapa duniani ni udhihirisho wa utashi wa Mwenyezi Mungu na ujuzi na chombo cha kutimiza kile alichokijaalia.

Uwezo wa ukuaji na maendeleo umekadiriwa kwenye kiini chenyewe hasa cha kila kitu. Mata, ambayo hutegemea sheria ya msogeo, ina uwezo wa kujitwalia maumbo tofauti na kupita kwenye taratibu tofauti nyingi. Chini ya athari ya mambo tofauti, hujitwalia jamii nzima ya hali na sifa tofauti. Hupata nishati kutoka kwenye vipengele fulani asilia ambayo huiwezesha kusonga mbele, lakini inapokutana na vipengele vingine fulani, hupoteza uhai wake na kutoweka kabisa. Wakati mwingine huendelea kusonga mbele kupitia hatua tofauti hadi inapokaribia kwenye kiwango cha juu zaidi cha maendeleo; wakati mwingine, inakosa ile kasi muhimu ya kuendelea kwenye hatua zingine zaidi za maendeleo na kusonga kwa kujikongoja. Kwa hiyo, matokeo ya mambo hayakuunganishwa moja kwa moja na majaaliwa na hatima kwa sababu chanzo ndio kinacho bainisha namna ya athari. Kwa kuwa vitu vinauhusiano na aina mbali mbali za vyanzo, ni lazima kwamba vitafuata njia mbalimbali; kila chanzo hukiweka kile kiumbe kilicho chini yake kwenye njia maalum.

Fikiria mtu anasumbuliwa na maradhi ya kidole tumbo. Hii ni 'hatima' itokanayo na chanzo maalum. 'Hatima' zingine tofauti mbili za ziada zinamngojea mgonjwa huyu; ama anakubali kufanyiwa upasuaji, ambapo matokeo yanayo tarajiwa ni kupona, au akatae kufanyiwa upasuaji ambapo matokeo yake ni kifo. Chaguzi zote hizi mbili zinawakilisha aina ya hatima.

Hatima zinaweza kubadilishana lakini uamuzi wowote utakaochukuliwa na mgonjwa na kuzitekeleza hautakuwa nje ya upeo ambao Mwenyezi Mungu ameujaalia. Mtu hawezi akakaa na kukunja mikono na kujiambia mwenyewe; 'kama haya ndio majaaliwa yangu, nitabakia hai, na kama sio majaaliwa yangu, nitakufa, hata kwa juhudi ya kiasi chochote nitakazofanya ili kutibiwa.' Kama ukitafuta tiba na ukapona, huu ndio mustakabali wako, na kama unakataa tiba na unakufa, pia huo, ndio mwisho wako. Popote uendako na lolote ufanyalo, upo katika kuzungukwa na hatima. Watu ambao ni wavivu na hukataa kufanya kazi, kwanza huamua kutokufanya kazi na halafu wanapokosa fedha, wanatupia lawama zote kwenye majaaliwa. Endapo wangekuwa wameamua kufanya kazi, fedha walizopata zingekuwa sawa na matokeo ya majaaliwa. Hivyo basi, hata kama wewe ni mtu mwenye bidii na jitihada au mvivu, kwa jinsi yoyote ile hujavunja kanuni ya majaaliwa.

Mabadiliko katika hatima, hayana maana ya kipengele fulani kuasi dhidi ya majaaliwa au upinzani dhidi ya kanuni ya usababisho. Hakuna jambo linalosababisha athari hapa duniani ambalo linaweza kusamehewa kuepukana na kanuni ya usababisho ya kilimwengu. Kitu kinachosababisha mabadiliko kwenye hatima, chenyewe ni kiunganishi katika mlolongo wa usababisho, udhihirishao mmoja wa majaaliwa na hatima. Kusema kwa

namna nyingine tofauti, hatima moja hubadilishwa kwa njia ya hatima nyingine.

Tofauti na elimu ambazo huelekea upande mmoja tu na kutoa mwelekeo fulani tu wa vipengele vya matukio, sheria za metafizikia hazihusiki na matukio katika mtizamo wa muungano wa matukio ingawa sheria hurekebisha matukio, hayajali uhusiano wa mwelekeo yanaouchukua. Kwa kweli, matukio yenyewe na mwelekeo wao yanategemea sheria pana na nyingi za metafizikia: mwelekeo wowote ule matukio yatayochukua, bado yapo kwenye mjumuiko wa sheria ambamo haviwezi kuepuka. Hali ni kama ile ya uwanda mpana na mkubwa sana; hata zile sehemu zake za upeo wa kaskazini na kusini zimejumuishwa kwenye uwanda huu.

Kwa ufupi, majaaliwa na hatima haziwakilishi chochote zaidi ya ueneaji wa kanuni ya usababisho ulimwenguni kote, huwakilisha ukweli wa metafizikia ambao haupimiki kama takwimu za sayansi. Kanuni ya usababisho husema tu kwamba kila tukio lina chanzo chake, yenyewe haiwezi kufanya utabiri, hii ikiwa ni tabia ambayo haipo kabisa kwenye utambuzi wa kimetafizikia. Kwa sheria za metafizikia, ambao ni muundo wa ujuzi unaojieleza na msingi madhubuti na imara kwa ajili ya matukio mbali mbali ya dunia, hautofautishi ni tukio gani mahsusi linatokea. Hii ni njia kuu ambayo wanadamu hupita katika safari yao kwa sababu umadhubuti na uimara wake haujali kabisa ni upande gani wanakoelekea.

Amirul-Mu'minin Ali (a.s), alikuwa anapumzika kwenye kivuli cha ukuta uliovunjika ambao ulielekea kuanguka. Ghafla alinyanyuka na akaenda kuketi kwenye kivuli cha ukuta mwingine. Aliulizwa: "Unakimbia lile ambalo Mwenyezi Mungu amelikadiria?" Alisema, "Ninakimbilia kwenye hifadhi ya Mwenyezi Mungu kutokana na lile ambalo Amelikadiria," akimaanisha, "Ninakimbia kutoka kwenye jaala moja na kwenda kwenye jaala jingine. Vitendo vyote viwili kuketi na kunyanyuka vilikuwa vipo kwenye majaaliwa sawa. Endapo ukuta uliokatika ukiniangukia na nikaumia, hayo yatakuwa majaaliwa na hatima, na kama nikiondoka kutoka kwenye eneo la hatari na kuepuka madhara yote, hayo pia ni majaaliwa na hatima."

Qur'ani Tukufu imeeleza kama kanuni, mifumo na sheria za asili ambazo hutawala juu ya dunia na kufuata njia zisizobadilika na zisizoepukika:

وَلَن تَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّـهِ تَبْدِيلًا ﴿٦٢﴾

"..........wala hutapata mabadiliko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu." (33:62).

Kanuni ya hukmu ya Mwenyezi Mungu isiyoepukika, miongoni mwa mambo mengine, inahukumu kwamba:

وَعَدَ اللَّـهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ...﴿٥٥﴾

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakafanya matendo mema, bila shaka atawafanya makhalifa katika ardhi....." (24:55).

Kwa mujibu wa Qur'ani, hii pia ni kanuni ya Mwenyezi Mungu isiyoepukika:

إِنَّ اللَّـهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ... ﴿١١﴾

".....Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo katika nafsi zao....." (13:11).

Kwa mtazamo wa kidini wa falsafa ya maisha, ukweli haukuwekewa mipaka kwenye eneo la usababishaji wa vitu. Matukio hayatakiwi kufikiriwa katika uhusiano wa utambuzi wa hisia tu na ukubwa wa mambo. Vipengele, visivyo vya kimaada vinaweza kufika kwenye nyanja ambazo vipengele vya maada vimefungiwa kabisa, na vina wajibu huru na wenye maamuzi katika kutokea kwa matukio.

Kwa hali yoyote ile dunia haijiingizi katika utofautishaji baina ya wema na uovu; matendo ya mtu hutoa athari fulani wakati wa maisha yake. Wema na ukarimu kwa wenzake wengine na upendo na huduma kwa viumbe vya Mwenyezi Mungu ni mambo ambayo kupitia njia zisizokuwa za kimaada, hatimaye husababisha mabadiliko ya hatima ya binadamu na huchangia kuwepo kwa utulivu furaha, na neema nyingi. Ukandamizaji, unyang'anyi, ubinafsi, uvamizi pia huzaa matokeo machungu na matokeo yake lazima yawe mabaya. Kwa hiyo, kwa mtazamo huu, aina fulani ya kulipa kisasi ni asili katika maumbile, kwani dunia ina utambuzi na ufahamu, inaona na kusikia. Namna ambayo hulipa matendo ni mojawapo ya udhihirisho wa majaaliwa na hatima, haiwezekani kulikimbia hilo, kwani popote utakapokwenda litakukamata.

Mtaalamu mmoja wa sayansi anasema: "Usiseme dunia haina utambuzi, kwani utakuwa umejishutumu mwenyewe kwa kukosa utambuzi. Wewe umekuja kuwepo kama sehemu ya dunia, na endapo hakuna utambuzi duniani pia wewe huna utambuzi." Kuhusu wajibu wa mambo yasiyo ya kimaada katika kuunda hatima. Qur'ani inasema yafuatayo:

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ آمَنُوا وَاتَّقَوْا لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ وَلَـٰكِن كَذَّبُوا فَأَخَذْنَاهُم بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٦﴾

"Na kama watu wa miji wangeamini na kuwa wacha-mungu, lazima tungewafungulia baraka za mbingu na ardhi, lakini walikadhibisha, tutawaangamiza kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma."(7:96).

وَمَا كَانَ رَبُّكَ مُهْلِكَ الْقُرَىٰ حَتَّىٰ يَبْعَثَ فِي أُمِّهَا رَسُولًا يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا وَمَا كُنَّا مُهْلِكِي الْقُرَىٰ إِلَّا وَأَهْلُهَا ظَالِمُونَ ﴿٥٩﴾

"Na Mola wako haangamizi miji mpaka ampeleke Mtume katika mji wao mkuu, awasomee Aya zetu: Wala hatuiangamizi miji mpaka watu wake wawe wamekuwa madhalimu." (28:59).

Dhana za majaaliwa na hatima zinatolewa na watetezi wa kadari kama mojawapo ya uthibitisho wao. Kwa maoni yao, haiwezekani kwa tendo lolote kufanywa na mtu yeyote kwa uhuru, kwani Mwenyezi Mungu amekwisha yakadiria matendo ya mtu, ya jumla na ya hususia, mabaya na mema, hivyo kwamba hakuna nafasi inayobakia kwa ajili ya matendo ya hiari upande wake.

Kuna tofauti baina ya kadari na hatima isiyobadilika. Kila tukio litaelekea kutokea pindi sababu zake zote zitakapokuwepo. Kiunganishi kimoja katika mlolongo wa sababu hizo ni hiari ya mtu, ambayo ina nafasi

ya wazi ya kipekee. Mwanadamu kiumbe ambaye amepewa hiari, kwa hiyo, matendo yake kufuatilia malengo yaliyo wazi, na katika kufuatilia malengo hayo, hafuati sheria fulani za asili zinazojiendesha zenyewe, kama ilivyo kwa matone ya mvua ambayo huanguka kwa mujibu wa kanuni ya nguvu ya uvutano. Kama ingekuwa vinginevyo, mwanadamu asingeweza, kwa kweli, kufuatilia malengo aliyonayo akilini mwake kama kiumbe chenye hiari.

Hii ni kinyume na fikra ya takdiri, ambayo inaiona hiari ya mtu kama isiyotumika na inahusisha sababu zote kwa Mwenyezi Mungu na mambo yaliyoko nje ya asili yake. Imani katika majaaliwa na hatima huishia kwenye takdiri hapo tu ambapo inapochukuliwa kuwa badala ya uwezo na hiari ya mtu, hivyo kwamba hakuna wajibu au athari inayohusishwa na matakwa yake katika matendo ayafanyayo. Kwa uhalisi, hata hivyo majaaliwa na hatima si vinginevyo isipokuwa ni mfumo wa asili na athari. Qur'ani inasema kwamba baadhi ya wale waliowapinga Mitume na wakanyanyua bendera ya uasi dhidi ya wateule wa Mungu wametafsiri majaaliwa na hatima katika namna ya takdiru. Hawakutaka hali iliopo ibadilike kwa namna ambayo utaratibu wa kijamii wa imani ya Mwenyezi Mungu Mmoja ingeshika nafasi ya desturi zilizooza ambazo waliambatana nazo.

Hizi ndiyo Aya zinazostahili:

وَقَالُوا لَوْ شَاءَ الرَّحْمَـٰنُ مَا عَبَدْنَاهُم ۗ مَّا لَهُم بِذَٰلِكَ مِنْ عِلْمٍ ۖ إِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿٢٠﴾ أَمْ آتَيْنَاهُمْ كِتَابًا مِّن قَبْلِهِ فَهُم بِهِ مُسْتَمْسِكُونَ ﴿٢١﴾

"Nao husema: Angelipenda Mwingi wa rehema tusingewaabudu sisi. Hawana ujuzi wowote wa hayo! Hawana ila kusema uwongo tu! Kwani tuliwapa Kitabu kabla ya hiki, na ikawa wao wanakishikilia hicho?" (43:20-21).

Kinyume na wafuasi wa makaadiru, wajumbe wa Mwenyezi Mungu na wafuasi wa mafundisho ya matakatifu hawakuhusika na kulinda hali kama ilivyokuwa lakini wao walihusika na kubadilisha desturi na kuangalia hali ya siku za baadaye.

Qur'ani Tukufu inaahidi jamii ya wanadamu mwisho wenye ushindi katika mapambano yake dhidi ya madikteta na inasisitiza kwamba serikali ya mwisho kutawala hapa duniani itakuwa ni serikali ya haki; upotofu utatoweka na matokeo ya mwisho ya mambo yote yatakuwa mikononi mwa wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu. Hii ndio ahadi ya Qur'ani:

وَنُرِيدُ أَن نَّمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَئِمَّةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ ﴿٥﴾

"Na tukataka kuwafadhili wale waliodhoofishwa katika ardhi na kuwafanya viongozi na wawe warithi."(28:5),

وَعَدَ اللَّـهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَـٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥٥﴾

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani

baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.

(24:55),

وَأَوْرَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِينَ كَانُوا يُسْتَضْعَفُونَ مَشَارِقَ الْأَرْضِ وَمَغَارِبَهَا الَّتِي بَارَكْنَا فِيهَا وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ الْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ بِمَا صَبَرُوا وَدَمَّرْنَا مَا كَانَ يَصْنَعُ فِرْعَوْنُ وَقَوْمُهُ وَمَا كَانُوا يَعْرِشُونَ ﴿١٣٧﴾

"Na tukawarithisha watu waliokuwa wanadharauliwa mashariki na magharibi mwa ardhi tuliyoibariki. Na likatimia neon jema la Mola wako juu ya wana wa Israili, kwa vile walivyosubiri. Na tukayaangamiza aliyokuwa akiyafanya Firauni na kaumu yake, na waliyokuwa wakiyajenga." (7:137).

Kwa hiyo Qur'ani inaoyesha upinzani kati ya imani na kutoamini, kati ya walionyang'anywa na madikteta, na inatuambia kwamba dunia inaelekea kwenye ushindi wa ukweli dhidi ya batili, wa walioonewa dhidi ya wakandamizaji, vuguvugu la kimapinduzi liko mbioni ambalo linayoendana na msogeo wa maumbile yote kuelekea kwenye ukamilifu.

Wito wa Mitume, thawabu na adhabu, pepo na moto wa jahanamu - yote haya yanathibitisha kwamba mwanadamu anazo kazi na wajibu, na kwa sababu hiyo Qur'ani inaunganisha ukombozi wa mwanadamu hapa duniani na baada ya hapa duniani kwenye matendo yake. Kwa mujibu wa kanuni ya majaaliwa na hatima, mtu yu huru na anawajibika kwa hatima yake na anaidhibiti. Majaaliwa na hatima kwa kweli hufanya kazi endapo watu fulani wanao uwezo na wengine wanyonge na dhaifu, kama jamii moja ina ushindi na inajivuna, na nyingine, imeshindwa na ni dhaifu. Hii ni kwa sababu tu kwamba majaaliwa na hatima huamua kwamba watu fulani hutumia uwezo wa kusonga mbele na kuendelea na kutembea kwenye njia ya heshima na hadhi, ambapo kundi lingine huchagua kujinyima na kutojali, na haliwezi kutegemea lolote isipokuwa kushindwa, fedheha na unyonge.

Qur'ani inasema wazi:

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّـهَ لَمْ يَكُ مُغَيِّرًا نِّعْمَةً أَنْعَمَهَا عَلَىٰ قَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ وَأَنَّ اللَّـهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٥٣﴾

"Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu habadilishi kabisa neema alizowaneemesha watu, mpaka wao wabadilishe yaliyomo ndani ya nafsi zao......"(8:53).

Bila shaka inaweza kutokea kwamba matakwa yetu hayatimizwi kama tunavyotegemea, lakini hii kwa hali yoyote haithibitisha kwamba mwanadamu analazimika na kukadiriwa katika vitendo vyake. Ukweli kwamba nafasi ya matendo ya hiari ya mwanadamu imewekewa mipaka kwa namna yoyote ile haipingani na kuwa kwake na hiari kuliko wazi; kukubali kwamba mwanadamu anayo hiari kwa namna yoyote ile kunamaanisha kwamba hiari yake haina mipaka. Mwenyezi Mungu ameweka mambo mengi sana ili yafanye kazi kwenye uwazi mpana wa maumbile. Wakati mwingine mambo haya, pamoja na matukio ambamo hutokea, yanadhihirika kwa binadamu na wakati mwingine hayaonekani. Tafsiri ya uangalifu ya fikra ya majaaliwa na hatima itamhamasisha

mwanadamu kujitahidi zaidi kujua na kutambua mambo yote hayo, ili kwamba kwa kuyazingatia, anaweza bado kutumainia mafanikio makubwa zaidi. Kwa kwa sababu hasa ya ufinyu wa uwezo wa binadamu kwamba hawezi kupata mambo yote yanayohitajika kwa ajili ya kufuzu ili kwamba matamanio yake, matakwa yake yanabakia hayajatimizwa.

Kwa mujibu wa kanuni ya jumla ya usababisho, hatima ya kila kiumbe imefungamana na vyanzo vinavyo kitangulia. Kama mtu atakubali kuwepo kwa kanuni ya ki-Mungu au hapana hana mwelekeo kwenye suala la uhuru na hatima ya binadamu, kwa sababu mtu anaweza ama kuhusisha mfumo wa chanzo na athari kwenye utashi wa Mwenyezi Mungu, au adhani kwamba inajitegemea na haina uhusiano na kanuni ya ki-Mungu. Hali ikiwa ni hivyo, pia haiwezi kufikiriwa kwamba majaala yanatokana na kuamini katika misinngi ya majaaliwa na hatima. Tunachomaanisha kwa majaaliwa ni kiunganishi kisichoachanishwa cha kila kiumbe na vyanzo vyake, pamoja na hiari na chaguo la mtu; kwa hakika hatukanushi usababisho.

Majaaliwa na hatima husababisha kuwepo kwa kila tukio kwa njia ya chanzo chake maalum. Utashi wa Mwenyezi Mungu hutawala pote duniani kama kanuni na sheria ya ulimwengu. Badiliko lolote linalofanyika pia ni katika msingi wa utaratibu au kanuni ya ki-Mungu. Kama mambo yasingekuwa hivyo, majaaliwa na hatima yasingekuwa na mwonekano wa nje kamwe. Taasisi yoyote ya fikra ya kisayansi inayokubali kanuni ya usababisho wa kijumla inalazimika kukubali ukweli wa uhusiano baina ya matukio na chanzo chake, ikiwa imma ni ya imani ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu au ya kiyakinifu katika matarajio yake.

Sasa, kama kiungo dhahiri kati ya kutokea kwa jambo - pamoja na matendo ya wanadamu - na sababu zake zinaelekezea kwa mwanadamu kuwa ni roboti, aliyekwishakadiriwa katika matendo yake, yote ya imani ya Mungu mmoja na ya kiyakinifu yako wazi kwa pingamizi, kwa kadiri yote yanavyokubali usababisho. Lakini kama hakielekezi kwenye mwisho huo (kama ambavyo kwa kweli kisingefanya hivyo), swali bado linajitokeza: ni tofauti gani, katika hali hii, kati ya uabudu Mungu mmoja na uyakinifu?

Tofauti ni kwamba mtazamo wa dunia wa kiimani ya Mungu mmoja ukilinganishwa na ule wa uyakinifu, unachukulia mambo ya kidhanifu na yasiyokuwa ya maada kuwa yanaweza kusababisha athari. mambo hayo kwa kweli ni yenye kutatiza sana na magumu katika utando wa maumbile kuliko yalivyo mambo ya kimaada. Falsafa ya maisha yenye msingi juu ya imani kwa Mwenyezi Mungu inatia moyo, lengo na maana kwenye maisha. Humpatia mwanadamu ujasiri, uimara, upana wa mawazo, kuzama katika umaizi na ushupavu wa akili; humzuia asiangukie kwenye lindi kuu la kutokuwa na lengo; na humchukua juu kwenye tao lisilo na ukomo wa kwenda juu.

Kwa hiyo, mtu anayemwamini Mwenyezi Mungu ambaye anasadiki kikamilifu kuhusu majaaliwa na hatima, ambaye anatambua kwamba kuna makusudio ya busara yanayofanya kazi kwenye uumbaji wa binadamu na ulimwengu, ataelekea kwenye njia iliyonyooka kupitia kumtegemea kwake Mwenyezi Mungu; akijijua mwenyewe kwamba anasaidiwa na kulindwa na Mwenyezi Mungu, atakuwa mwenye kujiamini zaidi na mwenye matumaini ya matokeo ya shughuli yake.

Lakini mtu ambaye amenasa kwenye falsafa ya maisha ya uyakinifu, ambaye mfumo wa akili yake humwelekeza kuamini katika majaaliwa ya kimaada na hatima, hapati yoyote kati ya manufaa haya. Anakosa msaada wa uhakika na usioshindika katika kujitahidi kufanikisha malengo yake. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba kuna tofauti kubwa kati ya mifumo miwili ya fikra kwa kiasi ambacho athari zao za kijamii na kisaikolojia zinavyohusika. Anatole France anasema: "Ni athari ya manufaa ya kidini ambayo humfundisha mwanadamu sababu ya kuwepo kwake na matokeo ya matendo yake. Mara tunapozikataa kanuni za falsafa za kiimani ya Mungu mmoja, kama wafanyavyo sasa karibu watu wote katika kipindi hiki cha sayansi na uhuru, hatuna tena njia ya kujua kwa nini tumekuja hapa duniani na nini tunatakiwa kufanikisha baada ya kukanyaga dunia hii.

"Mwujiza wa hatima umetukumbatia kwa siri zake zenye uwezo mkubwa, na kama tunataka kuepuka kabisa kukutana na kusikitisha kwa utata wa maisha, lazima tusifikiri kabisa.

Kwani mzizi wa huzuni zetu upo kwenye ujinga wa kutokujua kwetu sababu ya kuwepo kwetu. Maumivu ya kimwili na kiroho, mateso ya roho na akili - yote yangeweza kuvumilika endapo tungetambua sababu yao na kuamini kwamba Mwenyezi Mungu ameyaridhia. "Muumini wa kweli hufurahia mateso ya kiroho anayoyavumilia. Hata dhambi anazofanya hazimnyang'anyi matumaini. Lakini kwenye dunia ambamo mwale wa imani umezimwa, maumivu na ugonjwa hupoteza maana na huwa utani mbaya, aina ya dhihaka ya kisirani."

21

# MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

## SOMO LA ISHIRINI NA MOJA

### TAFSIRI ISIOFAA YA MAJAALIWA NA HATIMA

Baadhi ya wasomi bandia wanazo fikra potofu kuhusu majaaliwa na hatima na hudhani kwamba msingi huu husababisha kuvia na kutojishughulisha, humzuia binadamu na juhudi za aina yoyote za kuboresha maisha yake. Chanzo cha fikra hii katika nchi za Magharibi ni kutokuelewa vya kutosha kuhusu dhana hii, hususan kama inavyofafanuliwa katika mafundisho ya Kiislamu. Huko nchi za Mashariki fikra hii imepata athari kwa sababu ya kufifia na kurudi nyuma kimaendeleo.

Inajulikana vya kutosha kwamba wakati wowote watu au jamii za kihistoria zinaposhindwa kufikia malengo na mawazo yao, kwa sababu yoyote ile, hujifariji kwa maneno kama vvile 'bahati' 'ajali', 'hatima', 'majaaliwa'. Mtume mtukufu kabisa **(s.a.w.w)** alijieleza kwa ufasaha sana kuhusu jambo hili: "Wakati utakuja kwa watu wa umma wangu ambapo watafanya dhambi na dhuluma, na ili waweze kuhalalisha uovu na uchafu wao, watasema: 'majaaliwa na hatima yametuamulia kwamba tufanye hivi.' Ukikutana na watu kama hao, waambie mimi siwatambui, ninawakana hao."

Kuamini majaaliwa na hatima haimzuii mtu kufanya jitihada kufikia malengo yake katika maisha yake. Kama wale wenye ujuzi muhimuwa kidini wanavyotambua, Uislamu unawataka wanadamu kujitahidi sana katika kuboresha maisha yao, kimaadili na kimali. Peke yake hiki ni kipengele madhubuti katika kuongeza juhudi anayofanya mwanadamu. Mmoja wa mabingwa wa nchi za Magharibi ambaye anao uelewa mfinyu wa majaaliwa na hatima ni Jean- Paul Sartre. Anadhani haiwezekani kwa wakati moja kuamini majaaliwa na hatima chini ya uamuzi wa Mwenyezi Mungu na katika uhuru wa binadamu, na kwa hiyo, ni muhimu ama kuchagua kumwanini Mwenyezi Mungu au hiari ya mwanadamu: "Kwa sababu mimi ninaamini katika uhuru, siwezi kumwamini Mwenyezi Mungu, kwa sababu endapo ninamwamini Mwenyezi Mungu, lazima nikubali dhana ya majaaliwa, na kama nikikubali majaaliwa, nitalazimika kukana uhuru.

Kwa kuwa mimi ninaambatana na uhuru, simwamini Mwenyezi Mungu." Hata hivyo, hakuna ukinzani kati ya kuamini majaaliwa kwa upande moja, na uhuru wa mtu, kwa upande mwingine. Wakati inapochukulia utashi wa Mwenyezi Mungu kuwa wa kila mahali kiuwezo, Qur'ani Tukufu pia inahusisha wajibu huru na hai kwa binadamu, ikimwelezea kama mwenye uwezo kutengeneza hatima yake mwenyewe akiwa na utambuzi wa wema na uovu, ubaya na uzuri, na uwezo wa kuchagua kati ya hayo:

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

"Hakika sisi tumemuongoza njia, imma awe ni mwenye kushukuru au mwenye kukufuru." (76:3),

وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَـٰئِكَ كَانَ سَعْيُهُم مَّشْكُورًا ﴿١٩﴾

"Na aliyeitaka Akhera na akaifanyia juhudi, ile inayopasa, naye ni mwenye kuamini, basi hao ndio juhudi zao zitakubaliwa." (17:19).

Wale ambao mnamo siku hiyo ya Hukumu wataitafuta hifadhi kwenye uamini majaaliwa na kusema:

لَوْ شَاءَ اللَّـهُ مَا عَبَدْنَا مِن دُونِهِ مِن شَيْءٍ ﴿٣٥﴾

"Mwenyezi Mungu angetaka tusingeliabudu chochote badala yake....." (16:35).

Wanashutumiwa kwa kuhusisha utendaji dhambi wao na upotovu kwenye utashi wa Mwenyezi Mungu na majaaliwa.

Hakuna hata ndani ya Aya moja kwenye Qur'ani ambamo ufisadi na matendo maovu ya mtu au jamii yamehusishwa kwenye majaaliwa na hatima. Hivyo, majaaliwa na hatima ni mambo ambayo hayakuonyeshwa kama vikwazo kwa jamiii fisadi na ya kiuovu inayojirekebisha. Hakuna hata Aya moja inayoweza kupatikana ambayo kwamba utashi wa Mwenyezi Mungu umeshika nafasi ya hiari ya binadamu au ambamo inasemekana kwamba mtu alianza kuteseka kwa sababu ya majaaliwa na hatima.

Qur'ani imetamka kwa kurudia rudia ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ambayo itawakumba madikteta na mafisadi, kwa kuleta adhabu kali baada yake. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni mwenye mapenzi na huruma sana kwa waja wake, akiwa ametoa neema zisizohesabika juu yao na wakati huo huo ni mpole na yu tayari kukubali toba, wakati wote Ameacha wazi njia kwa mwenye dhambi anayetaka kurudi kwenye utakaso na unyofu. Kukubali toba kwa Mwenyezi Mungu, kwenyewe peke yake ni mfano mkubwa sana wa huruma Yake.

Ingawa upeo wa hiari ya binadamu ni mkubwa na mpana zaidi kuliko ule wa viumbe hai vingine vijulikanavyo na huchukua nafasi kubwa sana ya ubunifu zaidi, hiari yake ina athari kwenye maeneo yale tu ambayo yamewekewa mipaka na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya shughuli na matendo yake. Kwa hiyo, binadamu hawezi kutimiza kila kitu anachotaka katika maisha yake. Mara nyingi hutokea kwamba mtu huamua kufanya jambo lakini kila atakavyojitahidi, anakuwa hawezi kulitimiza. Sababu yake hili sio kwamba utashi wa Mwenyezi Mungu unajipinga wenyewe kuhusu hiari ya mwanadamu na kumzuia kufanya atakavyo. Ni kwamba hasa katika masuala kama hayo, vipengele vya nje visivyojulikana vilivyopo nje ya upeo wa ujuzi na udhibiti wa binadamu huzusha vikwazo kwenye njia yake na kumzuia kufanikisha malengo yake.

Watu binafsi na jamii wakati wote hukabiliana na vikwazo vya aina hii. Kuzingatia ukweli kwamba katika uwanja wa maumbile hakuna chanzo bila athari na hakuna athari bila chanzo, na kwamba uwezo wetu wa kutambua umewekewa mipaka katika dunia hii na kwenye milki ya binadamu, isiwe vigumu sisi kukubali kwamba matumaini yetu yanaweza yasitimie kama tunavyotaka.

Mwenyezi Mungu ameweka mabilioni ya vipengele katika utaratibu wa uhai. Wakati mwingine vipengele hivyo vipo dhahiri kwa mwanadamu, wakati mwingine havijulikani kwa binadamu na haviwezi kushirikishwa katika kufikiri kwake. Hali hii pia ina uhusiano na majaaliwa na hatima lakini sio tu kwamba haishii katika kumnyima mwanadamu hiari au kumzuia kujaribu kupata hali ya kujitosheleza katika maisha; pia humwongoza kifikra na kishughuli na humjaza ndani kabisa ya nafsi yake na matumaini makubwa. Binadamu hutafuta kuongeza ujuzi wake na

utambulisho wake, kwa usahihi kadiri iwezekanavyo, mambo ambayo humnyooshea njia ya kupata mafanikio makubwa zaidi katika maisha. Imani ya majaaliwa na hatima kwa hiyo ni mambo yenye nguvu katika kumwendeleza binadamu kuelekea kwenye malengo yake na ubora wake.

Suala la ukombozi au kulaaniwa kwa mwanadamu limetafutiwa ufumbuzi kwenye mazungumzo yaliyotangulia, kwani ukombozi na kulaaniwa hutokana na matendo ya mwanadamu si kutoka kwenye mambo ambayo yapo nje ya upeo wa hiari zao au kutoka kwenye matukio ya asili ambayo yamepandikizwa na Muumbaji kwenye uhai wa mwanadamu. Wala sio mambo ya kimazingira na urithi ama uwezo wa kimaumbile uliopo ndani ya mwanadamu ambavyo vina athari zozote kuhusu ukombozi wa mtu au laana yake; hayawezi kutengeneza hatima yake. Kile kinachokadiria mambo ya binadamu ya siku za usoni, ni ule mhimili ambamo ukombozi au kulaaniwa kwake huzunguuka na chanzo cha kupanda au kushuka kwake, ni kiwango ambacho mwanadamu kama kiumbe ambacho kimepewa hiari ya kuchaga, hutengeneza matumizi yanayofaa ya akili yake na ujuzi na uwezo mwingine.

Furaha na ukombozi havitegemei wingi wa uwezo wa kimaumbile. Hata hivyo, ni kweli kwamba mtu ambaye ana uwezo mkubwa zaidi kuliko wengine pia huwa na wajibu mkubwa zaidi. Kosa dogo kwa upande wake ni la wazi zaidi kuliko kosa hilo hilo ambalo limefanywa na mtu dhaifu na asiye na uwezo. Kila mtu ataitwa kuwasilisha mahesabu yake kwa mujibu wa vipaji na uwezo aliokuwa nao.

Inawezekana kabisa kwamba mtu ambaye uwezo wake wa asili na maarifa ni madogo anatakiwa kuendesha maisha yake kwa mujibu wa kazi zake na wajibu wake, alizopewa na kufikia hiyo furaha ya kweli ambayo hiyo peke yake inastahili ya kituo cha juu sana cha mwanadamu. Kitakachomwezesha kupata matokeo hayo ni ukubwa wa juhudi zake anazotumia ili kufanya matumizi sahihi ya uwezo mdogo aliopewa.

Kinyume chake, mtu ambaye amepewa maarifa ya ndani mwengi sana na uwezo mkubwa, sio tu anaweza kutozitumia kwa kujinufaisha mwenyewe, anaweza kutumia vibaya na kufedhehesha hadhi yake ya ubinadamu; na kujitumbukiza kwenye dimbwi la uovu na dhambi. Mtu kama huyu, bila shaka ni mwovu anayetegemewa kulaaniwa na kamwe hatapata hata sekunde moja ya kuona ukombozi. Qur'ani inasema:

"Kila nafsi itafungika (motoni) kwa (maovu) iliyoyachuma." (74:38).

Kwa hiyo, ukombozi au laana ya mtu hutegemeana na matendo yake ya hiari, sio katika hali yake ya kimaumbile au kisaikolojia. Huu ni udhihirisho wa wazi mno wa uadilifu wa Mwenyezi Mungu.

Moja ya kanuni bainifu za madhehebu ya Shia ni badaa, neno lenye maana kwamba hatima za wanadamu hubadilika pale ambapo mambo na vyanzo vinavyoyarekebisha hubadilika; kile kinachoonekana kama cha milele na kisichobadilika, hubadilika kwa mujibu wa mabadiliko ya tabia ya mtu na matendo yake. Kama ambavyo vipengle vya kimaada vinavyoweza kubadili hatima ya mtu, vipengele visivyo vya kimaada pia vinaweza kuchochea matukio mapya.

Inawezekana kwamba vipengele visivyo vya kimaada kama hivi vinaweza kudhihirisha wazi yale yaliyofichika na kinyume na mkondo

uliowazi wa matukio. Kwa kweli, kupitia kwenye mabadiliko ya sababu na mazingira, Mwenyezi Mungu ataamua kwamba tukio jipya litatokea, lenye manufaa zaidi ya lile lililobadilishwa. Hii inalingana na ile kanuni ya kutangua sheria iliyofunuliwa. Kama sheria ya mwanzo inatanguliwa kwa ajili ya nyingine, hii haionyeshi ujinga au kujuta kwa upande wa mtungaji-sheria za ki-mungu ila tu ni kwamba uhalali wa ile sheria iliyofutwa umefikia mwisho wake.

Hatuwezi kutafsiri dhana ya badaa kwa maana kwamba Mwenyezi Mungu anabadili mawazo Yake baada ya ukweli wa kitu ambacho mwanzoni hakukijua na akaja kukijua baadae. Hii itakuwa inapingana na kanuni ya ujuzi wa Mwenyezi Mungu unaojumuisha ulimwengu wote na kwa hiyo haiwezi kukubaliwa na Muislamu yeyote.

Maombi ya dua ni kipengele kingine, ambacho kwamba athari yake isidhalilishwe. Ni dhahiri kwamba Mwenyezi Mungu anatambua siri za ndani kabisa za kila mwanadamu, lakini katika uhusiano wa mtu na Mwenyezi Mungu, maombi ya dua huchukua nafasi kama ile ya juhudi na matendo katika uhusiano wake na maumbile. Mbali kabisa na athari zake za kisaikolojia, dua husababisha athari inayojitegemea.

Kila sekunde matukio mapya hutokea katika maumbile katika kutokea ambako sababu zinazotangulia hutoa mchango. Vivyo hivyo, katika fani moja mashuhuri sana ya maisha maombi ya dua yana athari kubwa sana katika kumwendeleza mtu kuelekea kwenye malengo yake. Kwa namna ileile tu ambayo Mwenyezi Mungu ameweka wajibu kwenye mfumo wa usababisho kwa kila kitu cha asili, vivyo pia, Ameweka wajibu kwenye maombi ya dua.

Mtu anapozungukwa na matatizo, asije akaangukia kwenye fikra za kukosa matumaini na kukataa tamaa. Milango ya huruma za Mwenyezi Mungu kamwe haikufungwa kwa yeyote yule. Inawezekana kwamba kesho hali mpya inatokea ambayo haiendani na vile alivyotegemea. Kwani, kama isemavyo Qur'ani:

".....Kila siku Yeye yumo katika mambo tofauti tofauti." (55:29).

Kwa hiyo, mtu anatakiwa asiache juhudi zake kamwe. Maombi ya dua ambayo hayaunganishwi na jitihada zinazofaa, kama Ali (a.s) Mkuu wa Wamwogopao Mwenyezi Mungu alivyosema, "Kama mtu anayetaka kuachia mshale kutoka kwenye upinde usiokuwa na kamba." Wakati anapofanya juhudi mfululizo, mtu anatakiwa kuweka matakwa yake mbele ya Mwenyezi Mungu, kwa kutumaini na kuamini, na kuomba msaada kwa moyo wote kutoka kwenye kile chanzo cha uwezo wa milele. Mwenyezi Mungu, kwa hakika atamshika mkono mhusika na kumsaidia.

Qur'ani inasema:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾

"Na waja wangu watakapokuuliza juu yangu basi hakika mimi nipo karibu, nayaitikia maombi ya muombaji anapoomba. Basi waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka." (2:186).

Roho ya binadamu itapaa juu kuelekea kwa Mwenyezi Mungu na kumtosa kwenye furaha ya kweli ikiwa atakwepa lindi la kuhitaji kwa

kuvunja uhu- siano na vyanzo vyote na kumgeukia Mwenyezi Mungu. Hapo atajiona ameungana moja kwa moja na dhati ya Mwenyezi Mungu na kuhisi kuguswa na neema na baraka Zake zisizo na ukomo. Imamu Sajjad (a.s) anamuomba Mwenyezi Mungu ifuatavyo katika dua yake ijulikanayo kama Dua ya Abu Hamza:

"Ee Muumba! Naona njia za kuombea na kulalamikia zinazoelekea Kwako zikiwa wazi na zilizosawazishwa, na sababu za matumaini Kwako zikiwa nyingi sana. Naona inaruhusiwa kuomba msaaada kutoka kwenye neema Yako na huruma Yako, na ninaiona milango ya dua ipo wazi kwa wote wanaokujia Wewe na kuomba msaada Wako. Ninao uhakika kwamba Wewe upo tayari kujibu maombi ya wale wanaokuomba Wewe na kutoa hifadhi kwa wale wanaoitafuta kutoka Kwako."[1]

Pia ipo hadithi kuhusu athari za dhambi na matendo mema: "Wale wanaokufa kwa sababu ya dhambi ni wengi zaidi kuzidi wale wanaokufa kwa sababu za kawaida, na wale wanaoishi kwa sababu ya kutenda matendo mema ni wengi zaidi kuliko wale wanaoishi kwa sababu ya umri wao wa kawaida."[2]

Ilikuwa ni athari za dua zilizomwezesha Zakariya, Mtume wa kweli ambaye alikuwa amekata tamaa ya kupata mtoto, kufanikiwa matakwa yake; ilikuwa athari ya toba iliyomwokoa Mtume Yunus na watu wake kutokana na janga na kuangamia. Sheria ambazo Mwumbaji Mkuu amezipandikiza kwenye mfumo wa ulimwengu, kwa namna yoyote ile haziwezi kuwa mipaka ya uwezo Wake usio na ukomo au kupunguza upeo wake. Anao uamuzi ule ule wa uhakika katika kubadilisha sheria hizo, katika kuthibitisha au kutangua athari

zao, kama Alivyofanya katika kuziasisi. Hiyo dhati ya Pekee, Ambayo usimamizi wake wenye uangalifu na mpana unajumuisha mfumo wote wa uhai, haiwezi kutiishwa kabisa na sheria na viumbe ambavyo Ameviumba Mwenyewe, au Apoteze madaraka na uwezo wa kufanya Atakavyo. Tunaposema kwamba Mwenyezi Mungu anao uwezo wakati wowote kubadili jambo ambalo Ameliumba katika dunia, hatuna maana kwamba Huharibu utaratibu wa dunia na kanuni zake zilizowekwa au anabadilisha sheria na kanuni za maumbile. Kutendeka hasa kwa mabadiliko hutokea kwa kulingana na kanuni fulani zisizojulikana na vigezo ambavyo vinaupita uelewa na utambuzi wetu mfinyu. Endapo mtu analitazama kwa uangalifu na umakini jambo lenyewe na akaufikiria wigo mpana wa uwezekano ambao unamkabili, utamzuia kufanya majaribio makubwa kwa shauku kabisa, ya kutabiri vitu vyote kwa msingi wa kanuni zile chache ambazo ameweza kuzichunguza katika nyanja ya maumbile.

1. Mafatih al-Jinan, 1, uk.185.
2. Safinatt al-Bihar, 1, uk. 488.

## ORODHAYA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na tatu
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Mashukio ya Akhera
30. Nafasi ya Ahlul Bayt
31. Uislamu mfumo wa maisha

Mwenyezi Mungu na sifa zake

258

32. Haki za wanawake
33. Adhana
34. Amateka
35. Udhuu kwa mujibu wa kitabu na sunna
36. Al-Amali
37. Nyuma yaho naje Kuyoboka
38. Amavu namavuko by ubushiya
39. Dua Kwa Mujibu Wa Ahlulbayt (as)

## BACK COVER MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE

Uislamu ni dini ya elimu na mtu hatakiwi afuate tu kibubusa bila kuelewa kile anachokifua na kukiamini. Misemo inayotumiwa na watu wavivu wakusoma kama vile; "mimi nina swali, ninafunga Mwezi wa Ramadhani na ninashiriki katika masuala yanayo husu dini, hivyo sina haja ya kujua mambo mengine ya dini," kauli kama hizi hazikubaliki katika Uislamu. Mtu lazima ajifundishe na ailewe dini yake vilivyo. Na kitu cha kwanza kwa Mwislamu ni kumjua Mwenyezi Mungu na Sifa Zake ili aweze kufanya ibada zake vizuri na kwa usahihi.

Kitabu hiki huelezea mtazamo wa imani ya Kiislamu ya Mungu Mmoja asiye na mshirika. Mwandishi wa kitabu hiki ameichambua itikadi ya Kiislamu na Umoja wa Mungu (tawhid) kwa kutumia uhojaji wa kifilosofia na maneno mepesi. Ili kukamilisha kazi yake hii ametegemea sana juu ya Sunna na nukuu nyingi kutoka kwenye Qur'an Tukufu. kwa uhodari mkubwa na ujuzi ameyapinga mawazo na mitazamo ya wakana Mungu na wale wanaomshirikisha Mwenyezi Mungu na viumbe vyake.

### SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

### MWISHO WA KITABU

## YALIYOMO

**1** .................................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
1 ................................................... KIMEANDIKWA NA
1 ............................ SAYYID MUJTABAA MUUSAWIY LARI
1 ............................................ KUHUSU MWANDISHI
3 .......................................... NENO LA MCHAPISHAJI
4 ......................................................... UTANGULIZI
**5** .................................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
**5** ....................................................... **SOMO LAKWANZA**
5 ......... USTAWI WA IMANI KATIKA VIPINDI MBALIMBALI
**11** ................................ **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
11 ....................................................... SOMO LA PILI
UNDANI WA NAFSI YA MWANADAMU HUMLAZIMISHA
11 ............................. KUMTAFUTA MWENYEZI MUNGU
**19** ................................ **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
19 .................................................... SOMO LA TATU
19 .. MWENYEZI MUNGU NA MANTIKI YA JARIBIO (JARABA)
**25** ................................ **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
25 ........................................................ SOMO LA NNE
KUAMINI UKWELI WA KISICHOONEKANA KUNAHUSISHA
25 ........................ MENGI ZAIDI YA MWENYEZI MUNGU
30 .............................. UMUHIMU WA KANUNI ZA UHAI
**33** ................................ **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
33 .................................................... SOMO LA TANO
33 ... KUONEKANA MWENYEZI MUNGU KATIKA MAUMBILE
**47** ................................ **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
47 ...................................................... SOMO LA SITA
HAJA YA ULIMWENGU KUMHITAJI YULE ASIYEHITAJI
47 ......................................................... CHOCHOTE
**54** ................................ **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
54 .................................................... SOMO LA SABA
54 .................... UKOMO WA NYORORO YA USABABISHO
**60** ................................ **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
60 .................................................... SOMO LA NANE
60 ................................ FITINA BANDIA ZA KISAYANSI
**71** ................................ **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
71 ...................................................... SOMO LA TISA

71 ....... QUR'ANII INAMUWASILISHAJE MWENYEZI MUNGU
**77** ............................... **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
77 ..................................................... SOMO LA KUMI
77 ...................... MASHARTI YA LENGO BORA LA IBADA
IBADA, NJIA BORA YA BINADAMU YA KUONYESHA
80 ........................................................ SHUKRANI
**85** ............................... **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
85 ........................................ SOMO LA KUMI NA MOJA
85 ..............KUTOLINGANISHIKAKWA SIFA ZA KI-MUNGU
87 ............... UPWEKE WA MWENYEZI MUNGU (TAWHIID)
**94** ............................... **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
94 ........................................ SOMO LA KUMI NA MBILI
94 ...............UWEZO WA MWENYEZI MUNGU USIOPIMIKA
**99** ............................... **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
99 ........................................ SOMO LA KUMI NA TATU
99 ......... ELIMU YA MWENYEZI MUNGU ISIYO NA MIPAKA
**104** ............................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
104 ........................................ SOMO LA KUMI NA NNE
104 .....MAONI KUHUSU UADILIFU WA MWENYEZI MUNGU
**109** ............................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
109 ....................................... SOMO LA KUMI NA TANO
109 ................... UCHAMBUZI KUHUSU BALAA NA DHIKI
**114** ............................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
114 ....................................... SOMO LA KUMI NA SITA
114 .......................... MATATIZO, SABABU YA KUAMKA
**118** ............................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
118 ...................................... SOMO LA KUMI NA SABA
118 ..................... BAADHI YA VIPENGELE VYA TOFAUTI
**124** ............................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
124 ....................................... SOMO LA KUMI NA NANE
124 ................... MTAZAMO WA JUMLAWA TATIZO HILO
**134** ............................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
134 ....................................... SOMO LA KUMI NA TISA
134 ............................................................. HIARI
**145** ............................. **MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
145 .............................................. SOMO LA ISHIRINI

145 . MIUNDO YA RIDHAA ZA MWENYEZI MUNGU NA HIARI
**153 ............................ MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE**
153 .................................. SOMO LA ISHIRINI NA MOJA
153 .......... TAFSIRI ISIOFAA YA MAJAALIWA NA HATIMA
ORODHAYA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH
158 ................................................... FOUNDATION
159 ....... BACK COVER MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE
159 ........................................ SHARTI YA KUCHAPA
159 ....................................... MWISHO WA KITABU
160 ..................................................... YALIYOMO